

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Pili – Tarehe 6 Aprili, 2011

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (K.N.Y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):

Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2007/2008.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI):

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2009.

SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Agustino Lyatonga Mrema. Siku hizi ni Dkt. Mheshimiwa Mrema, siyo kumwita tu! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Dkt. Mrema akae kwenye *Mic* sahihi na *Mic* sahihi ni hii hapa!

SPIKA: Amesikia tu, nenda kasimame tu kule, hakuna kilichoharibika.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana maana ni wewe ndiye ulituanzishia mchakato wa kupata hii *Degree* niliyonayo ya *Doctorate*. Ahsante sana.

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2009.

MHE. JUMA A. NJWAYO (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MASHIRIKA YA UMMA):

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2009.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mfahamu kwamba Wenyeviti wa Kamati hizi zote nilizozitaja wanatoka Kambi ya Upinzani ndvivo ilivyo kwa mujibu wa Kanuni zetu. Sasa hawa waliowasilisha wako huu upande huu mwingine, nadhani ni makubaliano yao katika Kamati zao. Tunaendelea.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya Ilemela, Dawa na Maabara

MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA aliuliza:-

Tangu tupate uhuru hadi sasa, Wilaya ya Ilemela haijapata Hospitali ya Wilaya, na kwa sababu hiyo huduma za afya katika Vituo vya Afya vilivyopo ni duni sana hali inayosababisha vifo visivyokuwas vya lazima:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Hospitali ya Wilaya kwenye Wilaya ya Ilemela?
- (b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa tatizo la uhaba wa dawa katika Vituo vya Afya vilivyopo pamoja na kuvipatia maabara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Ilemela tangu ianzishwe 2003, haina Hospitali ya Wilaya. Wananchi wa Wilaya ya Ilemela wanapata huduma za afya katika Vituo vya Afya vya Karume na Buzuruga ambavyo vinawezeshwa na Serikali kutoa huduma za afya zenye hadhi ya Hospitali ya

Wilaya ikiwemo kutoa huduma ya upasuaji mkubwa baada ya kujengewa vyumba vya upasuaji na hivyo kupunguza vifo visivyoya lazima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM II) imepanga kutumia shilingi 244,622,000/= ili kuendelea kuviwekea miundombinu muhimu Vituo vya Afya vilivyopo katika utoaji wa huduma za afya. Aidha, wananchi wa Wilaya hii wanahudumiwa katika Hospitali ya Mkoa ya Sekou Toure iliyoko katika Wilaya ya Ilemela na inatoa huduma zote kwa wananchi ndani ya Wilaya ya Ilemela na Mkoa mzima wa Mwanza chini ya umiliki wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Wilaya ya Ilemela inapata Hospitali ya Wilaya, Serikali imetenga eneo la kujenga Hospitali hiyo lililopo katika eneo la Buswelu jirani na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela. Hatua iliyofikiwa ni kuandaa michoro na mwongozo wa ujenzi wa Hospitali hiyo. Juhudi zinazofanywa na Serikali ni kupata fedha kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili azima ya kujenga Hospitali ya Wilaya iweze kutimizwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa dawa katika Wilaya ya Ilemela Serikali inafanya mikakati ya kuboresha mifumo ya uwasilishaji wa takwimu ili kujua mahitaji halisi ya dawa na vifaa tiba vinavyotakiwa kuagizwa kutoka Bohari ya Dawa (MSD). Aidha taarifa zinatakiwa kufahamu ni idadi ya watu wanaotegemea huduma kutoka kwenye Zahanati na Kituo cha Afya nazo zinatafutwa na zinahusika. Mkakati wa Serikali kwa sasa ni kufikisha dawa na vifaa tiba kwenye ngazi za Zahanati na Vituo vya Afya moja kwa moja bila kupitia ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, lakini pia ningeomba kufahamu kwamba Wizara ina mpango gani kuhakikisha kwamba wananchi hususan wa maeneo ya Kata kama ya Bugogwa, Sangabuye na Buswelu ambako wako nje ya mji na ni mbali na Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure; Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na *Ambulance* ya kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kuweza kufika Hospitali ya Sekou Toure kwa wepesi zaidi ili kuepusha vifo visivyokuwa vya lazima hususan kwa akina mama wajawazito ambao wanatembea mwendo mrefu na usafiri ni shida kufika Hospitali hiyo?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Naomba mjibu majibu kwa kifupi, maana maswali ya nyongeza majibu yake mnajibu kirefu mno!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA : Mheshimiwa Spika, nitakwenda ku-*check* katika orodha ya zile *Ambulance* ambazo zimetolewa na kuona kama yuko katika orodha, na kama hayuko basi tutaweka katika mpango. Lakini, kwa sasa hivi nitashindwa kujibu hapa. Nitakwenda kuangalia orodha yenyewe.

MHE. MICHEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kujenga Hopsitali za Wilaya kwa kila Wilaya na ni haki ya wananchi kupata Hospitali hizo, Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ambayo kila mwaka tunailalamikia huko Longido?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Mheshimiwa Lekule anazungumzia Wilaya ambayo ni mpya ambayo ni jirani na Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, ninalielewa tatizo alilonalo. Hili ni jambo ambalo linatakiwa lije katika mpango wa Halmashauri yenyewe. Likija katika mpango wa Halmashauri kama nilivyoeleza jana, sisi hatuna tatizo kabisa, pale pana matatizo, kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba kuna haja ya kuliangalia jambo hili.

Na. 17

Migogoro ya Mipaka ya Vijiji Tarafa za Loliondo na Sale

MHE. KAIKA S. TELELE aliuliza:-

Tarafa za Sale na Loliondo zimekuwa kwenye migogoro ya mipaka ya Vijiji na mashamba kwa baadhi ya koo za jamii ya Wamasai na Wasonjo au Wabatemi kwa muda mrefu sasa na kusababisha mapigano na mauaji kwa pande zote mbili:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za haraka za kutatua tatizo hilo kwa kupima mipaka ya Vijiji husika na kusimamia suala zima la amani kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migogoro iliyopo katika Tarafa za Loliondo na Sale ni migogoro oinayohusisha juamii za wakulima na wafugaji kugombania ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo. Migogoro hii inavihusisha Vijiji 13 (Vijiji 6 vilivyoko katika Tarafa ya Loliondo na Vijiji 7 vilivyoko katika Tarafa ya Sale).

Vijiji vya Tarafa ya Loliondo ni Soitambu, Oloipiri, Losoito, Maaloni, Magaiduru na Enguserosambu. Vijiji vya Tarafa ya Sale ni Malambo, Sale, Tinaga, Kisangilo, Mgongo, Yasimdito na Oldonyosambu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Halmashauri ya Wilaya pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya waliitisha vikao vya Serikali za Vijiji vyenye mgogoro kati ya tarehe 10 – 13/06/2006 kwa lengo la kupata suluhu ya migogoro hiyo. Maazimio ya kikao hicho yalikuwa ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya ardhi isaidie kuweka mipaka ya Vijiji kufuatana na Sheria ya Ardhi Na.5 ya mwaka 1999, eneo lenye migogoro liwe chini ya

uangalizi wa Mkuu wa Wilaya na hairuhusiwi mtu yeyote kufanya shughuli zozote za kibinadamu kwenye maeneo yenye migogoro mpaka suluhu itakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu wa kisheria wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, endapo Halmashauri za Vijiji vyenye mgogoro zitashindwa kufikia makubaliano ya mipaka kwa ushauri wa Halmashauri ya Wilaya, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 Kifungu Na.7(2) imeweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya mipaka ya Vijiji kuwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi ambaye atateua msuluhishi kati ya pande mbili zenye mgogoro ambazo zimeshindwa kuafikiana kuhusu miapaka ili muafaka uweze kupatikana. Hatua zinazochukuliwa na Serikali ni kutoa elimu kwa wananchi wa Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale juu ya umuhimu wa kuweka mipaka pamoja na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mkakati wa kuhakikisha elimu inatolewa ili wadau muhimu wakiwemo Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ngorongoo pamoja na wafugaji, wakulima na wananchi wote wa Tarafa za Loliondo na Sale wanaozunguka maeneo hayo sambamba na upimaji wa mipaka ya Vijiji vilivyomo.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini, nataka kusemakwamba Mheshimiwa Chiligati alipokuwa Waziri wa Ardhi, tulifikia hatua nzuri sana ya kutatua matatizo haya. Na mimi ninachoomba hapa tu leo ni kuiomba Serikali itupatie fedha ya kupima mipaka ya Vijiji hivi na mashamba ili kuondosha kabisa hii migogoro. Vinginevyo elimu na nini tulishafanya sana, tunahitaji hela tu sasa hivi ya kutusaidia kuweza kupima Vijiji, mipaka yake tuweze kusimamia sheria? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tutoe shukrani kwa Mheshimiwa Telele kwamba ametoa ushirikiano mkubwa sana katika mgogoro huu na ameshirikiana na Serikali katika jambo hili. Mheshimiwa Chiligati alikwenda kule kama ilivyoelezwa, na nataka tu nimitamkie kwamba katika mwaka wa 2009/2010, Mkoa ulitenga Bajeti ya kiasi cha shilingi 156,547,600/= kwa ajili ya kusaidia katika utatuzi wa mgogoro huo ikiwa ni pamoja na kupima na mambo mengine anayoyazungumzia. Kwa hiyo, Serikali imeliona hilo.

Na. 18

Mipaka ya Hifadhi ya Misitu na Wanyamapori

MHE. DKT. SEIF S. RASHID aliuliza:-

Mipaka ya Hifadhi ya Misitu na Wanyamapori hususan ile ya *Selous* upande wa Rufiji iliwekwa zamani sana kabla ya uhuru; na Vijiji vilivyoanzishwa baadaye viliendelea kukua sanjari na upanuzi wa maeneo ya uhifadhi na kuwanyima wanakijiji haki ya msingi ya kunufaika na maelewano duni kati ya Hifadhi na wanakijiji:-

Je, ni lini Serikali itashirikiana na wanakijiji wa Rufiji hususan Kata ya Mwaseni ili kupitia upya mipaka hiyo na kukubaliana juu ya matumizi bora ya maeneo yao ya kilimo na uvuvi na yale ya Hifadhi ili kuvutia Watalii na uhifadhi wa Wanyamapori?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mbunge wa Jimbo la Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007, jukumu mojawapo la Wizara ni kushirikisha jamii ambayo iko kwenye Vijiji vinavyozunguka maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori katika kusimamia, kuhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji inatekeleza mradi wa ushirikishaji jamii kwenye uhifadhi katika Vijiji 22 vya Wilaya za Rufiji na Kilwa ambavyo vinapakana na Pori la Akiba la Selous. Maeneo mawili ya Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori (WMAs) yanatarajiwa kuanzishwa ili wananchi wa Vijiji hivyo wanufaike na rasilimali ya Wanyamapori ambayo iko kwenye Vijiji vyao. Katika Wilaya ya Rufiji Vijiji 13 vinawezeshwa kuanzisha WMA na tayari Jumuiya ya Jamii iitwayo JUHIWANGUMWA (Jumuiya ya Hifadhi Wanyamapori Ngorongoro, Utete na Mwaseni) imesajiliwa kwa ajili ya kusimamia mchakato huo. Kati ya Vijiji hivyo 13 vimo Mloka, Mwaseni, Mibuyu-Saba na Mtanza-Msoma ambavyo ni vijiji katika Kata ya Mwaseni. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa wananchi wa Vijiji vya Rufiji vinavyopakana na Pori la Akiba Selous walishirikishwa kikamilifu katika kupitia upya mipaka hiyo. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna migogoro ya mipaka ili wananchi hao waweze kutumia maeneo yao kwa ajili ya makazi, kilimo, uvuvi na uhifadhi wa Wanyamapori.

MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ukamilishaji wa mchakato wa uanzishaji na kukamilisha kwake kwa Jumuiya hizi unategemea utendaji wa Sekretariati ambayo ipo Wizarani kwake, ambayo kwa ujumla inasuasua:-

- (a) Ni lini sasa Jumuiya hizi zitakamilisha mchakato huo na kuanza kazi?
- (b) Kwa kuwa, migogoro ya maeneo ya hifadhi na wanavijiji yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu sana, Ni lini Waziri atatembelea eneo hilo la Rufiji ili kushirikiana na kuweza kuonesha wananchi juu ya ushirikishwaji ambao Waziri ameueleza kwenye Bunge leo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwapo ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mchakato ya uanzishwaji wa WMA kwenye maeneo mbalimbali, sababu mojawapo kubwa imekuwa ni fedha kwamba miradi hii imekuwa ikianzishwa na kutekelezwa kwa usaidizi wa nchi au wafadhili.

Sasa kwenye hili eneo mradi huu unategemea kumalizika mwezi Desemba, 2011. Tumeshajiwekea malengo kwamba mradi utakapokuwa unakamilika Disema tuwe tumekamilisha kuanzisha WMA zote ambazo zinafadhiwa na mradi huu. Kwa hiyo, tunategemea mwezi Desemba tutakuwa tumekamilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili kwamba ni lini nitatembelea eneo hilo niseme tu kwamba nia yangu ni kutemebelea maeneo mengi iwezekanavyo kwa ajili ya kuona hali halisi ilivyo. Hata hivyo kwa kuzingatia wingi wa maeneo kwa kiasi kikubwa nimekuwa pia nikitumia wenzangu ambao tunao pale Wizarani. Kwa hiyo nimhakikishie kama si mimi basi wenzangu pale Wizarani nitawatuma haraka iwezekanavyo kwa ajili ya kwenda kusaidia kutatua matatizo yaliyopo.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika nashukuru sana, uanzishwaji wa WMA ambao Waziri ameutaja kwenye jibu la swali la msingi, ni kitu ambacho kinahitajika sana Wilayani Mbinga, katika Jimbo la Mbinga Mashariki, Kata ya Litumba Njosi, Waziri anawaahidi nini wananchi wa Itumba Njosi kuhusu uanzishwaji wa WMA?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, baada ya kupitishwa sheria Na.5 ya Mwaka 2009 ambayo imeruhusu na kuhimiza sana uwepo wa WMA, nia yetu kama Wizara ni kuhakikisha maeneo yote ambayo yapo jirani na hifadhi hizi yanakuwa katika mpango madhubuti wa kulinda kuhifadhi kupitia hizi WMA.

Nimwombe Mbunge kwa sababu mchakato huu unaanzishwa na wananchi wenyewe, kwamba wananchi wenyewe waanze mchakato wa awali kwa maana ya kuonesha nia na sisi kama Wizara tupo tayari kushirikiana nao kuhakikisha kwamba tunalinda rasilimali zilizopo maeneo hayo.

Na. 19

Elimu ya Sekondari Kufundishwa Kiswahili.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA aliuliza:-

Katika nchi nyingi Duniani, Elimu ya Sekondari hutolewa kwa kutumia lugha za nchi hizo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi. Hapa Tanzania Elimu ya Sekondari hutolewa kwa Kiingereza wakati zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi hawana uelewa mpana wa lugha hiyo:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kufundisha Elimu ya Sekondari kwa lugha ya Kiswahili na somo la Kiingereza likafundishwa kama somo maalum?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo baadhi ya nchi duniani ambazo hutumia lugha zao kufundishia masomo katika shule za Sekondari. Hata hivyo, Tanzania imeamua kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia masomo katika shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia ngaziya Elimu ya Sekondari ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ambayo inatamka bayana kuwa lugha ya kufundishia katika Elimu ya Sekondari itaendelea kuwa Kiingereza ila kwa masomo yaliyokubalika; na Kiswahili kitaendelea kuwa somo la lazima hadi mwisho wa ngazi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa lugha gani itumike kufundishia katika ngazi Yeyote ya elimu hutegemea mambo kadhaa yakiwemo mahusiano na nchi nyingine, msimamo wa kisera na utoshelevu wa lugha husika katika kushughulikia mambo yote ya kielimu katika ngazi husika kwa mfano upatikanaji wa vitabu vilivyoandikwa kwa lugha hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchini Tanzania baada ya mwanafunzi kumaliza Elimu ya Sekondari, hujiunga na Elimu ya Juu au ulimwengu wa kazi. Kuendelea kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia ngazi ya Elimu ya Sekondari huimarisha uelewa wa mwanafunzi katika lugha hiyo ambayo hutumika kufundishia katika ngazi ya Elimu ya Juu. Vivyo hivyo katika ulimwengu wa kazi, sekta binafsi ndiyo huchukua asilimia kubwa ya vijana wetu.

Sekta hii huwakutanisha Watanzania na watu wa mataifa mbalimbali, hivyo lugha ya Kiingereza ni muhimu katika kurahisisha mawasiliano.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa matokeo mabaya ya mtihani wa darasa la Kumi na Mbili la Mwaka jana yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na vijana wengi kutokufahamu Kiingereza ambao walitakiwa kufanya mtihani kwa kiingereza, na kwa kuwa walimu wenyewe wanaofundisha kiingereza katika shule za Msingi na shule za Sekondari kiingereza kinawapa matatizo hawakifahamu sawasawa.

Je, ili kuokoa vijana wetu wasiendeleo kufeli, Serikali ina mkakati gani wa maksudi angalau kuhakikisha kwamba Walimu ambao wanapangiwa kufundisha somo la Kiingereza katika shule za msingi na shule za sekondari wanakifahamu kiingereza vizuri?

(b) Nafahamu kwamba upo mchakato wa kuhariri na kuchapisha kitabu kinachoitwa *New Oxford English Course for Schools* kwa shule za Msingi, mchakato huo ulishaanzishwa na nafahamu unaendelea. Sasa umefikia wapi kwa sababu kama mchakato huo ukikamilika unaweza ukasaidia kuboresha ufundishaji wa somo la Kiingereza katika shule za msingi na shule za sekondari. Je, mchakato huu umefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama tulivyoongea kipindi cha nyuma kuhusu matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne ya mwaka 2010 ambayo yalitoka mwaka 2011, kwamba kuna Tume maalum itaundwa kwa ajili ya kufuatilia matatizo yaliyotokea mpaka vijana wetu wakafeli kwa kiasi kikubwa kile.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia kwa kina matokeo yale somo la Kiingereza wanafunzi wamefaulu na somo la kiswahili vile wanafunzi wamefaulu na kwa asilimia zinafanana. Kama wanakuwa wamefaulu asilimia 60 somo la Kiswahili unakuta na Kiingereza inakaribiana kwa asilimia 55. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba somo la Kiingereza liko chini sana kuliko somo la Kiswahili. Wanafunzi wanajitahidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu mafunzo ya Walimu wanaofundisha somo la Kiingereza, upo mpango mahsusi wa Elimu ya Sekondari awamu ya pili ambako kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya walimu wanaofundisha kiingereza pamoja na kununua vitabu vya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kitabu cha *New Oxford English for Schools* kwa shule za Msingi naomba swali hili nilipokee ili tukirudi Wizarani pale niangalie mwendelezo wa kulifuatilia tumefikia wapi ili kitabu hiki kiweze kutoka na kutumika katika shule za Msingi.

SPIKA: Ahsante tunaendelea. Wanaibuka watu ambao mimi sikuwaona kabla. Kwa hiyo, naendelea na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ni ukweli usiofichika kwamba wenzetu katika nchi za Kenya na Uganda wapo katika nafasi nzuri katika lugha ya Kiingereza kuliko upande wa Tanzania wakati sisi tukiwa na unafuu kwa lugha ya Kiswahili. Chini ya ushirikiano wa Afrika Mashariki, ni kwa nini Serikali isifikirie uwezekano wa kuweka utaratibu maalum na wenzetu hawa, ili tupate walimu wa Kiingereza kutoka Kenya na Uganda wakati sisi tukipeleka walimu wa Kiswahili katika nchi hizo?

WAZIRI WA USHIRIKIANO AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali hili la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya Mkataba wa Jumuiya wa Afrika Mashariki, tumekubaliana kwamba elimu kwa ngazi zote kuanzia chekechea, shule za Msingi hadi Vyuho Vikuu ilingane. Kwa hiyo, hatua moja iliyokwisha chukuliwa ni kuruhusu chini ya mkataba soko la pamoja kuruhusu walimu wote wenye Shahada mbili wafundishe katika nchi yeyote bila kipingamizi chochote na tayari walimu hao kutoka Kenya, Uganda na sehemu mbalimbali wameanza kuingia na tutaendelea kulegeza hilo kadri tunavyoenda ili hatimaye kabla hatujafika mbali sana viwango vya elimu, mitaala na pia ufaulu vilingane. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri, sasa naelekea swali jingine Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mtalaam wa kwanza wa *rap* nchini Tanzania.

Na. 20

Migomo ya Wanafunzi Vyuoni

MHE. JOSEPH O. MBILINYI aliuliza:-

Wanafunzi wa Vyuho karibu vyote nchini wamegoma kwa nyakati tofauti kutokana na kutopatiwa fedha za mikopo. Baadhi yao wamepigwa na kujeruhiwa na askari:-

- (a) Je, kwanini Serikali inaendelea kukumbatia utendaji mbovu na usiokuwa na tija wa Bodi ya Mikopo?
- (b) Je, ni kwa nini kazi ya kutoa mikopo kwa wanafunzi isifanywe na Benki yoyote itakayoteuliwa na Serikali kwani zina uzoefu wa kutoa na kurejesha mikopo tofauti na Bodi?
- (c) Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo itapunguza matumizi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika Vyuho Vikuu na taasisi za Elimu ya Juu, wamekuwa wakigoma kwa sababu mbalimbali zikiwemo, uhaba wa sehemu za malazi, ubovu na upungufu wa miundombinu, upungufu wa wanataaluma wenye sifa stahiki, baadhi ya Vyuho kudahili wanafunzi kwenye *program* ambazo haijaidhinishwa na Tume

ya Vyuo Vikuu(TCU), utendaji usioridhisha wa baadhi ya viongozi katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu na ongezeko la ada lisiloendana na mikopo inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi malalamiko kutoka kwa wadau kuhusu mfumo wa utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu wa Juu unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhaba wa fedha zitolewazo na Serikali ikilinganishwa na idadi ya mahitaji.

Hata hivyo ili kujiridhisha na utendaji wa Bodi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameunda Tume maalum ambayo pamoja na mambo mengine itapitia kwa kina mfumo wa uombaji na utoaji wa mikopo na kupendekeza jinsi Bodi ya Mikopo inavyoweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Ni matumaini yangu kwamba mapendekezo ya Tume hii yataboresha utaratibu mzima wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo na hivyo kufanya mfumo wa utoaji wa mikopo kuwa endelevu. Tume hii itamaliza kazi yake tarehe 15 Aprili, 2011.

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi wa Benki yenye uzoefu wa kutoa na kukusanya mikopo, Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inakinzana na Sheria ya Benki Kuu.

Kwa mfano Sheria ya Benki Kuu inayoongoza biashara za Mabenki hapa nchini hairuhusu benki yeyote kutoa kiasi cha mkopo kinachotolewa kwa wakati mmoja kwa wateja wa aina hiyo hiyo moja kama walivyo wanafunzi wanaosoma kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu.

Vilevile Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo iliyotungwa na Bunge lako Tukufu inaelekeza kuwa mikopo inayotolewa kwa wanafunzi husika isitozwe riba ya aina yeyote na inarejeshwa kwa kipindi kirefu cha miaka kumi baada ya mwanafunzi kuhitimu masomo yake.

(c)Mheshimiwa Spika, iwapo utoaji wa mikopo utafanywa na benki gharama za uendeshaji zitakuwa zaidi ya asilimia 10 ya kiasi kilichokopeshwa mbali na riba. Kwa sasa gharama za uendeshaji kwa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ni asilimia 3.5 na hakuna riba. Hivyo kutoa mikopo kupitia benki hakutapunguza gharama za uendeshaji.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI:Mheshimiwa Spika asante, kwa niaba ya wanavyuo wa Tanzania nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Waziri amesema kwamba matatizo ya wanafunzi kugoma ni zaidi ya tatizo la mikopo kwamba kuna matatizo ya upungufu wa fedha, malazi, miundombinu mibovu, uhaba wa Walimu na vitu kama hivyo, lakini Rais ameunda Tume ya kushughulikia tatizo la Mikopo bila kugusa matatizo mengine ambayo Naibu Waziri ameyataja. Je tutarajie migomo zaidi na Askari kuendelea kuwapiga wanavyuo?

(b) Toka programu ya mikopo ianze ni wahitimu wangapi wamesharudisha mikopo yao na ni kiasi gani cha fedha kimesharudishwa mpaka sasa?(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba ile Tume ya Bodi ya Mikopo aliyounda Rais, mbali na mambo mengine itachunguza utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya wanafunzi. Lakini kuna mambo mengine ambayo yanajitokeza Vyu Vikiu ni pamoja na Miundombinu, mambo kama ya maji, mabweni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kukuambia kwamba kuna mpango mahsusi unaitwa MEJU mpango wa maendeleo ya Elimu ya Juu ambapo Serikali kwa mwaka huu itatenga karibuni bilioni 100 kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye mabweni ya wanafunzi katika vyuo vyetu vya elimu ya Juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo siyo Tume ya Rais tu, Waziri Mkuu vile vile ameunda Tume inayotokana na Makatibu Wakuu ambao nao wanafuatilia matatizo ya uongozi wa vyuo na kupandishwa kwa ada bila mfumo mzuri na mambo mengine ya matatizo ya wanafunzi. Kwa hiyo Tume zote mbili watatuletea mfumo mzuri wa wanafunzi wa Vyu Vikiu kuishi kwa amani na bila kuandamana.

Mheshimiwa Spika, vile vile suala la Askari kuwapiga wanafunzi wetu pale wanapokuwa wameandamana, sheria za Wizara ya Mambo ya Ndani pale inapoonekana wanafunzi wameandamana pasipo ridhaa ya Polisi na zile zitaweza kuitwa sasa ni vurugu ni lazima maaskari wafike pale waangalie mfumo wenyewe. lakini ikitokea kama kuna vurugu Jeshi la Polisi haliko tayari kuvumilia wanafunzi wengine wakichapa viboko wenzao na hivyo sasa Serikali inachukua mkondo wake wa Kisheria. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika asante sana. Ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa, kuna wanafunzi ambao wanatoka katika Halmashauri kadhaa na wanasoma Vyu Vikiu wakiwemo Madaktari pale IMTU na wanakosa mkopo kutoka Bodi ya Mikopo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuziagiza hizo Halmashauri ziwali pie hawa wanafunzi Madaktari ili kuweza kupunguzia mzigo Bodi na pia kwa sababu hizo Halmashauri zinawahitaji hawa Madaktari kwa kiwango kikubwa sana.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa sera ya sasa hivi wanafunzi wote ambao wanasomea mafunzo ya Sayansi wakiwemo wale wanaosomea Udaktari katika Vyu mbalimbali, Vyu vya Serikali na Vyu visivyokuwa vya Serikali kwamba hawa wote watapewa mikopo asilimia mia moja na Serikali na Bodi ya Mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina taarifa na wanafunzi ambao wamekosa mikopo, kama wapo naomba taarifa hizo zifikishwe lakini hili ambalo Mheshimiwa Mluki amelipendekeza nalo tutaliangalia wakati tunapokea mapendekezo kutoka Tume ya Rais ambayo tunategemea mwezi huu tutapokea mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Swali hili limetumia dakika 10 kwa hiyo, naendelea na Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 21

Ununuzi wa Mafuta ya Mitambo ya IPTL

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Serikali imekuwa ikinunua mafuta kuendesha mitambo ya IPTL ili kupunguza mgao wa umeme nchini:-

- (a) Je, ni mafuta kiasi gani hununuliwa kila mwezi na kwa gharama ya shilingi ngapi?
- (b) Je, Serikali hununua mafuta haya kwa kampuni gani na utaratibu gani uliotumika kumpata mzabuni kwa mujibu wa sheria ya manunuzi?
- (c) Je, fedha za kununua mafuta hayo ziko katika bajeti gani; na Je, bajeti hiyo ilipitishwa na Bunge?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kiasi cha shilingi bilioni 46.4 au wastani wa shilingi bilioni 15.62 kwa kila mwezi zilihatajika kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa tani 36,800 za mafuta mazito kwa kipindi cha miezi mitatu, kuanzia 15 Novemba, 2010 hadi 14 Februari, 2011 sawa na tani 400 kwa siku.

(b) Kampuni mbili za *Oryx* na *Total* ndizo pekee zinazofanya biashara ya mafuta mazito nchini na ndizo zilizoombwa kushiriki katika mchakato wa ununuzi wa mafuta hayo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika kupata kampuni za *Oryx* na *Total* ni kwa *restricted tendering* ambapo, kampuni za mafuta zilitakiwa kufikisha mafuta katika maghala ya IPTL mwezi Novemba, 2010. Katika hali ngumu kama hiyo, maamuzi ya Serikali yalihitajika kufanyika haraka ili kupunguza ukali wa mgawo wa umeme kwenye mfumo wa *grid* ya Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha za kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL* zimetoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba shilingi bilioni 15 kwa mwezi ni fedha nyingi sana. Wakati tunapitisha bajeti ya Serikali mwaka 2010/2011 hapakuwa na provision yoyote ya bajeti kwa ajili ya mafuta kwa mitambo hii.

(a) Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge hili ni katika *vote* gani na kama ni ya Wizara yake au Wizara nyingine yoyote ambayo tunapata fedha (mabilioni) haya kwa ajili ya kulipia mafuta haya?

(b) Mheshimiwa Spika, *TANESCO* kila mwezi wanalipa *capacity charge* ya zaidi ya shilingi bilioni 3.6 kwa IPTL na fedha hizi zinawekwa kwenye *ESCO Account*. Sasa hivi *ESCO* imefikia zaidi ya shilingi bilioni 160 na kumekuwa na malalamiko na maombi na hoja mbalimbali za kutaka mitambo hii igeuzwe kuwa *gas* na imilikiwe na Serikali. Lakini mpaka sasa hakuna lolote ambalo limefanyika. Waziri haoni kwamba kuendelea mitambo hii kutumia mafuta kama hivi na bila utaratibu ambao labda mitambo hii imilikiwa na Serikali ni kuwa ni mradi wa watu wachache ambao wanafaidika na mafuta haya? (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya swali la nyongeza ambalo limeulizwa fedha hizi zinazotumika kununulia mafuta haya yanayoendeshea mitambo ya IPTL yanatoka katika *vote* na mafungu yapi nimwombe Mheshimiwa Zitto Kabwe kama anavyofahamu vizuri ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge suala hili ni la takwimu tunayo ofisi inayosimamia mambo yote ya Fedha, chini ya Wizara ya Fedha. Mimi na yeye tukutane baada ya kikao hiki ili tupeane taarifa kupitia Wizara ya Fedha.

Lakini sehemu ya pili kuhusu umuhimu wa kubadili mitambo hii ambayo inayotumia mafuta mazito kwenda kwenye matumizi ya *gas* asili ni kweli kwamba sasa hivi *TANESCO* kwa utaratibu uliopo fedha inayopaswa kulipwa kwa *IPTL* inalipwa kwenye akaunti maalum kama alivyosema Mheshimiwa Zitto kwa usahihi *ESCO Account* kwa sababu sasa hivi kuna mgogoro wa kisheria ambao uko mahakamani. Ni suala la taratibu za kisheria linajulikana ikifika mahali hapo lazima kuwe na utaratibu maalum hadi hapo mgogoro utakapokuwa umekwisha. Lakini kwa nini hatujaweza kufanikisha azma ya Serikali ya kubadili ile mitambo kutoka kwa kutumia mafuta mazito kutumia *gas* asili kilichotucheleweshwa hapa ni huo mgogoro ulioko mahakamani kwa sababu ya mgogoro hatuwezi kuendelea zoezi hilo linahitaji kufanywa baada ya kupatikana hatma ya mambo ambayo yanayobishaniwa mahakamani. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwa ujumla watuvumilie kwa sababu litakapoisha hilo suala

ambalo liko mahakamani azma ya Serikali iko pale pale kubadilisha mitambo ili itumike kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji umeme, lakini pia kupunguzia mzigo wa Serikali. Ahsante.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu wakati wa maswali, ni utaratibu gani huu?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46 (1) Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi Waziri atampa Mbunge mwuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa. Swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Kabwe halijajibiwa kabisa naomba lijibiwe. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu mbona mnachanganya maneno hili swali kwanza Spika, mimi peke yangu ninaruhusu kusema hujajibu kikamilifu. Lakini Mheshimiwa Mbunge yeyote kwa mfano wanasema apewe jibu kwa hilo kwa maandishi ndio unachokisema hapa. Sasa mimi nasema hivi bado tuna nafasi kwa mujibu wa kanuni niliyowaambia ya 50 (1), 28 (1) na ile nyingine kama ulivyosema jana. Kwa hiyo, mimi kwa kanuni hiyo ndio naweza kusema hili jibu lako siyo kamilifu Waziri rudia mimi ndio nina madaraka hayo. Lakini wewe una taratibu nyingine zinazokuruhusu wewe kufanya. Wewe una utaratibu mwingine. Kwa hiyo, tunaendelea. (*Makofi*)

Nilikuita Mheshimiwa Mnyaa lakini siwezi kukuita kwa sababu nimetumia vibaya muda kwa kukujibu. Tunaendelea kwa sababu tumetumia muda zaidi ya ule unaotakiwa.

Na. 22

Kupeleka Umeme Maeneo Mbalimbali Karagwe

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.N.Y. MHE. GOSBERT B. BLANDES)
aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi kupeleka umeme maeneo ya Bugene, Rwabwene, Kamagambo, Nyakagoyegoye na Nyakaiga na tayari Serikali ilishaanza kupeleka nguzo za umeme maeneo ya Rukaka, Ndama, Nyabwegira, Kakilo kuelekea Rwambaizi lakini hadi sasa hakuna chochote kinachoendelea licha ya Serikali kulieleza Bunge kuwa Mkandarasi wa kupeleka umeme maeneo ya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi hadi Ihembe angeanza kazi hiyo mwezi Mei, 2010 lakini hadi sasa hajaanza kazi:-

- (a) Je, ni lini umeme utapelekwa maeneo ya Bugene, Rwabwere, Kamagambo, Nyakagoyegoye hadi Nyakaiga kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme maeneo ya Rukaka, ndama, Nyabwegira, Kakilo hadi Rwambaizi?

(c) Je, ni lini umeme wa Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi hadi Ihemba utakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa William Ngeleja una matatizo na wenzako?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru, lakini sina matatizo nao ni rafiki zangu hawa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Bugene kina umeme na kuna mpango wa kusambaza umeme kwa wananchi wengi zaidi. Kijiji cha Rwabwere kimo kwenye mpango wa kupatiwa umeme mwaka huu wa 2011 chini ya bajeti ya *TANESCO*. Ili vijiji vya Kamagambo, Nyakagoyegoye hadi Nyakaiga viweze kupatiwa umeme kunahitajika kujengwa njia ya umeme msongo wa KV 33 umbali wa kilometa 45 ufungwaji wa transfoma tano kila moja yenye uwezo wa 100 kVA 33/0.4kV na ujenzi wa njia za umeme msongo wa kV na ujenzi wa njia za umeme msongo wa kV 0.4 zenye jumla ya kilometa 24. Mradi huu umeombewa fedha za utekelezaji kutoka kwa wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2011.

(b) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ndama kina umeme na jitihada zinafanyika kusambaza umeme kwa wananchi wengi zaidi. Mradi wa kupeleka umeme kutoka Kakilo hadi Runyaga na Vijiji vya Nyabwegira na Rwambaizi uko kwenye mpango wa kupatiwa umeme kutoka kwenye bajeti ya *TANESCO*. Kiasi cha shilingi milioni 39 zimeshatolewa na *TANESCO* kwa ajili ya kupeleka umeme Runyanga. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwaka huu 2011.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi na Ihembe unaofadhiliwa na wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) tayari umekwishaanza kazi za kufanya utafiti wa njia za umeme. Maandalizi ya kazi za ujenzi yanaendelea na inatarajiwa kazi kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2011.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 33 yenye urefu wa kilomita 26.6 usimikaji wa *transfoma* nane kila moja yenye uwezo wa 100 na ujenzi wa msongo kVA 33/0.4 yenye urefu wa kilomita 16.5 gharama za mradi ni shilingi 884,058,331.60.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa majibu mazuri sana ambayo yamewatia moyo wananchi wa Karagwe kwa vijiji vyote vilivyoainishwa katika swali na Mbunge wa Jimbo husika naamini atakuwa amefarijika sana. Je, atakuwa tayari kuwafariji na wananchi wa Kata ya Mgongo ambayo ni kata mpya ambayo tayari alishawaahidi kupitia swali la Mheshimiwa Killimbah mwaka jana kwamba atawapelekea umeme kupitia mradi wa umeme vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Chilolo hiyo Kata unayosema iko wapi?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunikumbusha. Nimesema kwa kuwa jibu la msingi limejibiwa vizuri sana. Je, atakuwa tayari kuwajibu vizuri na wananchi wa Mgongo Wilaya ya Iramba, tarafa ya Shelui? *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli maombi ya wananchi wa Kata ya Mgongo nafahamu na tumekuwa tukiyafuatilia na naomba kuwapa matumaini kwamba ombi tunalifanyia kazi na hasa kwenye Bajeti zijazo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya karagwe yanafanana kwa kiasi kikubwa sana na matatizo ya Jimbo la Kawe hasa katika Vijiji vya Mabopambe, Mbopo na baadhi ya maeneo ya Kata ya Bunju ambayo yako katika Jimbo la Kawe, katika Jiji la Dar es Salaam lakini hayana umeme.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaliambia Bunge hili Tukufu kwamba kuna mikakati yoyote ya kutatua matatizo ya umeme katika maeneo hayo kwenye Jimbo la Kawe?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ina mikakati ya kupanua huduma mbalimbali na hasa usafirishaji na usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Kwa Dar es Salaam tuna mradi maalum ambao tunafadhaliwa na wafadhili mbalimbali ambao pamoja na kupanua miundombinu ya kusafirisha lakini pia tunaongeza usambazaji kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuzidi kuwasiliana kwa sababu pia amekuwa akifuatilia ofisini kwetu kujua majaliwa ya wananchi wa maeneo mengine ambayo ameyaombea.

Na. 23

Kupotea kwa Vocha za Malipo ya Mbolea na Ruzuku

MHE. MOSES J. MACHALI aliuliza:-

Hivi karibuni vocha za malipo ya mbolea za ruzuku ziliibiwa wakati zikisafirishwa toka Dar es Salaam kwenda Kasulu na kufanya Halmashauri ya Wilaya

kuanza upya mchakato wa vocha mpya, na inasemekana gari iliyokuwa na vocha hizo askari pamoja na *DALDO* walikuwepo:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya uzembe huo?
- (b) Kwa sababu hali hiyo imeilazimu Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kutumia shilingi milioni 44 za vocha nyingine mpya. Je, hayo si matumizi mabaya ya fedha za umma na Serikali inawachukulia hatua gani wale waliohusika.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Serikali ilisikitishwa na taarifa za uzembe uliosababisha upotevu wa vocha hizo za ruzuku ya pembejeo za kilimo zilizokuwa zinapelekwa kwa wakulima wa Wilaya wa Kasulu. Kutokana na hali hiyo, Serikali imewachukulia hatua za kuwafungulia mashataka wahusika wote waliokuwa wamekabidhiwa dhamana ya kuzisafirisha vocha hizo.

Wahusika hao ni Afisa Msimamizi wa Vocha wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Askari Polisi wawili waliokuwa wanalinda msafara huo na Dereva wa gari Namba STK 5704. Aidha, Serikali imemwagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kukagua maeneo yote nchini yanayohusika na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kutumia mfumo wa vocha ili kubaini ubadhirifu uliotokea. Watendaji na mawakala watakaobainika kuhujumu utaratibu wa vocha watachukuliwa hatua kali za kinidhamu na za kisheria kulingana na makosa yao.

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu haijatumia fedha nyingine zozote kwa ajili ya ununuzi wa vocha mpya kwa kuwa baada ya upotevu huo vocha nyingine zilipelekwa Kasulu kufuatia maombi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. Aidha, baada ya kupata taarifa za upotevu huo, Wizara iliwasiliana na Benki ya *NMB* na kuzuia malipo ya vocha hizo kwenye matawi yote ya benki hiyo nchini. Kwa hiyo, hakuna upotevu wowote wa fedha za Serikali kutokana na malipo ya vocha hizo zilizopotea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwamba wahusika katika upotevu wa vocha hizo wamefunguliwa mashitaka mahakamani. Kwa kuwa washitakiwa hao bado wako katika vituo vyao vya kazi na imani yangu kwamba kwa mujibu wa Sheria zinazoongoza Watumishi wa Umma (*Public Service Regulation*) watu hao walipaswa kuwa nje ya vituo vyao vya kazi, lakini wako pale.

Je, Serikali inatamka nini kuhusiana na watu hao kuwa bado wako katika vituo vyao vya kazi?

Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba wamemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ili kusudi kuweza kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini hujuma ambazo zinafanywa katika ugawaji wa mbolea hizi za ruzuku. Lakini tukijaribu kungalia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimekuwa zinatolewa mara kwa mara na hazifanyiwi kazi.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufanya ziara ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kusudi tuweze kushughulikia na kubaini watu mbalimbali ambao wamekuwa wakihujumu zoezi zima la ugawaji wa mbolea kwa wakulima na wakulima wamekuwa wakilalamika sana na baada ya kuwabaini ili kusudi tuweze kuwakamata washughulikiwe kwa mujibu wa sheria? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu sehemu ya pili ya swali la nyongeza na sehemu ya kwanza atanisaidia Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba taarifa nyingi za CAG hazifanyiwi kazi, lakini siyo kweli. Taarifa zinazotoka ni nyingi tunajua mzigo ni mkubwa zinaendelea kufanyiwa kazi lakini hii ya pili aliyosema kwamba ni lini nitafanya ziara katika Wilaya ya Kasulu.

Nakumbuka nimefanya ziara katika Wilaya ya Kigoma na Kasulu sijaenda na tumezungumza na Mheshimiwa Machali kwamba, baada ya Bunge hili mimi nitatafuta muda ili nimalizie kiporo changu katika Mkoa wa Kigoma kwa sababu wilaya ya Kasulu sikufanya ziara na tuliishakubaliana jambo ambalo tutalifuatilia ni hili la vocha, hususani ule urubuni unaotendwa na baadhi ya mawakala kwa kuwapora wakulima. Kwa hiyo, hilo nitalifuatilia na ninakubali mwaliko wake.

Mheshimiwa Spika, naomba sehemu ya kwanza anisaidie Mheshimiwa Hawa Ghasia. (*Makofi*)

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Manispaa ya Tabora ina idadi kubwa ya wakulima wengi, cha kushangaza Halmashauri ya Manispaa yenye wakazi wengi wakulima na ina Kata nane, imepata mbolea ya ruzuku mwisho mwaka 2006.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka ruzuku ya mbolea kwa wakazi wa Manispaa ya Tabora na hatimaye kuwaondolea dhana kwamba kuna baadhi ya maeneo yanatengwa na Serikali?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuwa ameomba msaada kutoka kwa Waziri mwingine na nilikuwa nimeona Waziri wa Utumishi alikuwa amesimama kwa ajili ya kutoa majibu, swali la kwanza halikujibiwa katika maswali yangu ya nyongeza. Kwa hiyo, ningomba kupata majibu.

SPIKA: Uko sahihi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Machali swali lake la nyongeza kuhusu watumishi wa Umma ambao wanapelekwa Mahakamani na bado wanaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma, Mwajiri anaweza akamruhusu mtumishi kuendelea kufanya kazi au akamsimamisha kazi. Anaweza kumsimamisha kazi pale ambapo anahisi kwamba kuwepo kwake kazini kunaweza kukaharibu mwenendo wa kesi iliyoko Mahakami au kunaweza kukaharibu ushahidi wa kesi au uchunguzi kama kuna uchunguzi wowote unaoendelea, lakini kama ana uhakika kwamba kuwepo kwake kazini hakutaathiri suala lolote au hakutaathiri mwenendo wa kesi Mahakamani anaruhusiwa mtumishi kuendelea na kazi. Kwa hiyo, sio kosa mtumishi aliyeko Mahakamani kuendelea na kazi wakati kesi ikiendelea. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Ushirika ujibu swali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuongeza fedha za ruzuku kila mwaka. Kama Mheshimiwa Mbunge atakuwa anafuatilia, tulipoanza mwaka ule wa 2003/2004 tulianza na shilingi bilioni mbili tu, tena kwa Mkoa mine. Hivi sasa tumefikisha zaidi ya shilingi bilioni 148 na tunapeleka kwa Tanzania nzima, hakuna sehemu ambayo tunaitenga isipokuwa tu ni kujipanga katika msimu unaokuja. Maafisa Kilimo katika Manispaa ile ya Tabora, tushirikiane na Wizara kubaini maeneo ambayo tunaweza kuyapelekea ruzuku kwa sababu hatujaweza kumpa kila mkulima ruzuku hiyo, haitawezekana. Kwa hiyo, namuahidi tu kwamba tutashirikiana na Manispaa na wataalamu walioko kule kubaini takwimu ili tuweze kuhakikisha kwamba nao wanapata mgao wanaostahili.

Na. 24

Uanzishwaji wa Mashirika ya Umma Nchini

MHE. LUHAGA J. MPINA aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na kasi kubwa ya uanzishaji wa Mashirika ya Umma, Taasisi, Wakala na Tume ili kuboresha utoaji wa huduma kwa Watanzania wakiwemo wale wa Kisesa:-

- (a) Je, hadi sasa kuna mashirika mangapi?
- (b) Je, ni fedha kiasi gani zilitumika kama ruzuku kwa Mashirika hayo (*Government Subvention*) katika miaka ya 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010?
- (c) Je, ni mashirika mangapi yanayotoa gawio kwa Serikali na gawio hilo kukokotolewa kwa *formula* gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Jimbo la Kisesa, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya uwekezaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010, jumla ya Mashirika, Taasisi, Wakala na Mamlaka za Serikali zinazofanya kazi ni 214. Kati ya Mashirika hayo 174 yanamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 na Mashirika yapatayo 20 ambayo hayafanyi kazi na yapo katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji ama ufilisi. Aidha, Serikali inamiliki mashirika 40 kwa ubia, ambapo kati ya Mashirika hayo Serikali inamiliki zaidi ya asilimia 50 katika mashirika 50 katika mashirika 7 na mengine 33 chini ya asilimia 50.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010 Serikali imetumia jumla ya shilingi trilioni 3.3 kama ruzuku kwa mashirika ya umma.

(c) Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya mapato ya msajili wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 ni Mashirika 14 ambayo yametoa gawio na mawasiliano Serikalini. Hivyo jumla ya shilingi bilioni 26 zilipatikana.

Mheshimiwa Spika, idadi hiyo ya mashirika na kiwango kinachotolewa kama gawio hutofautiana kati ya mwaka na mwaka kulingana na faida inayopatikana, hali ya kifedha ya shirika na mipango ya uwekezaji katika shirika husika.

Mheshimiwa Spika, gawio linalotolewa katika shirika linakotolewa kwa kuangalia kiasi kilichotengwa kwa ajili ya gawio kwa wanahisa na idadi ama asilimia za hisa kwa wanahisa katika shirika husika. Aidha, kwa mashirika ambayo hutoa mawasiliano, hutakiwa kutoa asilimia 10 za mapato ghafi ya shirika. Hii ni kulingana na Waraka Na.8 wa Hazina wa mwaka 2008/2009. Hata hivyo, kiasi cha asilimia kinachotolewa huweza kupungua kutokana na hali ya kifedha na mipango ya uwekezaji wa shirika. Waraka huu unahusu mashirika yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 tu na yanayozalisha mapato yake kwa kujiendesha kibiashara ama kukusanya mapato yanayotokana na ushuru au ada mbalimbali.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa ninalo swali moja la nyongeza. Majibu aliyoyatoa Naibu Waziri hapa, licha ya Serikali kuwekeza fedha nyingi sana katika Taasisi zake, lakini inapata gawio la shilingi bilioni 5.2 tu kwa mwaka katika *average* ya miaka hiyo. Kwa hiyo, fedha hiyo ni kidogo sana na kwamba Serikali imekuwa ikigharimia kuyaendesha Mashirika hayo shilingi bilioni 660 kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mashirika haya yanazidi kuongezeka na kwa sababu Mashirika yenyewe ni mengi, ambayo idadi yake ni 214 na kwamba yanazidi kuongezeka siku hadi siku na kwamba gharama za shilingi bilioni 660 ni fedha nyingi sana ambazo tunazitoa katika kuendesha Mashirika haya na kwamba zinakinzana na jitihada, zinazoofisha jitihada za kukuza uchumi pamoja na kupunguza umasikini: Je, Waziri na Serikali watakubaliana na mimi kuwa umefika wakati muafaka sasa wa kuunda Tume ili ifanye mapitio ya sheria zilizoanzisha mashirika haya kuona kama zinaekwenda na wakati wa sasa, lakini pia zipitie mfumo wa mapato na matumizi ya mashirika haya, gawio linalotolewa Serikalini na uwekezaji unaofanywa na mashirika haya, kwa maana ya kuboresha na kwamba mashirika yasiyoleta tija yafutwe ili kupunguza mzigo wa Serikali usiokuwa wa lazima?

SPIKA: Ahsante. Hiyo ilikuwa hotuba Mheshimiwa Mpina. Mheshimiwa Waziri, jibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba ieleweke na Mbunge aliyeuliza swali kwamba wakati Serikali inaanzisha haya Mashirika au Taasisi au Wakala wa Serikali huwa inakuwa na malengo maalum. Hatuanzishi Mashirika au Taasisi tu bila malengo ambayo yanakusudiwa. Ndiyo hayo ambayo Serikali inatoa ruzuku kwa Mashirika hayo kwa maana ya kuyawezesha ili yatoe huduma au bidhaa bora kwa wananchi wa Tanzania wakiwemo na wananchi wa Kisesa. Sasa suala la kusema kwamba ruzuku ni kubwa, ni kweli kwamba unapotaka kupata huduma nzuri au bidhaa bora ni lazima utumie pesa, unapotaka kupata pesa ni lazima utumie pesa.

Mheshimiwa Spika, suala la kusema labda sheria ipitiwe upya, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kupitia sheria na kubadilisha na itaendelea kufanya hivyo, kwa mfano yale Mashirika au Taasisi ambazo hazitoi gawio Serikalini kwa sababu ya hasara huwa tunafanya utaratibu, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba kuna Mashirika 20 ambayo hayafanyi kazi, mashirika hayo tunayabinafsisha na kuyafilisi.

**Mafao ya Waliokuwa Wafanyakazi wa Hoteli ya
Saba Saba (77) Arusha**

MHE. GODBLESS J. LEMA aliuliza:-

Tarehe 31 Agosti, 2000, waliokuwa wafanyakazi wa Hoteli ya Saba Saba (77) walisitishiwa ajira zao na mpaka leo hawajakamilishiwa mafao yao na wanaishi maisha magumu.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya suala hilo, kwani ni muda mrefu tangu kusitishwa kwa ajira zao?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kuchelewa kuwalipa mafao yao ni kuwagandamiza na kuwaonea ikizingatia kwamba sarafu ya Tanzania inashuka thamani siku hadi siku na madai yao ni tangu mwaka 2000?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu la Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoteli ya Saba Saba au *Seventy Seven Limited* ilishindwa kulipa gharama mbalimbali ikiwemo mishahara ya wafanyakazi kutokana na hali mbaya ya kibiashara. Hivyo, Serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) ilichukua jukumu la kulipa gharama hizo ikiwemo mishahara ya wafanyakazi wote tangu Oktoba, 1999 hadi Agosti, 2000. Jumla ya shilingi milioni 571.2 zilitolewa na Serikali na kulipwa kama fedha za mafao ya wafanyakazi husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi mzuri wa Serikali wa kulipa mafao ya wafanyakazi hao, walijitokeza wafanyakazi 144 ambao hawakuridhika na mafao waliyolipwa na hivyo kuwasilisha malalamiko yao ya mapunjo ya malipo ya kisheria, mikataba ya hiari na kifuta jasho katika zoezi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi hao. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kujadiliwa kwa pamoja baina ya wafanyakazi, Serikali kupitia iliyokuwa *PSRC* na pia *CHC*, yaani *Consolidated Holdings Corporation* ambayo hivi sasa imechukua majukumu ya *PSRC*. Kimsingi, walalamikaji walionekana hawakustahili kulipwa mapunjo kwa kuwa wafanyakazi wote walioachishwa kazi walikwisha lipwa stahili zao kisheria. Aidha, katika kikao cha pamoja kati ya Menejimenti ya Hoteli 77, Tawi la CHODAWU Mkoa na CHODAWU Kanda, kilichofanyika tarehe 18 Januari, 2002, taarifa ya malalamiko ya waliokuwa wafanyakazi wa *Hotel 77 Limited* kuhusu mapunjo ya mafao, ilijadiliwa. Hata hivyo, baada ya uchambuzi uliofanyika, Wajumbe walikubaliana kwamba ni wafanyakazi saba tu walistahili kulipwa jumla ya Sh. 878, 100/= na hivi sasa wamekwishalipwa.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Oktoba, 2002 walalamikaji walijulishwa na Serikali kupitia iliyokuwa *PSRC* kwamba madai yao hayastahili kulipwa kwa kuwa walichostahili kulipwa ni stahili zao za kisheria (*Statutory Terminal Benefits*). Vile vile mnamo Desemba, 2008 *Consolidated Holdings Corporation* iliwaandikia wadai hao na kuwaeleza kwamba kulingana na kumbukumbu zilizopo wameshalipwa stahili zao na endapo hawajaridhika ni vyema wakatimia haki yao ya kisheria kwa kuwasilisha madai yao Mahakamani ili sheria ifuate mkondo wake.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwenye suala la mafao ya wafanyakazi wa Saba Saba kuna mchanganyiko ambao unanishinda kuelewa kwa sababu kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kikao kilikaa Menejimenti pamoja na CHODAWU, lakini ninazo nyaraka za CHODAWU hao hao miaka miwili nyuma wakiandika barua kwenda kwenye ngazi mbalimbali za Serikali kuomba mafao ya watu wa Saba Saba yashughulikiwe ambao mimi idadi ya majina niliyonayo ni zaidi ya 121 na kuendelea ambao walikuja ofisi kwangu mimi wakiwa wameandamana.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kunipa *list* ya majina ya watu waliolipwa haki zao pamoja na vielelezo na mimi nikiwa tayari kumpa majina ya watu wanaodai pamoja na vielelezo wote pamoja na barua ya kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo iliandikwa tu mwezi Juni ikiomba fedha hizi walipwe mara moja? Kwa kufanya hivyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na mimi kunipa vielelezo ili nitakapokwenda Jimboni kwangu niweze kuongea na watu ambao pia wameniletea vielelezo kwamba wanadai fedha hizo.

SPIKA: Huo ndiyo Ubunge wenyewe.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Mimi nadhani ukubaliane tu Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kama anavyosema na yeye inamkanganya na ameomba ushirikiano, mimi niko tayari ila sasa ningeomba yeye aanze na mimi nitafuata. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa anaomba ushirikiano, kwa hiyo, mshirikiane tu. (*Kicheko*)

Na. 26

**Ujenzi wa Barara ya Dodoma - Iringa na
Dodoma - Babati (Arusha)**

MHE. DAVID M. MALOLE aliuliza:-

Je, ujenzi wa barabara ya Dodoma - Iringa na Dodoma - Babati (Arusha) utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Iringa - Dodoma yenye urefu wa kilomita 260 imesainiwa tarehe 13 Januari, 2011. Fedha za ujenzi zinatokana na fedha za mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB* na Shirika la Maendeleo la Japan, *JICA*. Ili kurahisisha utekelezaji, barabara hiyo imegawanywa katika sehemu tatu za Iringa - Migori (km.95.2), Migori- Fufu (km 93.8) na Fufu - Dodoma (km.71). Kazi za ujenzi za barabara hii zilianza rasmi tarehe 15 Machi, 2011 kwa sehemu zote tatu. Aidha, ujenzi wa barabara ya Dodoma - Babati utafanyika kwa awamu na kwa kuanzia, tayari ujenzi wa sehemu ya Dodoma - Mayamaya (km.43.6) na sehemu ya Babati - Bonga (km 19.2) umekwishaanza. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu iliyobaki ya Mayamaya - Bonga.

MHE. DAVID M. MALOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile inaonekana kwamba fedha ya kujenga barabara hizi sasa hazitoshi:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri sasa anaweza kunisaidia niweze kujua kwamba fedha iliyokuwa imepangwa awali kujenga barabara zote hizi ilikuwa ni kiasi gani na inayopungua sasa hivi ni kiasi gani? Je anatarajia kwamba pesa ambayo inapungua itapatikana lini na ujenzi wa barabara hii utakwisha lini?

(b) Swali langu nilikuwa nimeuliza pia kuhusu ujenzi wa barabara ambazo ziko ndani ya mji wa Dodoma ambao mpaka dakika hii bado ujenzi huo haujaanza ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuunganisha pia kujibu maswali hayo?

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri kama hizo *figure* bado, unaweza kupata muda mwingine tu. Lakini naomba ujibu kwa kifupi sana, tuko nyuma ya muda.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge ameingiza suala la kwamba fedha hazitoshi. Mimi sikusema kwenye jibu langu la msingi kwamba fedha hazitoshi. Nataka nimweleweshe tu kwamba nimesema sehemu ya kwanza ambayo ni kati ya barabara ya Dodoma kwenda Babati, Mayamaya kilomita 46.6 itagharimu shilingi bilioni 40.6. Muda wa kukamilisha kazi itakuwa miezi 27, ujenzi ulichelewa kidogo kutokana na ucheleweshaji wa malipo, lakini nataka kusema tatizo hilo limeshatatuliwa na Serikali. Sehemu ya nyingine ya Bonga mpaka Babati kilomita 16.2 itagharimu shilingi bilioni 16.7 na mkandarasi ameshaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, vile vile kipande sasa cha Dodoma kwenda Iringa, tumesema nayo tumeigawa sehemu tatu, Iringa mpaka Migori kilomita 95.2 ni shilingi bilioni 84.2 na sikusema hatuna pesa. Pesa tunaipata kutoka *ADB* na imeshatolewa na kazi imeshaanza na sehemu ile ya Migori mpaka Fufu ni shilingi bilioni 73.6 na vile vile Fufu mpaka Dodoma tumeweka shilingi bilioni 64.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Dodoma Mjini na Kiwanja cha Ndege kwa sababu Wizara yetu sasa haishughulikii viwanja vya ndege, naomba Mheshimiwa Mbunge ajipange vizuri kuuliza suala lingine kuweza kupata ufafanuzi zaidi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge Malole ni Mjumbe wa Bodi yangu ya *CDA*. Namkumbusha tu kwamba tunazo fedha zaidi ya shilingi bilioni 30 zimetengwa na kandarasi zimeshatangazwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Dodoma Mjini. Namkumbusha tu. (*Makofi*)

Na. 27

Ufanisi wa Mkandarasi Tanga

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa mkandarasi anayekarabati barabara ya Muheza – Amani analalamikiwa sana kwa kutotekeleza vyema majukumu yake na kwamba mwaka 2010 hakufanya na kukamilisha kazi yoyote:-

- (a) Je, nini tathmini ya *TANROADS* Mkoa na Taifa juu ya ufanisi wa mkandarasi huyo (*Y.N. Investment*)?
- (b) Je, mbali na barabara ya Muheza – Amani na Muheza Mjini, Mkandarasi huyo amepewa barabara zipi nyingine?
- (c) Je, Mkandarasi huyo amelipwa kiasi gani kwa mkataba wa mwaka 2010/2011, na asilimia ngapi imebaki kwa barabara ya Muheza – Amani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya Muheza – Amani yenye urefu wa kilomita 31.85 ni moja kati ya barabara tatu zilizo katika mradi wa majaribio wa *Performance Basement Maintenance and Management of Lords PBMMR (Package Five* Mkoani Tanga). Barabara nyingine ni Tanga - Pangani yenye kilomita 45.2 na *Bozer Junction* kwenda Muheza kilomita 39.7. Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Januari, 2009 kati ya *TANROADS* na muungano wa makandarasi wawili, *YN Investment* na *Lack of Contractors JV* kwa

gharama ya Sh. 3,590,421,000/= kwa ajili ya kukarabati na kutunza barabara hizo kwa muda wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utendaji kazi wa mkandarasi *YN Investment* na *Lack Contractors* ambao wanatekeleza mradi wa majaribio, si mradi wa kuridhisha. Hadi sasa ukarabati kwa barabara ya Amani -Muheza haujafanyika kama mkataba unavyotaka. Kutokana na hali hiyo, Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkoa wa Tanga wamempa mkandarasi onyo kali ili aongeze kasi ya utekelezaji. Kama mkandarasi hataongeze kasi ya kazi mkataba wake utasitishwa.

(b) Katika barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS*, Mkandarasi *M/S YN Investment* hajapewa kazi nyingine zaidi ya hii ya *PMMR*.

(c) Mpaka sasa mkandarasi wa *YN Investment* na *Lack Contractors JV* wameshalipwa kiasi cha Sh. 1,264,504,561.31. Fedha za kuifanyia ukarabati na matengenezo ya barabara ya Amani - Muheza ni Sh. 916,279,790/= ambapo jumla ya Sh. 114,385,673.61 zimekwishalipwa na hivyo kusalia Sh. 801,903,816.39 ambazo ni sawa na asilimia 87.5 ya fedha ya mradi wa barabara ya Amani - Muheza.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa. Lakini ningepomba nianze kwa kumfahamisha kwamba *YN Investment* hawa wanaoitwa *Lack Contractors* japokuwa yeye anasema ni kampuni mbili. Lakini kampuni hizo zinamilikiwa na mtu mmoja kwa kila kitu na kwa vyovyote vile sio kampuni mbili na naomba alithibitishwe hilo kwa kuangalia taarifa ya Tume ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga ya mwaka 2010 ambayo pia mimi binafsi nilimpatia nakala Mheshimiwa Waziri Mkuu. Baada ya kusema hayo, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza nashukuru sana kwamba Wizara inakiri kwamba ukarabati haukufanyika na fedha nyingi zimelipwa. Onyo limetolewa, lakini mkandarasi huyu ana tabia unapokaribia wakati mvua zinanyesha ndiyo anakwenda katika eneo la kazi. Amefanya hivyo mwaka 2010, mwezi Aprili amekwenda kwenye *site* mvua iliponyesha katikati ya Aprili akaondoka.

Sasa hivi ninavyozungumza yupo kwenye *site* mwezi huu wa Aprili mvua zinaanza baada ya wiki mbili ataondoka na ataendelea kulipwa fedha na ndiyo utaratibu anaoufanya Muheza hata ukienda Kinondoni huko Dar es Salaam mkandarasi huyu pia ameharibu barabara. Je, hii haitoshi kudhihirika kwamba mkandarasi huyu hana uwezo na anadanganya kwamba kampuni hii ni moja lakini ameweka majina mawili?

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Rais aliiweka barabara hii ya kutoka Muheza kwenda Amani katika mpango wa ujenzi katika kiwango cha lami. Kwa kuwa mkandarasi huyu anaendelea kuvuruga barabara hiyo na Amani ndiyo eneo kubwa la uzalishaji wa chai inayotuletea fedha nyingi za kigeni, Mheshimiwa Waziri atatuambia nini kuhusu mkakati wa kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ya kuweka Barabara hii katika kiwango cha lami? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia nitajibu kwa kifupi tu. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mntangi kwa taarifa alizotoa kuhusu huyo mkandarasi. Lakini kwa sababu hili ni suala la kisheria, taarifa hizo na sisi tunazo, *TANROADS* nao wanazo, nataka kumhakikishia kwamba tunazifanyia kazi, hivyo Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato wa kuweza kumwajibisha mkandarasi umeshaanza kwa kumtolea onyo kali na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunamfuatilia kwa karibu sana. Ule ujanja wa kupeleka vifaa wakati fulani atategemea kuna mtu atakuja kumwangualia nafikiri umefika muda wa kuweza kukomeshwa. Tunaomba ushirikiano wako Mheshimiwa Mntangi tuweze kukomesha hii tabia kwa pamoja. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahadi ya Rais ya kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami. Amesema Rais aliahidi kutengeneza lami sijui kipande gani!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba tena nirudie kumwelezea Mheshimiwa Mntangi kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais alizozitoa, tumeshasema zaidi ya mara tano na Mheshimiwa Waziri Magufuli kwamba zote katika kipindi hiki cha miaka mitano tutazitekeleza. Namwomba Mheshimiwa Mntangi tutakapokuja na bajeti yetu keshokutwa hapa, basi atuunge mkono kwa nguvu na kwa hali na mali tuweze kutekeleza ahadi zote za Mheshimiwa Rais ambazo ni sehemu ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Ahsante.

SPIKA: Kama hiyo ndiyo njia ya kuongezewa fedha tu, basi tutaomba wote.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa kutoka wapi? Jamani mtakuwa na taarifa gani wakati tunaendelea na maswali? Naomba tumalize maswali kwanza.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa na taarifa kuhusu majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali la Mheshimiwa Malole,...

SPIKA: Mheshimiwa nani?

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali la Mheshimiwa Malole - Mbunge wa Dodoma Mjini, alitoa taarifa kwamba barabara ya Dodoma kwenda Mayamaya imeanza kujengwa, kitu ambacho sio kweli. Mimi leo usiku nimetoka Kondoa, hiyo barabara haijaanza kujengwa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mfuate utaratibu. Sasa ni kipindi cha Maswali na swali lile limeshapita na nimesema kwamba iwapo majibu ya Waheshimiwa Mawaziri yanakuwa sivyo ilivyo, tunayo kanuni ya 50 (1), tunayo kanuni ya 28 katika hali ya

kawaida unaweza kuja kusema. Sasa hapa sisi tumeshamaliza, mimi naendelea na maswali mengine, tukisema turudi huko sasa hatufanyi kazi inayostahili. Kwa hiyo, tayari tumetumia muda visivyo.

Tunaingia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Mbarouk Mohammed atauliza swali hili.

Na. 28

**Serikali Imejifunza Nini juu ya Migogoro ya
Nchi za Mashariki ya Kati**

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED aliuliza:-

Serikali ya Tanzania pamoja na viongozi wake wanao uelewa mzuri wa kutambua alama za nyakati kwa kuangalia mabadiliko yanayotokea katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo ile ya kuwasahau wananchi maskini na kuwakumbatia matajiri kwa lugha ya kuwa ni uwekezaji:-

Je, Serikali inajifunza nini kwa yale yaliyotokea Tunisia, Jordan, Syria, Misri, Algeria na hivi sasa Libya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA
KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayotokea katika nchi mbalimbali duniani hasa nchi za Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati yametokana na wimbi la maandamano na machafuko yenye lengo la kufanya mapinduzi ya kujenga demokrasia na taasisi zake, utawala bora, haki za binadamu, uhuru wa vyombo vya habari na ushiriki mpana katika uchumi. Inawezekana kabisa, kuwa sababu ya kuwasahau wananchi maskini na kuwakumbatia matajiri inaweza kuwa ya kweli, lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, haiwezi kuwa sababu ya pekee.

Mheshimiwa Spika, nchi za Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini ambazo nyingi zimekuwa zikiongozwa aidha na dola za kifalme au dola za kijeshi hazikuguswa na wimbi la mageuzi makubwa iliyozikumba nchi zilizokuwa zikifuata siasa za kijamaa kati ya mwaka 1989 hadi 1994, kwa sababu nchi za Ulaya Magharibi na Marekani zilichelea kushinikiza mageuzi katika nchi za Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati kwa sababu ya wasiwasi kuwa kuruhusu demokrasia kushamiri katika nchi hizo kungewapa fursa vyama vyenye mirengo ya kigaidi na siasa kali kukamata dola na hivyo kuhatarisha amani ya eneo hilo. Nchi hizo ziliachwa ziendeele na mifumo yao hadi wakati na mazingira yatakaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, ni nadra sana kwa maandamano na mapinduzi ya aina hii kutokea katika nchi ya kidemokrasia. Kamati yetu yenye taasisi huru za kidemokrasia, yenye kuheshimu haki za binadamu, haki za kiraia, uhuru mpana wa vyombo vya habari,

na kuheshimu mipaka ya mihimili mikuu ya dola, yaani Serikali, Bunge na Mahakama, katika nchi za kidemokrasia, maandamano ni haki kwa kila mwananchi lakini huwa ni maandamano ya amani, sio ya uasi wala mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mageuzi haya makubwa kwenye nchi za Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati ni fundisho kuwa tawala za kiimla hazina nafasi katika dunia ya leo ya utandawazi. Kwa mantiki hiyo, Tanzania iko katika njia sahihi. Tunayo kila sababu ya kujipongeza na kutoyumba kutoka katika mkondo huu wa kukuza demokrasia, kulinda haki za binadamu na kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika uchumi wa nchi bila ubaguzi. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, Ahsante. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu kule kuna lugha tunazozungumza kwamba ndaro ni udume, nakubaliana naye.

(a) Kwa kuwa kati ya nchi zilizokuwa na vurugu hizi zimo nchi za AU: Je, AU imechukua hatua gani za dhahiri kukutana na kiongozi wa Libya ili kuepusha vita ambavyo vinapoteza mali na roho za wananchi wengi waliokuwa hawana hatia?

(b) Tanzania imetoa mchango gani wa mazungumzo na kiongozi wa Libya ili tatizo hili limalizike kwa njia ya kidemokrasia kama ilivyofanywa kwa baadhi ya nchi kama vile Kenya, *Ivory Coast*, *Comoro* na kwingineko?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza kabisa AU imeunda kitu kinaitwa *High Level Panel* ya nchi za *South Africa*, Nigeria, Mauritania na Chad ili kuweza kufanya mazungumzo na uongozi wa Libya kulifikisha jambo hili katika hali ya amani. Lakini kwa masikitiko makubwa siku ya tarehe 17 ya mwezi uliopita, *High Level Panel* ilipojaribu kwenda Libya ilikatazwa na wakubwa kwamba isiruke kwenda Libya kwa sababu tayari Ufaransa, Marekani pamoja na Uingereza...

MHE. KABWE Z. ZITTO: Wakubwa akina nani? Na nyie mkakubali!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Naomba nijibu swali Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Usiwasikilize hao, we endelea kujibu tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakubwa wakakataza kwamba Libya ipo kwenye *no fly zone* na kwa hiyo, *High Level Panel* ikashindwa kwenda Libya badala yake, lakini Kamati ya Amani na Usalama, Baraza la Amani na Usalama la AU, yaani *Peace and Security Council* ya Afrika ilikutana mjini Addis Ababa tarehe 19 hadi 21 ikiunganisha na Mawaziri 15 kujadili hali ya Libya. Makubaliano yaliyofikiwa pale ni kama ifuatavyo:-

Kwamba Afrika kwa ujumla wake tunakubaliana na Azimio Na. 1973 ya Baraza la Usalama kwa sababu liko *legally binding*. Lakini pili, hatukukubaliana na namna linavyotekelezwa na hasa nia na madhumuni ya mwisho wake, kwa sababu wakubwa wenyewe niliowasema walipoanza kugawana kundi moja likasema lengo ni kutetea na kutunza maisha ya wananchi wa Libya. Lingine likasema lengo ni kumwondoa kiongozi Muammar Gaddafi. Kwa hiyo, tofauti hiyo ndiyo iliifanya Afrika isite na haikuchukua msimamo. Tunategemea kwamba ombi la Uganda na Tanzania la kuitisha kikao cha dharura cha AU cha viongozi wote litaleta maelezo na msimamo kamili wa Afrika kuhusu kile kinachotokea nchini Libya.

Kuhusu suala la pili, mchango gani Tanzania imeutoa, mchango wa Tanzania unapitia humo humo kwenye AU, hatuna mchango binafsi. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeshawaambia sina muda. Nakwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Na. 29

Upatikanaji wa Hati Miliki za Ardhi za Kimila

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa shughuli za wananchi huwa ni mgumu hasa pale mikopo inapotolewa na Taasisi za Fedha inapohitaji dhamana kama vile hati za nyumba na hati miliki za ardhi za kimila:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuondoa urasimu ili kurahisisha upatikanaji wa hati miliki za ardhi za kimila na kutoa elimu juu ya mchakato mzima wa upatikanaji wa hati hizo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hati miliki ya kimila hutolewa kwa mujibu wa Kifungu cha (3) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Serikali ilianza kutoa hati miliki za kimila kwa majaribio (*Piloting*) tangu mwaka 2003 katika Wilaya za Bariadi, Babati, Manyoni, Namtumbo, Mbozi na Iringa Vijijini. Tokea kuanza kwa utekelezaji wa Sheria hiyo, usajili na utoaji wa hatimiliki za kimila umeonyesha mafanikio makubwa kwani hadi sasa jumla ya hatimiliki za kimila 129,114 zimetolewa katika Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hakuna urasimu katika utoaji wa hati miliki za Kimila, kwani huandaliwa na kusajiliwa na

Serikali za Vijiji. Jambo linaloonekana na wengi kuwa ni kikwazo ni kushindwa kwa vijiji vilivyo vingi kutimiza masharti ya kisheria ili viweze kutoa hati hizo za kimila. Miongoni mwa masharti hayo muhimu ni uanzishwaji wa Masijala na Daftari la Ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua hilo imenuia kuharakisha utoaji wa hati miliki za kimila kuanzia mwaka wa fedha 20011/2012 kupitia programu ya maboresho ya Sekta ya Ardhi unaowezeshwa na mkopo wa Benki ya Dunia. Mpango huo utazisaidia Halmashauri za Wilaya kupata watumishi na vitendea kazi vya kutosha kutekeleza kazi ya upimaji wa mashamba na utoaji wa hati miliki za kimila. Aidha, Wizara yangu imendaa mwongozo unaoainisha mchakato wote wa utoaji wa hati miliki za kimila na utasambazwa hivi karibuni ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza kazi hiyo. Wizara itaendelea kuzisaidia Halmashauri katika utaalumu na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu hati miliki za kimila, Serikali imekuwa ikitoa elimu kupitia maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Nane Nane pamoja na vipeperushi vinavyoelezea utaratibu wa kupata hati miliki za kimila na faida zake, pia vitabu vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 pamoja na kanuni zake kuchapishwa na kutolewa kwa lugha ya kiswahili na kugawiwa kwa wananchi vijijini bure.

Mheshimiwa Spika, hati miliki za kimila zinahakikisha usalama, yaani *security* tosha kwa umiliki wa ardhi na zina hadhi sawa na hati za umiliki wa ardhi zilizotolewa chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na zinamwezesha mwananchi kupata mikopo kwa kutumia kama dhamana katika mabanki mbalimbali. Kwa kuzingatia umuhimu wa hati miliki ya ardhi kwa wananchi wote wanaomiliki ardhi kihalali ni vizuri Halmashauri za Wilaya zikachangia gharama za upimaji na utoaji wa hati Vijijini pamoja na ujenzi wa Masijala. Hivyo, natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya nchini kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa lengo la kujenga Masijala na kuanzisha daftari la ardhi ya kijiji katika maeneo yao.

MHE. AGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la ardhi ni jambo nyeti na limekuwa ni chanzo cha migogoro mbalimbali mijini na vijijini, matokeo yake uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya...

SPIKA: Usisome na uwe *direct*.

MHE. AGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni tatizo na ni chanzo cha migogoro kwa wananchi badala ya kuwa msaada wa kuwasaidia hawa wananchi.

Je, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, itakuwa tayari sasa kutoa maelekezo mazuri zaidi kwa wananchi ili waweze kujua ni kwa namna gani wanaweza kupata huu msaada wa kupimiwa hizi ardhi zao? Kwa sababu, inavyoonekana tatizo ni

kwamba wananchi wengi hawajui sheria. Sasa kutokujua kwao sheria ni kwamba yule mwenye uwezo wa kifedha mara zote ndio amekuwa akipata haki na asiyekuwa na uwezo wa kifedha inakuwa ni tatizo kupata haki yake. Nashukuru.

NAIBU WAZIRI YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia masuala mawili, la kwanza ni suala la Mabaraza ya Ardhi. Wizara inaandaa mpango maalum ambao utaboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba. Hatua mojawapo ni ile ya kutazama maslahi ya Wajumbe wa Mabaraza hayo kwani imekuwa ni moja ya vyanzo vya Mabaraza hayo kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu kwa wananchi kama nilivyoeleza awali ni kwamba tumekuwa tukifanya hivyo kupitia Wiki ya Utumishi wa Umma. Kwa bahati nzuri Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2010 sherehe zake zilifanyika mjini Mwanza karibu na Shinyanga na kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba wananchi wa Shinyanga walipata fursa ya kushiriki maonesho hayo na kwa maana hiyo, kupata maelezo sahihi juu ya taratibu za kupata hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuandaa taratibu zaidi za kuweza kuwahudumia wananchi ikiwa ni pamoja na kutumia Vyombo vya Habari, yaani redio na Magazeti pamoja na TV, kuwaelimisha wananchi kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012. Nashukuru sana.

Na. 30

Mahitaji ya Maji Safi na Salama Sumbawanga, Rukwa

MHE. DESDERIUS J. MIPATA (K.N.Y. MHE. ABIA M. NYABAKARI)
aliuliza:-

Ingawa wananchi wa Mkoa wa Rukwa wana bidii kubwa katika shughuli za uzalishaji katika nyanja zote, lakini jitihada za wananchi hao zinakwamishwa na tatizo kubwa sana la maji safi na salama jambo linalohatarisha afya zao na kurudisha nyuma maendeleo yao na Mkoa kwa ujumla wake:-

Je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za makusudi za kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Sumbawanga, kwani wanapata shida sana kwa kutumia maji ambayo sio salama kabisa kwa afya zao na isitoshe wanatembea umbali wa Kilometa tatu kufuata maji hayo ambayo sio salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sumbawanga ina Halamashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Manispaa. Kwa upande wa mji wa

Sumbawanga kuna uhaba wa maji hasa wakati wa kiangazi kutokana na kukauka kwa vyanzo vya maji vilivyopo katika msitu wa Mbizi. Serikali imetekeleza mpango wa dharura kushughulikia tatizo la maji katika mji huo kwa kutekeleza miradi miwili yenye kuleta matokeo ya haraka, ambayo ni:-

- (i) Uchimbaji wa Visima 13 katika Bonde la Mto Lwiche kwa gharama ya shilingi milioni 393; na
- (ii) Ukarabati wa mabomba ya zamani na ulazaji wa mabomba mapya kutoka kwenye visima hadi mjini kwa gharama ya shilingi bilioni 4.94.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa mabomba maeneo ya mjini umekamilika kwa umbali wa kilometa 46. Usanifu wa mtandao wa mabomba ya kutoa maji kwenye visima hadi mjini umekamilika na kazi zitakazofanyika ni kufunga pampu za umeme katika visima na kulaza bomba la kutoa maji katika visima hadi mjini. Mradi utakapokamilika utaongeza upatikanaji wa maji kutoka 0% hadi 80% ya mahitaji halisi ambayo ni lita milioni tisa kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha ubora wa maji, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Sumbawanga, inaendelea kuboresha mitambo ya kutibu maji iliyoko maeneo ya Majengo na Kizwite.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni asilimia 51.8 ya wananchi wanaopata maji safi na salama. Serikali kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inatekeleza miradi kwa kuvipatia maji Vijiji vya Matai, Kisumba, Mwazyee, Kamawe, Mwimbi, Laela, Kilyamatundu, Nankanga, Ikozi na Mpuu. Sumbawanga ipo katika kundi la Halmashauri ambalo wataalamu washauri wameshakamilisha usanifu wa miradi hiyo na zabuni ya kuchimba visima imeshatangazwa.

Mheshimiwa Spika, tangu programu ianze kati ya mwaka 2007/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imepata jumla ya shilingi bilioni 1.82 kwa ajili ya kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka. Kujenga uwezo wa Halmashauri katika Sekta ya Maji na kulipa gharama za Wahandisi Washauri. Katika kipindi cha mwaka 2010 – 2012, Halmashauri imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.42 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi ya maji.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, kwa vile tatizo la maji lililopo Mjini Sumbawanga linafanana kabisa na tatizo la maji lililopo kwenye mji mdogo wa Chala, mtandao wa mfumo unatoa huduma ya maji Chala, umeparaganyika kutokana na mvua nyingi zinazonyesha kwa kile kinachoitwa *land slide* na kusababisha hali mbaya kabisa ya huduma ya maji na wananchi wanakunywa maji hatarishi kwa afya zao. Je, Waziri yupo tayari kuchukua hatua za dharura kunusuru wananchi hao?

Mheshimiwa Spika, Mji wa Namanyere ambao pia ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi una tatizo kubwa sana la maji ambalo linasababisha akinamama kutoka saa 9.00

usiku kwenda kutafuta maji kipindi cha mwezi Agosti, Septemba na Oktoba. Kwa kuwa Halmashauri ilishabaini chanzo kizuri cha maji kilichoko Kate katika milima ya Zuma chenye kugharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili, ambacho kama kitatengenezwa kitaweza kuhudumia Vijiji vya Isale, Msiriofu, Kate, Chenje, Chonga na Talamila: Je, Waziri yupo tayari kwenda kuona utaratibu uliokwisha kubainishwa na Halmashauri ili kuweza kutoa msaada na kunusuru vijiji hivi pamoja na mji wa Namanyere?

SPIKA: Hilo swali lako, hata kama ulimwulizia kwa niaba, yeye alijiandaa kwa Swali la yule. Kwa hiyo, ukijibiwa kidogo ujue ndio hiyo sababu. Mheshimiwa Naibu Waziri, jaribu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kuhusu dharura iliyotokea katika mji mdogo wa Chala kwamba miundombinu imeharibika, nafikiri ni azma ya Serikali kwamba tutachukua hatua tuweze kuona ni nini kifanyike tuweze kurudisha Miundombinu ili wananchi wa Mji wa Chala waweze kupata maji.

Vilevile katika swali lake la pili kuhusu chanzo cha Kate katika eneo la Mji wa Nkasi ni kwamba maeneo haya yote tumeshamwajiri Mhandishi Mshauri ambaye anafanya tathmini ya kuona ni wapi maji ya kutosha yanaweza kupatikana kwa ajili ya kuyapeleka katika Mji wa Nkasi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu tutajipanga kwenda huko na kuweza kuona. Mapendekezo yake tutayazingatia.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, tumekwenda nje ya muda kabisa. Kwanza kabisa tunao wageni kama mnavyoona katika *Speaker's Gallery*, ni wageni wa kutoka Jumuiya ya Ulaya hapa Tanzania, wakiongozwa na Mheshimiwa Tim Clerk, huyu ndio kiongozi wa *EU*, Tanzania. Pia tunaye Balozzi wa *Netherlands*, Mheshimiwa Koekok na pia yupo Afisa wao ambaye anaongozana nao, ndugu Agnes Hant. (*Makofi*)

Hawa wamekuja kuongea na sisi, watakutana na mimi nadhani na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Usalama, kwa ajili ya mazungumzo tu ya kirafiki. Pia atakutana na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, baadaye. Ratiba nzima imeandaliwa kwa sababu hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini wakati huo huo tumewapeleka wenzetu kushiriki kwenye msiba wa Katibu Mkuu wa *TRAWU*, Marehemu Rwegasira, na mama Magreth Sitta ameongoza ujumbe huo. Pia anakwenda Mheshimiwa Zaynab Kawawa, Mheshimiwa Angela Kairuki na Mheshimiwa Dr. Kamani. Hawa wataondoka kwenda kushiriki kwenye mazishi ya Marehemu Katibu Mkuu wa *TRAWU*.

Pia, ninayo matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 6 April, 2011 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdala Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake Kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa B. Kwa hiyo, Wajumbe wote wanaohusika watambue hilo na watakwenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, twende katika hoja zinazofuata.

MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Utawala wa Mhakama wa Mwaka 2011 (The Judiciary Administration Bill, 2011)

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni
kwa Mara ya Kwanza)*

HOJA ZA KAMATI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama wenyeviti wa Kamati hizi ambazo zinashughulikia mambo ya fedha za Serikali walivyowasilisha taarifa zao Mezani, sasa kwa sababu katika nchi nyingine zote Kamati inayokuwa inatambulika ni ile ya *Public Accounts Committee*, sasa kwetu sisi kwa sababu ya kurahisisha mambo haya ya kuweza kufanya kazi vizuri zaidi, kwa hiyo, tumeweka *Public Accounts Committee* inashughulikia hesabu za Serikali kwa maana ya Wizara.

Halafu Kamati ya Mashirika ya Umma inashughulikia Mahesabu ya Mashirika ya Umma, halafu Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa inashughulikia hesabu za Serikali za Mitaa. Ukweli ingetakiwa iwe moja lakini kazi yake ingekuwa ni kubwa mno na isingeweza. Kwa hiyo, tumezigawa hivyo.

Sasa kwa sababu ukweli ni kwamba tunaiielezea Serikali, basi Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa yake, Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa atawasilisha taarifa yake na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Hesabu za Mashirika ya Umma atawasilisha taarifa yake, halafu tutachangia kwa siku nzima.

Waheshimiwa Wenyeviti hawa, watakuwa wanaangalia maeneo yanayowahusu watakapokuja kutoa ufafanuzi au vinginevyo, watafanya kwa nafasi yao.

Vivyo hivyo kwa Mawaziri wanaohusika, watu wanapochangia wajue kabisa maeneo yao na wajibu kikamilifu. Kwa sababu tukifanya vinginevyo tutajikuta tunarudia maneno yale yale. Kwa hiyo, ninaomba utaratibu huu uzingatiwe na kila anayehusika aweze kutoa maelezo yaliyo sahihi kwa hoja zitakazotolewa kwa Wabunge, ili wananchi waweze kufaidika kwa kadiri inavyostahili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nina shughuli nyingine pale ofisini, nitamwomba Naibu Spika, aje anipokee.

(Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Spika alivyoeleza sasa tuko kwenye hoja za Kamati. Kwa hiyo, moja kwa moja naomba kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Wakati Mwenyekiti anakuja, nikumbushe neno moja tu, kwamba ripoti hizi zinazowasilishwa Bungeni ni ripoti za Kamati, sio ripoti za Kambi ya Upinzani, ni ripoti za Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

TAARIFA YA KAMATI

Kamati ya Hesabu za Seriali (PAC)

MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nataka kuwashukuru wapigakura wa Bariadi kwa kunirudisha tena kwenye jengo hili na mimi ninawaahidi nitajitahidi sana kuwatetea wao pamoja na Taifa langu. Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2008 /2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 114 (15) cha Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoanzia Februari hadi Aprili, 2011. Katika kipindi hicho Kamati ilijadili Hesabu za Serikali za Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Sheria ya Ukaguzi wa Umma (*The Public Audit Act, 2008*) kifungu cha 39 (1) na (2) pia inatoa madaraka kwa Kamati za Bunge na hatimaye kwa Bunge zima kushughulikia masuala ya fedha za Serikali. Naomba kunukuu sehemu ya sheria hiyo kama ifuatavyo:- Lakini kwa kuwa imeandikwa kiingereza nataka wanaonisikiliza tu wajue kwamba sheria inatutaka sisi Kamati tatu tuangalie halafu baadaye tulete katika Bunge lako Tukufu.

“39(1) The Public Accounts Committee, Local Authority Accounts Committee, Parastatal Organisations Committee and any other Parliamentary Sectoral Committee as the case may be, shall discuss the reports of the Controller and Auditor General after they have been tabled in the National Assembly.”

(2) Upon the completion of hearing the Parliamentary Oversight Committees shall prepare and submit to the National Assembly reports which may include comments and recommendations.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha taarifa ya Kamati, naomba kutoa salamu za pongezi kwako kwa umakini wako katika uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge. Ni hakika haikuwa kazi rahisi. Nikuhakikishie kuwa uchaguzi uliufanya katika Kamati, hasa Kamati hii ya Hesabu za Serikali umepelekea Kamati kupata Wajumbe wanaojituma, wepesi wa kuelewa mambo na wenye weledi wa kutosha. Hii imesaidia sana kwa kipindi hiki kifupi kuweza kufanya kazi nzuri sana. Ni matumaini yangu kwamba umahiri wao waliouonesha kuanzia mwanzo utaendelezwa kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu pamoja na Taifa letu. Basi naomba kuwapa heshima inayostahili kuwataja mbele Bunge lako Tukufu.

Wa kwanza ni Mheshimiwa John M. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Ali Keissy Mohamed, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mheshimiwa Thuwayba Idrissa Muhamed, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Stephen Julius Masele na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya (8) ya Kanuni za Bunge, fasili ya 12, majukumu ya Kanuni ya Kamati ya Hesabu za Serikali ni haya yafuatayo:-

- Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yalioainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhiti Mkuu wa Hesabu za Serikali;
- Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali; na
- Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi wa kanuni hii, kila Afisa Mhasibu anapaswa kuja kwenye Kamati ya Bunge na kuhojiwa na kama inavyoeleza sheria, yeye afisa Mhasibu anahusika kibinafsi, kutetea utekelezaji wa bajeti ya fungu lake na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo kama inavyoelezwa katika Kanuni zilizotengenezwa na Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha (*Public Finance Act, No.6 of 2001*) Sehemu ya Pili zikieleza uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*), nanukuu.

“Every Accounting Officer shall be personally and pecuniarily responsible and accountable for the collection and receipt of all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote, and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC).” Kwa hiyo, hali ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilianza kutekeleza majukumu haya mara moja mara tu baada ya kuundwa rasmi. Tunaishukuru Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo mazuri sana ambayo imefanya na Kamati hii imeonyesha tayari weledi wake na imefanya kazi yake vizuri sana baada ya kupata mafunzo mahsusi ya awali kwa Wajumbe wa Kamati zinazosimamia fedha za umma iliyokuwa na lengo la kuwapa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizi, picha halisi ya kazi waliyochaguliwa kuifanya.

Semina ile ilikuwa ya manufaa sana kwa Wajumbe wa Kamati hizi tatu. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Kamati hizi zitatekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa kikanuni bila kuchoka ili kuweza kusaidia kuwepo kwa matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu pia italazimika kutembelea miradi mbalimbali ili kuweza kujua kama kuna tija kwa fedha zote ambazo zimetolewa kwa Wizara mbalimbali. Wazungu wanasema, *value for money*. Utaratibu huu utawezesha Kamati kuangalia siyo tu kiasi kilichotumika katika mradi ama malipo husika, bali tija ipatikanayo na malipo haya. Huu ndio mwelekeo wa kisasa wa ukaguzi ambao hata Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeanza kuutumia. Tumeshuhudia hivi karibuni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa taarifa za ukaguzi wa thamani ambazo zinalenga kupima ufanisi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, inahusu maswali ya ujumla, na swali la kwanza la ujumla tunataka kuzungumzia juu ya maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa, mapato ya nchi yetu yanakusanywa kutoka katika sekta rasmi. Makusanyo haya hukusanywa na Mamlaka ya Mapato Nchini (*TRA*). Pamoja na makusanyo toka *TRA*, vipo vyanzo vingine vya mapato ambavyo kama vikitumika vyema, vinaweza kusaidia kuongeza maduhuli zaidi kwa Serikali na hivyo kupunguza mzigo wa utegemezi. Aidha, Kamati imegundua kwamba mwelekeo katika miaka mitatu, uvukaji wa malengo ya ukusanyaji ya *TRA* yamepungua.

Katika mwaka 2008/2009 Idara ya Forodha haikufikia lengo lake kwa asilimia tisa ambalo ni sawa na shilingi bilioni 168 na Idara ya walipakodi wakubwa haikufikia lengo kwa asilimia 14 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 267, hivyo hivyo mapato ya Idara ya Kodi za Ndani ingawaje imefikia lengo, lakini kwa kiasi kidogo ambayo ni asilimia 1.2. Kamati iliagiza Afisa masuhuli kuhakikisha kwamba makisio yanayotoletwa mbele ya Bunge ni yale ambayo yamezingatia kikamilifu maoteo ya *TRA* kama Taasisi yenye Mamlaka ya kubuni na kukusanya mapato ya Sserikali kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Kamati iliagiza Idara ya Utafiti ya *TRA* iimarishwe ili iweze kubuni vyanzo vingi vya mapato.

Kamati yangu haijaridhishwa na mwenendo wa makusanyo ya maduhuli katika Wizara na Taasisi za Serikali. Zipo Wizara kadhaa ambazo zina vyanzo vizuri vya mapato, lakini makusanyo kutoka katika vyanzo hivyo yamekuwa siyo ya kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali, nyingi zikiwa ni za kimfumo. Mamlaka nyingi zinakusanya mapato ambayo hayaingii ambayo kama yangeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ingeweza ikatunisha huo mfuko, lakini fedha hizo zinabakia katika Taasisi hiyo. Mtindo huu unajonyesha zaidi katika Taasisi za Uthibiti (*Regulatory Authorities*). Kamati imemwagiza Afisa Masuuli afuatilie jambo hili kwa nia ya kutunisha Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati yangu inapitia hesabu za Wizara ya Maliasili na Utalii, iligundua kuwa kuna tatizo kubwa la uwajibikaji hasa katika kufuatilia maduhuli yatokanayo na vyanzo mbalimbali vikiwemo vitalu vya uwindaji na leseni za kuendesha biashara ya utalii. Kwa mfano, fedha nyingi za utalii zinalipwa nje ya nchi na fedha za matumizi madogo ndiyo zinalipwa ndani. Taarifa ya Ukaguzi ilionesha kuwa yapo baadhi ya makampuni ya kitalii ambayo yamekuwa yakifanya kazi bila leseni na hivyo kuikosesha Serikali mapato. Msako uliofanywa na Idara ya Utalii ulibaini makampuni 23 yaliyokuwa yakifanya kazi bila leseni. Kwa kuwa makampuni haya ya utalii hulipa ada ya leseni, kutosajiliwa maana yake ni kukwepa kulipa ada. Mamlaka husika ni lazima zifuatilie mara kwa mara vyanzo vyake vyote vya mapato ili kuhakikisha kuwa mapato yote stahili yanakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengine ambayo Kamati yangu inaishauri Serikali iongeze udhibiti na ufuatiliaji na ili ipate mapato mengi zaidi. Kwa mfano, Sekta ya Uvuvi, Mawasiliano na Mifugo. Aidha, Sekta ya Madini, mapato yaliyokusanywa toka vyanzo mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2008/2009 yalikuwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 13,052,196,275/= chini ya kiwango kilichokusudiwa cha Sh. 65,190,004,000/=.

Kamati inaamini kwamba Wizara hii inao uwezo mkubwa wa kukusanya mapato kwa kiasi kikubwa sana. Kamati pia iligundua kwamba baadhi ya sheria ndogo za Wizara ya Fedha zinaikosesha Serikali kukusanya mapato zaidi. Kwa mfano, GN No. 22 ya tarehe 5 Februari, 1999 ilisamehe makampuni ya madini kulipa ushuru wa mafuta (*fuel levy*) mpaka USD 200,000 kwa mwaka wa kwanza na kikomo hicho kikifikiwa, basi makampuni ya madini yanapaswa kulipa ushuru huo kama sheria ya ushuru wa mafuta inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, GN No. 99 ya tarehe 15 Aprili, 2005 iliyofuta GN No. 22 ilisamehe ushuru wa mafuta (*fuel levy*) kwa kuruhusu makampuni kulipa USD 200,000 mwanzoni na baadaye makampuni hayo hayapaswi kulipa tena. Uamuzi huu uliamuliwa uanzie mwaka 1999 na kuilazimisha *TRA* kurejesha kodi iliyokuwa imekusanya kwa kipindi cha takribani miaka sita (*retrospectively*). Kamati iliagiza Afisa Masuuli kupitia upya GN 99 ya 2005 kwa madhumuni ya kuifuta na kurejesha GN 22 ya 1999. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu katika mwaka wa fedha 2008/2009 ilionesha udhaifu katika makusanyo yake ya maduhuli. Taarifa ya maduhuli ya Wizara hii kwa kipindi kinachoishia Juni 30, 2009 inaonesha kiasi cha Sh. 61,039,560/= kilikusanywa ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa ya Sh. 100,078,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiujumla Kamati yangu imeona udhaifu mkubwa wa kubuni na kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika maeneo mbalimbali, hasa yale ambayo siyo makusanyo yatokanayo na kodi. Upo ulazima wa Serikali kujipanga vilivyo kukabiliana na changamoto hii. Kwa mfano, mapato yatokanayo na mauzo ya hisa (*capital gain tax*) kwa makampuni yaliyomo nchini na yameuzwa nje ya nchi kama vile Bulyang'hulu *Gold mine* ya *Barrick* kuuzwa kwa Kampuni mpya *Barric Africa*, *Zain* kuuzwa kwa *Airtel* na karibuni *Vodacom* kununuliwa na *Vodafone UK*. Lakini hakuna ushahidi wowote ni jinsi gani nchi hii imekokotoa *capital gain tax*. Kwa hiyo, tunahimiza Wizara iangalie uwezekano wa kupata kodi kwa mauzo haya yanayotendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mapungufu mengi sana katika matumizi ya fedha za Serikali. Sehemu kubwa ya mapungufu ambayo Kamati imeyaona yapo katika eneo ambalo linatumia sehemu kubwa ya fedha za bajeti, ni suala la manunuzi. Mafungu karibu yote ambayo Kamati yangu imeyapitia, yamekuwa na hoja zitokanazo na kutofuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kamati iliagiza Sheria ya Manunuzi ifuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa tatizo la utunzaji wa nyaraka nyingi ambazo zaidi zinahusiana na manunuzi, Kamati imefarijika kuwa tatizo hili limekuwa likipungua mwaka hadi mwaka. Hali ambayo inaonyesha maagizo ya Kamati kuhusu jambo hili yameanza kuzingatiwa na baadhi ya Maafisa Masuuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapungufu kadhaa ambayo yapo katika Sheria ya Manunuzi, bado Maafisa Masuuli wangeweza kufanya manunuzi yao kwa kuzingatia sheria hiyo, kwani siyo aina zote za manunuzi ambazo zinaathiriwa na mapungufu yaliyokuwemo katika Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004. Kamati imegundua kuwa Maafisa Masuuli wengi na Watendaji wao ama hawazielewi Sheria hizi za Manunuzi ili kuzifuata kikamilifu au wamekuwa wakifanya manunuzi kinyume na sheria kwa makusudi. Kwa kuwa tunao Muswada wa Sheria unaolenga kurekebisha sheria hii, ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaona umuhimu wa kuwafundisha Maafisa Masuuli na Watendaji wao misingi ya sheria hii na kanuni zake ili kuweza kufanya manunuzi kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala la manunuzi, kumekuwepo na tatizo kubwa la utunzaji wa kumbukumbu za malipo. Kamati yangu imekuwa ikisikitishwa na hoja zinazotokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu za malipo zilizopelekea wakaguzi kuhoji. Cha kushangaza ni kwamba baada ya kuhojiwa, nyaraka hizo hupatikana na hoja hufungwa ikimridhisha mkaguzi. Hii ina maana kwamba, upo uwezekano mkubwa wa wahusika kutengeneza nyaraka ili kuweza kuhalalisha malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imejiridhisha kuwa eneo hili la utunzaji wa kumbukumbu za malipo ni moja ya maeneo yanayosababisha hoja nyingi za kikaguzi ambazo zingeweza kuzuilika. Udhaifu huu unatokana na kuwepo na watumishi wasio na uwezo wa kutunza nyaraka mbalimbali. Kwa sababu hii, moja ya namna ya kurekebisha hali hii ni Serikali kuwaendeleza watumishi kwenye eneo hili la utunzaji wa kumbukumbu. Mafungu yote yaliyofika mbele ya Kamati kuhojiwa kwa hesabu za mwaka 2008/2009 yameonekana na udhaifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa tatizo la utunzaji wa nyaraka za malipo, Kamati yangu imefarijika kuwa tatizo hili limekuwa likipungua mwaka hadi mwaka, hali ambayo inaonesha maagizo ya Kamati kuhusu jambo hili yameanza kuzingatiwa na baadhi ya Maafisa Masuuli. Kauli mbiu ya Kamati ni “*Zuia Hojana usingoje Kujibu hoja.*” (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Kamati imeona lina matatizo sana ni utekelezwaji wa Sheria ya Fedha. Maafisa Masuuli walio wengi hawasimamii ipasavyo utekelezwaji wa sheria ya fedha. Mapungufu makubwa katika utekelezwaji wa sheria hii yameonekana katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Masurufu, sheria ya fedha inaelekeza kuwa masurufu yatatakiwa kurejeshwa ndani ya wiki mbili baada ya shughuli iliyokusudiwa kumalizika. Kinachojitokeza kwa Maafisa wengi wa Serikali wanaochukua masurufu, ni kwamba urejeshwaji wa masurufu haya huwa ni wa kusuasua sana kiasi cha kupitisha muda unaotolewa kisheria na hivyo kuleta hoja za kiukaguzi. Kwa maana nyingine eneo hili limekuwa ni sehemu ya kujikopesha fedha bila riba yeyote. Kamati yangu imekuwa ikikemea suala hili siku zote. Pamoja na kupungua sana kwa ucheleweshwaji wa kurejesha masurufu, bado tatizo lipo na kwa kupitia Bunge lako, Kamati inashauri tena Serikali kuhakikisha kuwa watumishi wote wanaochukua masurufu na kutorejesha kwa wakati, hatua stahili zinachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi tu ya mafungu ambayo bado yamekuwa na hoja hizi wakati wa ukaguzi ni haya yafuatayo:-

- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Sh 251,307,878/=;
- Menejimenti ya Utumishi wa Umma Sh.492,428,684/=;
- Mhasibu Mkuu wa Serikali Sh. 132,836,097.64; na
- Mamlaka ya Mapato Sh.198,972,779.89/=.

Pamoja na kwamba masurufu haya yaliendelea kurejeshwa, msisitizo wa Kamati ni kwamba masurufu hayo ni lazima yarejeshwe ndani ya kipindi kinachotakiwa kisheria, yaani wiki mbili baada ya kumalizika kwa shughuli husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imegundua kwamba kitengo cha kusimamia manunuzi ni dhaifu sana katika Wizara mbalimbali. Kunakuwa na matatizo ya mali kutoaingizwa vitabuni na vitu kama hivyo. Kitu tunachosisitiza, ni lazima pawepo na Maafisa Ugavi na zaidi katika Shule za Sekondari Walimu Wakuu ndiyo wanaonunua. Kamati inaona ni vizuri tukarudi kwenye utaratibu wetu wa zamani wa kuwa na *bursar* kwa kila shule. Sheria ya Manunuzi inaelekeza wazi kuwa lazima kuwepo na Kitengo cha Ugavi ambacho kitashughulikia masuala yote ya manunuzi katika fungu husika. Katika kupitia hesabu za mafungu mbalimbali, Kamati haikuridhika na jinsi masuala ya ununuzi yalivyokuwa yakiendeshwa kwa baadhi ya mafungu, hususan katika eneo la kuweka kumbukumbu za mali zilionunuliwa. Zilitokea hoja nyingi za mali kutoaingizwa vitabuni, mali kutolewa bila kuwekewa kumbukumbu na kadhalika. Kamati yangu ilikemea mambo haya na kuwaagiza Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa masuala haya hayajitokezi tena.

Hata hivyo, suala lililopo hapa ni kwamba mafungu mengi hayana watumishi wenye sifa za kutosha kufanya shughuli za manunuzi hasa katika ofisi za Wizara ama Idara za Serikali zilizopo nje ya Makao Makuu. Kwa mfano, Kamati ilijionea udhaifu mkubwa katika Wizara ya Elimu hususan katika mashule ambapo kimsingi hakuna Afisa Maalum mwenye sifa anayefanya shughuli za manunuzi. Shughuli hizi zimekuwa zikifanywa na aidha Mwalimu Mkuu ama Mwalimu Mkuu na Wahasibu. Kamati ilimwagiza Afisa Masuuli ashirikiane na wataalamu wake kuangalia uwezekano wa kurejesha utaratibu wa zamani wa kuwa na *bursar* kama sio Afisa Ugavi. Kamati inaamini kwa kufanya hivyo, hoja za kikaguzi zitokanazo na utaratibu mbovu wa manunuzi zitapungua sana.

Udhaifu katika manunuzi umeonekana katika mafungu mengi sana na kwa mantiki hiyo tunaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kurekebisha hali hiyo kwani fedha nyingi zaidi katika bajeti ya Serikali huenda katika Sekta ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu pia ilijadili ufanisi wa baadhi ya masuala katika Sekta ya Barabara wakati ikimhoji Afisa Masuuli wa Fungu 98, iliyokuwa Wizara ya Miundombinu. Moja ya eneo ambalo Kamati haikuridhika nalo ni eneo la mizani. Suala kubwa hapa ambalo Kamati inataka kulisisitiza ni kwamba kwanza faini zinazotolewa kwa wanaokiuka Sheria za Barabarani za mwaka 1973 lengo lake kuu ni kutoa adhabu ili wahusika wasirudie makosa husika na pia kulinda usalama wa barabara zetu. Suala la mapato ni yatokanayo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya mizani, kumekuwepo na tabia ya wasafirishaji kupunguzia mizigo iliyozi katika magari mengine madogo kabla ya kufikia mizani na baadaye kuirudishia mara baada ya kuvuka mizani. Suala hili linafahamika wazi ingawa Sheria ya Barabara haijaweka uhibitwa wazi wa suala hili. Kamati yangu inaona ipo haja kwa Serikali kutolifumbia macho suala hili kwa sababu linafahamika. Magari yanayozidisha mizigo yanaharibu barabara zetu, barabara ambazo zimejengwa na mabilioni ya shilingi za walipa kodi. Sheria ya barabara ya mwaka 1973 inabidi ifanyiwe marekebisho ili kwanza kuweka adhabu ambayo itatolewa kwa yeyote atakayebainika kutenda kosa la kuhamisha mizigo kwa utaratibu ulioelezwa na pili

kuongeza tozo kwa makosa mengine ambayo kiwango chake hakiendani na hali ya sasa. Aidha, pamekuwa na udanganyifu wa watumishi juu ya kiasi halisi kinachokusanywa na ucheleweshaji wa magari kwa uzembe ili mtu atoe rushwa. Kamati imeagiza mizani hizi ziangaliwe kwa makini ili barabara ziwe salama na ucheleweshaji wa magari kwa makusudi usiwe kero ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati yangu inashauri kuwa ili kupunguza uharibifu wa barabara zetu, zitumike njia za reli hasa kwa mizigo mizito kama vyuma, saruji, shaba na kadhalika ili barabara zibakie kwa mizigo mwepesi na abiria tu. Hili likitekelezwa, barabara zetu zitadumu kwa muda mrefu. Kamati inahimiza Serikali iongeze juhudi za kuzijenga upya reli na bandari zetu kama njia ya kuweka barabara salama na kupata usafirishaji kwa gharama nafuu itakayosaidia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kumekuwapo na tatizo kubwa sana la kuongezeka kwa madeni katika Wizara na Idara za Serikali. Matokeo ya kaguzi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 yamebainisha uwepo wa madeni mengi sana ya Serikali, yakijumuisha miadi (*commitments and liabilities*) mbalimbali ambayo Serikali huwekeana na wadau wake. Wizara na Idara nyingi za Serikali zimekuwa zikitumia huduma mbalimbali bila kulipa gharama za madeni hayo kwa wakati.

Aidha, kumekuwapo na madai mbalimbali kwa Serikali toka kwa watumishi wake. Kwa mfano, mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara ya Miundombinu ilikuwa na jumla ya madeni (*liabilities*) kiasi cha Sh. 742,920,080.58 na miadi iliyofikia kiasi cha Sh. 178,596,360,000/=. Haya ni madeni ambayo Wizara inakwenda nayo katika mwaka wa fedha unaofuata. Tatizo hili limejitokeza kwa Wizara nyingine nyingi. Wasiwasi wa Kamati katika hili ni kwamba, bajeti za miaka inayofuata haziwi halisi kwa kuwa kiasi cha bajeti kitatumika kulipa madeni, ikizingatiwa kwamba madeni hayo kwa nadra sana hukasimiwa katika bajeti zinazofuata. Jumla ya miadi yote ya mwaka 2008/2009 ambayo haikulipwa ilifikia Sh. 369,744,135,196/=. Hiki ni kiasi kikubwa sana cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo madeni mengine kadhaa katika Wizara na Idara za Serikali kama vile Wizara ya Elimu, Jeshi la Polisi, Magereza na Wizara ya Afya. Kwa ujumla wake, madeni haya na mengine mengi ambayo hayajatajwa kwenye taarifa hii yanatokana na udhaifu wa Maafisa Masuuli katika kufuata utaratibu wa *cash budget*. Tatizo hili husababisha mapungufu pia katika miaka ya fedha inayofuata kwa sababu madeni haya inabidi yalipwe. Suala hili linakwamisha jitihada za maendeleo, kwa kuwa fedha nyingi zinatumiwa kwa kulipia madeni na kwa zile Taasisi zinazoidai Serikali zinaathirika kwa kukosa fedha zinazodai.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limekuwa ni tatizo sana ni ucheleweshwaji wa kutolewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge, hasa fedha za miradi ya maendeleo. Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa utoaji wa fedha za maendeleo kwani umekuwa ukilegalega sana. Pamoja na kwamba fedha za maendeleo zimekuwa zikitolewa pungufu, bado kuja kwake kwa baadhi ya mafungu kumekuwa hakuna tija. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha tunaouzungumzia, Wizara ya Nishati na Madini

ilipokea sehemu ya fedha zake za maendeleo kiasi cha Sh. 7,500,000,000/= tarehe 25 Juni, 2009, siku tano kabla ya mwaka kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ni kubwa na kuna ulazima wa Serikali kulirekebisha mara moja. Mifumo ya upangaji wa bajeti, ukusanyaji mapato na mgawanyo wa mapato ni lazima uangaliwe upya ili kuondoa tatizo hili. Kwa ujumla wake kiasi cha Sh. 322,929,105,130/= hakikutolewa katika matumizi ya kawaida kama ilivyoidhinishwa na Bunge wakati kwa fedha za maendeleo jumla ya Sh. 813,932,845,656/= hakikutolewa. Fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka huu wa fedha ni Sh. 5,275,374,900,000/= kwa matumizi ya kawaida na Sh. 2,429,534,880,498/= kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kuchelewa kutolewa kwa fedha ama kutokutolewa kabisa kwa kiasi kikubwa yanatokana na utegemezi wa kibajeti. Kumekuwa na kusuasua sana katika kutolewa kwa fedha za Wahisani. Umefika wakati sasa kwa Serikali kuanza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi yote muhimu ya maendeleo. Nchi yetu imeshawahi kufanya hivyo kwa baadhi ya miradi kama miradi ya barabara, maji ya Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na ikawa na matokeo mazuri sana. Kitu cha msingi ni kusimamia vyema vyanzo vyetu vya mapato na kuelekeza fedha za ndani kwenye vile vipaumbele muhimu kwa mwaka husika. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza sana tatizo la utegemezi na pia miradi yetu haitakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, Kamati yangu ilijadili na Maafisa Masuuli, hasa wa Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu kuwepo kwa watumishi hewa (*ghost workers*). Kamati bado imeendelea kuisisitiza Serikali kupitia Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa zipo kumbukumbu sahihi za watu wanaostahili kulipwa. Kumekuwepo na malipo kadhaa ya fedha kwa watu ambao wamefariki, wamestaafu ama wamefukuzwa kazi. Kamati inasisitiza kuwa Maafisa Masuuli wa kila Fungu wawe wa kwanza kuhakikisha kuwa kumbukumbu sahihi za watumishi walio chini yao zinawekwa ili kuondokana na tatizo hili.

Ni matumaini ya Kamati kuwa suala hili litarekebishika na kwamba hakutakuwa na hoja za namna hii katika miaka ijayo ya fedha. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali itaanza kutumia mfumo maalum wa kompyuta utakaosaidia kuweka kumbukumbu za watumishi. Kamati inapongeza sana suala hili na kuisisitiza kuwa ni lazima tuondokane na tatizo hili. Pia Kamati ilimwagiza Afisa Masuuli wa Utumishi kuiletea taarifa Kamati kuhusu kiasi halisi kilichopotea kwa kulipa watumishi hewa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijadili Hesabu zilizokaguliwa za baadhi ya mafungu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2009. Katika mwaka huu wa fedha hati za usahihi wa hesabu zilikuwa kama ifuatavyo:

Taasisi		Hati inayoridhisha	Hati yenye Shaka	Hati
isiyoridhisha	Jumla			

	2007/8	2008/9	2007/8	2008/9	2007/8	2008/9	2007/8
2008/9							
Wizara/Idara/Wakala	35	46	11	5	3	1	49
Sekretarieti za Mikoa	14	18	7	2	-	1	52
21							21
Balozi	22	28	8	3	2	1	32
Jumla	71	92	26	10	5	3	102
Asilimia		70	88	26	9		5
100							3
							100

Jedwali 1: Mwenendo wa shahada za usahihi wa Hesabu

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, mwenendo wa shahada za usahihi wa hesabu umekuwa mzuri kwa kuwa hati zinazoridhisha zimeongezeka na kuna kupungua kwa hati nyingine. Haya ni matokeo ya kazi nzuri ya Kamati yako na pia kwa Maafisa Masuuli kufuata maagizo mbalimbali ya Kamati. Aidha, tumewashauri maafisa masuuli wote kwamba wahakikishe kuwa taifa linapata faida ya fedha walizokasimiwa (*Value for Money*). Katika sehemu hii tutaeleza baadhi ya masuala muhimu yaliyojitokeza kwa baadhi ya mafungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili fungu Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Kamati ilishauriana na Afisa Masuuli masuala kadhaa. Fungu hili lilikuwa na matatizo mengi ya kiujumla kama vile ufinyu wa bajeti, kuchelewa kupata fedha zake zilizoidhinishwa, hasa za maendeleo na pia kupata fedha pungufu. Suala kubwa ambalo Kamati yangu imeona ni vyema likafikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kuongezeka kwa kiasi kinachohitajika kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ipo Tume iliyoundwa kutoa mapendekezo juu ya namna bora ya kuendesha mfuko wa mikopo ya wanafunzi, Kamati yangu imeona bado ipo haja ya kuliongelea suala hili. Kwa taarifa ambayo Kamati ilipewa, mahitaji ya fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 takribani jumla ya shilingi bilioni 139 ambayo ni karibu asilimia 29 ya bajeti ya Wizara zilitumika kugharamia mikopo na kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 237 kitatumika mpaka kufikia mwisho wa mwaka. Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ilikuwa shilingi bilioni 486.6.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mzigo wa mikopo, mamlaka husika zimelezimika kukopa katika taasisi mbalimbali, hasa kutoka katika Mashirika ya Hifadhi ya Jamii, suala ambalo pia ni zito kwa sababu ulipaji wa madeni hayo hapo baadaye utakuwa mgumu kwa kuwa deni linaongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2008 Bodi ya Mikopo ilikuwa imekopa jumla ya shilingi 75,000,000,000 kutoka *PSPF*. Kwa mwenendo huu, suala la kukopesha wanafunzi halitakuwa himilivu (*sustainable*), kwa miaka ijayo. Suala hili tunaamini Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma inalifahamu kiundani na inalifanyia kazi. Sisi

kama Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu, tunashauri suala hili lipatiwe ufumbuzi haraka ikiwa ni pamoja na kuanzisha kodi ya elimu (*education levy*) na pia kuweka viwango maalum vya wanaostahili kupata mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia na kuchambua hesabu za Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu Mkuu wa Serikali, Fungu 22 - Deni la Taifa pamoja na Hesabu za Majumuisho ya Kitaifa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliweza kuona changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili kwa kirefu mwenendo mzima wa utoaji wa dhamana za Serikali (*government guarantees*) na mikopo kwa mashirika ya umma na taasisi binafsi. Kimsingi, Kamati yangu haina tatizo na serikali kutoa udhamini, huu ni utaratibu wa kawaida kabisa na unafanyika nchi zote. Msisitizo ambao Kamati yangu inatoa ni kuhusu utaratibu unaotumika kutoa dhamana hizi na hatari iliyopo kwa Serikali kuelemeza na madeni yatokanayo na dhamana zilizoshindikana kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kufikia tarehe 30 Juni, 2009 dhamana za serikali kwa taasisi binafsi na mashirika ya umma zilifikia kiasi cha Sh. 632,035,342,026.84. Kiasi hiki cha dhamana kinahusisha mashirika ya umma, biashara ndogo ndogo na za kati, dhamana ya mikopo kwa ajili ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi na *pia refinancing facilities*, kama ifuatavyo:-

Mashirika ya Umma (*Parastatals*); kiasi cha mkopo ni shilingi 454,093,169,047.12, kiasi kilichodhaminiwa ni shilingi 447,987,521,547.12 ambayo ni sawasawa na 99%. Biashara ndogondogo na kati, yaani *Small and Medium Enterprises* kiasi cha mkopo ni shilingi 4,765,662,000, kiasi kilichodhaminiwa ni shilingi 2,256,784,876 ambayo ni sawa na 47%. Mikopo kwa ajili ya kusafirisha bidhaa nje (*Export Credit Guarantee Fund*), kiasi cha mkopo ni shilingi 229,985,808,980.62, kiasi kilichodhaminiwa ni shilingi 181,725,850,003.72, ambayo ni sawa na 79%. *Refinancing Facilities* kiasi cha mkopo ni shilingi 65,185,600,000, kiasi kilichodhaminiwa ni shilingi 65,185,600,000, ambayo ni sawa na 100%. Jumla ya kiasi cha mkopo ni shilingi 688,909,825,627.74 na jumla ya kiasi kilichodhaminiwa ni shilingi 632,035,342,026.84.

Mheshimiwa Spika, hali ya dhamana za serikali mpaka kufikia Juni 30, 2009 inaonesha kuwa mashirika ya umma yalidhaminiwa kwa asilimia 99, wakati biashara ndogo ndogo na za kati zilidhaminiwa kwa asilimia 47. Kwa upande mwingine, mikopo kwa ajili ya kusafirishia bidhaa nje ilitolewa kwa asilimia 79 na ile ya *refinancing facilities* ilitolewa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo ya Serikali, Misaada na Dhamana ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebisha mwaka 2004, inaelekeza kuwa kiasi cha dhamana kinachotolewa kisizidi asilimia 70 ya kiasi kilichokopwa. Ninaomba kuinukuu kama ifuatavyo:-

“...the extent of the guarantee covered shall not be more than 70% of the amount borrowed...”

Kwa hali hii, ni dhahiri kwamba, Serikali yetu iko kwenye hatari kubwa ya kutumia fedha nyingi sana kulipia mikopo kama wakopaji wakishindwa kulipa. Lazima Serikali ihakikishe kuwa, inatoa dhamana kwa kiasi kinachohimilika na pia kwa kufuata taratibu na sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii haipingani na dhana ya kutoa dhamana, bali Kamati inasisitiza kuwa ni lazima Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 ifuatwe katika utoaji wa dhamana hizi. Hivi sasa tayari Serikali imeshaanza kubeba mzigo wa kulipa madeni ya mikopo iliyoidhamini ambayo imeshindikana kulipika kama lile la Kampuni ya Kusambaza Mbolea la TFC la thamani ya shilingi bilioni 4.5.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoripotiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali mwaka jana, suala la ulipaji wa madeni ya nchi yetu limekuwa likifanyika katika mamlaka tofauti tofauti. Ilipendekezwa kuwepo na taasisi moja ambayo itashughulikia madeni yote ya Taifa na pia pawepo na *database* moja ili kuweza kuwa na kumbukumbu sahihi ya madeni yaliyolipwa, yanayoendelea kulipwa na yale yasiyolipwa. Kwa kufanya hivi, hakutojirudia kasoro za deni moja kulipwa na mamlaka mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ina furaha kukuarifu kwamba, mchakato wa kuanzisha *database* moja (*Single Unified Debt Database- Sudd*) tayari umeanza na kwamba, Kamati imetoa agizo kwamba, *database* hiyo ianze kutumika kuanzia mwaka wa fedha ujao. Mchakato wa kuwa na ofisi moja inayoshughulikia madeni bado haujaanza na Kamati imeagiza jambo hili lishughulikiwe mara moja.

Mpaka sasa usimamizi wa Deni la Taifa unafanywa na Idara na Taasisi tofauti ambazo zinafanya kazi tofauti. Idara hizi ni pamoja na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Sera, Idara ya Kushughulikia Masuala ya Fedha za Nje (*External Finance*), Msajili wa Hazina, Idara ya Bajeti na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2008/09, Deni la Taifa limeongezeka kwa kiasi cha shilingi 1,143,834,887,616, sawa na asilimia 17.66 ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika mwaka 2007/08. Deni la Taifa kwa mwaka 2007/08 lilifikia kiasi cha shilingi 6,477,451,842,417.72 baada ya nchi yetu kusamehewa madeni. Mgawanyo wa deni hilo ni kama inavyoonekana hapa chini:-

Mwaka wa Fedha 2007/2008 deni la ndani lilikuwa shilingi 1,875,794,357,188.34, deni la nje ni shilingi 4,601,657,485,229.38, jumla ikawa ni shilingi 6,477,451,842,417.72. Mwaka wa Fedha 2008/2009 deni la ndani lilikuwa ni shilingi 2,234,640,367,491.17 deni la nje lilikuwa ni shilingi 5,386,646,362,542.62 jumla ikawa ni shilingi 7,621,286,730,033.80. *Increase* ya deni la ndani shilingi 358,846,010,302.80, *increase* ya deni la nje shilingi 784,988,877,313.24, ambayo ni jumla ya shilingi 1,143,834,887,616.08. *Percentage increase* ya deni la ndani 19.14%, *percentage increase* ya deni la nje 17.59%, jumla yake ni 17.66%.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa na Uongozi wa Hazina kuwa, pamoja na kuongezeka kwa Deni la Taifa, Serikali bado iko ndani ya kiwango kilichokubalika cha kukopa (*sustainable level*) cha 38.4% ya Pato la Taifa. Hata hivyo, ilibainika kuwa mchanganuo unaoonesha kiwango cha kumudu deni (*Debt Sustainability Analysis*) hakijumuishi dhamana za serikali (*Government Guarantees*), kwa mashirika na taasisi binafsi, suala ambalo limeonekana ni mzigo mkubwa kwa Serikali kwa vile mashirika mengi ya umma na taasisi binafsi yameshindwa kulipia madeni yaliyokopa na hivyo kuilazimu Serikali kulipia mikopo hiyo kwa niaba ya taasisi na mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Fungu 21: Katika Mwaka wa Fedha tulioujadili, Mamlaka ya Mapato nchini ilikusanya jumla ya shilingi 4,207,419,367,476 pamoja na Vocha za Hazina (*Treasury Vouchers*) shilingi 33,048,262,217. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 90.59 ya kiasi kilichopangwa kukusanywa cha shilingi 4,644,526,800,000, ikijumuisha Vocha za Hazina shilingi 43,676,900,000. Ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, kiasi hiki cha makusanyo kiliongezeka kwa asilimia 17.95, sawa na shilingi 632,183,178,648. Hii ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, Mamlaka ya Mapato ilikusanya pungufu ya kiasi ilichokusudia kukusanya kutokana na sababu mbalimbali. Kamati yangu ilijadiliana na Afisa Masuuli na Uongozi wa Mamlaka, juu ya mikakati ya kuongeza mapato nchini, mojawapo ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa kodi (*Tax Base*), kwa kubuni maeneo mengine ambamo kodi yaweza kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaamini bado tunaweza kukusanya zaidi ya tunavyokusanya sasa kama tukijipanga vizuri. Hii ni changamoto kwa Taifa letu. Bado hatujaweza kuitumia vema Sekta Isiyo Rasmi kupata makusanyo na hata kutoka Sekta Rasmi bado ukwepaji wa kodi ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini bado TRA inao uwezo wa kukusanya zaidi ya inachokusanya sasa. Hili litafanikiwa endapo tu vyanzo zaidi vya kodi (*Tax Base*) vitabuniwa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa, wote wanaostahili kulipa kodi, wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la malimbikizo ya kodi zinazodaiwa na TRA toka kwa walipa kodi mbalimbali ambazo hazijalipwa. Sababu za mlundikano wa kodi hizi ziko nyingi, lakini moja ya sababu inayojitokeza sana ni ile ya pingamizi zinazowekwa na walipa kodi mbalimbali. Zipo kesi nyingi mahakamani za madai ya kodi ambazo bado hatujajua hatma yake. Kama TRA ikishindwa kesi hizi, basi Serikali itakosa fedha nyingi sana. Mpaka wakati kamati yangu inapitia hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, jumla ya shilingi 395,043,688,157.96 pamoja na Dola za Kimarekani 47,954,784 zilikuwa hazijalipwa kwa TRA toka kwa wadaiwa. Fedha hizi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kuwa kesi nyingi zinazofunguliwa dhidi ya Serikali ama zile zinazofunguliwa na Serikali dhidi ya mtu ama kampuni binafsi, mara nyingi Serikali imekuwa ikishindwa. Suala hili linaipa wasiwasi Kamati kwamba, endapo

TRA itashindwa katika kesi zilizofunguliwa ama ilizofungua, nchi itapoteza fedha nyingi sana. Kamati inashauri kwamba, Mamlaka ya Mapato itumie makampuni binafsi ya kisheria (*Outsource Legal Services*) ili kuwaongezea nguvu Wanasheria wa TRA na kuweza kukabiliana na kesi hizi kwa mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi wa bajeti yetu, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, fedha zote zinazohitajika kukusanywa kisheria, zinakusanywa. Aidha, hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa watu binafsi, taasisi na makampuni yanayokwepa kulipa kodi kwa makusudi ili kujinufaisha. Suala la misamaha ya kodi halijashugulikiwa vya kutosha na Serikali. Kiwango cha misamaha ya kodi kisiathiri mapato yanayoweza kutumika katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Hesabu zilizokaguliwa za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea, Kamati yangu imebaini upungufu kadhaa katika baadhi ya mafungu, mafanikio katika mafungu mengine na changamoto kwa mafungu mengi. Kama nilivyoeleza katika sehemu zilizotangulia, bado Serikali ina changamoto kubwa katika kuhakikisha kuwa, fedha za umma zinatumiwa vema, kwa matumizi yaliyokusudiwa lakini pia kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Kamati yangu ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Serikali kupitia Wizara ya Fedha iongeze juhudi katika kusimamia dhamana inazotoa kwa taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada inazingatiwa kabla na baada ya kutoa dhamana na kwamba taasisi hizo zilizowekewa dhamana (za Serikali na zile binafsi), zinalipa mikopo hiyo iliyodhaminiwa kama ilivyopangwa na wale wasiolipa wadaiwe kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Sheria ya Mikopo, Dhamana za Serikali na Misaada (kama ilivyorejewa 2004), ifuatwe ipasavyo katika mchakato mzima wa kukopa ili kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linakua katika kiwango ambacho serikali itaweza kumudu kulipa bila kuathiri huduma muhimu za jamii.

Kamati inashauri pawepo na mawasiliano mazuri kati ya taasisi na idara zote zinazoshughulika na usimamizi wa Deni la Taifa. Kamati inashauri pia kuwepo na taasisi moja inayoshughulikia usimamizi wa Deni la Taifa, kama inavyofanyika katika nchi nyingine kama Mexico na kadhalika. Aidha, taratibu za kukamilisha mfumo wa kumbukumbu za mikopo (*Single Unified Debt Database*), unakamilika kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Serikali ihakikishe kuwa, panakuwepo mkataba wa kiutendaji kati ya Hazina na Benki Kuu, ambao utaainisha majukumu kati ya Hazina na Benki Kuu. Mkataba huo pia ni vema ukaweka wazi uhusiano wa kiuwakala kati ya Hazina na Benki Kuu ili kuifanya Benki Kuu iendelee na majukumu yake ya kuishauri Selikali na kuiacha Hazina kuchukua maamuzi ya kusimamia Deni la Taifa kwa uhuru zaidi.

Ili kudumisha maadili ya kiutendaji (*credibility*) ya pande hizi mbili, ni muhimu usimamizi wa Deni la Taifa ukawa nje ya Benki Kuu; vinginevyo, Benki Kuu na Hazina waandae mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa shughuli za usimamizi wa Deni la

Taifa ikiwa ni pamoja na kuendesha minada ya dhamana za Serikali unafanyika kwa umakini zaidi bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizi mbili.

Kamati inashauri kuwa, kasma zote muhimu za maendeleo zitengewe fedha za ndani ama zile za nje zenye uhakika, kutokana na uzoefu kuwa fedha zinazoahidiwa hazipatikani kwa muda muafaka katika mwaka husika wa fedha na wakati mwingine kutotolewa kikamilifu. Aidha, Kamati pia inashauri Serikali kutoingiza katika mahesabu ya bajeti zile ahadi ambazo hazijathibitishwa ili kuepuka kuwapa wananchi matumaini yasiyotekelezeka.

Maafisa Masuuli wote wahakikishe kuwa, wanafuata Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya Mwaka 2004 katika shughuli zao. Aidha, kwa kuwa tunao Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi, Kamati inapendekeza kuwa, Maafisa Masuuli na Maafisa Manunuzi wapewe mafunzo kuhusu Sheria hiyo na kanuni zake pindi itakapokamilika.

Serikali iweke mfumo wa kudhibiti masurufu katika mtandao wake wa malipo ili kuhakikisha yafuatayo; hakuna uwezekano wa kutoa masurufu kwa mtumishi ambaye hajarejesha masurufu ya awali; kunakuwepo na kumbukumbu sahihi za masurufu.

Kuhusu watumishi hewa (*Ghost Workers*), Serikali ihakikishe kuwa, maafisa waajiri wote wanaweka kumbukumbu za watumishi wao kwa usahihi na kutoa taarifa pale yanapotokea mabadiliko yoyote ili kuepuka watumishi hewa. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa waajiri ambao wataendelea kuwa na watumishi hewa. Aidha, Mradi wa kuweka kumbukumbu za watumishi kwa njia ya kompyuta ukamilike mara moja ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Serikali ifanye jitihada za kukusanya maduhuli katika maeneo yote yaliyo vyanzo vya mapato. Aidha, Serikali sasa itumie fursa katika Sekta ya Mifugo kupata maduhuli kutoka katika minada ya ng'ombe kwa utaratibu wa kupima uzito ili kujipatia maduhuli sahihi na Sekta nyingine kama uvuvi, Utalii, Mawasiliano na Madini.

Kamati inapendekeza kuwa, Serikali ipunguze vipaumbele vyake ili viwe vichache ambavyo vinaweza kutimizwa kikamilifu katika mwaka husika. Serikali ipunguze misamaha ya kodi. Aidha, hatua ya Serikali iliyochukuliwa mwaka 2005 kwa Tangazo la Serikali Namba 99 la Mwaka 2005, limeikosha Serikali mapato makubwa yatokanayo na ushuru wa mafuta kwa migodi. Kamati inapendekeza kuwa, Tangazo la Serikali Namba 22 la Mwaka 1999 litumike badala ya lile la Mwaka 2005. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, utoaji wa Matangazo ya Serikali ambayo utekelezaji wake huanzia miaka ya nyuma (*Retrospective Effect*) na kulazimu ulipwaji wa kodi zaidi ya zile zilizokusanywa ama kubatilisha zile zile zilizokusanywa, uachwe mara moja kwa kuwa hukwamisha juhudi za makusanyo yenye tija.

Kamati iligundua kwamba, kuna wizi wa kutumia mtandao kama ule uliotokea kwa TTCL ambapo takriban shilingi bilioni tano zililipwa lakini ziliyeyuka kwenye mtandao na jambo hili liko mahakamani. Kufuatana na shauli hili, Kamati inaishauri

Serikali iimarisha makusanyo ya mapato kutoka kwa mabanki yanayopokea fedha za TRA ili fedha zisikae kwa muda mrefu katika mabanki haya kabla hazijapeleka Benki Kuu. Jambo hili litazuia mabanki kuzifanyia biashara fedha za Serikali bila kuzilipia riba. Utaratibu wa sasa unaruhusu mabanki kupeleka Benki Kuu fedha za makusanyo ya kodi mara tatu kwa wiki na kwa kuwa fedha hizi ni nyingi ni rahisi kuzikopesha (*Overnight Credit*) na kutoa majaribu kwa watu kuziiba kwa kutumia mtandao.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Wizara na Idara za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naomba kukupongeza wewe binafsi kuwa Spika na Mheshimiwa Job Ndugai kuwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwenu kuliongoza Bunge. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza kazi nzito na muhimu tulizowakabidhi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoihusu Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza kazi zake ilikuwa ikisaidiwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Kamishna wa Bajeti. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati hii, Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuijadili na hatimaye lipitisha mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo. Tunakushukuru sana. Taarifa aliyokuwa anaiwasilisha ni ya Kamati ya Hesabu za Serikali ambayo yeye ni Mwenyekiti wake. Tunaendelea na Kamati ya pili kuwasilisha Taarifa yake na ninaomba kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Augustino Mrema.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA (MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, ninaomba kuwasilisha Taarifa

ya Mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Taarifa hii inatokana na shughuli za Kamati katika kushughulikia matokeo ya Ukaguzi uliofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 120 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, juu ya Muundo wa Taarifa za Kamati, Taarifa hii itakuwa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya Kwanza ni hii ya utangulizi ambapo unafanyika utambulisho wa Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati na kuelezea majukumu ya Kamati na namna yalivyotekelezwa.

Katika Sehemu ya Pili, Taarifa hii inatoa uchambuzi wa Kamati juu ya Fedha za Umma zilizotengwa kwa ajili ya Serikali za Mitaa katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, hali halisi ya Matumizi ya Fedha katika Serikali za Mitaa na matatizo sugu yaliyobainika katika matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati katika kupunguza matatizo sugu yaliyobainika katika matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa, mafanikio na Changamoto zilizopo katika utekelezaji wa Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, mwelekeo na Mipango ya Kamati kwa siku zijazo. Kipengele cha mwisho kabisa cha Sehemu ya Tatu kinahusu hitimisho na kinatoa ombi kwa Bunge kwamba liipokee, lijadili na kuiunga mkono Taarifa hii kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ambayo sasa inawasilisha taarifa hii ina wajumbe 15 wafuatao: Mheshimiwa Dkt. Augustino L. Mrema - Mwenyekiti, Mheshimiwa Idd M. Azzan - Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Rashid Ali, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Kafulila David Zacharia, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga na Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita.

Mheshimiwa Spika, utafiti, ushauri, uratibu na mawasiliano yaliyohusu shughuli za Kamati hii vilitekelezwa kwa wakati na ustadi mkubwa na Katibu wa Kamati hii Ndugu Bisile Dickson.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 chini ya Kanuni ya 115, kifungu cha 12 katika Fasili Ndogo (a) hadi (c). Majukumu haya yanahusu kushughulikia Taarifa ya Ukaguzi ya kila Mwaka juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati kwa kipindi kilichopita. Majukumu haya yalitekelezwa kwa namna kuu mbili; yaani kufanya ziara za ukaguzi wa ufanisi, yaani *Expenditure Tracking Site Visits* katika Halmashauri

nne za Mkoa wa Kilimanjaro na kuhoji kwa kukaa mezani taarifa za mapato na matumizi ya Halmashauri ishirini na moja.

Katika kipindi cha kuanzia tarehe 6 – 11 Machi, 2011, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri za Wilaya ya Same, Mwanga, Rombo na Moshi Mkoani Kilimanjaro. Lengo la ziara lilikuwa ni kujiridhisha na thamani ya matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa Miradi. Kwenye Miradi ya Maji, Kamati ilipenda kuona maji yanapatikana kwa wanajamii waliolengwa na miradi hiyo. Kwenye Miradi ya Barabara Kamati ilipenda kuona barabara zina ubora unaostahili na zinapitika. Kadhalika, kwenye vyumba vya madarasa, Kamati ilitaka kuona viwango vya Miradi hiyo vinashabihiana na thamani ya fedha zilizoелеkezwa kwa ajili hiyo. Hata hivyo, ni katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga tu ambapo Kamati iliweza kukagua Miradi. Katika Halmashauri tatu zilizobaki, zoezi hili halikutekelezwa kutokana na kukosekana kwa usahihi wa Taarifa za Mapato na Matumizi ya Halmashauri hizo. Kamati inatoa wito kwa watendaji wetu katika Halmashauri kuwajibika kusimamia utekelezaji wa Miradi hii kwa ufanisi na kwa wakati. Kamati inatoa wito kwa Madiwani katika Halmashauri husika kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Miradi hii kwa namna yenye kuleta tija kwa Wananchi waliowachagua.

Mheshimiwa Spika, kati ya masuala yaliyobainika na kuchukuliwa hatua kali na Kamati ni haya: Kutokuwa sahihi kwa taarifa za mapato na matumizi ya baadhi ya Halmashauri; kukosekana kwa usimamizi wa dhati wa kiutawala kwa baadhi ya Maafisa Masuuli; kukosekana kwa uwajibikaji wa pamoja kwa Wakuu wa Idara katika baadhi ya Halmashauri; bei za kughushi katika manunuzi ya vipuri na mafuta ya magari katika baadhi ya Halmashauri kwa baadhi ya miradi ya maendeleo; matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya posho kuliko utekelezaji halisi wa Miradi (TASAF, UKIMWI, Miradi ya Kilimo (*DADPs*), *Capital Development Grant (CDG)*); Miradi ya Maboresho na Miradi ya Uhifadhi wa Mazingira; uwezo mdogo wa Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani; na udhaifu mkubwa katika mifumo ya udhibiti na ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo dosari hizi zilionekana kuzidi na kubainika kuwa za makusudi, Kamati ililazimika kutumia mbinu za haraka kudhibiti angalau kwa kiasi mwendelezo na athari zake. Baadhi ya mbinu hizo ilikuwa ni pamoja na kupendekeza kwa mamlaka husika za nidhamu, adhabu ya tozo na makaripio ya maandishi dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, Sehamu ya Pili - Uchambuzi wa Ruzuku ya Serikali Katika Serikali za Mitaa Kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, jumla ya Halmashauri 133 zilifanyiwa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa pamoja Halmashauri hizo zilikuwa na jumla ya Sh. 1,526,000,059,515. Kati ya fedha hizo, Sh. 107,628,203,817 zilikuwa ni mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini wakati Sh. 1,418,371,855,698 zilitolewa kama ruzuku na Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi katika Serikali za Mitaa. Kiasi cha Sh. 1,014,297,041,910 cha ruzuku ya Serikali (71.6% ya jumla ya ruzuku), zilitengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kiutawala (*Recurrent*) wakati Sh.

404,074,813,788 (28.4% ya ruzuku) zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo (*Development*).

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu, ni dhahiri kwamba, utekelezaji wa shughuli za maendeleo hutengewa fedha kidogo kuliko shughuli za utawala. Mpangilio kama huu siyo mwafaka kwa maendeleo ya Taifa. Kwa maneno mengine, *recurrent budget* ni mara 2.5 ya *development budget*. Kiasi cha uwekezaji katika Miradi ya Maendeleo ni kidogo mara 2.5 ya kiasi cha fedha kinachotumika kwa ajili ya mishahara na shughuli za utawala. Katika hali kama hiyo, yaweza kuwa vigumu kuona Miradi ya Maendeleo ikitekelezwa kwa wakati kila mahali inapotakiwa. Serikali Kuu ni vema ikauangalia upya utaratibu huu ili shughuli za maendeleo ziwe zinatengewa kiasi cha fedha chenye kuweza kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, mikakati na jitihada za dhati zinahitajika katika kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Bado yapo matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri mbalimbali. Katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, jumla ya shilingi milioni 792.9 zililipwa kama mishahara kwa watumishi hewa katika Halmashauri 40 nchini, shilingi bilioni 88.7 kati ya shilingi bilioni 328.2 zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo (*Development Funds*), hazikutumika katika Halmashauri 132, shilingi bilioni 1.09 zilizokusanywa kama mapato ya ndani katika Halmashauri 43 hazikurejeshwa na mawakala kwenye Halmashauri husika. Katika mwaka huo huo, Halmashauri 113 zilikuwa na jumla ya madeni yaliyofikia shilingi bilioni 51.3 kwa wazabuni mbalimbali wakati zenyewe zilikuwa zinadai shilingi bilioni 35.6. Katika mwaka huo huo, jumla ya vitabu 1,341 vya makusanyo ya mapato mbalimbali havikupatikana kwa wakaguzi katika Halmashauri 50. Kutaja mifano michache tu.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha za umma kinastahili kupata uangalizi wa kibunge kwa niaba ya wananchi. Hii ndiyo kazi ambayo Kamati hii imekuwa ikiifanya na kuomba kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma vimetajwa hapo juu, nidhamu ya matumizi ya fedha iliyopo sasa katika Serikali za Mitaa, haiwezi kulinganishwa na hali halisi iliyokuwepo miaka kumi iliyopita. Halmashauri zetu zinazidi kuimarika japokuwa kasi ya uimarikaji inapaswa kuhimizwa zaidi. Kwa mfano, endapo kigezo cha Hati Safi ya Ukaguzi kitatumiwa kama kipimo cha nidhamu ya matumizi bora ya fedha za umma, ongezeko la Hati Safi lililopo kuanzia Mwaka 2000 mpaka kufikia Mwaka 2009, linaashiria kuimarika mwaka hadi mwaka kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Hati zisizoridhisha zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, zipo Hati zenye Shaka zikiashiria kuwepo kwa dosari katika mienendo ya matumizi ya fedha za umma. Dosari hizi ndiyo matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma yatakayojadiliwa katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mojawapo ya majukumu ya msingi ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ni kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya

matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati imebaini dosari zifuatazo kuwa zinaathiri sana nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa: kukosekana kwa usahihi wa taarifa za mapato na matumizi ya baadhi ya Halmashauri; kukosekana kwa usimamizi wa dhati wa kiutawala kwa baadhi ya Maafisa Masuuli; kukosekana kwa uwajibikaji wa pamoja kwa Wakuu wa Idara katika baadhi ya Halmashauri; bei za kughushi katika manunuzi ya vipuri na mafuta ya magari katika baadhi ya Halmashauri kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo; matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya posho kuliko utekelezaji halisi wa Miradi mfano, TASAF, Mazingira na Miradi mingine ya Maboresho; uwezo mdogo wa Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani; na udhaifu mkubwa katika mifumo ya udhibiti na ukaguzi wa ndani. Hata hivyo, Kamati itapenda kuzungumzia masuala matano tu ambayo yameonekana kuwa sugu zaidi katika matumizi mabaya ya fedha katika Serikali za Mitaa. Matatizo haya ni mishahara kwa watumishi hewa; ukusanyaji usioridhisha wa mapato ya ndani ya Halmashauri; gharama kubwa za matengenezo na manunuzi ya mafuta ya magari; kutozingatiwa kwa Sheria na Kanuni za Manunuzi; na usimamizi mbovu wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maelezo kwa kila tatizo lililoonekana kuwa sugu hapo juu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara kwa watumishi hewa ni malipo yatolewayo na mwajiri kama ujira kwa watumishi ambao hawapo kazini na hawakustahili malipo hayo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, ilibainika kwamba, jumla ya shilingi milioni 792.9 zililipwa kama mishahara kwa watumishi hewa katika Halmashauri 40 nchini. Pia kiasi cha shilingi bilioni 1.7 cha mishahara isiyokuwa na wenyewe (*Unclaimed Salaries*) hakikurejeshwa Hazina kutoka katika Halmashauri mbalimbali. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa na inastahili kudhibitiwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa sasa wa Programu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), ambapo ruzuku ya shilingi milioni saba hutolewa kwa ajili ya ujenzi wa chumba kimoja cha darasa, kiasi hiki cha mishahara hewa ni sawa na vyumba vya madarasa 113 na ni sawa na vyumba vya madarasa 264 kwa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM). Hivyo, lazima Serikali iweke mpango madhubuti wa kurejesha fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, utaratibu uliotumiwa na Serikali Kuu (Hazina) wa kuwalipa watumishi mishahara yao moja kwa moja kwenye akaunti zao, umechangia sana kukua kwa tatizo hili. Mfano, mnamo mwezi Agosti, 2008, Hazina walipeleka mishahara hii kwenye akaunti za wahusika pasipokuwasiliana na waajiri ili wawajulishe kama watumishi hao wapo kazini au la!

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zingine zinazochangia kukua na kukomaa kwa tatizo hili ni kukosekana kwa mifumo imara ya udhibiti wa ndani katika Halmashauri zenyewe. Mifumo inapokuwa imara inaweza kubaini haraka muda wa watumishi kuajiriwa na kustaaifu, inaweza kubaini uwepo na kutokuwepo kwa watumishi kazini; ni vema Serikali ije na mkakati wa kuimarisha mifumo hii kwa teknolojia za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya 2.2 hapo juu, uchambuzi umeonesha kwamba, kiasi cha shilingi bilioni 1.09 zilizokusanywa kama mapato ya ndani katika Halmashauri 43 hazikurejeshwa na mawakala kwenye Hazina za Halmashauri husika. Wakati huo huo, kiasi cha shilingi bilioni 2.06 zilizotakiwa kulipwa kama *cashewnut export levy* kwa Halmashauri zinazotegemea ushuru wa korosho kama mapato ya ndani, hazikulipwa kiasi hicho cha fedha kutoka kwenye Bodi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini sababu mbalimbali za ubovu huu. Sababu zingine ni za makusudi kwa ajili ya wakusanyaji wasio waaminifu kujineemesha wenyewe kwa njia za wizi. Sababu zingine ni za kitaalam hasa pale Halmashauri husika inapokuwa haina ujuzi na teknolojia ya kutosha kubaini vyanzo vya mapato vilivyopo kwenye maeneo yao. Mara nyingine matatizo huanzia katika mikataba yenye vipengele visivyozinufaisha Halmashauri. Kwa mfano, katika Mkataba (2005 - 2010) wa ukusanyaji wa ushuru katika kituo cha mabasi cha Ubungo, Ukaguzi Maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibaini kuwa, kwa wastani, mkusanyaji (M/S Smart Holding Company Ltd) anakusanya shilingi milioni 4.6 kwa siku, lakini mwenye mali (Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam), hurejeshewa shilingi milioni 1.5 kati ya hizo. Kwa lugha nyingine, Halmashauri ya Jiji ilikuwa inalipwa 32.6% ya mapato yatokanayo na ushuru huo kwa siku. Huu ni uzembe mkubwa ambao haustahili kuendekewa na huu umejitokeza katika Halmashauri nyingi, zinaibiwa na zinaporwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba ujitahidi kwenda kwa *summary* kwa sababu umebakiwa na dakika 15. Ahsante, naomba uendelee.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA (MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA): Kamati imebaini kuwa, upo mwanya mkubwa wa matumizi mabaya ya fedha za umma kupitia kwenye matengenezo ya magari na ununuzi wa vipuri na mafuta kwa ajili ya magari ya Miradi mbalimbali katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati), ilitumia shilingi milioni 15 kununua *injector pump ya landcruiser hard top*, wakati bei ya wastani katika soko ni shilingi milioni tatu. Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilitumia shilingi milioni 394 kununua mafuta ya magari katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na 2008/2009. Hii ni mifano michache tu, japokuwa marekebisho ya tabia hii yanapaswa kufanyika kwa Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutozingatiwa kwa Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma: Matatizo ya msingi katika suala hili yanahusu malipo kwa wazabuni kabla hawajatoa huduma, manunuzi bila ushindani na kutoweka kumbukumbu za bidhaa ama huduma zinazonunuliwa kwenye vitabu vya mali za Halmashauri. Taarifa za kikaguzi zinaonesha kwamba katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, mali zenye thamani ya sh. mil. 111.2 zilionunuliwa na Halmashauri mbalimbali hazikuandikwa kwenye vitabu vya mali za Halmashauri husika, shilingi bilioni 1.8 zililipwa na Halmashauri mbalimbali mapema kabla ya kupatiwa huduma na wazabuni husika na manunuzi yenye thamani ya

shilingi milioni 168.5 yalibainika kufanyika pasipo ushindani kwenye Halmashauri mbalimbali. Wakati huo huo, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilitumia shilingi milioni 158 kununua mafuta ya magari ambayo matumizi yake hayakujulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa Kamati kwa sasa na kwa miaka iliyopita unaonesha kwamba, Miradi mingi hasa ya ujenzi, haifanani na thamani ya fedha zinazotajwa kulipwa. Mojawapo ya sababu ni kwamba, miradi hiyo hutekelezwa chini ya usimamizi mbovu wa Wakuu wa Idara za Ujenzi. Usimamizi mbovu nao pia husababishwa na vitu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa vyombo vya usafiri wa kumuwezesha msimamizi kufika eneo la Mradi kila anapotakiwa. Sababu nyingine ni uzembe wa makusudi unaotokana na wasimamizi kutingwa na masuala yao binafsi kuliko yale ya kiofisi. Hatimaye malipo kwa wakandarasi hufanyika bila ya kuwepo kwa usimamizi na ukaguzi wa kina juu ya ubora wa kazi iliyotendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya Halmashauri, Kamati imeshindwa kubaini namna fedha za maendeleo ya miradi zilivyotumika. Hata Watendaji wa Halmashauri zenyewe walishindwa kuijulisha Kamati kwa uwazi zaidi juu ya fedha hizo.

Kwa Mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ilipokea kwa kuchelewa shilingi bilioni 1.18 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Halmashauri hii ilishindwa kuonesha katika Taarifa zake zilizoletwa mbele ya LAAC, namna fedha hizi zilivyotumika; ni vema Serikali ikawa makini na mtiririko na matumizi ya fedha hizi katika Halmashauri mbalimbali. Mojawapo ya njia za kuzuia dosari hii ni kwa Serikali kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa baadhi ya matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa, yanatokana na taratibu za Serikali Kuu katika utendaji wake, japokuwa kwa kiasi kikubwa sababu za ubadhirifu ziko ndani ya Halmashauri zenyewe.

Baadhi ya masuala yanayoamuliwa ama kutekelezwa na Serikali Kuu na kuchochea matumizi mabaya ya fedha katika Halmashauri ni pamoja na haya yafuatayo: Serikali kulipa Mishahara ya Watumishi wa Halmashauri moja kwa moja kwenye akaunti za watumishi hao pasipo kupitia kwa mwajiri (Halmashauri); Serikali kuchelewa kupeleka fedha za ruzuku ya utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri; Serikali kupeleka kiasi kidogo cha fedha za maendeleo katika Halmashauri; na Serikali Kuu kuchelewa kuchukua hatua dhidi ya ubadhirifu na wabadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za matumizi mabaya ya fedha ambazo asili yake ni ndani ya Halmashauri zenyewe ni pamoja na kutokuwepo kwa mifumo madhubuti ya udhibiti wa ndani; kutokuwepo kwa Sera za Tahadhari na Majanga; malipo makubwa ya awali kabla ya kupata huduma za Wazabuni; kukosekana au kutofuata Mipango ya Manunuzi ya Mwaka; kukosekana kwa uaminifu miongoni mwa watumishi; teknolojia hafifu katika kuandaa taarifa na kutunza kumbukumbu za mapato na matumizi; na mbinu hafifu za usimamizi kutoka kwa baadhi ya Mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa mishahara hewa, upungufu katika usahihi wa taarifa za mapato na matumizi ya Halmashauri, kupaa kwa bei za manunuzi kusikofanana na bei halisi katika soko, uwepo wa malipo bila vielelezo vya malipo hayo, kupotea kwa vitabu vya mapato, ni matokeo ya udhaifu katika mifumo ya udhibiti na ukaguzi wa ndani katika Halmashauri zetu. Kamati za Fedha katika Mabaraza ya Madiwani na Wakaguzi wa Ndani, ni vema wakawa wanapatiwa mafunzo na nyenzo za kuwatosha kutekeleza majukumu yao katika muda mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kinidhamu dhidi ya wabadhirifu ni kitu muhimu sana katika kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha katika taasisi zetu. Mazingira yaliyopo sasa yana ushahidi kwamba, watendaji wanaobainika kuhusika na ubadhirifu wa mali za Halmashauri na wale wenye kutumia vibaya madaraka yao, hawachukuliwi hatua mara moja hata kama ushahidi upo wazi. Kwa kufanya hivyo, Mamlaka husika zinaonekana kana kwamba, zinashabikia ama kulea ubadhirifu. Ushahidi mwingine unaonesha kwamba, Mamlaka husika katika masuala ya Halmashauri imekuwa ikitumia uhamisho wa watendaji wake kutoka eneo moja wanalobakia kufanya ubadhirifu kwenda eneo lingine kama hatua za kinidhamu. Hii siyo sahihi. Kamati inaona kwamba, kuwahamisha watendaji wanaobainika kuhusika katika vitendo vya kibadhirifu katika Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine ni sawa na kuusambaza ubadhirifu ulio ndani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu kwa Kamati za Bunge za Usimamizi wa Fedha za Umma, mathalani LAAC, kuanza kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma mara moja fedha hizo zinapopelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo. Umuhimu huu unatokana na ukweli uliobainika kwamba, utaratibu uliopo sasa wa kufuatilia matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo miaka miwili au mitatu baada ya matumizi hauleti tija sana. *Value For Money (Audit) Reports* za Ofisi Taifa ya Ukaguzi ni vema zikawa zinazifikia Kamati mara moja ili Kamati husika zijiridhishe na nidhamu ya matumizi ya fedha hizo ndani ya mwaka husika wa fedha. Kukagua matumizi ya fedha ndani ya mwaka mwingine wa fedha, kunazifanya Kamati zishindwe kubaini uhalisia wa matumizi hayo hasa pale Miradi hiyo inapokuwa imetumia fedha za mwaka mwingine tofauti na zile za mwaka unaofanyiwa ufuatiliaji na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu - Maoni na Mapendekezo, Mafanikio na Mwelekeo wa Kamati: Haya ni maoni ya Kamati kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Maoni haya yanatolewa kwa kila tatizo lilionekana kuwa sugu katika matumizi mabaya ya fedha hizo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mishahara kwa watumishi hewa, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mpango mzuri utakaohakikishia kwamba, fedha zote zilizotolewa kama mishahara kwa watumishi hewa (shilingi milioni 792.9) ikiwa ni pamoja na mishahara ambayo haikurejeshwa Hazina (shilingi bilioni 1.7)9 vinarejeshwa.

Kamati ingependa kuona kwamba, Serikali Kuu inahusika kikamilifu katika kutafuta ufumbuzi juu ya suala la mishahara kwa watumishi hewa, kwa sababu inahusika

pia katika kusababisha na kukuza tatizo hili. Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, katika mwaka 2008, Hazina walilipa mishahara ya watumishi mbalimbali (shilingi bilioni 1.4) moja kwa moja kwenye akaunti za watumishi hao pasipokufanya mawasiliano na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri husika kwa ajili ya taarifa za kina juu ya uwepo wa watumishi hao kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kwamba, nambari za cheki za mishahara kwa kila mtumishi wa umma hutolewa na Hazina; lakini upo ushahidi kwamba, baadhi ya watumishi wana namba hizo zaidi ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushahidi pia kwamba, mishahara iliyolipwa kwa watumishi hewa inarejeshwa. Katika mahojiano ya tarehe 25 Machi, 2011 kati ya Kamati na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, ilibainika kwamba, kiasi cha shilingi milioni 64.6 kilichokuwa kimelipwa kama mishahara kwa watumishi ambao walikuwa wamestaafu kimerejeshwa na Halmashauri hiyo. Huu ni ushahidi kwamba, Serikali ikiamua kwa dhati kurejesha fedha hizo itaweza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Memoranda ya Fedha katika Serikali za Mitaa (*The Local Authorities Financial Memorandum, 1997: Order No. 9-16*), imeeleza umuhimu wa kuwapo kwa Mifumo ya Udhubiti wa Ndani katika Halmashauri kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la udhaifu katika mifumo ya ndani lina uhusiano wa moja kwa moja na suala la kuwepo kwa mishahara kwa watumishi hewa na bei za kughushi katika manunuzi ya vipuri na mafuta ya magari.

Kamati inashauri kwamba, Serikali ichukue hatua za makusudi za kuimarisha udhubiti wa mifumo ya ndani ya Halmashauri ili kuhakikisha kwamba, masuala ya mishahara kwa watumishi hewa, mishahara isiyorejeshwa Hazina, nambari za cheki za mishahara kuwa zaidi ya moja kwa mtumishi mmoja na bei za kughushi katika manunuzi vinakoma kabisa.

Kamati inashauri kwamba, Serikali iharakishe mchakato wa kuongeza uhuru (*independence from the control of the Executive Directors*) wa wakaguzi wa ndani ili watende kazi kwa kuzingatia taaluma na taratibu za kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo yote yanayopendekezwa yatatekelezwa lakini udhaifu ukawa bado upo, Kamati inashauri Serikali isisite kuwachukulia hatua za kinidhamu wahusika wote kila watakapobainika kuhusika katika kusababisha ubadhirifu wa fedha za umma katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi mbovu wa Miradi ya Maendeleo. Kila Mradi unaotekelezwa ndani ya Halmashauri una msimamizi wake, ambaye ni Mkuu wa Idara ambayo Mradi huo upo. Hivyo ni ushauri wa Kamati kwamba, Maafisa Masuuli pamoja na Wakuu wao wa Idara wahusike kikamilifu katika kusimamia utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini yao bila kusubiri msukumo wa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo sasa katika Kamati ni kwamba, Miradi inayokaguliwa ni ile ambayo matumizi yake yalikuwisha kufanyika miaka miwili iliyopita. Kamati inashauri pawepo na namna ambayo itaziwezesha Kamati za Bunge za Usimamizi wa Fedha za Umma kufuatilia matumizi ya fedha za Miradi mbalimbali ndani ya mwaka husika wa fedha ili kusaidia utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo. Lengo la Kamati ni kuhakikisha kwamba, angalau kila senti ya walipa kodi na wafadhili inaleta tija katika maendeleo ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine inayopendekezwa na Kamati ni ile ya kuwa na Ukaguzi Jamii (*Social Audit for Government Accountability and Transparency*) kama ilivyo kwa Polisi Jamii katika dhana ya Ulinzi Shirikishi. Katika Ukaguzi Jamii, Wananchi, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Waandishi wa Habari na Wadau wengine, wajengewe uwezo wa kusaidia kusimamia utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo pasipo kusubiri ukaguzi unaofanywa na Kamati za Bunge. Kwa mtazamo wa kisasa wa Kamati, wadau wote hawa ni marafiki wa ukaguzi na usimamizi wa fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara (TAMISEMI) ina Kitengo cha Ukaguzi wa Serikali za Mitaa (*Local Government Inspectorate*), Kamati inashauri kitengo hiki kiimarishwe pia ili kiweze kuwa na mifumo *sensitive and responsive* zaidi katika kupata habari za utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Halmashauri. Kadhalika, Kamati inashauri Kitengo cha *Value for Money Audit* katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kiongeze idadi ya wataalam, kiongeze wigo na kasi zaidi ya kuzifikia Halmashauri mbalimbali ili kuweza kuona namna fedha za umma zinavyotumika kuanzia pale tu zinapotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushauri wa Kamati kwamba, Kamati za Fedha, Mipango na Utawala katika Mabaraza ya Madiwani, zijengewe uwezo wa kusimamia kitaalam mipango ya maendeleo katika Halmashauri zao ili kuziwezesha Halmashauri kuwa na Miradi inayofanana na thamani ya fedha zinazotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Watendaji wazingatie Sheria na Taratibu za Manunuzi ya Umma. Serikali izitumie vema Taarifa na ushauri wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma juu ya taratibu za siku hadi siku kuhusu manunuzi ya umma na wakaguzi wa ndani wajielekeze zaidi katika kuangalia taratibu na uhalali wa manunuzi yanayofanyika katika taasisi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri pia Serikali ifuatilie na kuchukua hatua stahiki dhidi ya Watendaji waliobainika na watakaobainika kuhusika na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ya umma pasipo sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kughushi katika matengenezo na manunuzi ya vipuri na mafuta. Kamati inashauri Serikali itafute teknolojia maalum ya kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma yanayotokea kupitia katika manunuzi ya

mafuta na vipuri vya magari. Kamati imebaini kwamba, manunuzi ya aina hii hutumiwa kama mwanya wa kupotezea fedha nyingi za Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, kwa mara moja tu Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilifanya matengenezo ya pikipiki (STK 3746) kwa shilingi milioni 2.9, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilinunua *injector pump* ya gari *Toyota Landcruise hardtop* kwa gharama ya shilingi milioni 15 ambayo bei ya wastani katika soko ni shilingi milioni tatu. Katika mwaka 2007/2008 na 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilitumia kiasi cha shilingi milioni 394.4 ambacho ni sawa na wastani wa shilingi milioni 197.2 kwa kila mwaka kwa ajili ya kununua mafuta ya magari ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mifano michache tu; ni vema Serikali kupitia wakaguzi wa ndani ikawahi kudhibiti matumizi ya aina hii ambayo ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali irejee upya miongozo ya matumizi ya fedha katika baadhi ya Miradi kama vile TASAF, UKIMWI, Miradi ya Kirimo (*DADPs*), *Capital Development Grant (CDG)* na Miradi ya Uhifadhi wa Mazingira. Taarifa za matumizi (*Expenditure Details*) zinazoletwa na Halmashauri kuhusu Miradi hii inaonekana ipo kwa ajili ya posho zaidi kuliko kazi za msingi. Kwa mfano, katika Miradi ya Mazingira, Kamati ingependa kuona gharama za tafiti mbalimbali za masuala ya mazingira, gharama za upandaji miti, uhifadhi wa uoto na viumbe vingine vya asili na kadhalika kuliko kuona taarifa zinasheheni posho za mafunzo kwa watumishi kuliko waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia Taarifa za Kaguzi Maalum zilizofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Halmashauri za Wilaya za Mwanga na Rombo. Maoni ya Kamati ni kwamba, endapo Serikali itatekeleza ipasavyo maoni ya ukaguzi yaliyomo katika Taarifa hizo, nidhamu ya matumizi ya fedha na madaraka katika Halmashauri itaimarika sana, siyo tu kwa Halmashauri hizo mbili, bali pia kwa Halmashauri zingine nchini. Ushauri wa Kamati ni kwamba, Serikali itekeleze ipasavyo maoni ya ukaguzi yaliyotolewa na chombo husika katika Kaguzi hizo Maalum. Kamati itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maoni na mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi miwili tangu utangaze kuundwa kwa Kamati za Bunge, Kamati hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa, kuijulisha Serikali na Umma wa Watanzania kwamba, ipo na itafanya usimamizi makini wa matumizi ya fedha na mali za umma katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 1 Aprili, 2011, tayari Kamati imekwisha kupokea malalamiko ya kimaandishi juu ya ubadhirifu wa fedha za umma na usimamizi mbovu wa Miradi ya Maendeleo kutoka kwa raia wema wa Halmashauri za Mji wa Kigoma, Mbozi, Muheza na Jiji la Mbeya. Kamati inathamini sana taarifa hizo na itazitumia katika ziara zake. Ni ushauri tu kwamba, Halmashauri husika ziendeleo kuboresha huduma na maendeleo ya jamii pasipokusubiri hatua za Kamati hii.

Mnamo tarehe 21 – 26 Machi, 2011, Kamati ilipata mafunzo juu ya utekelezaji bora wa majukumu yake. Tarehe 06 – 11 Machi, 2011, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri za Wilaya za Same, Mwanga, Rombo na Moshi Vijijini Mkoani Kiliamanjaro. Tarehe 21 Machi, 2011, Kamati ilikutana na Uongozi wa Wizara (TAMISEMI), ambapo masuala mbalimbali yahasuyo usimamizi wa nidhamu ya matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa yalijadiliwa na kuafikiwa. Tarehe 21 Machi - 1 Aprili, 2011, Kamati ilijadili Taarifa za Mapato na Matumizi ya Halmashauri 21 ikiwa Mkoani Dar es Salaam. Haya ni mafanikio makubwa yakilinganishwa na uhai wa Kamati tangu ulipoiunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya yameanza kujengwa katika misingi imara ifuatayo: Nia njema ya Kamati katika kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma nchini; uwepo wa miongozo yako (Spika) madhubuti katika kusimamia utendaji wa Kamati za Bunge; uwazi na uwajibikaji wa Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao; uratibu na ushauri wa kina wa Katibu wa Kamati juu ya masuala ya taratibu za Kibunge na Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzitaja tu japo kwa uchache, changamoto zinazoikabili Kamati kama ifuatavyo:-

- Muda wa siku 40 kwa mwaka huitoshi Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha hata kama itachagua maeneo yenye matumizi mabaya zaidi ya fedha za umma. Hii ni kwa sababu za ongezeko la Halmashauri na kupanuka kwa wigo wa ukaguzi katika Halmashauri.
- Bajeti ya Kamati huitoshi pia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake yote ya msingi hususan kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku zijazo mipango ya Kamati itaendelea kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mpango Mkakati wa Ofisi yako. Kamati itazidi kujikita katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati itaendelea kuzingatia nguzo kuu za mafanikio na uimara wa Kamati za Usimamizi wa Fedha za Umma ambazo ni umoja na ushirikiano wa Wajumbe pasipokujali tofauti za vyama vyao vya siasa, uwajibikaji na uwazi wa Wajumbe, utiifu kwa Katiba, Sheria na Kanuni zinazoongoza utekelezaji wa shughuli za kibunge, elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, uongozi imara na shirikishi na utafiti katika kila jambo linalojadiliwa kabla ya kufikia maamuzi juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametekeleza wajibu wake juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2008/2009. Mkaguzi ametoa mapendekezo yake juu ya alichokiona katika Hesabu hizo. Kamati

inaunga mkono mapendekezo yake yote kama yalivyo katika Taarifa yake ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pamoja na kumuunga mkono Mkaguzi, lakini tumeona kwamba, hii tabia ya kwenda kukagua mahesabu ya 2008/2009, mahesabu ya nyuma, ni kama mtu ameshafariki dunia unamfanyia *post moterm*; ni dhahiri huyo mtu hawezi kushtuka tena. Sasa fedha nyingi zimeshaibiwa, zimeshaporwa walioiba wenyewe wamekufa na wengine wamehama. Mimi nilikuwa napendekeza kitu kingine ambacho tunaweza tukakifanya hapa kinachoitwa *social audit*. *Social audit* ni wakati pesa zinakwenda kwenye Halmashauri za Mitaa, tuwe na utaratibu wa kuzifuatilia kama vile tunavyounda sungusungu katika kudhibiti ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sungusungu wanakamata wezi wanawapeleka kwa polisi, hawangojei mpaka watu waibe au wafanye uhalifu ndiyo walinde. Sisi tulikuwa tunafikiri katika hii *social audit*, tulikuwa tunapendekeza kwamba, fedha zinapokwenda na sisi tuwe na utaratibu wa kuwa na watu wetu kwenye Halmashauri za Wilaya. Wapo wazalendo, watu wema, waadilifu, wacha Mungu, ambao wangeweza kutuambia juu ya ufujaji wa fedha. Kwa mfano, kule kwangu Kahe tunataka kujenga barabara, sasa watu wamepeleka kifusi cha udongo wananchi wamekwenda kupiga kelele wanasema ni kifusi cha udongo siyo changarawe au mtu anachimba kisima, anakwambia ni mita 60 kumbe ni mita 12. Sasa vitu hivi vinafanyika Wananchi wanaona. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Bunge hili lianzishe utaratibu mpya, mahesabu ya zamani tuendeleo kuyafuatilia lakini kuwe na utaratibu huo sasa wa kufuatilia fedha kabla hazijaliwa tuweze kujua mambo yatakwendaje.

Jukumu la Bunge hili ni kuisimamia Serikali katika kutekeleza maoni ya ukaguzi na mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati hii katika suala hili. Pale Serikali itakaponekana kushindwa kuyatekeleza maoni na mapendekezo haya ni vema ikalijulisha Bunge sababu za kushindwa kwake. Ninayo imani kwamba, Serikali haitashindwa kutekeleza maoni na mapendekezo hayo. Lengo letu ni maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wake makini ambao umeniwezesha mimi kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni na umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kufuatia maelekezo yake thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako. Ninafikiri tulikutana ukatutia moyo kwamba endeleeni hata kama watu wanapiga kelele ninyi endeleeni kukemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa uvumilivu, uwazi, umakini na uwajibikaji waliouonesha muda wote Kamati ilipokuwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dokta Thomas Kashililah, kwa uratibu wa shughuli za ofisi yake katika kuliwezesha Bunge na Kamati za Bunge kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kwa dhati kabisa, namshukuru Katibu wa Kamati yetu, Ndugu Bisile Dickson, kwa juhudi zake katika kuandaa Rasimu ya Taarifa hii na kwa ushauri wake katika masuala yaliyohusu uendeshaji wa shughuli za Kibunge na Kamati za Bunge.

Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Wafadhili mbalimbali wa Mradi wa *PFMR*, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza ziara mbalimbali za kukagua Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Maafisa wote kutoka Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, kwa kurekodi mijadala mbalimbali ya Kamati na kwa kuchapa Taarifa hii. Shukrani pia kwa Maafisa wa Polisi kutoka Kitengo cha Ulinzi cha Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha usalama katika ziara zote tulizoambatana nao. Nawashukuru Watumishi wote wa Bunge, walioisaidia Kamati kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, nawashukuru Wataalam kutoka Ofisi ya Mhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wataalam kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wataalam kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri mbalimbali nchini, kwa uadilifu wao kila walipotakiwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala mbalimbali mbele ya Kamati. Nawashukuru kipekee waandishi wa habari na watangazaji kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari, kwa namna walivyouelimisha umma juu ya majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Kamati na kufanya Wananchi watuunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na kunielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa mawasilisho yako Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunazo Kamati tatu za Mahesabu ambazo zitawasilisha Taarifa zake kwa pamoja na baada ya hapo, mjadala wake utafanyika kwa pamoja. Kila Mbunge atakayesimama, ataamua mwenyewe kuchangia ama katika maeneo yote au Kamati moja; ni uhuru wako wewe mwenyewe.

Mpaka sasa nina maombi 70 mezani kwangu. Baada ya Mheshimiwa Zitto, ambaye nitamwita hivi karibuni kumaliza kuwasilisha Taarifa ya Kamati yake ya Hesabu za Mashirika ya Umma, nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, baadae kidogo atupe pendekezo ambalo mkiafiki linaweza kutusaidia katika kuona namna gani uchangiaji wetu utaenda. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Zitto Kabwe.

MHE. KABWE Z. ZITTO (MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Pamoja na masuala mengine, naomba nikupongeze wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, pamoja na Spika wa Bunge letu Tukufu. Vile vile Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge. Mimi pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati yetu, tunakuahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Bunge, Kanuni za Bunge, mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii adimu, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge na zaidi nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kutuchagua kuwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii ya Kamati inatoa uchambuzi wa kina, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, juu ya Hesabu, ufanisi wa Mashirika ya Umma na utekelezwaji wa Sera ya Ubinafisishaji nchini. Maoni na Mapendekezo haya ni kufuatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Mashirika ya Umma nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati yameainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, chini ya Kanuni ya 115, kifungu cha 13 katika Fasili Ndogo (a) hadi (e). Majukumu hayo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2009, jumla ya Mashirika ya Umma 156 yaliwasilisha Taarifa za Hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ambapo Taarifa za Mashirika 51, hii ikiwa ni sawa na 32.6 % ya Taarifa zote zilizowasilishwa zilikaguliwa na kukamilika, Taarifa 105 zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi ambazo ni sawa na 67.4% ya Taarifa zote zilizowasilishwa. Aidha, Mashirika kumi hayakuwasilisha Taarifa zao za hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili zikaguliwe kama sheria inavyoelekeza.

Mashirika ambayo hayakuwasilisha hesabu zao kwa ukaguzi ni pamoja na Bodi ya Kahawa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma, *General Tyre East Africa Limited*, Kilimanjaro Airport Development Company, CARMATEC, Baraza la Kiswahili la Taifa, Taasisi ya Chakula na Lishe na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).

Kamati imemtaka Msajili wa Hazina alete Taarifa rasmi kwa Bunge kupitia Kamati yako ni kwa nini Mashirika haya hayakuwasilisha Taarifa zao kwa ukaguzi na hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi ya Watendaji na Bodi za Wakurugenzi kwa kukiuka Sheria ya Mashirika ya Umma na Sheria ya Ukaguzi ya Taifa. Kwa upande wa Kampuni ya *General Tyre East Africa Limited*, Kamati itatoa maelezo yake rasmi hapa chini. Kampuni ya KADCO inahitaji uchunguzi maalumu na utashughulikiwa katika shughuli za Kamati zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Kamati, Taarifa za Mashirika 78 kati ya Taarifa za Mashirika 105 zilizokaguliwa zimejadiliwa kikamilifu. Hii ni sawa na 74.2% ya Taarifa za Hesabu Zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa za kila mwaka za Mashirika hayo na kutoa mapendekezo na ushauri wa namna ya kuyaondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchunguzi wa Kamati, imebainika kuwa, maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za umma yanahusisha ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake na kuchelewa kurejesha marejesho ya masurufu; kwa mfano, katika Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN), hadi juni 30 mwaka 2008, shilingi milioni 146 zilikuwa hazijarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limekuwa ni tatizo kubwa katika Mashirika mengi ya Umma ni kutokuwepo miongozo toka kwa Msajili wa Hazina, itakayosaidia Mashirika kufuata sheria na taratibu ama miongozo hiyo kutozingatiwa na Wizara Mama au Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ya Mashirika. Aidha, uzoefu umeonesha kuwa, kutowajibika ipasavyo kwa Bodi za Mashirika, kunaathiri ufanisi wa mashirika. Kutowajibika huko kunachangiwa na ukosefu wa ubunifu katika Menejimenti nyingi za Mashirika ikiwemo kutofikiria namna bora ya kuongeza tija katika kipindi hiki na siyo kutoa huduma tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mikataba (*Contract Management*), limeendelea kuwa tatizo kubwa na limeleta hasara kwenye mashirika mengi ya umma. Mikataba mingi imeingiwa kwa gharama kubwa na masharti yake ni magumu kiutekelezaji, hali inayosababisha mashirika kupata hasara kutokana na utekelezaji wa Mikataba hiyo. Baadhi ya Mikataba iliyobainika kuwa na kasoro ni pamoja na ule wa matangazo ya Hifadhi za Taifa kupitia TTB na *cable news network* ulioigharimu TANAPA shilingi 246 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni Serikali kutoa udhamini (*guarantee*), kwa mikopo ambayo ni vigumu kulipika na hivyo kuleta hasara kubwa kwa Mashirika ya Umma. Miongoni mwa mikopo hiyo ni ile inayotolewa kwa makampuni binafsi na ile ambayo Serikali inakopa hususan kutoka kwenye Mifuko ya Pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Juni, 30 mwaka 2008, Serikali ilikuwa imetoa udhamini wa jumla ya shilingi 367,362,994,845.41 kwenye Mashirika ya Umma na hadi kufikia Juni, 30 mwaka 2009, udhamini wa Serikali kwenye mikopo hiyo uliongezeka hadi kufikia shilingi 410,111,988,412.86, hali inaonesha namna gani ambavyo udhamini unaongezeka sana na inayodhihirisha umuhimu wa Serikali kutoendelea kutoa dhamana kwa mikopo ambayo hailipiki na udhamini unaongezeka sana na hatari kwa Taifa.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo ili kuondoa matatizo hayo. Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati kwa Mwaka 2009/2010 na Majibu ya Serikali juu ya hoja za Kamati, vilipata nafasi ya kujadiliwa hapa Bungeni baada ya kuwasilishwa tarehe 21 Aprili, 2010. Hata hivyo, kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa na Kamati, Kamati yetu imeendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake kila mara. Tunatarajia kuwa, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Serikali italeta majibu ya hoja za Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu ili kukamilisha *accountability loop*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Kamati kwa Mwaka 2008/2009, hoja zifuatazo ziliibuliwa na Kamati ili kuweza kupata ufafanuzi wa kutosha toka Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Mashirika ya Umma:-

Kwanza, suala la kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa huru kiutendaji na kuipa rasilimali za kutosha sambamba na kurekebisha Sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi hiyo (*CAP 418*) ili kuipa uwezo wa kuyasimamia Mashirika ya Umma ipasavyo, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Mashirika ya Umma Nchini; hadi hivi sasa jambo hili halijatekelezwa kikamilifu. Licha ya marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina yaliyofanyika katika Bunge la Tisa, bado Sheria haikidhi haja ya kuwa na Ofisi inayosimamia ipasavyo Mashirika ya Umma (*Office of Public Enterprises – OPE*). Hali hii inakwaza utendaji na ufanisi wa Mashirika na hatimaye Serikali kujikuta inabeba mzigo mkubwa wa kuendesha Mashirika ambayo kimsingi inapaswa yajiendeshe.

Pili, orodha ya Mashirika na Makampuni ambayo Serikali imewekeza mitaji bado haijatolewa na kumekuwepo na tofauti ya Taarifa ya idadi ya Mashirika yaliyopo kwenye orodha ya Msajili wa Hazina na ile ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Taarifa hii ni muhimu katika kuhakikisha fedha za umma zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Miongoni mwa mashirika ambayo Serikali ina hisa lakini vyeti vya hisa havijawasilishwa ni pamoja na Airtel Tanzania iliyojulikana kama *celtel* na Zain hapo awali, *Mbeya Cement Company*, *BP Tanzania* na *National Bank of Commerce*.

Tatu, Serikali ijiepushe na kuingilia mipango kazi ya Mashirika ya Umma hasa kuagiza utoaji wa fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ambayo hayakupangiwa bajeti na

Mashirika husika. Mfano, katika jambo hili ni deni la shilingi bilioni 53 ambapo mpaka sasa hivi limefika bilioni 75 ambazo Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ilikopa kwa udhamini wa Serikali toka kwenye Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma (*PSPF*) na Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali amelielezea deni hili kwa ufasaha kabisa ambalo halijalipwa na linaendelea kukua kutokana na riba. Kamati imeitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu mkopo huu na namna ambavyo utalipwa ili kuhakikisha kuwa, Mfuko wa *PSPF* unaendelea kutoa huduma zake.

Nne, Kamati ilipendekeza kwa Serikali juu ya uanzishaji wa *Special Investment Fund* kama ilivyokuwa imependekezwa hapo awali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili fedha za ziada zinazotolewa na Mashirika ya Umma ziwekwe kwenye Mfuko huo kwa madhumuni ya uwekezaji na upatikanaji wa mitaji. *Tanzania Public Investments Fund* utakuwa ni kama *Sovereign Wealth Fund* na utawekeza kwenye Mashirika ya Umma yenye kuhitaji Mitaji na baada ya Mashirika kuanza kupata faida kuuza hisa katika Soko la Hisa na kurejesha fedha. Mfuko utokane na makato ya asilimia kumi ya Mapato ya Mashirika ya Umma yenye kupata faida. Mfuko huu utaondoa mzigo kwa Serikali kutoa mitaji kwa Mashirika kila wakati. Serikali inapaswa kutoa jibu kuhusu hoja hii.

Tano, pendekezo la Wabunge kutokuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma bado halijatekelezwa na Mawaziri bado wanateua Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Pendekezo hili limetolewa na Kamati kwa miaka mitatu mfululizo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameendelea kulitolea mapendekezo. Kamati itaandaa orodha ya Wabunge wote walio kwenye Bodi za Mashirika ya Umma na inashauri waondolewe ili Wabunge wabaki na kazi ya kuisimamia Serikali (*Oversight Role*). Kitendo cha Mawaziri kuendelea kuteua Wabunge kwenye Bodi za Mashirika ya Umma ni dharau kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bunge lako Tukufu.

Sita, ilipendekezwa kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), ligawanywe ili kupata Mashirika mawili ya Umma; moja likisimamia utoaji wa leseni na udhibiti wa uchimbaji (*Upstream Regulator*), *Tanzania Petroleum Authority or National Hydrocarbons Authority* na lingine kuwa Kampuni ya kibiashara ya mafuta na gesi (*National Oil and Gas Company*), ambapo kila sehemu ya Muungano itakuwa na Kampuni yake na kuondoa malalamiko ya sasa juu ya mafuta na gesi. Pendekezo hili Serikali haijalitolea majibu wala utaratibu wa kulitekeleza ili kuboresha usimamizi wa Sekta ya Gesi na Mafuta. Vile vile pendekezo hili litaweka msingi wa Sekta ya Mafuta na Gesi kusimamiwa na chombo cha Muungano badala ya sasa ambapo kinasimamiwa na *TPDC* ambayo siyo Shirika la Muungano. Pendekezo hili litekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni jambo la umuhimu mkubwa kwa Serikali kuzingatia maelekezo ya Kamati kama yalivyokuwa yametolewa hapo awali na kuazimiwa kwa Azimio la Bunge lako Tukufu tarehe 21 Aprili, 2010, kwa kuyafanyia kazi kwa haraka ili kukamilisha maudhui ya Kamati katika kufanikisha mchango wa Mashirika ya Umma kwa maendeleo ya Taifa letu.

(d) Kufanya Tathmini ya Ufanisi wa Mashirika ya Umma: Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma katika kutekeleza jukumu lake lililopo katika fasili ya 13(d) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, iliendelea kufanya tathmini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma, kuangalia iwapo Mashirika hayo yanatimiza malengo ya uanzishwaji wake. Kwa muhtasari, tathmini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma imebainisha mambo kadhaa katika mashirika yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usambazaji Maji Dar es Salaam (DAWASA), imeendelea kuwa na matatizo makubwa ya kiutendaji, hali inayozorotesha ufanisi wa Shirika hilo muhimu kwa Wananchi. DAWASA imepata hasara ya jumla ya shilingi bilioni 26.6 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2008 ukilinganisha na hasara ya shilingi bilioni 10.4 kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2007, hali hii ni hatari kwa uwepo wa Shirika kwa siku zijazo kama hatua ya kudhibiti upoteaji wa maji. Kamati imejulishwa kwamba, 57% ya maji yanayozalishwa Dar es Salaam hupotea *ilhali* Wananchi wanapata kero kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wakazi wa Dar es Salaam wanaotumia maji ya kununua kwenye madumu, yaani Wananchi wa kawaida, gharama za maji ni kubwa kuliko Wananchi wanaotumia maji ya DAWASCO. Utafiti wa Shirika la *Water Aid* unaonesha kuwa, Mwananchi wa kawaida, masikini wa Manzese, analipia gharama za maji mara kumi na tano zaidi kuliko Mwananchi mwenye uwezo anayeishi Masaki! Kamati imelitaka Shirika la DAWASA na DAWASCO kurekebisha mara moja hali hii na hasa eneo la upoteaji wa maji kama ilivyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN), kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, limelimbikiza madeni yanayofikia shilingi bilioni 2.6 na ufanisi kimapato ulishuka kwa kukusanya shilingi bilioni 8.0 ukilinganisha na shilingi 11.5 bilioni zilizokusudiwa kukusanywa, hii ikiwa ni tofauti ya asilimia 31 ya lengo lililokusudiwa. Kamati imemwomba Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kukagua upya Hesabu za TSN kufuatia kutoridhishwa na mahesabu na hata utendaji wa Shirika.

Maoni ya Kamati ni kuwa, Shirika hili liongeze juhudi katika ukusanyaji madeni na pia kuzingatia Sheria ya Manunuzi na kuepokana na ukiukaji wa Sheria katika manunuzi ya magari chakavu kwa gharama kubwa. Kwa kuwa Serikali inamiliki asilimia 100 katika Shirika hili na ili kuhakikisha TSN inakuwa ni mali ya umma badala ya mali ya Serikali (*public newspapers* badala ya *government newspapers*) na kwamba Shirika linaweza kujiendesha kwa faida, basi asilimia 50 ya Hisa za TSN ziuzwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam haraka iwezekanavyo. Hii itaongeza ufanisi wa Shirika na kuwa kisemeo cha Wananchi badala ya sasa ambapo Taifa linapata habari za magazeti binafsi na ya Serikali pekee. Tunashauri TSN ichapishe magazeti ya umma kwa kuruhusu umma kumiliki sehemu ya Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*), imeendelea kutoa huduma katika maeneo ya Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Kamati

inaipongeza kwa dhati Kampuni ya Huduma za Meli ambayo imejiendesha kwa muda mrefu bila kupata ruzuku ya Serikali licha ya kwamba, ipo kwenye orodha ya Mashirika ya kuuzwa (*specified*). Hata hivyo, Kampuni hii ina changamoto nyingi sana ikiwemo ya uchakavu wa meli, kunyang'anywa mali zake na kupewa Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) na kutofanywa maamuzi kuhusu hatma ya Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii iliwekwa chini ya usimamizi wa *CHC* ili ibinafsishwe mwaka 1998, lakini hadi leo Serikali haijachukua maamuzi juu ya hatma ya Kampuni hii ili kuipa ufanisi. Kamati inaitaka Serikali kufanya maamuzi juu ya Kampuni hii ili Wananchi wanaotumia usafiri wa maji wapate huduma stahili na bora.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, ilianza kutekelezwa Nchini ikiwa ni malengo ya kutekeleza mipango ya kiuchumi katika kuongeza uwekezaji na kukuza uchumi chini ya mpango ujulikanao kama (*Structural Adjustment Programme SAP*) ili kuinua Sekta Binafsi na kuipa Serikali nafasi ya kutekeleza mipango muhimu ya kisera.

Katika utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji na kwa kuzingatia Tathmini iliyofanywa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2008/ 2009, Kamati ilibaini kuwa kuna mambo yanatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

- Urejeshaji wa umiliki wa Mgodhi wa Kiwira uliokuwa umebinafsishwa hapo awali kwa Serikali kuingia ubia na Kampuni ya *Tancoal Power* (Serikali ikimiliki hisa 30%) bado haujakamilika. Kamati ilitembelea Mgodhi huu mnamo mwezi Machi, 2011 na kujiridhisha kuwa Serikali inatakiwa kukamilisha mchakato wa kurudisha Mgodhi huu ili apatikane mwekezaji mwingine aanze kuzalisha makaa ya mawe na umeme mapema iwezekanavyo.
- Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*), litamaliza muda wake kisheria tarehe 30 Juni , 2011; ni vema Serikali ikafanya uamuzi wa haraka na wa makusudi kuliongezea muda Shirika hili ili kulipa nafasi ya kukamilisha utekelezaji wa majukumu yaliosalia ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa madeni ambayo Serikali inayadai kwa baadhi ya Mashirika yaliyobinafsishwa yanayofikia shilingi 23,610,024,841 hadi tarehe 28 Februari, 2011. Serikali ni vema izingatie kwamba, bado kuna mali ambazo *CHC* inazisimamia na kuna watu wengi wanadaiwa kutokana na kununua Mashirika ya Umma na mali zake bila kulipia kikamilifu. Mabadiliko ya Sheria ya *CHC* yasiweke kikomo cha muda wa Shirika bali kikomo kiwe ni kazi kukamilika. Kamati inatahadharisha kwamba, kuiacha *CHC* kumaliza muda bila kukamilisha majukumu yake, kunaweza kupelekea upoteaji mkubwa sana wa mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, imetumia nyenzo na mbinu zifuatazo kama msingi na mwongozo wa utekelezaji wa majukumu yake:-

(a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kama ilivyofanyiwa marekebisho, mara kwa mara na hasa kuhusu mamlaka ya Bunge na Kamati zake, Ibara ya 63 ya Katiba na ibara nyingine husika;

(b) Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007;

(c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka ulioishia 30 Juni, 2009;

(d) Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 na Sheria iliyoanzisha kila Shirika husika;

(e) Taarifa za Msajili wa Hazina;

(f) Taarifa za mahesabu za kila Shirika kwa Mwaka wa Fedha unaojadiliwa ikiambatanishwa na majibu ya Hoja za Ukaguzi kutoka katika Manejimenti ya kila Shirika lililojadiliwa; na

(g) Taarifa za kitafiti kutoka maeneo mbalimbali juu ya mambo yanayogusa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali ili kutekeleza wajibu wake zikiwemo:-

(i) Semina za mafunzo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Msajili wa Hazina. Lengo la semina hizi za mafunzo lilikuwa ni kupata taaluma ya jinsi ya kusoma na kutafsiri mahesabu.

(ii) Kujadili na kuchambua Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika mbalimbali kwa kuwaita Maafisa Masuuli (*Accounting Officers*) na Wenyeviti wa Bodi mbele ya Kamati).

(iii) Kufanya ziara za kujiridhisha na thamani na uhakika wa kuwepo kwa miradi/mashirika husika (*value for money audit and expenditure*) katika Miradi iliyo chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) ya Mchuchuma, Liganga na South Ngaka na pia Mradi wa Kiwira, ambayo inategemewa kuwa ukombozi wa Sekta ya Umeme na Viwanda kwa Taifa letu kwa siku za hivi karibuni.

(iv) Kuunda Kamati Ndogo ili kufuatilia masuala ambayo Kamati ilihitaji maelezo ya kina kuhusiana na Hesabu za Shirika husika. Kwa Mfano, Kamati Ndogo imeundwa kufuatilia ubinafsishwaji na hatma ya Kampuni ya *General Tyre East Africa Limited*, ambayo imeshindwa kufanya kazi na kwa kuzingatia ukweli kuwa Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 74 katika Kampuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2009 ulibaini kuwa kwa kipindi hicho kulikuwapo na

jumla ya Mashirika ya Umma 196 yaliyo hai na Mashirika 18 ambayo yalikuwa kwenye hatua mbalimbali aidha kufunga shughuli zake, kubinafsishwa, kuundwa upya au kufilisiwa. Umiliki wa hisa za Serikali ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Serikali iliwekeza kiasi cha shilingi 6,143,567,862,966.68 katika Mashirika ya Umma. Mtiririko wa gawio kwa muda wa miaka miwili ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka	Mtaji uliowekezwa	Gawio lililopatikana
2007/2008	5,140,499,602,257.00	76,951,126,934.16
2008/2009	6,143,567,862,966.68	31,223,253,590.26

Chanzo cha Taarifa: Maelezo ya Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yaliweza kuchangia mapato Serikalini kutokana na gawio, mikopo na riba na michango mingine. Gawio kutoka Mashirika ya Umma limepungua kutoka shilingi 76,951,126,934.16 mwaka 2007/2008 mpaka shilingi 31,223,253,590.26 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, gawio na michango mingine (*remittances*), inategemea sana utendaji wa Mashirika ya Umma kwa mwaka husika. Kupungua kwa gawio na michango mingine kutoka Mashirika ya Umma kwenda Serikalini ni ishara kuwa Mashirika ya Umma yamepungua ufanisi na hivyo kupata hasara. Kamati inaendelea kumtaka Msajili wa Hazina aimarishe usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yafanye kazi kwa ufanisi na kutoa faida kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo Mashirika ambayo Serikali inashikilia hisa za asilimia 50 na chini ya hapo hayana usimamizi (*oversight*) wa Kibunge. Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hana Mamlaka ya kukagua hesabu hizo na hivyo Kamati hii haikupata fursa ya kujadili Taarifa za Hesabu zao na hatimaye kutokujua mtaji wa umma unaendeshwa namna gani. Mashirika hayo na hisa zilizopo ni kama ifutavyo: BP (hisa 50%); Zain Tanzania (hisa 40%); *Abood Soap Industries* (hisa 23%); NBC (hisa 30%); na Kilombero Sugar (hisa 25%).

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 111 wa Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Juni 30, 2009 yameainishwa mambo yanayochangia kurudisha nyuma utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi Umma Nchini kuwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji ya kutosha kwa shughuli za Mashirika husika, uongozi usio imara katika Mashirika hayo, kutowajibika ipasavyo kwa Bodi za Wakurugenzi, upungufu katika mipango kazi ya Mashirika, upungufu katika kuzingatia taratibu za manunuzi na utunzaji wa mali za Mashirika hayo. Kamati ilifanya juhudi sana katika kufuatilia na kutoa maagizo kwa mashirika mbalimbali yaliobainika kuwa na aina hiyo ya udhaifu.

Kamati pia imefanya tathmini na kubaini matatizo sugu katika Mashirika yetu ya Umma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo yanayotatiza ufanisi katika Mashirika ya Umma ni kutowajibika ipasavyo kwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika ambazo kimsingi ndiyo zimekabidhiwa jukumu la kuhakikisha utendaji wa Mashirika unakuwa na ufanisi.

Kamati ilibaini kuwa katika baadhi ya Mashirika, Wajumbe wa Bodi wamekuwa hawazisimamii Menejimenti za Mashirika yao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuziacha Menejimenti zikitekeleza majukumu ya Bodi za Wakurugenzi, hali inayoondoa dhana nzima ya uwajibikaji katika Mashirika ya Umma. Ushauri wa Kamati ni kuwa imefika wakati muafaka sasa kwa Serikali kuingia Mikataba ya Utendaji (*Performance Contracts*) na Wajumbe wa Bodi za Mashirika ili kupima utendaji wao kwenye Bodi husika na pale pasipokuwa na ufanisi, Wajumbe hao wa Bodi waondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma kutokuwa na Mipango ya Manunuzi kwa mwaka (*Annual Procurement Plans*) na Vitengo vya Manunuzi (*Procurement Management Units*) ni miongoni mwa sehemu ambazo kiasi kikubwa cha fedha za umma zinapotea. Hivyo, kusipokuwa na udhibiti wa kutosha eneo hili litaendelea kupoteza fedha nyingi za umma na kwa muda mrefu kubainishwa kama chanzo kikubwa cha sifa mbaya ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika mashirika na Serikali kwa ujumla. Kamati inashauri kwamba, Sheria na Taratibu zote za Manunuzi zinapaswa kuzingatiwa. Mifano michache ya manunuzi yasiyozingatia Sheria katika manunuzi ya umma ni pamoja na:-

- Ununuzi wa magari yaliyokwishatumika uliofanywa na Shirika la Magazeti ya Serikali (*TSN*) kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, ikiwamo ununuzi wa gari aina ya NOAH kwa gharama ya shilingi milioni 30, bei isiyokuwa halisi kwa soko; hivyo, kulinyima shirika thamani ya fedha inayolipwa.

- Manunuzi ya magari yalifanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*), kwa jumla ya shilingi 102,285,441 bila kufuata Sheria ya Manunuzi.

- Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano (*TCRA*), iliingia zabuni ya kupitia muundo wa ofisi, tathmini ya utendaji kazi na kupitia ngazi za mishahara (*organisation review, job evaluation*) na *job grading* ambayo awali ilitangazwa tarehe 16, 17 na 20 Agosti 2007 na kuingia Mkataba tarehe 28 Januari, 2008 kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Tathmini (*Evaluation Committee*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji wa mali za kudumu za mashirika (*Fixed Register*) na kuziweka katika kumbukumbu ili zitumike pale zinapohitajika, imekuwa ni zoezi gumu kwa mashirika mengi ya umma. Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa, matokeo ya kutokuwa na rejesta za mali za kudumu, yanaweza kusababisha upotevu au wizi wa mali ya umma kama hatua za haraka hazitachukuliwa kwa kuboresha mifumo ya utunzaji kumbukumbu ya mali kwa kutumia mifumo ya kielektroniki. Miongoni mwa Mashirika yaliyobainika kuwa na tatizo hilo ni pamoja na Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yana matatizo makubwa sana ya mitaji ya kuwekeza (*recapitalization*). Kukosekana kwa mtaji kunaathiri Mashirika ya Umma kuendeshwa kwa ufanisi. Mashirika yaliyoathiriwa zaidi na tatizo hili na kiasi cha mtaji wanachohitaji kwa sasa ili kujiendesha ni kama ifuatavyo:-

S/N	SHIRIKA	KIASI CHA MTAJI KINACHOHITAJIKA
1.	Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)	Milioni 2,877,586.82
2.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Bilioni 1.5
3.	Shirika la maendeleo la Taifa (NDC)	Bilioni 4.8
4.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Bilioni 169
5.	Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)	Bilioni 2.4
6.	Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)	Bilioni 18.2

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili bado linaendelea. Hivyo, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuyaongezea mashirika hayo mitaji ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hata hivyo, ipo haja ya Bunge kujiridhisha na sababu za kupungua kwa mitaji ya Mashirika hayo. Kuanzishwa kwa *Tanzania Public Investments Fund* kutasaidia sana kumaliza tatizo hili la mitaji kwa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa, kuna Taasisi za Serikali na hasa Wizara, ambazo zimekuwa mara kwa mara zikichelewesha kuwasilisha michango ya kisheria kama waajiri kwa Mifuko ya Pensheni. Ucheleweshaji huu wa kuwasilisha malipo ya kisheria kwenye Mifuko ya Pensheni siyo tu unatatiza utendaji wa Mifuko ya Pensheni lakini pia unawanyima watumishi husika haki zao za kisheria za kupata malipo pindi watakapostaafu, tatizo ambalo limewakumba wastaafu wetu wengi kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*) hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2008 ulikuwa unazidai Wizara zifuatazo kiasi kikubwa cha fedha ambazo hazikuwasilishwa kwa muda mwafaka:-

Na.	WIZARA/ IDARA	KIASI INACHODAIWA (Tshs)
1.	Afya na Ustawi wa Jamii	413,560,330
2.	Elimu na Mafunzo ya Ufundi	386,841,586
3.	Mifugo	113,050,717
4.	Kilimo na Chakula	69,361,728
5.	Mahakama	53,230,902
6.	Mali asili na utalii	46,122,503

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2009 katika sehemu ya utangulizi wa Taarifa yake, alibainisha

Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma kama kikwazo cha uwajibikaji katika Mashirika ya Umma.

Kwa kuzingatia dhana ya Utawala Bora na Misingi ya Uhuru wa Bunge kama mhimili wa kuisimamia Serikali; ni vema kabisa Waheshimiwa Wabunge wakawa huru nje ya Bodi za Mashirika ya Umma ili watekeleze wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kwa ukamilifu. Kamati inampongeza kwa dhati, Gavana wa Benki Kuu, kwa kutoa mwongozo wa kuwaondoa Waheshimiwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Fedha hapa Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa, Mamlaka mbalimbali za uteuzi zimeendelea kuteua Waheshimiwa Wabunge kuwepo kwenye Bodi za Mashirika ya Umma. Baadhi ya Mashirika ambayo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo: TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kubaini kuwa, kuna baadhi ya Mashirika ya Umma yameshindwa kuweka kumbukumbu sahihi za mali zao, hali inayochangia upotevu wa mapato. Kwa mfano, katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), idadi ya wanafunzi waliopo kwenye *ledgers* na Idara ya Uhasibu zinatofautiana. Tatizo hili kwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha limesababisha kutokusanya ada za wanafunzi kwa ukamilifu, ikiwa ni pamoja na madeni ya malipo mbalimbali yaliyotakiwa kufanywa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la michango inayopokelewa kutoka kwa waajiri kwenda kwenye Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii kutowekwa takwimu sahihi kwa wakati muafaka limeendelea kujitokeza kwenye Mifuko ya Pensheni ya PPF, NSSF na PSPF kwa muda mrefu sasa.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa, fedha hizi zinapokelewa na kutowekwa takwimu sahihi za mahali zinapotoka zimekuwa zikiandikwa kama *unallocated funds*, hali inayoweza kusababisha upotevu wa fedha za Wanachama wa Mifuko husika hasa watakapokuwa wanastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa mfano katika Mfuko wa PSPF, suala la fedha kutokufika kwa takwimu sahihi limekuwa likibebeshwa kama mzigo wa mwanachama na siyo mwajiri. Kamati ilichukua hatua mara moja ya kuzuia vitendo vyovyote vitakavyofanyika kuwanyanyasa wanachama wa Mifuko kwa makosa yanayofanywa na waajiri na badala yake Mifuko ya Hifadhi za Jamii imeagizwa kufanya jitihada za kutunza kumbukumbu za wanachama wao kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali lifuatalo linaainisha fedha zilizoshindwa kuwekwa takwimu sahihi na Mifuko ya Pensheni:-

S/N	MFUKO	UNALLOCATED CLAIMS/RECIIVABLES
1.	PPF	1,673,514,000 (Tarehe 07.10.2008)

2. PSPF 148,993,261 (Tarehe 30.06.2009)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika mbalimbali ya Umma yamekuwa yakilipa mafao tofauti tofauti kwa Watumishi wao kutokana na Mikataba ya ajira inavyoainisha. Aidha, kumekuwapo na mifumo kadhaa ya kutoa motisha kwa Watumishi ili kuwapa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi ya Mashirika yanalipa mafao hayo kinyume na Sheria za Utumishi wa Umma na pia Sheria za Kodi ya Mapato, hali inayosababisha baadhi ya Watumishi kupata mafao mara mbili (*Double Benefits*) kinyume na Sheria ya Mafao kwa Watumishi wa Umma. Mfumo wa Kiinua Mgongo (*Gratuity*) na *Endowment Scheme* ni mifumo ambayo inatumika sasa hivi kwenye Mashirika ya Umma. *Gratuity na Endowment* kwa pamoja ni makosa kimaadili, kwa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) kuwa, kuna Watumishi wa Mkataba wanaopata malipo ya *gratuity* pindi wamalizapo Mikataba yao ya kazi na pia hulipwa Pensheni wanayochangiwa na kuchangia kila mwezi na zaidi hulipwa pia Mafao ya *Endowment Scheme*. Upungufu mkubwa uliogunduliwa na Kamati katika jambo hili ni kuwa, kumekuwa na utekelezwaji wa sheria za mafao ya aina mbili kwa wakati mmoja kinyume cha sheria na pia ilibainika kuwa ni kada ya Watumishi wa ngazi ya Menejimenti tu ndio wanaofaidika na mfumo huu na siyo Watumishi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na tatizo hilo, Kamati ilimwomba Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kushirikaiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, kufanya uchunguzi wa malipo ya fedha hizo kwa kuanzia na *PPF* na Mifuko mingine yote ya Pensheni na katika Mashirika mengine ya Umma ili kuhakisha uhalali wa kisheria wa malipo hayo na kisha kutoa mwongozo kwa Mashirika yote ya jinsi ya kulipa mafao kwa Watumishi wao, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kodi ya Mapato. Uchunguzi huu maalumu utakaofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mara utakapokamilika na kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati itatoa taarifa rasmi hapa Bungeni na kupendekeza hatua za kuchukua ili kudhibiti hali hii ambayo imeanza kushika kasi miongoni mwa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya pili mfululizo, Kamati ya *POAC* inawasilisha Bungeni ushauri wa kuitaka Serikali kuacha kutoa udhamini kwa taasisi zake na mara nyingine kwa kampuni binafsi ili zipate mikopo toka kwenye Mashirika ya Umma. Uzoefu wa Kamati umeonesha kuwa, baadhi ya mikopo yenye udhamini wa Serikali hailipwi kwa wakati na muda mwingine hailipwi kabisa, hali inayoweza kusababisha Mashirika ya Umma kufa. Baadhi ya mikopo ya namna hiyo ni kama ifuatavyo: Mkopo wa shilingi bilioni 53 toka *PSPF* kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Mkopo wa bilioni 14.1 pamoja na riba toka *NSSF* kwenda *General Tyre*; na Mkopo wa shilingi 12 bilioni toka *NSSF* kwenda *TanPower Resources* (Kiwira).

Mheshimiwa Naibu Spika, urejeshaji wa mikopo hiyo umekuwa mgumu na wa kusuasua sana, hali inayohatarisha usalama wa fedha za umma kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsisishaji wa Mashirika ya Umma kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Fasili ya 13(e) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni, Toleo la Mwaka 2007. Katika eneo hili, Kamati inatoa taarifa kuhusu jinsi ilivyotekeleza wajibu huu kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ripoti ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa zinaonesha kwamba, mpaka mwezi Juni 30, 2009 mashirika 277 na vitengo 366 vilikuwa vimebinafsisishwa na mikataba ya mauzo kusainiwa au makampuni hayo kupelekwa kwa mfilisi. Katika kipindi hicho, Serikali ilipata mapato ya jumla ya shilingi 6.7 bilioni kutokana na ubinafsisishaji huo. Vilevile Serikali bado inadai baadhi ya wawekezaji jumla ya shilingi 110.1 bilioni ikiwa ni pamoja na mikopo iliyotolewa wakati wa ubinafsisishaji ambayo ni shilingi bilioni 93.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*) hadi kufikia 30 Juni, 2009 kwa mashirika 62 yaliyobinafsisishwa ni mashirika 12 tu ndiyo yalikuwa yanaendelea vizuri na uzalishaji, mashirika 27 yalikuwa katika hali ya wastani kiutendaji na mashirika 23 yalikuwa yamefunga shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikamilishe Tathmini ya Mashirika yaliyobinafsisishwa ili taarifa kamili iwasilishwe mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imekuwa na utaratibu wa kupima ufanisi wa Mashirika ya Umma kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na utendaji halisi wa Shirika katika kufikia malengo ya kimsingi yanayowekwa na shirika lenyewe kwa mujibu wa sheria ama taratibu zinazotawala kuanzishwa kwa shirika hilo; uwezo wa kifedha wa Shirika; uwezo wa kifedha wa Shirika hupimwa kwa kuangalia faida au hasara inayopatikana katika mwaka husika wa utendaji wa shirika; uwezo wa shirika katika kurekebisha hasara zinazojitokeza; na uzingatiaji wa mtizamo wa C Tano (*Corporate Good Governance, Capitalization, Compliance with laws, Competency of Managers, Corruption free and collusion*).

Mheshimiwa Naibu Spika, imebainika kwamba, ufanisi wa mashirika huathiriwa na mambo makubwa matatu. Moja ni Mikakati hafifu ya Mashirika yenyewe katika kutekeleza majukumu yake. Mbili ni mwenendo ama maamuzi ya Serikali Kuu juu ya Mashirika hayo, kwa mfano, Serikali kuendelea kukopa kiasi kikubwa cha fedha kutoka katika mashirika ya hifadhi, mashirika kukaa kwa muda mrefu bila Bodi za Wadhamini, kwa mfano, hadi tarehe 30 Machi, 2010, Mashirika yafuatayo yalikuwa hayana Bodi za Wadhamini hivyo kuyapunguzia uwezo wa kufanya kazi ipasavyo; Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Bodi ya Tumbaku Tanzania, Bodi ya Utalii Tanzania, Mashirika kuwa chini ya watu wanaokaimu madaraka kwa muda mrefu na kadhalika. Tatu ni athari zinazotokana

na mabadiliko mbalimbali katika mazingira ya dunia kwa ujumla; mfano Mdororo wa Uchumi Duniani, ambao umeathiri sana Mashirika ya TANAPA na Ngorongoro.

Tathmini ifuatayo ilifanyika katika mashirika mahususi kama inavyojieleza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya ufanisi katika Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), ilibaini mambo yafuatayo ambayo yamesababisha Kampuni hii kushindwa kabisa kujiendesha; Kampuni inakabiliwa na madeni yanayofikia shilingi 23.3 bilioni; Kampuni ina mtaji hasi (*negative capital*) wa shilingi 14 bilioni; kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali ilisitisha rasmi utoaji wa ruzuku ya shilingi milioni 500 kwa mwezi kwa *ATCL* hivyo kuiacha Kampuni bila msaada au ruzuku yoyote; na kwa zaidi ya miaka mitano sasa, Serikali imetafuta mwekezaji wa kuwekeza kwenye *ATCL* bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za makusudi zinatakiwa kufanywa ili kuiokoa *ATCL* ili hata kama mwekezaji atapatikana, aikute Kampuni ikiwa inajiendesha. Kamati imetoa mapendekezo yake kuhusu ufufuaji wa *ATCL* kwenye sehemu ya maoni katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Machi, 2011 Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) ili kujadili Taarifa ya Hesabu za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Kamati ilibaini kuwa, Taarifa ya Hesabu za *TANESCO* hazijasainiwa na Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) sababu ikiwa ni deni la shilingi bilioni 94.0 zinazodaiwa na Dowans (*Contingent Liability*); hivyo *CAG* alihitaji kujiridhisha na vitabu ambavyo deni hilo lingepaswa kuonekana. Baada ya kikao hicho, Kamati iliazimia kufanya kikao cha pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na ile ya Nishati na Madini pamoja na Bodi ya *TANESCO* ili kufikia mwafaka kuhusu *contingent liability* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Machi, 2011, Kamati ilikutana na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha na Nishati na Madini pia na Bodi ya *TANESCO* na Mwakilishi wa *CAG*, kwa majadiliano ya kina ikiwa ni pamoja na kupokea taarifa muhimu kuhusiana na *contingent liability* ya shilingi 94.0 bilioni. Baada ya majadiliano ya kina, Kamati iliazimia kuwa ni vema deni hilo lisitokee katika Vitabu vya Hesabu za *TANESCO* kama Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyokuwa amependekeza hapo awali kutokana na mazingira ya uingiaji mkataba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *General Tyre East Africa Limited* (*GTEAL*), ilianzishwa mwaka 1969 ikiwa ni ubia wa Serikali ya Tanzania na *General Tyre USA*, baadaye Kampuni ya *General Tyre USA* iliuzua hisa zake kwa Kampuni ya Kijerumani ya *Continental AG*, Serikali ikiwa inamiliki Hisa 74% na *Continental AG* asilimia 26%. Kiwanda kilijiendesha kwa faida hadi mwaka 1997 kilipoanza kupata hasara na kuwa na madeni makubwa na kiasi cha kufikia hatua ya kufungwa kutokana na ushindani wa kibiashara. Tokea mwaka 2008 Serikali iliendelea kufanya jitihada kukifufua kiwanda hiki kwa kushirikiana na mwanahisa mwenza bila mafanikio yoyote hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa jitihada hizo zimeonekana kugonga mwamba na kwa kuzingatia uwekezaji wa umma uliofanyika katika kiwanda hicho na Taarifa zilizopo kwenye Kamati, Kamati imeamua kuunda Kamati Ndogo yenye Wajumbe wafutao ili kwa kushirikiana na Wataalamu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya *CHC*, kuchunguza mambo kadhaa ndani ya *GTEAL*. Wajumbe wa Kamati hiyo ni Mheshimiwa Muhamad Chomboh, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mheshimiwa Esther Matiko na Wajumbe wawili kutoka Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mwenyekiti wa Kamati hii bado hajatuletea majina. Kwa hiyo, tungeomba atuletee majina wakati tunaanisha hoja hii tuweze kuwataja Wabunge hao ili waweze kuanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii Ndogo ya Bunge imeazimia na kukubaliana kutekeleza Hadidu zifuatazo za Rejea katika uchunguzi wao kuhusu *GTEAL*:-

- Kufuatilia mkopo kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) wenye jumla ya Dola za Kimarekani milioni kumi uliotolewa kwa *GTEAL* na kuona kama taratibu zilifuatwa wakati wa kutoa mkopo huu.

- Kufuatilia matumizi ya mkopo kama yalitumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kama yalitumika ilikuwaje kiwanda kisimame kufanya kazi muda mfupi tu baada ya kupokea fedha za mkopo.

- Kufuatilia sababu zilizoifanya *GTEAL* kujiendesha kwa hasara na sababu za mwekezaji kushindwa kukataa kutoa mkopo.

- Kufuatilia mali za Kampuni na hali ya mali hizo kwa sasa.

- Kufuatilia msimamo wa Serikali kuhusu kufilisi Kampuni na sababu za kufikia msimamo huo na kama kuna maslahi kwa umma.

- Kutoa mapendekezo ya namna ya kufufua kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati hii Ndogo, uchambuzi na maoni yake kwa ufasaha yatawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu mapema kwa kadiri itakavyowezekana ili kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika katika Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma (*PSPF*), ulibaini tatizo kubwa la madeni ambayo Mfuko unaidai Serikali, mengi yakiwa ni ya siku za nyuma kabla ya mwaka 1999, ambapo baadhi ya Watumishi wa Umma walitakiwa kulipwa pensheni lakini hawakuwa wakichangia kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii; hivyo, Serikali ikachukua deni hilo la shilingi trilioni 2.6 na shilingi bilioni 719 ambazo *PSPF* imekwishalipa wastaafu baada ya kuanzishwa kwake. Baada ya kupokea hoja za ukaguzi za Taarifa ya Hesabu ya *PSPF*, Kamati ilipata wasiwasi juu ya ukubwa wa deni hilo na hivyo kuamua kukutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi ili kulijadili deni hilo kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikao hicho muhimu kilifanyika tarehe 25 Machi, 2011 ambapo majadiliano hayo yalizaa matunda, Kamati inapenda kuliariifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilianza mara moja kulipa deni hilo na kwa mwezi Machi 2011, Serikali imeilipa *PSPF* shilingi bilioni 30 kwa bajeti ya mwaka 2009/2010 na imetoa uthibitisho wa kuendelea kulipa deni hilo kwa kutenga kipaumbele katika bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma imebaini tatizo la nafasi za juu katika Mashirika kama *CHC*, *PSPF* na *TANESCO* kuwa zinakaimiwa na maafisa wengine kwa muda mrefu hali inayoweza kuzorotesha ufanisi katika mashirika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma, Kamati imebaini kuwa, yapo mafanikio na changamoto mbalimbali ambazo Mashirika hayo yanakabiliana nazo. Kwa mfano, suala la upungufu wa mitaji ya kutosha kutekeleza mipango ya kila mwaka ya Mashirika, baadhi ya mashirika kukosekana kwenye orodha ya Msajili wa Hazina; hivyo kumnyima fursa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulikagua Shirika, kuwepo maelekezo ya Serikali yanayoathiri utekelezaji wa mipango mkakati ya Mashirika, kutofautiana kwa kiasi kikubwa kwa viwango vya posho zinazolipwa na mashirika, kuchelewa kuundwa kwa Bodi za Wadhamini/Wakurugenzi wa baadhi ya Mashirika na baadhi ya Watendaji katika nafasi muhimu za Mashirika kukaimu kwa muda mrefu (mfano *CHC*, *PSPF*). Katika mazingira ya changamoto hizi, ndipo ambapo Kamati inapenda kutoa ushauri wake kwa ajili ya maboresho katika ufanisi wa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni yetu juu ya mambo yaliyotajwa hapo juu, ni vema nikatoa maelezo machache juu ya mafanikio ambayo Kamati imeyapata tokea kuanzishwa kwake:-

(i) Utendaji kazi wa Kamati umeweza kuyakumbusha Mashirika kuhusu uwepo wa uangalizi (*oversight*) wa Bunge katika nidhamu ya matumizi ya fedha na rasilimali za umma. Hali hii ni tofauti na nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma iliyokuwepo katika mashirika kabla ya Kamati hii kuundwa.

(ii) Kamati imehakikisha kuwa Serikali inaanza kulipa deni inalodaiwa na Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali (*PSPF*), kwa mwaka huu wa fedha bilioni 30 zimelipwa mwezi Machi 2011 baada ya Kamati kuagiza hivyo.

(iii) Kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Msajili wa Hazina na Wadau mbalimbali wa maendeleo, Kamati imeweza kuandaa Makongamano kadhaa ya kujadili mwenendo wa mashirika kiutendaji kwa lengo la kutambua matatizo yanayoyakabili na kupendekeza kwa Serikali namna bora ya kutatua matatizo hayo.

(iv) Kamati imesaidia Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) kufutiwa malimbikizo na riba waliyokuwa wanadaiwa na Mfuko wa *PPF* zaidi ya shilingi milioni 600 na sasa wanalipa makato ya kisheria kwa muda mwafaka.

(v) Kamati imelisaidia Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) kuharakisha mchakato wa Utekelezaji wa Miradi ya Mchuchuma, Liganga na South Ngaka, ambayo italisaidia Taifa kuondokana na tatizo la umeme na kuharakisha maendeleo ya viwanda.

(vi) Maagizo ya Kamati yamechangia kwa kiasi kikubwa kuitoa TANESCO kutoka katika mazingira ya kujiendesha kwa hasara. Mwaka wa 2006/2007 Shirika hilo lilikuwa likiendesha kwa nakisi ya shilingi bilioni 67 mpaka kufikia nakisi ya shilingi bilioni tano mwaka 2008/2009 na kuna uwezekano mkubwa kwa Shirika hili kuanza kupata faida iwapo mgawo wa umeme utamalizika.

(vii) Kamati kwa kushirikiana na vyombo vya habari imeongeza uwajibikaji na uwazi katika Mashirika ya Umma kwa kuwahusisha waandishi katika ukaguzi wa Miradi inayotekelezwa na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha na thamani halisi za Miradi hiyo.

(viii) Maagizo na usimamizi thabiti wa Kamati umesaidia kuongezeka kwa Hati Safi za Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kinyume na miaka iliyopita (Hati Safi 45 kati ya mashirika 51 sawa na asilimia 88 ya Mashirika yaliyokamilisha Taarifa za Hesabu zao kwa mwaka 2008/2009).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi huo wa kina, Kamati inashauri mambo yafuatayo kutekelezwa na Serikali kwa lengo la kuboresha zaidi hali ya mashirika na taasisi za umma nchini ili zilete tija katika kutoa huduma kwa Watanzania na katika kukuza uchumi wa nchi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie upya utaratibu wa kudhamini Makampuni Binafsi na Taasisi za Serikali zinazokopa fedha kutoka katika Mashirika mbalimbali ya Umma ili usiwe udhamini wa kufilisi Mashirika. Utekelezwaji wa ushauri huu uende sanjari na Serikali yenyewe kulipa kwa wakati madeni yanayotokana na ukopaji wake wa fedha kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mashirika mengine ya Umma pamoja na kusaini ipasavyo hati zote za makubaliano ya ukopaji wa fedha hizo. Mifano ya mikopo inayoongelewa hapa ni kama ifuatavyo; Mkopo wa shilingi bilioni 53 toka *PSPF* kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; mkopo wa shilingi bilioni 14.1 pamoja na riba toka *NSSF* kwenda *General Tyre*; na mkopo wa shing 12 bilioni toka *NSSF* kwenda *Tan Power Resources* (Kiwira).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aliweza kuainisha maeneo 17 ambayo yana upungufu mbalimbali na kuwaomba wadau ambao ni Serikali, Bunge na Mashirika husika, kuyatekeleza ili kutoa ufanisi kwa mashirika. Maeneo makubwa yalihusu Utawala Bora katika Mashirika, mifumo ya udhibiti wa ndani, matumizi bora ya rasilimali na uwajibikaji. Kamati imebaini kuwa maeneo mengi bado kushughulikiwa

ipasavyo; hivyo, Kamati inapendekeza uwajibikaji wa kutosha katika kutekeleza maoni yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa muda mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Wadhamini ndizo zenye jukumu kubwa katika kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma ili kuyapa ufanisi. Kutokuwepo kwa Bodi hizi kwa baadhi ya Mashirika siyo tu kwamba, kunaathiri kasi ya maamuzi na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya mashirika hayo, bali pia kunaathiri ratiba za utendaji kazi wa Kamati yetu. Kwa mfano, kwa mwaka wa Taarifa hii, Kamati ilishindwa kujadili Taarifa za Hesabu za Mashirika yafuatayo: Bodi ya Utalii na Taasisi ya Ustawi wa Jamii nchini kwa sababu hayakuwa na Bodi za Wadhamini. Kwa maana nyingine, Kamati haina maoni yoyote juu ya hesabu za mashirika hayo kwa mwaka wa pili mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa Mamlaka nyingi za Maji hapa nchini zinafanya kazi kwa kutumia mitandao ya kizamani sana katika kusambaza maji kwa Wananchi. Mitandao hiyo imechoka hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha upotevu wa maji yanayosambazwa kwa gharama kubwa (*Unaccounted Water*). Mfano dhahiri ni Kampuni ya Usambazaji Maji Dar es salaam (*DAWASA*), ambayo kwa mwaka 2008/2009 ilikuwa inapoteza 57% ya maji yote yanayozalishwa. Kamati imeiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya ukaguzi maalumu kuhusiana na hali hiyo ili kuweza kujenga mkakati utakaozisaidia Mamlaka zote za Maji Nchini kuimarisha makusanyo ya mapato yao. Kamati inashauri kwamba, Serikali ijipange kupitia Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*) kuhakikisha mitandao ya maji inakarabatiwa upya ili kutozitia Mamlaka hasara ya kusambaza maji kwa gharama kubwa. Njia mojawapo ya kujipanga ni kwa Serikali kudhamini mikopo kwa Mamlaka za maji ili zifanye uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya maji ambayo kwa asilimia kubwa ni chakavu. Kamati inashauri pia kwamba ili kuleta ufanisi wa kutosha kwa Mamlaka za Maji nchini ni vema Serikali ikaangalia utaratibu wa kulipa ankaru za maji kwa taasisi zake kupitia Wizara Mama za taasisi husika ili kuondoa udhaifu unaonekana dhahiri kwa Taasisi za Serikali kuzembea kulipa ankaru hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mtanzania mmoja mmoja na kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kwa maana hiyo basi, ufanisi wa Shirika la Usambazaji na Ugawaji wa Umeme nchini ni muhimu sana. Kamati imebaini kuwa, Shirika hili linayo mipango muhimu sana ambayo ikitekelezwa ipasavyo, nchi inaweza kuwa na umeme wa uhakika na wa kutosha. Tatizo lililopo hapa ni ukosefu wa fedha za kutekelezea mipango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo imani kwamba, Bunge hili litakubaliana kwa kiasi kikubwa na mtazamo kwamba, *TANESCO* wanafanya kila jitihada kujinasua na hali mbaya ya kifedha kwa kupunguza nakisi toka bilioni 26 (mwaka 2007) hadi nakisi ya bilioni tano (mwaka 2008). Kwa msingi huo basi ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali yetu ijipange vya kutosha kuhakikisha kwamba, Shirika hili linatafutiwa fedha za kutosha kukamilisha mipango yake. Mojawapo ya vyanzo vya fedha hizi ni kwa Serikali kuishawishi Mifuko ya Hifadhi za Jamii nchini kuwekeza katika Miradi ya Uzalishaji wa Umeme nchini kama ilivyo kwa nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya kuiimarisha *TANESCO* ni kwa kuhakikisha kuwa, Bodi ya Wakurugenzi inatimiza majukumu yake ikiwamo utoaji wa zabuni mbalimbali bila kuingiliwa na mara nyingine kusimamiwa na Wizara Mama na Mamlaka nyingine, hali inayosababisha utendaji wa *TANESCO* kuwa duni na hasara kama ilivyojitokeza kwa Kampuni za Richmond na baadae Dowans.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii imeendelea kufanya vizuri kwa muda mrefu na kwa tathmini iliyofanyika hivi karibuni na Wataalamu kutoka Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii Nchini (*Social Security Regulatory Authority (SSRA)*), imeeleza wazi kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendelea vema ila kutoa angalizo sehemu kadhaa za kutiliwa mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikathamini mchango wa Mifuko ya Jamii Nchini kwa kuhakikisha kuwa haitoi dhamana ya ukopaji wa Fedha za Mifuko kwa Makampuni binafsi kwani uzoefu umeonesha mara nyingi fedha hizo zinapotea bila kurudishwa. Aidha, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iongeze juhudi katika kusajili wanachama wapya ili kuongeza mapato yao. Kamati inaishauri Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*), kuanza mara moja jitihada za kushughulikia Sheria za Ukokotoaji wa Mafao ili kuwa na hali ya kufanana miongoni mwa Mifuko yote. Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni yake inayodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati ili kuwezesha Mifuko kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upotevu mkubwa wa mapato ya Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*), kupitia viwango vidogo vya *concession fees* zinazolipwa na wamiliki wa hoteli za kitalii zilizopo hifadhini. Mapato ya *concession fees* yanapitwa kwa kiasi kikubwa na yale yanayotokana na upigaji wa mahema (*Camping*) ambapo mtu mmoja hulipa USD 50 kwa siku katika Hifadhi ya Serengeti wakati *concession fees* ni wastani wa USD 7 - 10 kwa mtu mmoja kwa siku. Malipo kama haya yameisababishia *TANAPA* kutopata mapato ya shilingi bilioni 19 kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. *TANAPA* ilikusanya jumla ya shilingi Bilioni 2.4 kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 kutokana na malipo ya *concession fees*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* imependekeza viwango vya *concession fees* vitozwe kwa kuzingatia *fixed rate* kwa hoteli zote ili kudhibiti upotevu wa mapato; hivyo, Kamati inapendekeza maoni hayo ya *TANAPA* yaliyofikiwa kitaalamu ndiyo yatumike ili waweze kutoza kati ya Dola za Kimarekani 20 hadi 30 kutokana na hoteli husika kwa viwango vya *fixed rate* ili Taifa letu lipate thamani halisi ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Novemba mwaka 2007, Bunge lako Tukufu lilipitisha mabadiliko ya Sheria Namba 26 ya Mwaka 2007 iliyokuwa inaanzisha Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na badala yake ikaanzisha na kukasimisha majukumu kwa Shirika Hodhi la Yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*) ili itekeleze majukumu ya iliyokuwa *PSRC*. Tokea kuanzishwa kwake, *CHC* imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maslahi ya Serikali

na Umma kwa ujumla yanalindwa ipasavyo katika utekekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji. Kwa mfano, kwa mwaka 2009 *CHC* wamekusanya shilingi bilioni 2.6 ukilinganisha na shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2008 na pia kukusanya shilingi bilioni 14.3 kama gawiwo na kwenye hisa mbalimbali. Mafanikio makubwa yamepatikana ikiwamo ukusanyaji wa madeni na pia tathmini ya matokeo ya Sera ya Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa uhai wa *CHC* unafikia ukomo kisheria mwezi Juni mwaka 2011. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea *CHC* muda wa kutosha mapema iwezekanavyo ili ikamilishe shughuli ambazo bado hazijakamilika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa deni la Serikali linalofikia Jumla ya shilingi 23,610,024,841 hadi tarehe 28 Februari, 2011. *CHC* kwa niaba ya Serikali ndiyo wenye taarifa muhimu za wadaiwa na waliobinafsishiwa mali za umma; hivyo iwapo hawatapewa muda zaidi wa kukamilisha majukumu yao, kuna hatari kubwa ya Serikali na Umma kwa ujumla kupata hasara kubwa kwa wadaiwa kuficha taarifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), inapitia kipindi kigumu cha uendeshaji kwa kukosa mtaji wa kuweza kufanikisha shughuli zake. Kampuni hii kwa sasa haina uwezo wa kurusha ndege yoyote kutokana na mzigo mkubwa wa madeni unaolikabili Shirika hili likiwa na madeni yanayofikia 23.3 bilioni na mtaji hasi (*Negative Equity*) wa shilingi 23.3 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri na kupendekeza kwa Serikali kuchukua madeni yote ya *ATCL* na baada ya hapo kutoa mtaji unaofikia Dola za Kimarekani 31 bilioni wa kuanza kuliendesha Shirika hili ikiwa ni pamoja na kutoa dola laki saba ili kuirudisha Ndege ya *ATCL* iliyopo kwenye matengenezo ili ianze kufanya kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikubaliani kabisa na kuendelea kusubiri mwekezaji kwenye *ATCL* kwa zaidi ya miaka mitano sasa, Shirika likiwa limesimamisha shughuli zake bila kujua hatma yake. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunda upya Bodi na Menejimenti ya *ATCL* ili iweze kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Shirika hilo kwa haraka na kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) ni chombo muhimu kinachoweza kulisaidia Taifa katika kuhakisha shughuli zinafanyika kwa Tija ikizingatiwa uchache wa rasilimali tulizonazo. Shirika hili lilianzishwa mnamo mwaka 1974, likilenga kutoa mafunzo ya menejimenti, upimaji tija na kutoa huduma za ushauri na kuchangia harakati za Taifa kujenga uchumi imara na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili ambalo likitumiwa vizuri litapunguza upotevu wa fedha za umma unaofanyika katika nyanja za mafunzo toka kwa taasisi ambazo baadhi hazina nyenzo na uwezo wa kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa, halipati ruzuku toka Serikalini ili kujiendesha kwa ufanisi. Kamati inashauri kuwa, kupitia Wizara Mama ya Shirika hili (Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana), kuingiza mpango kazi wa Shirika hili utakaogharimu shilingi bilioni 1.5 ili kulipa uwezo na nyenzo za

kufanyia kazi ili liweze kuwa *think tank* ya Taifa katika maeneo ya kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la ubinafsishaji ni kuinua uchumi wa Taifa na watu wake. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inashauri Msajili wa Hazina aweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji walioshindwa kutekeleza masharti ya uwekezaji. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali ichukue uamuzi wa kurudisha chini yake umiliki wa baadhi ya mali zilizouzwa kwa wawekezaji na baada ya hapo zimetelekezwa au matumizi yaliyoainishwa kwenye Mikataba ya Ununuzi yamekiukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yalianzishwa kwa makusudi makubwa ya kutoa huduma kwa Wananchi kwa gharama nafuu na kwa muda mrefu yamekuwa yakifanya hivyo japo yanakabiliwa na changamoto kubwa. Kama tulivyoeleza hapo awali, changamoto kubwa ni mitaji ya kujiendesha ipasavyo. Baadhi ya Mashirika yamekuwa yakizalisha ziada kutokana na huduma wanazotoa. Mashirika haya ni kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Bandari Tanzania, *EWURA*, *TCRA*, *SUMATRA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaafikiana na ushauri uliotolewa na CAG wa kuanzisha Mfuko Maalumu wa Uwekezaji (*Special Investment Fund*) ili mashirika yanayozalisha ziada yawekeze fedha hizo katika Mfuko Maalum ambao utatumika kwa ajili ya kusaidia mashirika yasiyokuwa na mitaji katika kuwekeza ili kusaidia kufanikisha mchango wa Mashirika ya Umma kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Endowment Funds* za Mashirika ya Umma zisimamiwe na *Independent Fund Managers*. Mashirika mbalimbali ya umma yanatumia mfumo wa *endowment scheme* kama moja ya njia ya kutoa motisha kwa wafanyakazi wao na kuongeza ufanisi wa Shirika pindi watakapostaafu. Kamati ilibaini upungufu katika uendeshaji wa Mifuko hiyo ya Wafanyakazi hasa ilipobainika kuwa shirika husika ndilo pia linaendesha Mfuko wa *Endowment*. Kwa maoni ya Kamati, utaratibu kama huu haukubaliki kwa Sheria za Fedha; hivyo, kamati inashauri Mamlaka ya Udhhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii Nchini (*SSRA*) kuhakikisha kuwa, Mashirika yote yenye Mfuko wa *Endowment*; mfano, *TANAPA* na *NSSF*, wanaanza mchakato wa kutenganisha *endowment funds* ili ziwe chini ya uangalizi wa *Independent Fund Managers* (*Best Practice On Financial Management*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ziara ya Kamati kukagua Miradi ya Mchuchuma, Liganga na Kiwira, inayoendeshwa chini ya usimamizi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) na ule wa Kiwira ambapo Kamati ilifuatilia utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji, naomba kuwasilisha Mapendekezo na Maoni ya Kamati juu ya Miradi hiyo muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalipongeza Shirika la *NDC* kwa hatua kubwa waliyofikia katika Miradi ya Mchuchuma, Liganga na South Ngaka. Hata hivyo, juhudi zaidi zinatakiwa ili kuhakikisha kuwa, Miradi hii inatekelezwa katika muda mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Ubia baina ya Shirika la *NDC* na Kampuni ya Sichuan Hongda toka China ili kuendeleza Mradi wa Mchuchuma, Liganga ni muhimu usainiwe sasa na haraka na Serikali ishauriwe kutimiza wajibu wake kwa hatua ambayo *NDC* imefikia ikizingatiwa faida za kiuchumi za Mradi huu. Mazingira ya sasa ya uchumi wa Dunia na mahitaji ya Taifa ni mwafaka kwa Miradi ya Makaa na Chuma. Kuchelewa kuanza kwa Miradi hii kunaweza kusababisha Miradi isifanyike kabisa, kwani uchumi wa dunia kwenye bidhaa za chuma huwa unayumbayumba sana (*fluctuations*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni tanzu itakayoundwa ili kuendesha Miradi hii ifuate taratibu zote za uchimbaji ikiwemo kusainiwa kwa Mkataba wa Uendelezaji Migodi (*Mineral Development Agreements - MDA*), kwa madhumuni ya kulinda maslahi ya Serikali, Watu wa Ludewa na Kampuni yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la Ubia bado halijaamuliwa, Kamati inashauri kuwa ubia uzingatie kanuni ya faida (*Profitability and Pay Back Period*). Kwa mfano, *NDC* wanaweza kuanza kwa kuwa na hisa 20% lakini mara baada ya Mradi kulipa (*Payback Period*) mgawo wa hisa uwe ni sawa kwa sawa. Pendekezo hili pia lizingatiwe kwa Mradi wa Ngaka ambapo *NDC* wanahisa 30% kwenye Kampuni tanzu ya *TANCOAL Energy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini iharakishe kutoa leseni ya uchimbaji wa Makaa ya Mawe kama ilivyoombwa na Kampuni ya *TANCOAL*, ambayo inamilikiwa kwa ubia na *NDC* ili uchimbaji wa makaa uanze na hivyo kuanza kuzalisha Umeme. Inapendekezwa kuwa, umeme unaotokana na Makaa ya South Ngaka uzalishwe kutokea Wilaya ya Kyela ili kurahisisha kuunganisha na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kwa Kamati ya Nishati na Madini kuanza mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini kwa lengo la kutangaza Rasilimali za Makaa ya Mawe na Chuma kuwa ni Rasilimali za Kimkakati (*Strategic Resources*) na kwamba, leseni za kumiliki vitalu vya madini haya zitamilikiwa na Mashirika ya Umma tu. Pendekezo hili linatokana na ukweli kwamba, kuna leseni nyingi sana za kumiliki madini haya ambazo zimemilikishwa kwa watu binafsi (*speculators*). Inapendekezwa kwamba, leseni zote za kumiliki vitalu vya Chuma na Makaa ya Mawe zinazomilikiwa na Watu Binafsi au Makampuni ya Nje zifutwe na kumilikishwa kwa ama *STAMICO* au *NDC*. Hata hivyo, ifikiriwe kuundwa kwa Shirika la *Tanzania Iron and Coal Corporation* itakayomilikiwa kwa ubia na *STAMICO* na *NDC* na Shirika lingine lolote la Umma kwa lengo la kuendeleza rasilimali ya Makaa ya Mawe na Chuma hapa Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalitaka Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) kuanza kuwekeza katika msongo wa kusafirisha umeme (*Transmission*) kuelekea kwenye Miradi hii ili kufanya Miradi hii iwe na maana. Kamati imefurahishwa na wazo la Wabia wa *NDC* kujenga msongo wao wa umeme. Hata hivyo, Kamati inaamini kuwa suala la msongo wa umeme liendeleo kuwa chini ya Shirika la *TANESCO*

au Serikali iunde Kampuni nyingine ya Umma kwa ajili ya *transmission* peke yake. Kwa ajili ya uharaka wa msongo wa sasa, Kamati inashauri kuwa, wabia wa *NDC* wajenge msongo huu kama mkopo kwa Shirika la *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa manunuzi yote yanayofanywa na Mashirika ya Umma. Aidha, ni vema ikafahamika kuwa miongoni mwa Mashirika yote ya Umma hapa Nchini ni *TANESCO* ndiyo wanaofanya manunuzi ya gharama kubwa kwa mwaka ukilinganisha na Mashirika mengine. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa pale ambapo Serikali ina hisa katika Kampuni ambayo inazalisha hapa hapa Nchini baadhi ya bidhaa zinazohitajika na Mashirika ya Umma, basi Mashirika ya Umma yatoe kipaumbele cha manunuzi yao bila kuathiri ubora. Kwa mfano, haiingii akilini Shirika la Umeme Tanzania kununua nyaya kutoka nje wakati Serikali inamiliki hisa katika *East African Cables* ama kununua transfoma kutoka nje wakati Serikali ina hisa *TANELEC*. Kisingizio ni Sheria ya Manunuzi. Sheria gani inayotoa fursa za kukuza Viwanda vya nje na kunyima kazi na ajira kwa viwanda vya ndani?

Kamati inapendekeza kwamba, Mashirika ya Umma yaingie mikataba ya muda mrefu (*Supply Contracts*) na Viwanda vya ndani vyenye kuzalisha bidhaa wanazotumia ili kuimarisha viwanda vya ndani na pendekezo hili lianze kwa *TANESCO* kuhusiana na transfoma na nyaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kwamba, Taarifa ya Kamati imeeleza namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake ya msingi na mafanikio iliyopata katika utekelezaji wa majukumu yake; hivyo, kuridhihirishia Bunge lako umuhimu wa Kamati hii katika kusimamia ufanisi wa Mashirika ya Umma nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, kwa jinsi tulivyoshirikiana katika kuweka mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa Bunge na Kamati zake hususan Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kukushukuru wewe binafsi, kwa uongozi wako makini, ambao umeniwezesha mimi kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni na umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe - Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Ninawashukuru sana kwa uadilifu wao, michango na hoja zao zilizolenga maslahi ya Taifa kwa muda wote. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto – Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Felista A. Bura, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Muhamad A.

Chomboh, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Ali Kheir Khamis, Mheshimiwa Prudensiana W. Kikwembe, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Zainab R. Kawawa, Mheshimiwa Aina M. Mwidau na Mheshimiwa Ester A. Bulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Shukrani zaidi kwa Idara ya Kamati za Bunge, kwa kuendelea kuipangia Kamati, Katibu makini na ambaye ameratibu na kuishauri Kamati kwa ufasaha, juu ya mwenendo bora wa shughuli za kila siku kwa kuzingatia miongozo ya utendaji kazi za Bunge na Kamati zake kwa muda wote. Huyu ni Ndugu Erick Maseke.

Naomba kutumia fursa hii kuishukuru Benki ya Dunia kwa Programu yake ya Urekebishij wa Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma inayojulikana kama *Public Financial Management Reform Programme* (PFMRP), kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza ziara mbalimbali za kukagua ufanisi wa mashirika.

Nawashukuru pia Maafisa wote kutoka Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, kwa kurekodi mijadala mbalimbali ya Kamati na kwa kuchapa Taarifa hii. Shukrani pia kwa Maafisa wa Polisi kutoka Kitengo cha Ulinzi cha Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha Usalama katika Ziara zote tulizoambatana nao. Nawashukuru Watumishi wote wa Bunge walioisaidia Kamati kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, nawashukuru Wataalam kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*), Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*) na Maafisa kutoka Shirika Hodhi Linaloshughulikia Madeni na Mali ya Yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*), kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza majukumu yake vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Wakurugenzi mbalimbali wa Mashirika ya Umma nchini, kwa utayari wao kila walipotakiwa kutoa maelezo, elimu na ufafanuzi wa aina mbalimbali, kila walipohitajika kufanya hivyo mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia hizi Taarifa tatu za Kamati za Usimamizi wa Fedha za Umma za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite zaidi katika kuchangia Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Halmashauri za Serikali za Mitaa na nitachangia maeneo machache kwa sababu ya ufinyu wa muda. Naomba nizungumzie juu ya suala na tatizo kubwa sana linalokabili Mamlaka za Serikali za Mitaa hasa hasa katika matumizi ya fedha ambazo Halmashauri zinapata kama ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa Ripoti ya Hesabu za Mwaka 2009 inaonesha kwamba, katika mwaka 2008 zaidi ya shilingi 99,114,000,000 za fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mamlaka 111 za Serikali za Mitaa hazikutumika kabisa hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na hiyo ilikuwa ni asilimia 37 ya fedha zote zilizotengwa. Mwaka wa Fedha 2008/2009, jumla ya shilingi 88,720,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 27 ya fedha zote, vilevile hazikutumika kwa Miradi ya Maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchini mwetu. Kwa hiyo, kwa kipindi cha miaka miwili 2007/2008 na 2008/2009, jumla ya shilingi 187,834,000,000 ambazo zilitengwa na Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Wananchi hazikutumika ; na Ripoti ya Makaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inasema kwamba, tatizo hili ni ushahidi kwamba, Miradi ya Maendeleo ambayo ilitengewa fedha na Serikali hazikutumika na haikutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika orodha ya majedwali yanayoambatana na Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda ya mwaka jana, kwenye Bunge hili Tukufu ilionekana kwamba, jumla shilingi 12,976,000,000 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya uendeshaji wa mashule katika Halmashauri mbalimbali nchini hazikutumika. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya shilingi 21,396,000,000 au asilimia 38.5 ya fedha zote zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya kuendesha mashule vilevile hazikutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wetu katika maeneo mbalimbali nchini wamechangishwa kwa nguvu michango ya kujenga Sekondari za Kata, wanaendelea kuchangishwa kujenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, kununua karatasi na kulipia gharama za mitihani na ni michango ya nguvu wakati mabilioni ya fedha yanayotolewa na Serikali kwa ajili maendeleo ya Wananchi hayatumiki. Sasa hizi takwimu zinaonesha nini? Zinaonesha kwamba, pengine Mamlaka zetu za Halmashauri za Mitaa hazina uwezo wa kutumia fedha za Serikali.

T A A R I F A

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafuatilia vizuri maelezo ya msemaji aliyekuwa anaendelea, labda niseme tu kwamba, kusema Halmashauri zetu nyingi hazijui kutumia fedha hizi si sahihi. Fedha nyingi ambazo zinaonekana hazikutumika kama anavyoeleza, zinatokana na taarifa ambazo kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, nyingi ni za misaada zilizoelekezwa kwenye shughuli za maendeleo, zinakwenda nusu na zinacheleweshwa kupelekwa kule. Mwaka wa Fedha ukiisha zinapaswa kurudi Hazina na baadae mwaka unapoanza zinatolewa tena. Sasa zile fedha kwenye mahesabu lazima zionekane hazijatumika zimerudi; lakini si sahihi kwamba, Halmashauri zimepokea fedha zinakaanazo na zinashindwa kuzitumia. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, unaweza kuikubali taarifa au vinginevyo.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kama anayoyasema Mheshimiwa Mbunge ni ya kweli, Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ingesema hivyo. Ingesema kwamba, hizi fedha hazijatumika kwa sababu hazikupelekwa kwa wakati. Anayoyasema hayako kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kwa hiyo ni maneno ya kuokoteza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwamba, takwimu hizi zinaonesha Halmashauri zetu hazina uwezo wa kutumia fedha; lakini inawezekana vilevile kwamba, Halmashauri zetu na Wananchi wetu hawana matatizo ya fedha, ndiyo maana fedha hazitumiki. Kama huu uwezekano wa pili ungekuwa wa kweli, Wananchi wasingekuwa wananyang'anywa mifugo yao, wananyang'anywa fedha zao, wanafungwa kwa sababu ya michango ya kujenga miundombinu ya elimu kama shule za kata, zahanati na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, Wananchi wetu wananyang'anywa vitu vyao mara nyingi bila kufuatwa utaratibu wa kisheria, si kwa sababu fedha hakuna bali ni kwa sababu kuna tatizo katika Halmashauri zetu na hili tatizo linahitaji kutafutiwa dawa. Wakarugenzi na Watendaji wa Halmashauri wadhibitiwe, wawajibishwe kwa kushindwa kutekeleza kwa kushindwa kutumia fedha za Serikali zinazotumiwa badala yake wanachangisha wananchi wetu bila sababu yoyote ya maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna suala la fedha za fidia zinazotolewa na Serikali Kuu kwa Halmashauri zetu. Mwaka 2002, Serikali ilitoa Tangazo la Serikali Namba 230 lililopiga marufuku viziwi vilivyowekwa kwa ajili ya kukusanya ushuru wa mazao. Tangazo la Serikali Namba 230 la Mwaka 2002, lilipiga marufuku mageti yote nchi nzima na lilisainiwa na aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi. Sheria hii bado iko kwenye vitabu vyetu vya Sheria na inasema ni marufuku kuweka mageti ya mazao katika barabara kwa ajili ya kukusanya ushuru wa mazao, lakini Tanzania nzima Wananchi wanakabwa, wananyang'anywa fedha zao wakati Serikali Kuu inalipa fidia kwa Halmashauri kutokana na vyanzo vya mapato vilivyofutwa; kama huu si ufisadi naomba niambiwe ni kigu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nisichukue muda mwingi wa Bunge lako; Serikali inatoa fedha kwa ajili ya kupelekwa kwenye Vijiji kwa ajili ya kupelekwa kwa

matumizi ya Serikali za Vijiji na Kata. Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali inasema kwamba, kuna zaidi ya shilingi bilioni tatu ambazo zilipaswa zipelekwe Vijijini, kwenye Kata na kwenye Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya Wananchi; na hiyo haijafanyika. Kwa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Singida peke yake, hawajapeleka Vijijini shilingi milioni 288, halafu wanawaambia wanakijiji wangu, wapigakura wangu, wachangie miundombinu ambayo imetolewa fedha na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nilisema nisiende Dar es Salaam kabla sijachangia hoja hizi. Naomba na mimi niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68. Ninaomba kupata mwongozo wako; iwapo msemaji anapewa taarifa na Mbunge anaikataa lakini ukweli unabaki kwamba, yule Mbunge aliyesimama kumpa taarifa Mbunge anayekuwa anazungumza, taarifa hiyo ni ya kweli; na mimi nasema hili kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, alilolisema Mbunge, nadhani alikuwa Mheshimiwa Masele kama sikosei, ukweli ni kwamba, pesa nyingi ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri zinabaki bila kutumika zinakwenda mwezi wa tano na mwezi wa sita; na hili sisi ndiyo tulikuwa tunagombana na Serikali kwa sehemu kubwa kwamba, kwa nini pesa ziende mwezi wa tano na mwezi wa sita wakati huo huo taratibu za kutumia pesa zile ni ndefu, kwa sababu Sheria ya Manunuzi ya Umma inazitaka Halmashauri zifuate taratibu za *procurement* ambazo zinachukua kama tunavyojua, si chini ya siku 45 ili pesa zile ziweze kufanya kazi. Sasa, inapofika mwisho, Wakurugenzi hawana namna, wanalazimika kuzirudisha zile pesa Serikalini. Katika mazingira hayo, Mbunge anapopewa taarifa anaikataa wakati jambo ni la kweli kwamba pesa ziko kule, ni kuupotosha Umma na Watanzania wakaona pesa ziko nyingi, Wananchi wanashindwa kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru Mheshimiwa kwa kutaka mwongozo kutoka kwangu. Kanuni zetu zinasema kwamba, Mbunge anapokuwa anaongea, Mbunge mwingine anaweza kumpa taarifa. Baada ya kupewa taarifa hiyo, yule Mbunge wa awali anaweza akaikubali au akaikataa. (*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Kwanza, niwapongeze Wenyeviti wote waliotoa ripoti zao hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaongelea mambo mawili hasa katika Taarifa ya Kamati ya Mashirika ya Umma pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa bahati mbaya, hatujatumia vizuri mashirika yetu ili yaweze kuisaidia Serikali katika shughuli za maendeleo. Tunadhani tumeanzisha mashirika mengi, lakini hatuhakikishi kama mashirika hayo yanafanya kwa faida na kwa sababu hiyo, tupate gawio na kwa sababu hiyo tuweze kupeleka pesa nyingi kwenye Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mashirika yote ambayo tuna *share*, mashirika yale ungemkabidhi *private people* mmoja leo, baada ya muda mfupi angekuwa ni bilionea katika Afrika hii, kwa sababu angekwenda kuyasimamia vizuri. Watu wetu wanaosimamia mashirika yetu pale Wizara ya Fedha, hawajafanya kazi ya kutosha. Ningewaomba wayasimamie mashirika haya ili yawewe kufanya kazi kibiashara. Kama biashara ipo, uwezo wa kuleta pesa upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nianze na suala la *ATC*. Suala la *ATC* linatia uchungu sana. Tumefanya makosa, tukasahihisha makosa yetu. Wakati ule ilikuwa Shirika letu halifanyi vizuri sana, tukaamua kutafuta ubia na *South African Airways*. Ubia ule tukaona hauna msaada kwetu, tukaamua kuachana nao; jambo jema na mimi naliunga mkono. Nilitegemea baada ya kuamua tunaianzisha wenyewe, sasa tungeanza kufanya kazi kuhakikisha Shirika letu linafanya vizuri. Kwa kweli biashara ya ndege Tanzania ni kubwa sana. Ameanza Nicola na ndege moja tu, leo ana ndege nne; anaruka kwenda Zanzibar, kwenda kwenye Mbuga za Wanyama, haendi Ulaya wala nchi yoyote ya Afrika. Leo Nicola ana-*make a lot of money*. Ameanza *Precision* na ndege moja tu, leo yuko mbali. Inawezekanaje Serikali ama *ATC* yetu isifanye biashara? Lipo tatizo, tulitatie, tusitafute mtu wa kumpeleka mgogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kwanza *ATC* ni la mtaji. Wakati tunaungana na *South African Airways*, Serikali ilikuwa inapeleka milioni 500 kila mwezi. Tumeanza wenyewe hatupeleki, hatujiamini, hatuna *management* nzuri, kama tatizo ni *management*, iondolewe. Kama tatizo ni wafanyakazi wengi, tuwapunguze ili wabaki ambao wanaweza kulifanya shirika lile liendelee kutoa huduma na kufanya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, suala la *ATC* tusilifanyie mzaha. Leo mwananchi anayekwenda Kigoma ni shilingi 900,000 *go and return*; ni jambo la hatari sana kwa maendeleo ya watu wengine. Inabidi ukitaka kwenda Kigoma kwa ndege, uende Mwanza, Mwanza ndiyo uende Kigoma. Siyo jambo jema kwa Watu wa Kigoma na sisi ni sehemu ya Jamhuri hii. Ninaimba Serikali, tunahitaji bilioni 14 tu zitafutwe ziweke ndege yetu ianze kuruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna ndege mbili, hatuwezi kuziacha zife eti kwa sababu kuna watu hawataki kufanya maamuzi. Ninaomba sana ndege hizi zirudi zifanye kazi. Tukishaanza kazi, tutafute fedha, tupunguze wafanyakazi, libaki shirika dogo, tutafute *management* na baadae tutafute mbia ambaye ni wa maana ili na sisi tuingie kwenye biashara ya ndege. Biashara ya ndege Duniani lazima uwe kwenye *team*, huwezi kuifanya peke yako. Umefika wakati na sisi tuweze kufanya kama wafanyabiashara wengine wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka kuongelea suala la *good governance*. Ukisoma Ripoti hapa ya Mwenyekiti wa PAC, anaongelea sana habari ya *good governance*; lakini *good governance* ni pana sana ingawa unaona tunataka kufanya kama jambo rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza aliulizwa juzi tu wala siyo muda mrefu sana kuhusu suala la *good governance* hasa katika Nchi za Afrika, Tony Blair akasema, *good governance* siyo suala la kuondoa *corruption* peke yake, *good governance* ni kuhakikisha *systems are effective, institutions are effective*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipata haya mambo mawili, *then good governance in the country* utakuwa umeipata. Sisi unaona tunapoongelea *good governance* maana hapa iko hoja kubwa inasemwa mara tatu tatu, “Wabunge wasiwe Wajumbe wa Bodi.” Kwanza, Bodi hazifanyi kazi, siyo watendaji *on daily basis, that is number one*. Bodi ni suala la *Policy* tu. Humu ndani Wabunge wote wanazo *expertise, wanazo professions* ambazo zinaweza zikasaidia maendeleo ya mashirika yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nikwambie, mashirika yale ambayo kuna Wabunge, kama ni Mbunge ana hakika anajua vizuri sekta yake, wamesaidia sana hayo mashirika kutokufa, kwa sababu wale *COs* kule, wakishaona kuna Mbunge, wanaogopa. Mkifanya hawa watu walio-*retire* peke yake, ndugu zangu tutakuwa tunapiga kelele, mashirika yatakufa. Ninachoomba Wabunge wachaguliwe kwa *merits*, kwa uwezo wao, lakini pia tuondoe ubaguzi, tuchague wote tu. Kama yuko wa CHADEMA ana uwezo, mchagueni akatusaidie, kama yuko wa CUF ana uwezo, achaguliwe akatusaidie, maana hapa ni nongwa tu hii tuiondoe. Tukiondoa hii, kelele hizi zitakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilitaka pia niongelee suala la mwisho kwenye Ripoti ya Mzee Cheyo. Mzee Cheyo nimpongeze sana kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini niombe Serikali, umefika wakati turudi kwenye *basics*, tufanye kazi ya *cash budgets*. Leo moja ya matatizo makubwa tuliyonayo tunalimbikiza madeni, madeni yana *interests*, kwa sababu tunaingia vitu vingi bila kuwa na fedha za kulipa. Kupanga ni kuchagua, Mwalimu alituambia, turudi kwenye *cash budget*, tutumie kulingana na tulichonacho, tuta-*save* pesa nyingi sana za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwaombe Watu wa Serikali, tufanye *bulk procurement*, tununue vitu kwa pamoja, tununue vitu kwa *manufacturer*, tuache ku-*deal* na watu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Serikali sasa ina madeni makubwa ya ndani. Madeni makubwa ya ndani ni ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Hawa tukiwaacha wakafa, wenye mitaji midogo tuna-*suffocate economy* yetu. Mimi ningeomba, kuna mtu ana hoteli moja, anadai milioni 500, huyu mtu hawezi ku-*survive!* Mtu anafanya biashara ya matairi, anaambiwa alete matairi, anadai milioni 200, milioni 300, huyu anadai karatasi; hawa wafanyabiashara wadogo tunawahitaji kwa ajili ya *growth* ya *economy* yetu. Niwaombe Serikali tufanye juhudi za kuwalipa. Kwa nini tunashindwa kuwalipa? Turudi kwenye *cash budget*, tununue vile tunavyoweza kuvilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna *laxity* hapa katika matumizi ya Serikali, unaamua tu unaagiza; utalipa lini? Tumeshuhudia hapa, tumeingia mikataba kwenye bajeti wala hakuna; hii ni hatari sana. Leo asubuhi hapa Waziri wa Nishati ameulizwa swali, *very pertinent question* na Mheshimiwa Zitto kwamba; hizo pesa za mafuta zinatoka wapi, ni Mfuko Mkuu. Ukiwaambia waseme Kifungu, hakuna. Hii ni hatari sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunataka kujenga barabara, ni jambo jema sana. Mwaka jana kuna barabara zimejengwa, kwenye bajeti hazimo, leo matokeo yake tuna madeni makubwa yata-*accrue interest*. Yote haya ni namna ya ku-*manage economy* yetu, lazima tui-*manage*, *in doing so*, Serikali isipate hasara, lakini na Wananchi wasipate hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wenzetu Serikalini, umefika wakati turudi kwenye *drawing board* tufanye yale yaliyo ndani ya uwezo wetu. Tukiji-*stretch* sana, matokeo yake tatalipa *interest*, tatalipa kila kitu na matokeo yake tutapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nikushukuru, lakini niwaombe rafiki zangu wa Upinzani na Mheshimiwa Zitto kwamba, suala la *Board Members* ni muhimu; waingie watu kwa uwezo wao na ikiwezekana tutangaze nafasi zao ili watu washindane. *In doing so*, tutapata watu wazuri, watasimamia mashirika yetu; na twende kwa Wabunge wote ili nongwa hii iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mchangiaji aliyemaliza kuzungumza hivi punde, kuna maneno ambayo ameyatumia yasiyokuwa ya kawaida; neno *nongwa* na nikirejea pia maneno hayo, ni baada ya Hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Zitto

Kabwe, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Sasa nilikuwa ninaomba, inaonekana kuna Wabunge wanaweza kuwa na *interest* katika Bodi mbalimbali za Mashirika ya Umma. Ninaomba Mjumbe aliyemaliza kuchangia hivi sasa, aweze ku-*declare interest*, lakini pia na maneno hayo aweze kuyafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeeleza mapema kwamba, wako wachangiaji 84; kama tutatumia muda wetu katika taratibu hizi, mjue kabisa kwamba muda wenu wa kuchangia utakuwa ni mdogo sana. Duniani Mabunge yanaongozwa kwa Kanuni, Katiba, Sheria mbalimbali, Miongozo na uzoefu; sasa kwa Wabunge wa Bunge lililopita la Tisa alikuwepo Mheshimiwa Sitta hapa na moja ya *rulings* zake ilisema Wabunge ni vizuri tuwe na ngozi ngumu.

Tuwe tayari kuwaruhusu wenzetu kujaribu kusema wanachotaka kukisema mradi hawatukani. Kwa hiyo, kusema neno *nongwa* kwamba sasa nalo hili siyo neno la kawaida, itakuwa Bunge la jabu sana, kwa sababu ukweli ni kwamba ni *nongwa*. Taarifa hii kumbukeni ni ya Kamati, nilieleza mwanzoni hii siyo Taarifa ya Upinzani, zote hizi ni Taarifa za Kamati na *issue* inayozungumzwa hiyo inahusu Wabunge wote, kwa maana Mbunge asiwe au awe. Kwa hiyo, Mbunge awe yeyote, ukisema maslahi au siyo maslahi, basi labda lisiongelewe kabisa, maana kila atakayegusa ni Mbunge. Kwa hiyo, Wabunge wataendelea kujadili hoja zilizoletwa na Kamati *pro or against*, mimi nitaendelea kuzipokea na Wenyeviti wa Kamati wataendelea kuzisikiliza na Wajumbe wa Kamati husika wataendelea kuzisikiliza. Naomba nimwite Mheshimiwa Anne...

MHE. ANNE K. MALECELA: Kilango Malecela.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda hauko upande wetu. Muda uliobaki ni mdogo sana. Kama nilivyosema, muda hauko upande wetu, tukivumiliana, tutachangia wengi zaidi kwa kuokoa muda, kusikilizana na kuvumiliana, isipokuwa yule ambaye anajaribu kuvuka mipaka kabisa ndiye ambaye tumrudishe kwenye mstari. Basi kwa *session* ya jioni, kwanza, nitakachofanya kwa Mbunge ambaye hayuko humu ndani, hatutahangaika naye. Kwa yule ambaye atakuwepo na yuko katika orodha hapa, ndiye tutakayem-*pick*. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuata Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa Masoud Abdalla Salum. Tutajaribu ku-*balance* jinsia, Muungano, Vyama vya Siasa na kadhalika ili kuhakikisha kwamba, ushiriki unakuwa ni mpana iwezekanavyo.

Kwa hatua hiyo, ninaomba basi kusitisha Shughuli za Bunge hadi leo saa 11.00 jioni tutakapoendelea na shughuli iliyo mbele yetu.

(*Saa 6.59 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na atafuataiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kukushukuru wewe pekee kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Kamati ya Serikali za Mitaa, inayoongozwa na Mheshimiwa Augustino Mrema. Wajumbe wa Kamati niombe radhi kwamba, mlipokuja Wilaya ya Same sikuwepo lakini nilipaswa niwepo na mimi niwapokee kwa sababu mimi ndiyo mwenye Same kwa upande mmoja. Naomba niende moja kwa moja kwenye mambo yaliyobainika katika Wilaya yangu ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu unapokosea ni vema ukakiri. Mimi kwa niaba ya Halmashauri yangu ya Wilaya ya Same, tunakiri yote mliyoyagundua hapa kweli yalikuwa ni makosa yetu. Halmashauri yangu imekiri kwamba, yale yote yalikuwa ni makosa na mtu kukosa ndiyo kujifunza. Wamekaa siku tatu bila kupumzika, wamejirekebisha, wameandika kitabu cha hesabu za mwisho na tuna uhakika sasa tutakuwa tupo salama. Tumeandika barua kwa Kamati kuomba radhi kwa yote, kwa hiyo, naomba jamani hata hiki kifungu cha mwisho cha Kamati itaziarifu mamlaka husika juu ya hatua zingine, basi jamani mkiache naomba radhi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la fedha. Halmashauri za Wilaya jamani zinafanya kazi nzuri zikisimamiwa vizuri na hasa zikikaguliwa vizuri. Alizungumza Mheshimiwa Masele hapa kwamba, Serikali wakati mwingine inapeleka pesa ikiwa imechelewa, jamani tukubali ni kweli. Kwa wale ambao mnafuatilia vizuri Halmashauri zenu, kwa wale Wabunge wa Majimbo mnaokwenda na kuangalia vizuri, zinakwenda zikiwa zimechelewa halafu zinarudi.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu, mimi napenda kuzungumza nikiwa nina *supporting documents*, naomba Waziri wa *Local Government* mwenyewe anisikilize vizuri ambaye ni Waziri Mkuu. Mtiririko wa fedha kwa mwaka 2010/2011, *General Fund* fidia na *OC* waliyopelekewa Halmashauri ya Same Januari 2011, fedha zilizopaswa kupelekwa ni 35,987,000, fedha zilizopelekwa ni 6,000,000; hivi kweli hii Halmashauri itakwenda?

Mheshimiwa Spika, aidha, pesa ziende zikiwa zimechelewa, zikichelewa hazirudishwi au pesa ambazo zilikuwa zinategemewa milioni 35 wapelekewe milioni sita; dhana iliyojengeka Tanzania ni kwamba, pesa nyingi sana zinakwenda kwenye Halmashauri zetu, lakini wakati mwingine sivyo. Wakati mwingine zinakwenda zimechelewa au zile ambazo zilikuwa zinatakiwa zipelekwe zinapelekwa kidogo. *Imagine*, kutoka milioni 35 upeleke milioni sita, pungufu ya milioni 29; hiyo Halmashauri itaweza kufanya kitu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naisihi sana Serikali, kule kwenye Halmashauri ndiko Wananchi waliko, hizi pesa ziende kama ambavyo bajeti imepangwa na ziende kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaniwia radhi nizungumze hili jambo kidogo hapa, Madiwani wetu *morale* ya kazi iko chini; kwa nini iko chini? Kwa sababu hii nayo inachangia katika utendaji kazi; iko chini kulingana na maslahi wanayopata. Wote humu ndani Waheshimiwa Wabunge hasa wale wa Majimbo, tunawategemea Madiwani wetu kwa sababu wapo karibu na Wananchi. Naomba niseme ukweli nina-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa *ALART* Taifa. Kikao kilichopita Waziri wa *Local Government* ambaye ni Waziri Mkuu, nilimwambia hili tatizo akasema, ninakiri ni kweli, naomba Wabunge muanze mapema ili turekebishe hili tatizo. Naomba Waziri nikwambie nimeanza leo, kwa hiyo, turekebishe Madiwani nao wapate kitu kitakachowafanya wawe na moyo wa kufanya kazi ili Halmashauri ziboreshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili, baadhi sisemi kote, baadhi ya *DCs* wanawaingilia mno Wakurugenzi. Mimi nina mfano na nikisema kitu ninakuwa nimeshika kitu. Kwangu kule sasa hivi napambana na *DC* wangu, leo ameita *Press Conference* kubwa anajitetea uwongo *document* hii hapa. *DC* anaingilia kazi ambazo si zake. Mimi nimeshika karatasi kwa sababu nina *supporting documents* kwamba, anavyofanya sivyo! Kazi za Mkurugenzi amwachie Mkurugenzi yeye afanye zake za maafa, kazi za ulinzi; si ana kazi nyingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasihi sana ili kule Halmashauri kazi ziende vizuri, Mkurugenzi na Wakuu wa Idara, waachwe wafanye kazi zao. Mheshimiwa *DC* wewe pale inapobidi unaingia kati kwa sababu ni mkubwa hapa mmefanya makosa, iwapo na wewe utaingia kwenye kuidhinisha matumizi ya pesa za Wananchi kwenye Miradi yao ambayo wao wenyewe wanatakiwa waidhinisha; hivi atakayemkosoa mwenzake ni nani? Nina vithibitisho hapa kwamba amefanya. Leo anasema ooh sijafanya, amefanya. Mimi nikisema jambo nina mahali nimeshika. Yeye na aite *press conference* mara tatu kama *dose* mimi nitampeleka kwa wakubwa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Wabunge tuachiwe tufanye kazi zetu, Wakurugenzi wafanye kazi zao na Halmashauri ifanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Kamati ya Mheshimiwa Mrema ifanye kazi kwa nguvu zake zote, kwa sababu ni kweli kuna Halmashauri zingine zinatafuna pesa za Wananchi. Madiwani wenzangu tuwasimamie imara Wakuu wa Idara, ule urafiki wa kuwa karibu ndipo tunaposhindwa kufanya kazi. Tusimame imara, ile ndiyo Serikali kama sisi tulivyo huku nyuma na wale wenzetu walivyo pale mbele pale. Tuwe na urafiki wa kiasi, lakini kama kila saa wewe Diwani umekaa na Mkuu wa Idara kwenye baa; kesho utaweza kumdhibiti? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wenzangu naomba wasimame imara, wahoji matumizi ya pesa za Halmashauri. Ninawashukuru Watanzania ni Wananchi wazuri

sana, wanachangia sana, Miradi inapokwenda kwenye sehemu zao wanachangia kwenye Miradi ya Vijiji mapato na matumizi yatoke ili tupunguze kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa leo naomba niseme namshukuru sana Mheshimiwa Mrema, alipokuja Same, yote aliyoyazungumza kuhusu Same yangu wametutendea haki, hiki kitu cha mwisho naomba wakiache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante. (*Makofi*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mimi nitajikita zaidi kwenye Taarifa ya Kamati ya Mashirika ya Umma na sana katika suala la *General Tyre*. Nitakuwa makini kwa sababu nimechaguliwa leo pia kuwa Mjumbe wa Kamati ya kufuatilia *process* nzima ya *General Tyre*, kwa hiyo, nitaishauri tu Serikali na mambo mengine ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *General Tyre* kilikuwa ni kiwanda cha msingi sana cha kutengeneza matairi Tanzania na hivi karibuni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, alipokuja Arusha Mjini, tulifanya nae ziara, tuligundua kwamba, kilisimama kwa sababu ya uzembe wala hapakuwa na sababu nyingi za msingi. Pia kuna ufisadi mkubwa ambao upo ndani ya Kiwanda cha *General Tyre*, ambapo kuna baadhi ya Wabunge kutoka Chama Tawala walishawahi kuliongelea suala hilo mwaka 2002. Pesa zaidi ya dola milioni kumi ambazo zilitolewa na *NSSF* kwa ajili ya ku-*revive* Kiwanda cha *General Tyre* na bilioni moja ilitolewa kwa ajili ya ushauri wa ufufuaji wa Kiwanda hicho lakini mpaka leo kimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, Kiwanda kimekufa kwa sababu ya uzembe na ukiangalia sababu ya kufa wakati nchi nzima hatuna kiwanda cha matairi; unagundua kwamba *demand* ya matairi nchini Tanzania ni kubwa na leo tunanunua matairi China, Korea, Ujerumani mpaka na Marekani na Japani wakati tulikuwa na kiwanda ambacho siyo tu kiliweza kusababisha ajira na kuuza matairi pia kilisababisha *secondary employment* kwa wakulima wa mipira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna tetesi na nimefuatilia nimegundua ni kweli kwamba, lile eneo la *General Tyre*, *NSSF* walikuwa wanataka kulichukua kwa ajili ya kuuza na ku-*compensate* pesa yao ambayo waliikopesha kwa ajili ya ufufuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi hapa ni moja tu kwamba, zilichukuliwa dola milioni kumi ambazo ni zaidi ya bilioni kumi na tano kwa *rate* ya leo na ilitolewa bilioni moja kwa ajili ya ushauri kwa Kampuni ya *Dye Consultation* kuhusu ufufuaji wa Kiwanda cha *General Tyre*; mpaka leo toka mchakato umeanza hakuna kitu chochote ambacho kimeendelea na pesa hizo hazijulikani zimekwenda wapi lakini *NSSF* wanayo *proposal* ya kuuza ama kugawa ardhi ya eneo lile kwa ajili ya kufanya fidia ya pesa ambayo walikikopesha kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Taifa kama Tanzania lenye Serikali kubwa kama yetu, Wabunge wengi, Wakuu wa Wilaya wengi kwamba leo tunaweza tukadiriki kuanza kuwa na *proposal* ya kuhakikisha kwamba Tanzania kunakuwa hakuna kiwanda

cha matairi na badala yake tunategemea matairi yanayotoka nchi nyingine za jirani. Kwa kuwa pesa zilikwishatolewa zaidi ya dola milioni moja kwa ajili ya *revival*, bilioni moja kwa sababu ya ushauri, mimi naiomba Serikali iwafafanulie Wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini na Wananchi wa Tanzania kwamba pesa hizo zilikwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa zilizopo ni kwamba, aliyekuwa Mkurugenzi ama aliyekuwa Meneja wa Kiwanda hicho alidiriki kutumia pesa nyingi, zaidi ya dola milioni moja kukaribisha ndugu zake kutoka nje na kwenda Ngorongoro na Serengeti kuangalia Twiga wakati kiwanda hakina kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hilo kuna wafanyakazi wengi pale ambao walikuwa wakifanya kazi hawakulipwa mafao yao pale, wakati *General Tyre* inafanya kazi kipindi hicho cha miaka ya nyuma ilikuwa inaajiri kati ya watu 400 mpaka 470 na mahitaji ya matairi yalikuwa ni mahitaji machache sana kwa sababu Tanzania ilikuwa haina magari mengi kama ilivyo sasa. Leo ukienda Arusha Mjini ama ukienda Dar es Salaam, Morogoro au Mbeya, utagundua kwamba, *demand* ya matairi imeongezeka sana kwa sababu watu wanaotumia magari kwa sasa mijini ni wengi, kwa sababu tuna asilimia kubwa ya watu ambao ni *middle class* na *working class* ambao wamethamini sana usafiri wa magari. Ninajiuliza ni kwa nini Serikali sasa isichukue hatua za msingi kukifufua Kiwanda cha *General Tyre* kwa sababu mahitaji ya matairi ni soko kubwa na tunanunua matairi mengi sana kutoka nchi za nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi kupata mwekezaji kama atahakikishiwa kwamba matairi yote ya Taasisi za Umma na Serikali yatanunuliwa kutoka katika Kiwanda cha *General Tyre*, tayari inamshawishi mwekezaji kuja kuwekeza kwa sababu tunakuwa tumeshamtengenezea nafasi ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufisadi na kuangalia *the way forward*, mimi ningeomba wale wote waliojishughulisha ama waliohusika katika ufisadi wa Kiwanda cha *General Tyre* mpaka leo kunakuwa na *proposal* ya kuuza eneo lile, wapo wanajulikana, siyo kwamba ni siri, washughulikiwe mapema kwa sababu pengine tusipowashughulikia mapema wanaweza wakafariki ghafla kwa sababu ya tukio la leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba washughulikiwe mapema siyo kwa maana ya kurudisha zile pesa lakini kwa maana ya kuwa na Serikali ambayo itakuwa na nidhamu kwenye matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba pia nichangie Taarifa ya Mheshimiwa Mrema, Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* kwamba, wizi katika Halmashauri zetu ni mkubwa sana. Nilishangaa sana kusikia kwamba, eti kuna Halmashauri moja pikipiki imetumia *diesel* lita elfu moja. Kwanza, pikipiki hapa Tanzania inayotumia *Diesel* ni ipi? *Diesel* lita elfu moja ni mafuta mengi sana, pesa zinatumika nyingi, Halmashauri zina ufisadi mkubwa kama ambavyo ripoti ilisomwa hapa. Waziri katika Ofisi ya Utumishi, aliongea leo asubuhi, nilisikitika kidogo kwa sababu ni kama aliwa-*promote* wale watu wanaofanya ufisadi ndani ya Serikali kwamba,

yawezekana watu wakawa na kesi Mahakamani lakini vile vile wakaendelea kuwa wanawajibika katika ngazi za kazi katika idara tofauti wakati wakiwa wameshtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba kwamba, yafanyike marekebisho ya Sheria kwa Mtumishi yeyote wa Umma atakayetuhumiwa kwa ubadhirifu wa aina yoyote ile, asiendeleo kuwepo kazini mpaka tatizo lake litakapokuwa limekamilika. Vinginevyo, kwa hotuba ya leo ambayo imesikilizwa na watu wengi, maana yake ni kwamba, tunaweza tukawa tume-*entertain* vitu ambavyo vinaweza vikalisababishia Taifa hili hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo machache, ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia Taarifa hizi tatu za *PAC*, *POAC* na *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimtazamo na mwelekeo, Watanzania walio wengi na hasa maskini, wamechoka kusikia fedha zao zinaendelea kuibiwa na wajanja wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi walidhani baada ya Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 18 hapa Bungeni Dodoma, kwamba, wizi, ubadhirifu, uzembe na ufisadi hautavumiliwa. Rais aliendelea kusema kwamba, tutakuwa wakali sana. Jambo la kushangaza ni kwamba, tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotoa maelezo hayo, bado Watanzania hawajasikia ni watu wangapi wamechukuliwa hatua za kinidhamu ambao wamebainika wazi wakitumia vibaya fedha za Halmashauri au Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambayo imetolewa hivi punde na watoa taarifa, kuna mishahara ya jumla ya shilingi milioni 792 imetolewa kwa watumishi hewa. Tulidhani basi Serikali kabla ya hapo ilikuwa itoe maelezo sahihi kabisa kwamba, watu au aina gani ya watu na wako wapi na hatua gani ambazo zimechukuliwa dhidi yao. Vilevile kuna mishahara ambayo haikurejeshwa Hazina kiasi cha shilingi bilioni 1.7, taarifa imetolewa haikurejeshwa imekwenda wapi; na kwenye mikono ya nani? Huu ni ufisadi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anaposema wizi, ubadhirifu, uzembe na ufisadi, kwa ujumla hautavumiliwa, lakini bado kuna wajanja wachache wanatumia fedha za umma na Serikali imekaa kimya! Sisi kazi yetu kama Wabunge, kwa mujibu wa Katiba, ni kuisimamia na kuishauri Serikali lakini Serikali ambayo itakubali kweli kushauriwa; hilo ni suala la msingi. Ukiangalia taarifa mbalimbali ambazo zimetolewa, inaonekana waziwazi kwamba, mwaka 2006 hadi 2009 kuna watumishi wapatao 921 walifikishwa mahakamani kwa ubadhirifu wa mamilioni ya fedha, lakini hakuna hata mmoja ambaye alifungwa. Watumishi 14 ndiyo angalau walishushwa madaraka, lakini wengine walipewa uhamisho. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hivi sasa wamekata tamaa, kwa sababu wao ni walipa kodi maskini, mara nyingi wanapewa msukumo wa kulipa kodi, lakini fedha zao jinsi zinavyotumika kwa kweli ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wanaoendelea kuiba wana sababu zao, wameiga wanaona hakuna kinachofanyika. Kama kweli inaonekana kitu kinachofanyika wasingendelea kuiba, lakini kuanzia mwaka 2001 mpaka 2005, zaidi ya shilingi bilioni 4.403 ziliibiwa. Serikali ndiyo ilileta taarifa hapa Bungeni kwa kiini macho au changa la macho ikasema kwamba, fedha hizi hazikupatikana kwa sababu wahusika wametoroka; wengine wamefariki na mwingine sijui alifia Marekani; na wengine hakuna hata vilio hatuna taarifa yake yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikifikia wakati kama Serikali inakwenda kushtaki mahakamani kesi 321, lakini hakuna kesi Serikali iliyoshinda hata moja; hapa pana kiini macho. Naiomba Serikali kama kweli wajibu wetu na ndiyo wajibu wetu sisi kama Wabunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikubali kwamba, upungufu unaotokea hasa matumizi mabaya ya fedha za umma, wahusika wakamatwe wapelekwe mahakamani ili Wananchi wapate angalau imani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu Serikali inakuja hapa Bungeni na mkakati wa misamaha ya kodi asilimia 18, Tanzania yenyewe ina tegemezi 28. Ukiangalia taswira au picha kwa ujumla utaona kwamba, sisi tuna vivutio vingi kabisa vya uwekezaji; tuna madini, tuna ardhi na maliasili nyingine, lakini tunachokifanya hivi sasa kwa kuwa bajeti yetu ni tegemezi, tunakula hasara kubwa sana. Wenzetu Kenya na Uganda hawajafikia hata asilimia tano ya misamaha ya kodi, wao wana vivutio vidogo sana vya uwekezaji. Hili nalo linapaswa kuangaliwa kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina kigugumizi gani; hivi kila siku sisi Wabunge tunapotoa malalamiko ya kupotea kwa mabilioni ya fedha ni kwa nini hazichukuliwi hatua za kisheria? Hivi Mheshimiwa Rais anaposema kwamba taarifa hata zile Ripoti za Mdhumbi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitapewa uzito unaostahili; kauli ya Mheshimiwa Rais tunadhani ikitolewa basi utekelezaji utakuwepo. Kwa masikitiko makubwa, hali ya maisha ya Watanzania inaendelea kuwa mbaya, hata Watendaji wanaochukua hizo fedha hakuna wanaowajibishwa; ni shamba la bibi kila mtu anavuna anachotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna fedha ambazo zimegundulika shilingi bilioni 12.8 katika manunuzi ya mambo mbalimbali kwa mwaka 2008/2009 zimetumika vibaya. Hili liligusiwa kidogo hapa. Pamoja na kuoneshwa njia, waliohusika ni akina nani; bado Serikali haichukui hatua zozote. Ningependa nihoji mabilioni yote ya fedha haya yanapotea ukiachia huyu ambaye amekufa huko Marekani, ambaye kwa mujibu wa sheria haipaswi kuzungumza amefariki; ni wahusika wangapi ambao wamefikishwa mahakamani na kuchukuliwa hatua za kinidhamu?

Watanzania na Wabunge tutaendelea kulalamika mpaka lini; hivi sisi wajibu wetu wa kuishauri Serikali unazingatiwa kiasi gani? Kwa kweli ni kilio kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani wakati umefika, Serikali isikilize kilio cha Waheshimiwa Wabunge, lakini kauli za kijumla zilizotolewa na Serikali kupitia Mawaziri wetu humu Bungeni kwamba, Serikali ni sikivu imesikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge, mambo tunayoyashughulikia mipango kabambe iko mbioni, nia ni njema, vuta subira hadi mchakato utakapokamilika, hautufikishi mahali popote pale. Hizi ni lugha za kijumla jumla, michakato isiyoisha siku zote umaskini Tanzania unapaa; ni vema tukae tuambiane ukweli, ukienda vijijini Watanzania ni maskini sana, umaskini umekithiri, umaskini unapaa, lakini michakato isiyoisha na upembuzi yakinifu kwa siku zote Wananchi wanaendelea kuumia; hili ni tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi ujumbe wangu kwa Serikali kwa leo na wale waliowasilisha ndio huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, nina tangazo; naomba kuwatambulisha wageni ambao wako kwenye *Galley* jioni ya leo, ambao ni Maafisa wa Habari, Elimu na Mawasiliano; ninaomba msimame wote hapo mlipo. Wako 89 kutoka Wizara, Idara, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikali ambao wanaongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Bwana Clement Mshana. Karibuni sana Bungeni, tunawakaribisheni na tunatumaini mtafanya kazi nzuri mkiwa hapa Dodoma.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mada iliyoko Mezani, hususan katika Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*). Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na Wapigakura Umoja wa Wanawake wa Tanzania Mkoa wa Pwani kwa kuniwezesha kwa mara ya kwanza kuwa Mbunge katika Bunge hili tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya *LAAC*, lakini niliona nichukue fursa hii nichangie katika maeneo machache ambayo ninaamini yanachangia katika kuona Halmashauri zetu zinakuwa na matumizi mabaya pia makusanyo hafifu ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Ripoti ilivyowasilishwa asubuhi ya leo ni kwamba, tumekuwa tukiona upungufu mbalimbali katika eneo la matumizi ya fedha za Serikali na mapato katika Halmashauri za Mitaa. Mawazo yangu ni kwamba, upungufu huu unachangiwa na udhaifu wa Wakaguzi wa Hesabu za Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakaguzi wa Hesabu za Ndani wapo kwenye Halmashauri kwa mwaka, lakini utashangaa kuona kwamba, kadiri miaka inavyoendelea upungufu huu unaongezeka. Utaona katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka huu kwamba, maeneo ya makusanyo ya mapato

yasiyorejeshwa kwenye Halmashauri na maeneo ya upungufu wa nyaraka za matumizi, yamekuwa yakiongezeka mara kwa mara. Utashangaa CAG anakwenda pale kwa muda wa wiki tatu tu, lakini Mkaguzi wa Ndani yupo kipindi chote na wapo baadhi ya Wakaguzi wa Ndani wamewezeshwa vizuri, lakini utashangaa upungufu huo umeendelea kujitokeza mara kwa mara.

Katika eneo hili, natambua jitihada za Serikali na naipongeza sana kwa kukubali kuanzisha nafasi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani atakapoteuliwa, ninashauri eneo la kuanzia kufanya kazi liwe ni kutafuta kiini cha kushindwa kuwajibika ipasavyo kwa Wakaguzi wa Hesabu wa Ndani.

Pia natambua Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi ya Wakaguzi hawa wa Ndani, lakini pia bado hawajajipanga vizuri. Kwa hiyo, naamini hata kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia kwa mujibu wa Taratibu za Ukaguzi wa Kimataifa ni lazima ategemee wakati mwingine Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu wa Ndani. Kwa hiyo, tukikiimarisha kitengo hiki na kwa mipango ambayo Serikali imejipangia, ninaamini upungufu unaojitokeza kwenye Halmashauri zetu ama kwa hakika unaweza ukapungua siku za usoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie katika eneo la fedha za maendeleo zinazopelekwa kwenye Halmashauri. Katika eneo hili naomba Serikali itambue kwamba, inatumia utaratibu wa *cash budget* na inategemea makusanyo ya mapato ya Serikali Kuu. Ninawaomba hata wale wafadhili wetu wanaotufadhili Miradi hii, wawasilishe fedha hizi mapema kwenye ngazi ya Halmashauri ili Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa kipindi hicho itekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeomba nijielekeze ni namna gani watunza hazina wetu wa Halmashauri wanavyowajibika. Katika kupitia Hesabu za Halmashauri tumegundua kwamba, waweka hazina wengi hawawajibiki na wapo wenye elimu za kutosha, wapo wenye *CPA* wapo wenye *MBA*, lakini utaona taarifa inayowasilishwa TAMISEMI au kwenye Mabaraza ya Madiwani, inayowasilishwa kwa CAG, inayowasilishwa hata kwenye Kamati ya LAAC, taarifa hizi hazishabihiani kabisa. Kwa hiyo, ni wazi kabisa suala si kwamba hawana elimu, lakini dhamira njema.

Ninaamini wakiwa na dhamira njema, wanaweza wakafanya vizuri na fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zikatumika katika maeneo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, niombe kwa Waheshimiwa Wabunge wenzagu, kazi ya kupambana na matumizi mabaya ya fedha za umma si kazi ya Bunge peke yake, lakini pia ni kazi inayohitaji wadau mbalimbali kuweza kusaidiana.

Ninaamini Waheshimiwa Wabunge sisi sote ni Madiwani katika Halmashauri zetu, basi tutenge muda ambao tutaweza kushiriki hasa kwenye vile vikao muhimu; kwa

mfano, Kamati ya Fedha, Baraza la Madiwani tuweze kusaidiana nao katika kuchambua taarifa mbalimbali zinazowasilishwa kwenye Halmashauri hizo, kwa sababu ninaamini kumsubiri Mdhambi anayekuja baada ya mwaka wa fedha kupita zaidi ya miezi 12, kuisubiri Kamati, kwa mfano, leo tuko 2011 tunajadili Ripoti ya Mwaka 2008/2009, miaka miwili iliyopita; lakini sisi tupo kwenye Mabaraza basi tuweze kushirikiana nao pamoja ili upungufu mwingine tuweze kuubaini na kuweza kuushughulikia haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango wangu huo, naunga mkono hoja na ninashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu; kwa kweli umeongea vizuri sana pamoja na kwamba ni mara ya kwanza.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Tunapozungumzia matumizi ya Serikali katika dhana pana tunazungumzia uwezo wa Serikali kutawala. Tunapozungumzia uwezo wa Serikali kusimamia matumizi, tunazungumzia uwezo wa Serikali kutawala. Ningependa nianze na hiyo ili tujipime kama Serikali yetu ina uwezo wa kusimamia rasilimali zetu au inashindwa kusimamia rasilimali zetu.

Ninazungumza haya kwa machungu kwa sababu ukisoma Taarifa ya CAG, kama Serikali inahitaji *constructive position* basi Ofisi ya CAG ndiyo Chama cha Upinzani ambacho ni *very constructive*. Bahati mbaya sana ni kwamba, Serikali pamoja na kujiita ni sikivu, lakini bado inashindwa kutekeleza yale ambayo yanapendekezwa na CAG na zaidi hata pale ambapo Kamati za Bunge zinapotoa mapendekezo yake. (*Makofi*)

Nitaanza na moja; nimesoma Taarifa ya PAC wanazungumzia GN Namba 22 iliyotolewa na Wizara ya kufuta GN Namba 99 ya kufuta GN Namba 22 ambapo mwaka 1999 tukiwa na GN Namba 22, Migodi ya Madini ilikuwa inaruhusiwa kutoa dola 200,000 lakini baada ya mwaka wa kwanza inaendelea kulipa kwa mujibu wa sheria.

Mwaka 2005 Waziri wa Fedha akabadilisha ikapelekwa GN Namba 99 na kufuta GN Namba 22, ambayo zaidi tu ya kuifuta lakini vilevile ilifuta Sheria yenyewe ya Makampuni haya kuweza kutozwa ushuru wa mafuta.

Ukisoma Ripoti ya Bomani, *impact* sasa ya uamuzi huo, kwa mujibu wa Ripoti hiyo; miaka mitatu tu mwaka 2005/2006 tulipoteza bilioni 32, mwaka 2006/2007 tulipoteza bilioni 59 na mwaka 2007/2008 tulipoteza takriban bilioni 90 kwa sababu ya uamuzi huo. Imezungumzwa hapa kwenye Bunge la Tisa, wengine tulikuwa hatujaingia Bungeni kwamba, GN Namba 99 ifutwe ili Serikali iweze kupata fedha hizo. Mpaka leo Serikali haijafuta.

Kibaya zaidi, uamuzi huo wa mwaka 2005 wa kuyasamehe makampuni haya ya madini kuweza kulipa ushuru Serikalini, badala ya kusema uanze mwaka 2005 na kuendelea, ukaanza mwaka 1999 na kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo mambo ambayo yanasababisha hasira kwa Wananchi. Kwa nini Serikali haichukui hatua? Ninajua Waziri mhusika leo hayupo hapa; Waziri aliyefanya uamuzi huo, Waziri yupo kwa maana ya Ofisi ipo, lakini pengine Waziri aliyehusika moja kwa moja leo hayupo.

Kwa mujibu wa Sheria, uamuzi huu kimsingi ulitoshwa kabisa kuwa jinai, ulitoshwa kabisa mtu huyu kufikishwa mahakamani na kama ana kesi mahakamani aongezewe shitaka lingine. Hatuwezi kupoteza bilioni 181 haiwezekani; ni fedha nyingi sana. Sisi Watu wa Kigoma leo tunazungumza Reli ya Kati kufanyiwa matengenezo ya muda mfupi tu walau tupate unafuu wa usafiri wa reli; ni bilioni 63 kichwa mgogoro; lakini kuna fedha zinapotea tu na hakuna hatua ambayo inachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo yanawafanya Wananchi wakasirike na waone kwamba, Serikali inashindwa kusimamia nchi yao. Mheshimiwa Cheyo, amejaribu kuonesha hapa ni kwa namna gani Serikali inaacha baadhi ya vyanzo vya mapato na kushughulika na mapato ambayo kimsingi kwanza ni kero kwa sababu ni kodi ambazo zinakera Wananchi.

Kuna kitu kinaitwa *capital gain tax*, hii ni kodi ambayo mashirika kama ya VODACOM walipowauzia VODAFONE walipaswa walipe *capital gain tax* ndani ya nchi yetu, lakini bahati mbaya sana kwanza hatujui hata mtaji wenyewe wana kiasi gani, kwa sababu ya udhibiti duni na zaidi tunashindwa kuibana kampuni ambayo imo ndani ya nchi yetu.

VODACOM wanawauzia VODAFONE mtaji wao, lakini baada ya hapo Serikali inashindwa kuwatoza kodi ambayo ipo kisheria. ZAIN wamewauzia Airtel; ni bilioni ngapi ambazo Serikali inazikosa kwa kushindwa tu kuwatoza kodi?

Serikali hii inashindwa kuwatoza hawa kwa misingi gani wakati sheria zinaruhusu? Je, ni makusudi tu au kuna nguvu ya ziada ambayo inaifanya Serikali isitoze kodi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado mambo ambayo yanawafanya Watanzania waone kwamba Serikali yao inashindwa kuwatumikia. Mheshimiwa Cheyo asubuhi alipozungumza kwamba inabidi Serikali kutawala, kutawala siyo kuzuia maandamano tu, kutawala ni kusimamia rasilimali, hivi vyanzo ambavyo vinapotea ndio misingi ya kushindwa kutawala. Kwa hiyo, tunahitaji Serikali ianze kuwajibika. Kama inahitaji *constructive opposition* na *constructive ideas* vitabu ya CAG viko wazi. Kuna mapendekezo ambayo yametolewa tangu Bunge la Tisa mpaka leo hayatekelezeki, watu wanaiba mabilioni ya shilingi lakini Serikali inasema taratibu za kiutumishi zina urasimu kuna hiki na kile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Spika wa Bunge la Tisa aliwaambia wakati Rais anahutubia ndani, alimwambia kwamba Mheshimiwa Rais kama kuna sheria zinasababisha tatizo la uwajibikaji kwa hawa watu ambao wanapora mali za nchi ziletani,

sisi Wabunge si ndio wenye sheria. Kama kuna tatizo na sheria za utumishi ambazo zinasababisha Serikali ishindwe kuwabana hawa watu ambao wananyonya uchumi wetu zileteni Mbunge gani atakataa kupitisha hapa? Wabunge wote watapitisha. (*Makofi*)

Lakini kwa sababu ambazo pengine Serikali inazijua yenyewe tumbaki siku hadi siku tunaambiwa tu taratibu za utumishi mtu anaiba Halmashauri ya Same anapelekwa Halmashauri ya Kasulu anaiba Halmashauri ya Kasulu anapelekwa Kigoma Kusini. Yaani mwizi aliyeiba Halmashauri moja anapelekwa Halmashauri nyingine.

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mbunge aliyekuwa anaongea sasa anasema kwamba Serikali yetu haitozi *capital gains tax* na anasema kwamba ni kwa mujibu wa Sheria isipokuwa Serikali yetu inafanya uzembe.

Napenda nimjulisha kwamba katika nchi yetu Sheria ya *Capital Gains Tax* kwa sasa hakuna inayoyabana makampuni ambayo yanafanya biashara ya kuuzia makampuni ambayo yako Tanzania lakini biashara inafanyika nje ya Tanzania. Kwa hiyo, napenda nimpe hii taarifa asifikiri kwamba Serikali inafanya uzembe labda tu kama angeweza kuja kuleta ombi la kurekebisha sheria ili biashara zinazofanyika nje kuhusu makampuni ya ndani waweze kutozwa *Capital Gains Tax*. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokizungumza hapa kimefanyiwa utafiti, anayezungumza alete hiyo sheria hapa Bungeni. Siyo unaokota *information* halafu unazungumza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Mimi mchango wangu nitaelekeza zaidi kwenye Bajeti ya Serikali na hasa miradi mingi inakwama kutekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Wakati tunajaribu kuchangia pale mwanzoni ukitazama Bajeti yetu tunatumia asilimia 60 kwa fedha za ndani. Asilimia 63 kwa maana ya mikopo ya ndani na mapato tunayokusanya kutoka ndani. Lakini asilimia 37 inatokana na asilimia 15 ambayo ni mikopo ya nje na asilimia 22 ambayo ni misaada.

Lakini ukitazama miradi mingi ambayo inatumia fedha za nje utekelezaji wake umekuwa ni mgumu sana ukilinganisha na miradi ambayo inatumia fedha za ndani. Tumeshuhudia kwenye ripoti ya *PAC* tumeona miradi mingi kama wa *Lake Victoria* kuleta maji Shinyanga umetumia zaidi ya shilingi bilioni 240 ambazo ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika asilimia 37 ambayo tunasema kwamba tunapokea kutoka nje fedha ambazo Serikali inazipokea ukiangalia kwa ujumla ni asilimia 50 tu. Ukitazama kwa mwaka 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 mpaka 2009/2010 ni asilimia 50 tu fedha ndizo zinazopokelewa na Serikali. Kwa kufanya hivyo

maana yake zile *commitment* ambazo Serikali inakuwa imeingia tunashindwa kuzitekeleza.

Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali tuanze kidogo kidogo sasa kutumia fedha zetu za ndani kwenye miradi na nina hakika tutaweza kukamilisha miradi yetu. Nasema hivyo kwa sababu leo hii kwenye Wizara ya Ujenzi Serikali inaingia hasara zaidi ya shilingi bilioni 123 ambazo zinatokana na miradi ambayo Serikali imeingia na wakandarasi mbalimbali, watu wanafanya *mobilization* wakitegemea watalipwa. Lakini kwa ucheleweshaji wa fedha tunashindwa kulipa na hatimaye tunapelekwa mahakamani ama tunalipa tozo kwa wakandarasi.

Sasa ukiangalia ule mfumo ambao Serikali inatumia wa *cash budget* nina hakika hata hizi asilimia 63 ambazo Serikali yetu inachangia kwenye Bajeti kutokana na mapato yetu sisi wenyewe itapanda mpaka itafikia asilimia 82 kama Bajeti ya Serikali kwa mapato yetu ya ndani na mikopo ya ndani. Ukichukua kiwango na wastani tunazipokea kutoka nje. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutakuwa na Bajeti halisi ambayo tutaweza ku-*fulfil commitment* ama miradi yote ambayo tunaifanya kuliko hivi sasa tunakuwa tuna *figure* kubwa sana lakini kiukweli fedha tunazokuwa nazo ni kidogo na Waheshimiwa Wabunge kweli wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inapoweka *target* kwa *TRA* ya makusanyo ya mwaka ni vyema Serikali ikae na *TRA* wakubaliane. Lakini kwa hivi sasa inavyofanyika ni kwamba Serikali yenyewe inapeleka kwa *TRA* inawapa makisio wakusanye kiwango fulani cha fedha ambacho *TRA* wanashindwa kukusanya.

Mimi imani yangu kwamba *TRA* bado wana nafasi ya kukusanya fedha zaidi endapo watadhibiti mianya kwa maana ya *revenue leakage* ambazo zipo, kwa sasa tumeziona kwenye sekta kwa mfano za migodi kuna mianya mingi ya watu kukwepa, wiki mbili zilizopita imeripotiwa hata Shinyanga pale almasi ya thamani kubwa *karate* 176 imepatikana lakini kodi haijalipwa. Tumeona na maeneo mengine kama kwenye *telecom* Mheshimiwa Kafulila alikuwa anaeleza hapa *capital gains tax* ukiangalia kweli *Vodafone UK* imenunua asilimia 65 za *Vodacom South Africa* kwa hiyo, *ownership* pale imebadilika, lakini *Vodacom Tanzania* ambayo wao wanakuwa wanajibika kwa *Vodacom South Africa* sisi ambao wana-*operate* hapa tunanufaika na nini? Ukiangalia kwenye mikataba hata ya wacheza mpira kama timu ndogo ya Tanzania imemkuza mchezaji akaenda timu moja ya wastani Ulaya anapokwenda kwenye timu nyingine ya juu bado ile timu iliyomkuza huku chini na yenyewe inanufaika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, bado na mimi naona Serikali bado ina nafasi ya kupata kodi kupitia mashirika ya simu. Lakini tatizo labda tuangalie je, *TRA* imejiandaa kikamilifu ku-*control* mifumo inayotumika ya kudhibiti mapato kwenye mashirika yale kwa maana ya *human resources* tunayo? Kwa sababu *TRA* kwa sasa inapokea taarifa zinazoletwa na *tax payer* lakini yenyewe haina mfumo wa-*control* kuona hii taarifa tunayoletewa iko sahihi au kuna fedha zingine zimechenga?

Kwa hiyo, ni vyema *TRA* ikajiimarisha kisayansi kwa maana ya teknolojia na wafanyakazi kwa maana *human resources and technology* wawe na uwezo wa ku-*monitor* na kuona kwa mwezi, kwa mwaka kampuni hizi zinaingiza kiasi gani ukilinganisha na kile ambacho wanalipa kwenye *corporate tax*. Kwa kufanya hivyo nina hakika mapato yetu yataongezeka na sio kusubiri taarifa za mlipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kwenye deni la Taifa. Ukilitazama deni la Taifa sehemu kubwa Wizara kwa mfano ya Elimu walimu wanadai fedha nyingi kwenye deni la ndani, kwa mfano Jeshi la Polisi peke yake linadai zaidi ya shilingi bilioni 25 kama malipo yanayopaswa kulipwa kwa askari wanapohamishwa, walimu pia wanadai fedha nyingi. Mimi naiomba Wizara ya Fedha iweke kipaumbele cha kulipa madeni haya ya ndani. Kwa kufanya hivyo itakuwa siyo vizuri kuwakopa wafanyakazi wetu. Askari wale wanapokwenda kufanyakazi anahamishiwa kituo amekopwa hata *morale* yake ya kufanyakazi inashuka. Tunaweza kulipa mambo mengi sana kwa fedha nyingi lakini tuweke kipaumbele kuhakikisha madeni ya ndani ya wafanyakazi hasa polisi, walimu yanalipwa. (*Makofi*)

Lakini pia kwenye kudhibiti Deni la Taifa na hasa sehemu ya dhamana nilikuwa naomba Waziri wa Fedha azingatie sheria ya fedha ya mwaka 1974 ya mikopo. Anapofanya maamuzi ya kutoa dhamana kwa mashirika ya umma. Tumeona Mashirika mengi ya Umma yameitia hasara kubwa Serikali kwa kupewa midhamana na baada ya miaka miwili yanakufa. Lakini kwa taratibu zilivyo na sheria inavyoelekeza Waziri wa Fedha kabla hajafanya maamuzi ya kutoa dhamana ni lazima apate ushauri wa Kamati inayosimamia mikopo. Kamati ile ina Kamati ya Ufundu ambayo ndio inatoa ushauri wa kiufundi kwamba Shirika hili ninapolikopesha litalipa? Lakini tumeona mashirika mengi kama *TFC* na mengine yamepokea mikopo lakini yameshindwa kulipwa na mzigo wote umehamia Serikalini. Sheria ile inajitosheleza lakini Waziri lazima aizingatie na aifuate, hata kama ni maelekezo ya Baraza la Mawaziri ni vyema sheria na taratibu za mikopo na dhamana zifuatwe. Rais akielekeza jambo hamaanishi uvunje sheria, anakuelekeza jambo ulifanye lakini kwa kuzingatia sheria iliyopo ili kufanya mambo yote yafuate taratibu na sheria ya mikopo ya mwaka 1974 na iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bodi ya mikopo kusema kweli Serikali sasa hivi inatumia shilingi bilioni 237 kwa kulipia mikopo ya wanafunzi. Kila mwaka *speed* inaonyesha wanafunzi wataendelea kuongezeka. Kamati imependekeza hapa, nilikuwa naomba Wabunge wapokee mapendekezo haya tuanzishe *education levy* ili kusaidia bodi ya mikopo iweze kuwa *sustainable, otherwise* tukifikisha wanafunzi 100,000 na wote wakapokea shilingi 10,000 kwa siku, Serikali itapaswa itumie shilingi bilioni moja kwa kila siku kuhudumia wanafunzi wa elimu ya juu ambapo itachukua sehemu kubwa ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na kuacha Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari ikiwa haina kitu.

Kwa hiyo, ni lazima tuweke mkakati wa ku-*control* kwanza ongezeko la wanafunzi linavyokwenda, tuweke vigezo ambavyo tutadhibiti na ku-*control*, kama ni *academic criteria* zinatumiwa, basi zitumike wapate mikopo wanaostahili kupata mikopo.

Lakini kwa *current trend* inavyokwenda bodi ya mikopo *very soon* itakuwa siyo *sustainable*, hatutaweza kumudu kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Asante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana kwa Bajeti ya muda. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini awali ya yote naomba niwapongeze Wenyevit wote wa Kamati tatu kwa uwasilishaji wao wa taarifa nzuri na zenye uchambuzi wa kutosha kabisa. (*Makofi*)

Naamini kwamba Serikali itasikiliza kwa sababu Wabunge waliopita wamezungumza taarifa ya *CAG* inazungumza kila mwaka mapendekezo mazuri yenye lengo la kujenga nchi yanatolewa lakini cha kusikitisha linapokuja suala la utekelezaji mambo yanakuwa hayasogei, sasa tatizo sijui liko wapi. Tunatekeleza wajibu wetu wa kuisimamia na kuishauri Serikali, Serikali inasikiliza na inaweka kwenye Kabati. Tunaomba msikilize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumza kwa uchache na nitaanza na masuala mazima ya uhai wa Mashirika yetu ya Pensheni. Hakuna ubishi juu ya mchango wa Mashirika ya Pensheni katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Sote tumeshuhudia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo katika kampeni za mwaka jana CCM walikuwa wanatumia kama mzizi wa kutafutia kura. Yamefanyakazi kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa la Serikali linajua kuchukua fedha kwenye mifuko, linapokuja suala la kurudisha fedha ile mifuko iwe *sustainable*, ili mifuko yetu iweze kufanyakazi kubwa za maendeleo kama ambayo tumeambiwa wanataka kushiriki *project* za umeme inakuwa ni tatizo. Kuna utafiti ulifanywa *actuary evaluation* ili kujua uhai wa mifuko yetu. Wakati Mwenyekiti wa *POAC* akizungumza asubuhi alizungumza ni kwa namna gani Kamati yake walitumia nguvu wakaweza kuliokoa Shirika la *PSPF* lisife. Shirika husika lilikuwa *li-collapse* mwaka 2011 Mfuko huu ulianzishwa rasmi mwaka 1999 kuchukua nafasi ya Mfuko ambao ulikuwepo. Serikali iliji-*commit* kuhakikisha kwamba wale wastaafu ambao walikuwepo kabla ya mwaka 1999 ambao walikuwa hawachangii gharama za pensheni Serikali ingekuwa inapeleka fedha *PSPF* ili wastaafu waweze kulipwa mafao yao. Serikali kama ilivyo kawaida haikutekeleza hilo. (*Makofi*)

Mwaka 2007 Serikali ilifanya *actuary evaluation* juu ya uhai wa mifuko ikagundua kwamba kutokana na Serikali kutokupeleka fedha *PSPF* kuna deni la shilingi trilioni mbili *point* kadhaa. Leo (miaka mitano) baadaye tumeambiwa limekaribia shilingi trilioni 3 Serikali imeji-*commit* juzi kutoa shilingi bilioni 700 kwa kuanzia ni jambo jema na tumeambiwa imetoka shilingi bilioni 30 tunaomba isiishie hapo, tuokoe mashirika yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Serikali haya mashirika tukiyalinda na kuyatunza *PSPF* ndio mhimili wa wastafu wote wa *central government*, ni mhimili wa wastaafu wa hizi *agency za central government* tunasikia kero za wastaafu kila siku Mfuko uki-*collapse* tutafika, nchi itakwenda wapi? Mfuko wa *Local Government* tunaambiwa leo michango ikisimamishwa mwaka 2018 mfuko una-*collapse*. Sasa hatutarajii yatokee kama yaliyotokea kwenye *PSPF* tunasubiri mpaka *last minute* mfuko unakwenda kumpa shilingi bilioni 30 kwenye Mfuko wa Hifadhi wa Jamii *is nothing*. Kwa hiyo, sisi tunaomba nchi yetu sote mwaka 2009 iliji-*commit* kuiokoa *PSPF* haikufanya hivyo, mwaka 2011 tunaambiwa mmetoa shilingi bilioni 30 muendele kutoa haya matrilioni mnayodaiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamezungumzia ni kwa namna gani hakuna uwajibikaji wa Bodi za Mashirika ya Umma. Leo tukiwauliza Wajumbe wa Kamati ya *POAC* pamoja na kazi nzuri wanayoifanya hebu tutajieni katika haya Mashirika mnayoyasimamia Shirika gani linaendeshwa kwa faida sijui hata kama yatafika matano. Lakini wakati huo huo tunajua kwamba Serikali ime-*invest* zaidi ya *seven trillion* kwenye mashirika haya. Kinachotokea ni nini wenzetu wanaopewa fursa ya kuyaendesha hayo Mashirika wanaona ni sehemu yao ya ulaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siyo fursa ya kuyaendesha mashirika hayo. Wenzetu wanaopewa fursa ya kuyaendesha hayo mashirika wanaona ni sehemu yao ya ulaji. *CAG* amekuwa anapendekeza kila mwaka kwamba Serikali iingilie makubaliano na Bodi za Mashirika za ku-*perform* tufikie malengo haya, mkishindwa kufikia malengo haya imeondolewa hoja nyingine ambayo wanaibia hizi mpya. Lakini siku hizi Bodi ni kama ni *fashion* tu. Ukipewa miaka yako mitatu hata ukila weee, una uhakika iishe hadi mwingine, ifike sehemu tuwajibike. Ushahidi ni lile deni ambalo walikopa Bodi ya Mikopo mwaka 2006 toka *PSPF* ambayo inakufa la shilingi bilioni 58 hazijalipwa hadi leo. Bodi husika licha ya kwamba sera ya chombo inasema kwamba *limit* ya kutoa fedha ni shilingi bilioni 30 sijui kwa *pressure* za Serikali sijui kwa *pressure* za nini, wakaidhinisha shilingi bilioni 60, baadaye wanakuja kubadilisha *policy* ili kwenda kukidhi zile fedha walizotoa, aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tubadilike, kama tunawaambia Watanzania kwamba nyie ni wasikivu, basi mtusikie na sisi wawakilishi wao, maana sauti zetu sisi ndiyo sauti zao, sijawa na mapendekezo mazuri sana. Sasa sijui hatusomi, maana yake Watanzania tuna uvivu wa kusoma, pengine unakuta ripoti zinakuja zinawekwa kabatini, kumbe kwa kutumia ripoti ya *CAG* tungeweza kuibadilisha nchi, kwa kutumia mawazo ya Wabunge tungeweza kuibadilisha nchi.

Mheshimiwa Naibu spika, mimi mwaka wangu wa sita huu, kila siku Wabunge wanalalamika jamani Mkurugenzi wa eneo fulani ameiba kule ameletwa kwangu, Wakurugenzi ni matatizo, sisi tuko kwenye Manispaa zetu huko ukim-*face* Mkurugenzi hashikiki. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa January Yusuf Makamba na Mheshimiwa Murtaza Mangungu, ajiandae. (*Makofi*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Asante, Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ningependa kuwapongeza Wenyevitani wa Kamati zote tatu kwa kutuwasilishia taarifa dhidi ya ufuatiliaji zaidi wa fedha za umma, lakini kubwa tunahitaji kuangalia zaidi mapungufu kwa sababu mafanikio tutakwenda zaidi katika kuyarekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza na baadhi ya vipengele. Lakini jambo la kwanza ni kwenye suala zima linalohusu fedha za utawala kwamba asilimia kubwa ya ufasidi kwa maana ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali zimekuwa zikielekezwa zaidi katika *issue* nzima za kiutawala, wakati huo huo ukiangalia katika Halmashauri zetu na Taifa zima kwa ujumla fedha za kwenda katika miradi ya maendeleo zimekuwa ziko chini kuliko fedha za utawala. Utawala unavyolitafsiri suala la kiutawala maana yake ni suala ambalo linaweza lisionekane thamani yake yaani *value* yake kwa wakati ule. Lakini miradi ni *issues* ambazo zinaonekana moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya Mkaguzi Mkuu ya mwaka 2008/2009 fedha ambazo zimeelekezwa katika Halmashauri hususan fedha za ruzuku toka Serikalini shilingi trilioni moja, bilioni kumi na nne na milioni 297. Lakini zilizoelekezwa katika masuala mazima ya maendeleo utakuta ni shilingi bilioni 404,074,813,778. Sasa hapa ukipima tu unaona hili Taifa si Taifa ambalo linaelekea katika suala zima la kuleta maendeleo kwa wananchi ni Taifa ambalo linaangalia wale wanaoendesha ile miradi. Sasa unapokuwa na mradi, na *administrative costs* zinapokuwa kubwa kuliko pesa za miradi yenyewe, hakuna maendeleo yoyote ambayo yanaweza kupatikana. Sasa hili ni suala ambalo Serikali inahitaji kuliangalia kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mifano katika Halmashauri na ni mifano dhahiri kwa sababu unakwenda katika Halmashauri. Kikao cha kujadili mradi labda wa shilingi milioni tano mnakaa dakika 10 mpo jumuiya ya Madiwani wengi na jopo zima la *administrative* ambao wako pale kama utawala, mnatumia dakika 10, 15 mmaliza mnagawana posho na mambo mengine baada ya hapo hakionekani kitu chochote cha msingi. Sasa kwa hili ndiyo tunasema kwamba Serikali iwe makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ambalo tunahitaji Serikali iende kuliangalia zaidi kwenye ripoti ni Sheria ya Manunuzi. Wakati tunazunguka katika kipindi hiki kwenda kuwashukuru wananchi na kutembelea miradi majimboni kwetu, wananchi wamekuwa wakipendekeza kwamba Serikali inatoa ruzuku, wananchi tunachangia juu ya miradi ya maendeleo, lakini vitu vinaletwa kwa *tender*, hapa hili suala la *tender* kwa maana ya uzabuni lazima tuliangalie upya kwamba wazabuni wanaomba *tender* na zile *tender* zenyewe zinakuwa zimepangiwa bei tofauti tofauti na bei ile ukiangalia kiuhalisia ni tofauti na zilipo kwenye maduka ambazo wananchi wanazifahamu. Sasa *tender* inachukua miezi mitatu, pesa mwananchi anakuja kulipa baadaye.

Mheshimiwa Naibu spika, unamwambia kwamba mfuko wa *cement* kwa sababu ya mzabuni tumenunua mfuko wa *cement* kwa shilingi 55,000 lakini dukani unakwenda kukuta mfuko wa *cement* ni shilingi 15,000 mwananchi ataelewa nini juu ya Taifa lake mwenyewe?

Sasa haya ndiyo maeneo ambayo Serikali inabidi kuyaangalia kwa sababu tutaendelea kulalamika. Kwa sababu kila mwaka, tangu mimi nasoma ninaona kabisa ripoti zinazoletwa ndani ya Kamati zimekuwa zikilalamika na kuainisha matatizo mbalimbali ya hili Taifa kwamba tuna tatizo katika Halmashauri. Matatizo yanatokana na moja, mbili, tatu. Lakini tumeshindwa kuwa na azimio, *time limit*, tunashindwa kuwa nayo kwamba hili azimio letu *time limit* yake ni hii kwamba tunahitaji mwaka unaokuja, mnapokuja Bungeni mnatuletea taarifa kamili kwamba au taarifa ya CAG mangapi yametekelezwa, mangapi hayajatekelezwa na mangapi tuyafanyie kazi na mtoe sababu ni kwa nini hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hicho kitu hakifanyiki na hii ninachoweza kukuambia ni kwamba hata tutakapokuwa tunaongea na viongozi wakubwa, wanasema mtaongea lakini mwisho wa siku mambo yatakuwa vile vile. Sasa ndivyo yanavyosemwa kwamba walikuwepo watu wakawazungumzia yakapita na ninyi mtayazungumzia yatapita. Sasa tunalipeleka wapi Taifa kwa mfumo huo? Sasa hili ni suala ambalo lazima tulifanyie kazi na tuangalie upya juu ya sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kwamba suala la usimamizi wa miradi. Ukiacha Kamati Tendaji zinazofika kusimamia miradi, jambo hili sasa kama Wabunge ndiyo tunahitaji kuwa watu wa kwanza kwa mfano kwenye kusimamia miradi. Halafu tunakwenda kwenye upande wa Madiwani ili tuweze kufikia yale malengo tunayoyawekea. Kwa mfano, mimi safari hii nimepitia miradi yote ya jimbo langu, nimepitia miradi ya shule, nimepitia miradi ya afya, nimepitia miradi ya barabara, nimepitia karibu miradi mpaka ya maji, yote nimepitia, kuhakikisha kwamba wapi kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unakwenda katika Vikao vya Halmashauri ambako Madiwani ndiyo wasimamizi wake, watendaji wake, miradi yote haijapitia, lakini ripoti imeandikwa. Unakwenda unakuta mradi wa shilingi milioni 400 hakuna aliyepitia na mradi hauonekani kama ni mradi wa shilingi milioni 400, unaonekana ni mradi wa shilingi milioni tano au sita. Lakini kwa sababu ule mradi umepelekwa maeneo ya mbali ambako hayawezi kufikika na Serikali haiwezi kwenda kule basi ndiyo Taifa na pesa za Serikali zimekuwa zikienda. Lakini kitu ambacho tunahitaji tukilogope ni ubadhirifu umekuwa ni mkubwa sana. Ubadhirifu wa fedha za umma umekuwa ni mkubwa kupita maelezo tofauti na miaka iliyopita. Tumetoka kwenye mamilioni, zamani tulishangaa ubadhirifu kufanyika katika mamilioni, sasa tumetoka kwenye mabilioni na sasa tunahamia kwenye matrilioni ya fedha. Hili Taifa linakwenda wapi na bado sisi wenyewe tunatapa na kuyapitisha hayo mambo. Watanzania wanatuelewaje, hii ni kwa sababu tumeshindwa kuchukua hatua. Unajua sheria ni msumemo, angalau tufanye sheria ambayo kabisa kwamba tufilisi hata baadhi ya watu tuonyeshe mfano, ili

iwe *sample* kwa hili Taifa liweze kwenda katika mfumo makini. Mimi naamini tungekwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ili tuweze kuokoa Taifa katika hii miradi katika ubadhirifu mkubwa wa fedha usiyo kuwa na msingi, tunahitaji sasa kuwa na madaraka. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde, nikisimama uwe unakaa. Unaposema kuna ubadhilifu wa matrilioni na sisi tunakaa hapa kubariki mambo hayo, unataka kusema Bunge langu hili tukufu linabariki mambo hayo?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nilichojaribu kukisema ni kwamba tumetoka katika ubadhirifu wa mamilioni, tumekwenda kwenye mabilioni na sasa tunaelekea katika matrilioni. Kubariki haina tafsiri kwamba tunakubali kuyapitisha, lakini tunapokaa kimya wakati mambo yanaendelea kutendeka maana yake tunabariki, mfano, madeni fulani yanaendelea kupatikana. Kwa sababu unapolikuta deni linafikia katika maana ya trilioni maana yake kuna uwezekano wa kutokulipika, na kama lile deni halitalipika basi sasa tunaingia katika ile njia ya panya, kwa mfano madeni ya *EPA*, madeni sijui ya sehemu gani, sehemu gani, lakini mwisho wa siku tunakuja kugundua kabisa makosa yanaanza kufanyika kwetu sisi viongozi. Ndicho nilichokuwa nakimaanisha. (*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Bunge kama ulivyosema na Kanuni zetu zinaturuhusu kama liko jambo unalileta unalisema Bungeni, unaweza ukalileta kama kauli ya wewe mwenyewe Mbunge. Unaweza ukalileta kama hoja mahsusi. Lakini hatuwezi kuwa tunayajumuisha mambo. Tumekaa humu kama kazi yetu sisi ni kupitisha mambo maovu peke yake. Nadhani hatulitendei haki Bunge hili, imefika wakati twende kama lipo jambo tulitatie kama jambo lilivyokuja. Tusiongee katika ujumla wake. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde malizia dakika zako karibu zimeisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Sawa, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Silinde. Baada ya Mheshimiwa Silinde, sasa anafuata Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Murtaza Mangungu ajiandae. Mheshimiwa January simuoni, Mheshimiwa Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. Lakini kwanza kabisa pamoja na kuwa nitachangia katika hesabu za Kamati mbili kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa na Kamati hizi. Lipo jambo ambalo

limenistaajabisha kidogo, badala ya Wajumbe wenzangu kuchangia taarifa hizi ambazo tumeletewa wengi wamekuwa wanazungumzia mambo ambayo yako nje hata ya hizi taarifa ambazo zimewasilishwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako leo limeshuhudia baadhi ya wachangiaji wakisema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa, hiyo siyo kweli. Mpaka hivi tuko hapa ni mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi ambao uliwahi kusemwa, wanasema *lift your eyes beyond the true damage of today to mean hopes of tomorrow*, kwa hiyo, hilo tulizingatie. Lakini tukirudi katika hili, tunazungumzia masuala ya matumizi mabaya ya Serikali. Serikali imefanya jitihada kubwa sana kukusanya pesa mpaka zikapelekwa kutumika, kutumika vibaya katika njia ambayo inaonekana kama taarifa hizi za hesabu inamaanisha kwamba Serikali imefanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ambalo mimi naliona matumizi mabaya ya Serikali tuangalie zaidi katika mfumo ambao tunatumia kutekeleza Halmashauri zetu kwa mfano siku nyingi ambazo kama Waheshimiwa Wabunge waliopita wametangulia kusema Wakurugenzi, Watendaji wa Halmashauri wanapokea kasma ya mapesa lakini utendaji wao uko chini. Serikali *i-re-act* haraka kama vile ambavyo taarifa hizi zimeainisha, tusitumie muda mrefu zaidi kutekeleza wajibu wetu. Kama Sheria ambavyo zinasema hazitafsiri vizuri kuwawajibisha hawa, tubadilishe mfumo wa ajira na tuwaingize katika mikataba ama vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hesabu hizi za Serikali za Mitaa tatizo kubwa zaidi ambalo limejionyesha na kuna mwanya mkubwa zaidi ni eneo la wakandarasi. Wakandarasi wengi sana wanapewa pesa nyingi sana lakini miradi haitekelezwi vile ambavyo inatakikana. Kwa hiyo, ningependa tushirikiane baina yetu sisi Wabunge pamoja na watendaji hawa wa Serikali tuwawajibishe wale ambao wanatumia mianya hii kupoteza pesa za Halmashauri hizi na ile *practice* ya kusema *value for money i-apply* vile ambavyo inatakikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine, Madiwani kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Anne Kilango hapa tunawapa kazi kubwa sana ya kuzisimamia hizi Halmashauri, lakini kimsingi pamoja na uzito wa kazi ambayo tunawapa tuangalie uwezekano wa kuwaongezea maslahi yanayotosha ili waweze kuzifanya kazi hizi inavyotakikana, hatuwezi kuwapa kazi kubwa ya kusimamia Halmashauri lakini kiasi cha maslahi ambacho wanayapata wao hakiwezi hata kutekeleza kazi zao za siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Kamati ya Mashirika ya Umma imefanya kazi kubwa sana kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Bunge kama zinavyoelekeza, lakini ni jambo la kustaajabisha Kamati inapofanya kazi kutoa maamuzi yake na ushauri wake kama Kanuni zinavyoelekeza wapo watu wengine wanatoka kwenye vyombo vya habari

kwenda kuzungumzia mambo ambayo Kamati imetolewa maamuzi kama vile yale mambo Kamati haijayazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatolea mfano hapa, tulizungumzia suala la *consention fees* kwa TANAPA na taarifa ya Kamati imeonyesha, hatua ambazo zinatakiwa kufanyika. Lakini siku ya pili magazeti yameanza kututukana sisi na kutuandika vibaya kama vile tumefanya dhambi wakati tumetekeleza wajibu wa Kanuni na Katiba. *(Makofi)*

Nashukuru taasisi ambazo zilikubali kuitikia ushauri, lakini naomba kupitia Bunge lako hili, Serikali nayo vile vile iwe inachukua maamuzi kwa haraka inavyotakikana kwa sababu haya mambo yanakaa mwaka hadi mwaka matokeo yanakuja kuwa ni gharama kubwa zaidi kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali pamoja na mapungufu ambayo yanaonekana katika utekelezaji huu sasa tuongeze nguvu ya kutekeleza yale ambayo tunayazungumza hapa. Isiwe kila siku tunayarudia yale yale. Ukiangalia tatizo ambalo limezungumziwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa, tulipofanya kikao cha pamoja lile suala lilitatuliwa ndani ya saa moja na siku ya pili tu, utekelekezaji ukaanza na *PSPF* inafanya kazi kama kawaida sasa hivi. Sasa utekelezaji kama huu ndiyo ambao sisi kama Wabunge tunategemea upatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hiyo kengele ya kwanza. Ningependa Bunge lako Tukufu litupe nafasi zaidi kama Wajumbe wa Kamati ili tuweze kufanya kazi zetu. Naamini Mwenyekiti ametangulia kusema kabisa, muda wa kufanya kazi kwa Kamati ni mdogo. Kwa hiyo, tuangalie uwezekano tuongezewe nguvu ili tuweze kufanya kazi ya kuisimamia Serikali kama Katiba inavyotamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache mimi naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu kwa kutuweka sawa. Sasa Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe miongoni mwa watu watakoachangia jioni hii ya leo. Lakini pia na mimi napenda kusema kuwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, lakini kuna baadhi ya mambo ambayo naona ni vyema niyazungumze katika Bunge lako Tukufu ili tuweze kuyatilia mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kuanza kuchangia katika DAWASA. Tunajua kabisa maji ni uhai na bila maji maisha ya Watanzania hayawezi kwenda sawa. DAWASA inajishughulisha na suala zima la kuandaa miundombinu ya maji na katika *cubic metre* milioni 95.6 ambazo DAWASA inazalisha inasikitisha kuona ni *cubic metre* milioni 41 ndizo ambazo zinalipiwa ankara ya maji, nyingine zilizobaki hazijulikani zilipo ambazo ni 57%. Idadi hii ya upotevu wa maji ni kubwa sana na laiti

kama ingekuwa inadhibitiwa ipasavyo basi jiji la Dar es Salaam historia ya shida ya maji isingekuwepo hivi leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upotevu mkubwa wa maji DAWASA inaingia hasara ya shilingi bilioni 26, hili ni ongezeko kubwa sana. Katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, taarifa ya mwaka 2007 ilionesha ni hasara ya shilingi bilioni 10 iliyotokana na upotevu wa maji. Nadhani unaona ongezeko linavyozidi kukua kila mwaka, kutoka shilingi bilioni 10 kuja shilingi bilioni 26. Ushauri wangu ni vyema Serikali ikafanya *monitoring* katika DAWASA ili kuweza kudhibiti upotevu mkubwa wa maji na wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam tatizo la maji liwe ni historia kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanikiwa kutatua tatizo la maji kwa kuboresha miundombinu; kwa sababu hapa inakuwa inachanganya kidogo na mimi nakaa najiuliza hivi huu upotevu mkubwa wa maji ni kwa sababu DAWASA wanaendelea kutumia miundombinu ya zamani au kuna mchezo ambao unachezeka kiujanja ujanja ili tu ionekane maji yanapotea lakini kumbe kuna wajanja ambao wanaunganisha kwa njia nyingine? Ni vyema DAWASA ikawajibika ipasavyo na kuona ni namna gani ambavyo wanaweza wakazuia tatizo hili lisitokee tena. Shilingi bilioni 26 ni nyingi sana na 57% ya maji inayopotea ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa wataalamu (Wahandisi wa Maji) katika usafirishaji wa maji sawa kutakuwa na maji ambayo yanapotea, lakini sio 57%, haizidi 27% ambayo ndio ya maji yanayoweza kupotea katika kuyasafirisha katika njia yake. Ningeomba Serikali itilie mkazo katika kuhakikisha kwamba tatizo hili linaisha na ili wananchi wa Dar es Salaam waweze kupata maji; tumalize Dar es Salaam tuendeleo kushughulikia matatizo mengine ya maji ukiwepo Mkoa wa Mara nao wawe na uhakika wa kupata maji salama na ya uhakika. (*Makofi*)

Baada ya kuzungumzia DAWASA ningependa pia niende katika Mashirika mengine. Najua kabisa kwamba Serikali ilikuwa na dhamira ya dhiti ya kuruhusu ajira za mkataba, lakini nina masikitiko makubwa kuona baadhi ya Mashirika ya Umma yanatumia mwanya huo wa Serikali kuruhusu ajira za mikataba kujilipa fedha nyingi sana baada ya kumaliza mikataba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kutaja ni shirika gani lakini ningependa kutolea mfano tu wa shirika la PPF, kwa mwaka huu wamejiandaa kutumia zaidi ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuwalipa watu wawili tu katika *level ya management*; hizo ni fedha nyingi sana kwa mtu mmoja, kulipwa zaidi ya shilingi milioni 150 kama kiinua mgongo cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kuna haja ya Serikali kuangalia upya na kuweka kiwango maalum cha malipo ya mkataba katika Mashirika ya Umma. Najua lengo lilikuwa ni zuri lakini wamepewa uhuru uliopitiliza, menejimenti zinaweza zikakaa zikajipangia zenyewe na matokeo yake ni fedha nyingi zinaenda kwa mtu mmoja badala ya kufanya shughuli nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio ulikuwa mchango wangu ambayo nimeona ningependa kuyasisitiza leo ili tuokoe upotevu wa zaidi ya shilingi bilioni 26 katika masuala mazima ya maji, kwa sababu mengi nimeyachangia kwenye Kamati, lakini pia Serikali iweze kuingilia kati katika kupanga kiasi maalum cha watu ambao wanajilipa fedha nyingi baada ya miaka mitano kwa sababu, naamini hiyo shilingi milioni 150 ni zaidi ya viinua mgongo vya Wabunge wawili. *(Makofi)*

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia sehemu hii ambayo imewasilishwa kuhusu Taarifa za Kamati za Hesabu za Serikali, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika ya Umma. Nawashukuru kwa uwasilishaji wao mzuri, wa kina na wa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sehemu ya *TANAPA* nikitoa mfano wa Hifadhi ya Serengeti. Katika Wilaya ya Serengeti 70% ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti pamoja na mapori mawili ya akiba, Ikorongo na Gurumeti, jumla kunakuwa na mchango wa kiutalii wa 94%, kwa hiyo 6% ndio inakuwa sehemu ambayo wananchi wanaishi. Sehemu hii mchango wa utalii katika nchi yetu mapato makubwa kwa mfano fedha za ndani ni 47% kwa fedha za nje utalii unachangia mpaka 27%, hii ni pamoja na mchango mkubwa wa Hifadhi ya Serengeti. Lakini mapato haya yangeweza kuongezeka zaidi kama *TANAPA* wangejipanga ili kusudi kujenga mazingira rafiki kati ya wananchi pamoja na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona yapo manyanyaso makubwa ya wananchi pale ambapo kunakuwa na kunyang'anyana maeneo na wanyama na mipaka iliyopo. Mimi naomba haya mazingira rafiki yajengwe vizuri ikiwemo kupanua ajira kwa wananchi katika maeneo haya ya hifadhi, hususan Serengeti, kwa mfano matumizi ya vifaa vya kawaida katika wawekezaji walio kwenye Hifadhi ya Serengeti. Hawana sababu ya kwenda kununua Arusha kwa sababu wazabuni wapo ndani ya Wilaya wanapatikana na wanao uwezo; haiwezekani hata *toilet paper* eti ziagizwe Arusha wakati zinaweza kupatikana hata Mugumu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sehemu kubwa ambako Serikali inapoteza fedha nyingi ni sehemu hizi za utawala pamoja na manunuzi. Manunuzi haya utashangaa inatangazwa *tender* lakini wale wazabuni watakaokuja katika kushindana kila mmoja amefanya *quotation* karibu na *ceiling* ya mradi husika; hivi taarifa hizi wanazipataje? Kwa hiyo, udhaifu huu ambao upo wa kutoa taarifa za ndani na ni siri ya Serikali, hawa wanazipataje? Ndio mwanzo wa kupotea kwa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia kwa utaratibu, nimejaribu kufuatilia karibu, zaidi ya 30% kwenye manunuzi na kwenye utawala, sasa hii ni karibu 60% ya fedha ambazo zinakwenda katika maeneo ya Serikali, ni fedha nyingi sana zinapotea katika njia hizi. Lakini pia yapo maeneo ya msingi ambayo yanasababisha upotevu wa hela za Serikali kwa sababu ya hali ya mishahara. Maeneo mengi utakuta kwamba kile kifungu cha 250311, ambayo ni *perdiem domestic* ni fedha nyingi kweli kweli.

Mimi nashauri kwamba sehemu hii iboreshwe na fedha zielekezwe katika mishahara; mbona nchi nyingine duniani ndivyo wanavyofanya? Pale ambapo mtumishi anasafiri unakuta kwamba anapewa fedha ya nauli na kulala. Kwa sababu kama angekuwa hajasafiri, si analipwa mishahara na kula, kwa hiyo, fedha hiyo aitumie wakati wa safari ili kusudi mishahara iweze kuongezeka, isaidie tija na tunapunguza zile nafasi za kuchukua fedha za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hata wengi wanaokwenda katika safari ni wale watumishi ambao mishahara yao haijambo kidogo, sasa wale watumishi wa ngazi za chini pamoja na *operational staff* ni lini wanasafiri na wanalipwa vipi hizo *per diem*? Na ndio kundi kubwa ambalo linaumia na hii pia itasaidia kupunguza kodi kubwa ambazo zipo kwenye mishahara. Unaweza kukuta mtumishi kulingana na ngazi yake ya mishahara anakatwa *income tax* mpaka 34%, ni fedha nyingi sana. Hili naomba lirekebishwe ili lisaidie kujenga ari na kuongeza tija katika maeneo ya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukijaribu kuangalia, Wakurugenzi ni taasisi, lakini taasisi hii inakwendaje? Kweli unaweza kukuta anao Wakuu wa Idara baadhi wana *qualified level* kulingana na uwezo wao wa kikazi. Kwa hiyo, tunaona zipo *CPA*, kuna wengine wana *Post Graduates*, kuna wengine wana *B Com* na wengine wana *Advanced Diploma*, hawa ambao ni ma-*DT*. Lakini hii kama taasisi ile *collective responsibility* ikoje? Wakuu wengine wa Idara wanajulikana vipi ili kusudi sasa unapotengeneza seti nzima ya Halmashauri katika *financial performance* inakwendaje?

Kwa hiyo, suala hili ni la kuliangalia ili kusudi kama ni huyu mchezaji ambaye anacheza vizuri, *let say* Drogba, akiwa yeye mwenyewe haitawezekana hiyo Chelsea ishinde ni lazima wachezaji wenzake nao wacheze kwa pamoja, wacheze vizuri waweze kufunga magoli. Kwa hiyo, naomba Wakuu wa Idara wengine na Wakuu wa Vitengo katika Halmashauri waimarishe uwezo. Kwa sababu mimi kwa bahati nzuri nimefanya kazi katika mfumo wa Serikali kwa zaidi ya miaka 25, kwa hiyo, ninao uzoefu mkubwa sana katika Serikali za Mitaa. Bila kuwa na watendaji wazuri ambao wanasaidiana na Mkurugenzi utafukuza Wakurugenzi wote katika nchi hii na hapatakuwa na tija. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia suala zima la mifumo mizima ambayo inakuwa-*introduced* na sio mwingine ila ni *push* ya nchi za wenzetu ukijaribu kuangalia *computer systems* ambazo zimefika katika Halmashauri, kulikuwa na utaratibu mzuri chini ya *EPICOL*; sasa inafika mahali tunasema *EPICOL* tunaacha tunakwenda *computer system* nyingine. Hata pale ambapo *computer system* ya *EPICOL* ilikuwa haijakamilika bado ulikuwa unakuta kuna mtendaji mmoja au wawili wenye uzoefu na ujuzi wa kutumia *computer system* hiyo. Kwa hiyo, mifumo hii ambayo inakuja ni vizuri tunaipokea *smoothly*, tunakwenda nayo kwa wakati kwa ajili ya kujenga uwezo ambao ni endelevu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukijaribu kuangalia suala zima la *ghost workers* limezungumziwa sana katika maeneo yote ya wenzetu ambao wamewasilisha taarifa hizi.

Lakini *ghost workers* hawa huko nyuma kulikuwa na suala la kulipa mshahara dirishani, tukasema hapana...

(*Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji*)

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika ni kengele ya kwanza hiyo; tukasema hapana. Sasa kutokana na hilo likaja suala zima la watumishi kuingia katika akaunti chini ya Hazina, lakini bado tunaona kwamba kuna *ghost workers*. Basi urudishwe utaratibu wa kufanya *screening* ili kuwe na *National Pay Day* ili isadie kufanya *screening* ya *ghost workers* la sivyo hii itaendelea kwa sababu ni wengi sana wanalipwa kwa njia ya *computer* na mtandao na fedha ndio hizo nyingi zinapotea chini ya mtandao; tatizo hili litazidi kuwa kubwa na sugu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ninachoomba ni suala la ucheleweshaji wa fedha, kama nilivyosema kwa uzoefu wangu wa fedha Serikalini hakuna mwaka hata mmoja fedha zimekuja kwa wakati na za kutosheleza. Wakati mwingine inachekesha, ile tarehe 30 Juni, saa 06.00 usiku unaambiwa fedha iliingia halafu ikatoka. Ukienda *technicaly* ni kweli fedha hiyo ilikwenda katika Halmashauri, ilikwenda katika Mkoa, halafu haikutumika imerudi. Hii sio halali; naishauri Wizara ya Fedha ilianganalie tatizo hili linasababishwa na nini? Kama ni *pledges* ambazo zinatoka katika maeneo mengine ifanye *tracking* kwa sababu wanasema *experience is a very good teacher*. Ili kusudi tatizo hili la kuchelewesha fedha kwenda katika Halmashauri, kwenda Mikoani, liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia suala la usimamizi. Ukijaribu kuangalia fedha hizi kiusimamizi kuna mtiririko ambao unategemeana, kuna sekretarieti za mikoa ambazo zinasaidia *Local Government Authorities*. Lakini uwezo umejengeka vipi katika *Regional Secretariat*? Kwa sababu unakuta mtendaji mwingine anakwenda kusimamia ngazi ya Wilaya lakini hana uwezo wa kukagua Halmashauri. Kwa hiyo, ujengeke uwezo katika *Regional Secretariat* kusudi kuwe na usimamizi mzuri ambao upo *linked* na unategemeana na kimfumo. Lakini ni vipi wakuu wetu wa Wilaya wamewezeshwa? Ni kichekesho, kama wewe huna kitu huwezi ukawa na sauti; haiwezekani Mkuu wa Wilaya umsimamie Mkurugenzi ambaye Mkuu wa Wilaya unakwenda kupiga magoti kuomba mafuta, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya namna hiyo yanasababisha hata upotevu wa fedha. Kwa sababu Mkurugenzi akitoa shilingi milioni tano za mafuta una uhakika wa kiasi gani kuwa ni shilingi milioni tano? Anachukua *loophole* hiyo anatoa shilingi milioni 10 halafu anakuambia ni shilingi milioni tano na siku nyingine Mkuu wa Wilaya hutakuwa na meno ya kumkemea wala kumsimamia kwa sababu unampigia magoti kuomba mafuta. Asante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku lakini kwa bahati mbaya kifua changu sio kizuri, nitaomba radhi. (*Makofi*)

Kwanza naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Wenyevitani wa Kamati zote tatu kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa niaba ya Bunge hili. Lakini vile vile naomba niwaombe wenzangu kwamba mapendekezo yaliyomo ndani ya taarifa za Kamati hizo yote tuyapitishe ili yaweze kutekelezwa kama vile walivyopendekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mimi naomba kuishauri Serikali jambo moja; mwaka 2005 Serikali ilikuja na sera ya kuyauza Mashirika ya Umma na kwamba Serikali haitafanya biashara. Serikali haijarudi tena Bungeni hadi leo kusema kwamba sera hiyo imebadilika, leo tuna Mashirika tena mapya 214 ambayo kati ya hayo Serikali ime-*guarantee* si chini ya shilingi trilioni sita na hatuna hakika kwamba fedha hizo zitarudi tena Serikalini. Sasa Serikali inapobadilisha sera, sera ambazo hazikupangiliwa vizuri matatizo yanabaki pale pale. Na ni kwa nini wasiweze kupanga vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisoma taarifa ya *POAC* sababu zile zile ambazo zilisababisha kuyauza Mashirika ya Umma ndizo ambazo zimejirudia. Sababu ya kwanza ni Mashirika yale yalikuwa na mtaji mdogo sababu hiyo bado inaendelea kuwepo, sababu ya pili ilikuwa ni kuonekana zile Bodi hazina uwezo sababu hiyo bado inaendelea kuwepo, sababu ya tatu ilikuwa ni Menejimenti sio nzuri bado sababu hizo zinaendelea kuwepo, manunuzi hayakuwa mazuri bado sababu hizo zipo, kwa hiyo, sababu zile zile ambazo tulianzisha Mashirika hayo na baadaye tukayabinafsisha kwa bei ya chee leo tena tunarudia makosa yale yale. Hivi Serikali inakusudia nini inapofanya hivyo? Tuwaambie nini Watanzania kwamba sisi kila siku tunafanya majaribio ambayo yanahatarisha Taifa letu, kwa sababu leo deni la shilingi trilioni saba ambazo hazijulikani ni lini zitalipwa na ni namna gani zitalipwa kwa Mashirika ambayo kila siku yanaendelea kudidimia, ni hatari kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, moja ninaloliomba Serikali ni kuwa inapobadilisha sera iangalie yale mambo yaliyosababisha kukwamishwa sera je, yataendelea kuwapo yale yale au yataondoka? Vinginevyo hakuna sababu ya kubadilisha sera, tunapoteza gharama nyingi kwa kutunga sera mpya, tunakusudia kufanya marekebisho makubwa halafu tunarudi nyuma pale pale. Leo tuna Mashirika 214 mapya, ndio taarifa iliyokuja hapa asubuhi. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anasema kwamba Mashirika hayo 80% yamedhaminiwa na Serikali na haijulikani ni lini fedha itarudi. Fedha ya mkulima, fedha ya mfanyakazi wa chini inaendelea kupotea, mimi nasema hiyo ni kasoro moja kubwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sasa, Kamati zetu zifanye tathmini ya madeni haya, Mashirika yaliyokopeshwa tuyajue, Serikali iliyoyawekea *guarantee* tuyajue, tufanye uchambuzi wa kina ili Bunge hili liridhike kwamba kweli tunaendelea na Mashirika hayo au tunachukua hatua nyingine. Hatuwezi kuendelea kupokea taarifa tu, halafu taarifa hiyo ikabaki katika nadharia na vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ukisoma taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pamoja na Kamati zetu, utakuta Mashirika yetu ya Hifadhi za Jamii yamefanya kazi nzuri sana. Lakini vile vile yapo malalamiko ya wale wanaolipwa pensheni, wanachukua mpaka miezi nane mpaka tisa hawajalipwa pensheni zao. Si jambo jema hata kidogo, wakati Mashirika haya yanatumia fedha nyingi huku lakini wachangiaji wa mfuko huo

wanapofanya *retirement* hawapati haki zao kwa muda unaotakiwa. Na sababu ni zile zile kila siku, vyeti vya kuzaliwa havipatikani, nyaraka sijui zimepungua, kama mfanyakazi anakaribia ku-*retire* miaka miwili kabla ni kwa nini *documents* zote zisitafutwe ili siku anapofikia *retirement* yake anapata haki yake kwa wakati, kuna tatizo gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mitandao yote ipo, *system* zipo, lakini kwa nini watu hawa wanaendelea kuteseka, bahati mbaya narudia tena kusema hatokei afisa wa juu hata mmoja akachelewa kulipwa kiinua mgongo chake, hata siku moja. Lakini wafanyakazi wa chini wanaendelea kila siku kupata matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nimesoma taarifa ya LAAC, nilitegemea katika kipindi hiki sasa kwa muda angalau tuwe na Manispaa moja au Halmashauri inajitegemea, ni aibu kwa Manispaa kama ya Dar es Salaam bado inaendelea kupata ruzuku ya Serikali, nenda Johannesburg, California zote zile zinasaidia kuchangia Bajeti ya Serikali sio zenyewe zinapokea Bajeti ya Serikali. Vyanzo vikuu vya mapato viko Dar es Salaam, kwa nini Manispaa za Dar es Salaam zishindwe kujitegemea zinapata ruzuku kama Halmashauri ya Lindi ambako hakuna biashara yoyote, lakini kwa sababu hakuna usimamizi mzuri, hakuna udhibiti mzuri na Manispaa na Halmashauri hizi zimeendelea kuwa tegemezi kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, misamaha ya kodi bado ni tatizo katika Taifa, asilimia 18 ya misamaha ya kodi, ukiangalia na kiwango cha Bajeti yetu tegemezi asilimia 28, haingii akilini hata kidogo. Serikali imekuja katika Bunge hili mara zote ikiahidi kwamba kuna mchakato wa namna gani tunaweza kupunguza misamaha ya kodi, hadi leo kiwango cha kupunguzwa misamaha ya kodi hakijaonekana faida yake katika Taifa hili. Matokeo yake tunaenda kuhemea kwa wafadhili na wahisani kila siku, hata tunapokuwa na sera za msingi kutoa tunashindwa kwa sababu tunahemea misaada na mikopo ya wahisani, wakati Taifa hili linauwezo wa kujitegemea wenyewe kwa misamaha tu ya kodi. Tukichukua kiwango cha asilimia tano na sita cha wenzetu wa Uganda inatosha kabisa kutuondolea misamaha ya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sasa Serikali ije na mkakati katika kipindi hiki cha Bajeti itueleze hasa mkakati madhubuti wa kupunguza angalau asilimia 50 ya misamaha ya kodi ili tuondokane na Bajeti tegemezi. Halmashauri nyingi zimeshindwa kufanya kazi, Wizara ya Elimu imeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya uchache wa Bajeti. Bajeti ambayo wangeipata kama misamaha ya kodi isingekuwepo wanafunzi tungeweza kuwalipia mikopo yao, hatuhitaji miujiza kufanya hayo. (*Makofi*)

Suala la mapato ya Serikali, ukiangalia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonyesha ni kwa kiwango gani Wizara mbalimbali zinashindwa kukusanya mapato ya Serikali na watu wamepewa taaluma nyingi lakini mpaka leo hali ni ile ile, mimi naiomba Serikali kuanzia sasa Wizara ambayo itashindwa kukusanya mapato tuone hatua madhubuti zinachukuliwa na Bunge hili litaarifiwa, hayo mambo ya jumla jumla kila siku tutaendelea kusoma taarifa hizi na hali inaendelea kuwa hivyo hivyo, sio hali nzuri, tunahitaji kuirekebisha hali hiyo mapato ya nchi hii ni makubwa lakini kwa bahati mbaya hayasimamiwi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba suala la matumizi ya Serikali, matumizi ya Serikali bado ni makubwa ukisoma taarifa zote hizi, ukisoma hata ule mkopo wa shilingi trilion saba ukiuliza *economic impact* iliyoonekana katika mkopo huu huioni, inawezekana kabisa matumizi ya mikopo hiyo yameenda sehemu ambazo haiwezi ku-*generate* mapato yoyote katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kusimamia matumizi ya Serikali, Serikali ni kubwa inahitaji kupunguzwa, Serikali ina mambo ambayo ukipitia mtiririko wa Bajeti kuna vifungu chungu mzima vinahitaji kuangaliwa na tunaweza kupunguza matumizi ambayo siyo ya lazima. Ukienda kwenye *employment allowance* utaangalia vifungu vingapi vinahitaji kupunguzwa ili tuweze kupata fedha za kuendesha Serikali, hii hali sio nzuri tunahitaji kuikazia vizuri sana. Maliasili na Utalii kuna rasilimali nyingi sana Waziri akikazana vizuri na wenzake wakikazana vizuri tutaondokana na Bajeti tegemezi. Serikali lazima tuwe makini katika kutumia rasilimali za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed *mic* zetu zilikuwa zinaleta taabu tangu mwanzo lakini nashakuru wataalam wetu wamerekebisha sasa. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani kwa kunipa nafasi hii na nakumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yangu ya PAC Mzee John Momose Cheyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kusema kweli tusilalamike kama ni nchi maskini, mimi ni mara yangu ya kwanza kabisa kuwa Mbunge, lakini nchi hii ni tajiri kuliko Ubelgiji, Denmark, lakini cha ajabu leo tunaenda kukopo mikopo Denmark na Ubelgiji wakati ni tajiri sana na rasilimali zote tunazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli tujipange, tuishi kutokana na mishahara yetu, mtu kama ana tamaa na nchi hii ndugu zangu aache kazi aende akalime, atafute jembe akalime awaachie wenye moyo wa kujenga nchi hii wabaki kufanya kazi ya Serikali. (*Makofi*)

Nazungumzia kuhusu kilimo kwanza, naiomba Serikali ifanyie utafiti kuhusu *power tillers*, hizi *power tillers* kwenye mikoja nyingi hazifai, zimebaki kubeba mizigo na kuwaingiza wakulima na zinauzwa bei ya ajabu wilaya hadi wilaya. Mpaka sasa ukienda wilaya nyingi kazi yao ni kubeba mizigo tu hazifanyi hata kazi yoyote ya kilimo bora hata kilimo cha ng'ombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kitu kingine kinachotutia hasara katika nchi yetu ni vitambulisho vya uraia, cha ajabu Serikali imefanya mikakati mikubwa kuandika *tender* na kuomba makampuni mbalimbali yaingie katika harakati za kutaka kutengeneza vitambulisho. Wakati *licence* nzuri kabisa *TRA* wanatengeneza, *passport immigration* wanatengeneza hapa hapa Tanzania. Sasa itakuwa kila mwaka tunaandika *tender* ya

kuanzisha vitambulisho wakati sekta zetu hapa, Wizara zetu zinaweza kutengeneza vitambulisho, tuingie *tender* na makampuni yenye bei za ajabu ajabu. (*Makofi*)

Mimi naishauri Serikali iipe Wizara ya Mambo ya Ndani itengeneze yenyewe vitambulisho, inunue mashine, iweke pale pale Wizara ya Mambo ya Ndani itengeneze vitambulisho vya nchi yetu. Tutapoteza hela nyingi sana kuwapa hao wakandarasi kwa ajili ya hiyo *tender* ya kutengeneza vitambulisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Ndege, halifai kabisa kulisaidia, lina wafanyakazi wanapata mishahara, kuna bodi inakaa bure kupata mishahara na ndege hawana. Kwa hiyo, hili shirika ndugu zangu tulifute kabisa, tutafute shirika lingine, watu wenye moyo waweze kufanya hiyo kazi. (*Makofi/Kicheko*)

Kuhusu Kiwira mpaka leo watumishi zaidi 400 wanalipwa mshahara wanafanya kazi gani pale Kiwira na haijulikana deni la Kiwira atabeba nani msalaba wa Kiwira. Nchi hii ni tajiri, tujipange ili tuokoe uchumi wa nchi yetu bila kuoneana huruma, nimesikia kwanza kama *EWURA* ndugu zangu *EWURA* wanalipa *gym* ipo pale *Oysterbay*, kila mfanyakazi dola 400 kwa mwezi akienda kufanya zoezi asiende kufanya zoezi, sijui Bunge gani limeipitishia *EWURA* wajilipe mshahara wa namna hii na posho ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tujisafishe ndugu zangu hamna kuoneana aibu, nchi ni yetu sote, tujipange. Kuhusu vocha za pembejeo za kilimo, sehemu nyingi imefeli, tusidanganye, imeshindikana, mkoa wa Rukwa walikuwa wanaandika mpaka maiti, hata mwaka huu imeshindikana ni miradi ya watu, wafanyakazi wachache wananufaika na wakulima wachache wananufaika. (*Makofi*)

Naiomba Serikali ipunguze mbolea kwa wakulima wote nchi nzima tuondokane na tatizo hili, nchi hii ni ya kwetu sisi wote kwa pamoja haiwezekani kumpa mtu vocha na mwingine kumnyima vocha, kuna mashamba darasa wanapewa wachache mashamba ya darasa wengine hawapati mashamba ya darasa. Kwa hiyo, naomba Serikali ipunguze mbolea Mbeya na ipeleke mbolea vijijini na kwa wakati muafaka ili tuondokane na wizi wa mbolea. Serikali inapoteza hela nyingi sana kwa watu wachache wanaandika mpaka maiti. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kijiji cha Wapembe hawalimi lakini ndiyo iliyoongoza kuchukua vocha za mbolea mwaka juzi wanalima mihogo hata mfuko mmoja wa pembejeo wa mbolea haukwenda lakini ndiyo kijiji kiliongoza mkoa wa Rukwa, wilaya ya Nkasi hususan kwa ruzuku ya mbolea. Sasa hii tutafika wapi, nchi yetu tajiri ndugu zangu hii miaka 50 tungekuwa tunakopesha Rwanda, Burundi, Malawi wangukuwa wanakopa kwetu, leo tunaenda kubembeleza kwenda kukopa nje wakati nchi tajiri tuna bandari, mlango wa bahari wa kupitishia kila kitu, leo tunakuwa watu wa nyuma kwenda kuomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unafikia hapo tujirekebishe, nchi yetu ni tajiri hakuna kusikia nchi yetu maskini, sio kweli. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana, la kwanza nataka kushukuru kwa kuniweka niwe wa mwisho, Mungu akubariki. (*Makofi*)

Vilevile nataka niwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati tatu, hususan Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa John Cheyo pamoja na Mheshimiwa bwana Kabwe Zitto, wamefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamenifilisi, nimesema hivyo kwa sababu wachangiaji wenzangu wamechangia yale mambo muhimu sana ambayo nilikuwa nataka niyaongee leo hapa. Lakini inakuwa kwamba wenzangu tayari wameshaongea ila nitachangia mawili au matatu. Kwa upande wa Mheshimiwa Augustino Mrema, naomba apewe meno, pale alipofikia aongeze zaidi, kwa sababu anafanya mambo mazuri lakini umalizikiaji unakuwa mzito, haongezewi nguvu kiasi ambacho wale wanaofanya wizi awafikishe mwenyewe mahakama na wapatiwe majibu haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumempa nguvu vizuri sana, anakwenda kila wilaya na anatoa maelekezo mazuri na watu tunajua kabisa watu ni wezi, lakini cha kushangaza ikishafika kwenye vyombo vinavyohusika inakuwa inapigwa mpira, hilo tu ndiyo nilikuwa nataka nichangie kwa Mheshimiwa Mrema. (*Makofi*)

Lingine lilikuwa masuala ya pesa, nilitaka niongeze tu nguvu kwamba Serikali zile pesa ziletwe kabisa mwezi wa kwanza, tukisema hivi tuna sababu kuna tabia ambayo inafika mahali Halmashauri zinawachangisha mpaka wale wanaolima mashambani. Lakini ni kwa sababu ya kukosa zile pesa kwa wakati sasa inafika mtu anakwenda shambani kulima mahindi, anabeba mahindi yake anayaleta nyumbani, kabla hajapeleka sokoni anakuta mtoza ushuru yuko pale, sasa nitafanya kazi ngapi, nilime mazao yangu, niyaleta nyumbani kwangu bado niyalipie ushuru kabla sijakwenda kuyauza sokoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tunaomba sana Serikali ihakikishe kwamba kila inapofika mwanzo wa mwaka Halmashauri zipelekewe ili hawa wapiga kura wetu wasiburuzwe. (*Makofi*)

La pili nataka niende kwa Mheshimiwa Kabwe Zitto ameongelea sana Mashirika ya Umma hapa, lakini nashangaa kule katika jimbo langu kuna Kiwanda cha *Timber Cheap Board* mbona hakionekana hapa na kuna wananchi wengi wamekaa pale kwa muda mrefu kile kiwanda hakifanyi kazi na uwezo wa kufanya kazi upo lakini kimekaliwa na watu tu, wananchi wangu wanapata shida wakitaka kuuliza masuala haya twende kwa nani wanakosa majibu yake. Naomba Mheshimiwa Kabwe Zitto uangalie na pale Mkumbara pale pana kiwanda ambacho kilikuwa kinatoa mbao nyingi tu Tanzania hii na kila mtu anaifahamu, aende na huko nako akaangalie utaratibu huu ni utaratibu gani ambao umetumika. (*Makofi*)

Suala lingine ni suala la Halmashauri zetu hizi, Halmashauri zetu zina sehemu ambazo zingeweza kupata mapato lakini cha kushangaza Mamlaka ya Mkonge hawawezi kuchangia hata siku moja ushuru ambao wanatakiwa walipe kwenye Halmashauri,

matokeo yake Halmashauri zinakuwa zina wakati mgumu sana kuendeleza Halmashauri zao.

Sasa naomba yale mapato ambayo wanadaiwa hawa watu wa mamlaka ya mkonge wayalipe kwa sababu inakuwa kama kuna mtu anawazuia zuia hivi wakitaka kubananishwa walipe ushuru zile zinazotakiwa wao wanakwepa, matokeo yake mashamba yanakuwa misitu, watu hawapewi, sasa inakuwa ni dhambi sana hii. Naomba Serikali iangalie kwa hawa watu wanaolima mkonge, walipe zile seti ambazo zinatakiwa ziende kwenye mifuko ya Halmashauri ili wapiga kura wetu wasisumbuliwe kwa sababu nasema hivi ikifika wakati wa uchaguzi utakuta geti zaidi 50 wanazungushwa watu wanazungushwa watu kila unapofika mahali mpaka mtu anasema hii nini, unamkuta mtu anatumia chuki lakini ni kwa sababu ya kuwalea watu wachache. *(Makofi)*

Naomba Serikali iangalie kwa hawa, vilevile wamezungumza masuala ya madini lakini kwangu mimi katika wilaya yangu kuna madini, yako kule Kalalani kuna wachache wanayachimba yale madini, mtu akienda kuchimba madini pale anapata usumbufu. Je, hizi hela wanazotoa wao wanampa nani?

Mimi naomba Serikali itafute utaratibu mzuri, mtu akitaka sehemu ya kuchimba madini basi aende kwenye Halmashauri, aonekane kama huyu ni mlipa kodi kweli kweli kuna wengine wamezuia maeneo hawafanyi kazi, watu wakifika pale wanatishiwa na bunduki, wananchi wetu wanapata shida na hayo maeneo hawayaendelezi, sasa Serikali safari hii naomba waangaliwe, tusiwape watu tu, wachimba madini waende pale kwa kutisha kwamba mimi nimewekwa na fulani hakuna haja ya kuwekwa na fulani kwa sababu Watanzania wote wanaujua uchungu wa mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wenzangu wamenifilisi sana, maneno waliongea wenzangu ni ya busara sana ambayo ninatakiwa mimi niyaunge mkono mia kwa mia. Nikiongea sana nitakuwa nakosea ila tu naomba sana Serikali iwe makini kuzipeleka hela zile Halmashauri mapema mno kama walivyosema Wabunge wenzangu, asante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante Mheshimiwa Stephen Ngonyani. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza asubuhi kwa kweli orodha ya Wabunge ambao walipenda kuchangia masuala yaliyoletwa mbele yetu na Kamati hizi tatu orodha ni kubwa sana. Kwa vyovyote vile tusingeweza kuimaliza ajenda hii katika ratiba iliyopangwa ya siku moja leo. Kwa hiyo, ningomba wale wote ambao hawakupata nafasi ya kuweza kusema humu Bungeni tusameheane kwa sababu ya suala lenyewe na muda tutapata nafasi mambo mengine yanayofuata wakati mwingine na kwa maana hiyo hiyo ya muda sasa wachangiaji wote wanafuata baada ya hapa wataenda kwa dakika tano, tano, nitaanza na baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri dakika tano, tano na kengele itakayolia ni moja tu ikilia hiyo moja basi unakaa chini maana yake dakika tano imeisha. *(Makofi)*

Halafu tutafuatiwa na Wenyeviti waliotuletea mambo haya ya leo na wenyewe vilevile kila mmoja ni dakika tano kwa sababu hizi ni hoja za Kamati zetu, naamini

kabisa kila mmoja atajitahidi kutumia dakika zake tano. Naomba sasa nianze na Mheshimiwa Omari Nundu, Waziri wa Uchukuzi na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Waziri wa Viwanda na Biashara ajiandae. (*Makofi*)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika taarifa zilizotolewa na Kamati hizi tatu. (*Makofi*)

Kwanza nizipongeze Kamati zote tatu kwa kazi nzuri waliyofanya, lakini kabla sijaendelea kuongea nachukua nafasi hii kutoa rambirambi zetu kwa kifo cha Katibu Mkuu wa *TRAWU* ndugu yetu Sylvester Rwegasira.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mengi lakini mimi nitajikita katika lile la *Air Tanzania* ambalo limeongelewa na Wabunge kadhaa wa kadhaa. (*Makofi*)

Katika Kamati ya Mashirika ya Umma, imeonyeshwa kwanza kwamba *Air Tanzania* inapata hasara na ni kweli ile *figure* ya shilingi bilioni 23 zilizotolewa pia ni ndogo kuliko hasara ambayo *ATCL* imepata hadi sasa. (*Makofi*)

La pili inadaiwa kuwa Serikali haikuwa inaipa ruzuku *ATCL* ya nusu bilioni kila mwaka hizo kwa mwaka mzima ni shilingi bilioni sita na kwa miaka mitatu ni shilingi bilioni 18. Napenda Kamati ielewe kuwa kwa njia moja au nyingine Serikali imekuwa ikilisaidia shirika la *ATC* kulipatia fedha ambazo ni ruzuku mara kadha wa kadha na kwa kipindi cha miaka mitatu 2007 - 2010 fedha hizo zimefika shilingi bilioni 42 ambazo ni shilingi bilioni 24 zaidi ya zile shilingi bilioni 18 ambazo ziliombwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Kamati ilipendekeza kuwa shirika lipewa USD bilioni 31 kwa ajili ya kipindi kijacho cha bajeti ya 2011/2012, hiyo hesabu ilikopatikana na sisi hesabu tulizonazo inaonekana hizi zinatokana na *business plan* ya *ATCL*. Lakini katika *business plan* hiyo kutakuwa na vitu vingi ambavyo vimeorodheshwa hapo ni gharama za utendaji ambazo sio pesa ambazo Serikali kama mwekaji mwenye mali anatakiwa awekeze. Sasa nayasema haya ili kuhitimisha kuwa shirika letu la *ATCL* pamoja na kuwa Serikali inataka riboreke lifanye kazi vizuri hili sio suala la kuliangalia juu juu. (*Makofi*)

Sisi Serikalini tunaangalia kwa dhiti mikakati gani tufanye ili tukija hapa wakati wa Bajeti tuwaeleze kinaga ubaga ni mipango gani, ni fedha ngapi na mbinu gani ambazo tutazitumia ili Shirika letu la *Air Tanzania* lifanye kazi kama ambavyo linatakiwa liwe kama mwakilishi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hivyo basi, niseme tu kuwa sasa hivi mbinu ambazo tunazishughulikia ni pamoja na kuitisha wawekezaji na tuko katika hatua za juu za kujadiliana na wawekezaji kuhusu hilo. Naliomba Bunge lako tukufu liruhusu Serikali na kuipa uhuru wa kupanga mipango yake ili tuweze kulinasua shirika letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kampuni ya Huduma za Meli pia imetajwa hapa. Mimi naungana na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa kusifu kazi ambayo inafanyika kwenye Kampuni hii, Kampuni hii linafanya kazi kweli katika hali ngumu, meli zao nilikwenda kuziona mwenyewe zimekuwa nzee na Serikali iko mbioni na ina majadiliano tunayoyafanya na Serikali ya Denmark kutafuta meli mpya za kuweka katika maziwa yetu matatu yaani Tanganyika, Victoria na Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja zote tatu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri Dkt. Cyril Chami atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIAFHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na wachangiaji wote kwa kuwapongeza Wenyeviti pamoja na wajumbe wa Kamati hizi kwa taarifa zao nzuri. Ninazo hoja saba hapa lakini naomba nianze na ile ya *General Tyre* muda ukiisha nyingine tutazipeleka kwa maandishi kwa Wenyeviti husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba Kamati ya Mashirika ya Umma itaunda Kamati ndogo kwa ajili ya kuchunguza suala zima la *General Tyre* hususan matumizi ya dola milioni 10 ambazo zilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuonyesha kwamba suala hili Serikali imeliona, imelifanyia kazi na taarifa tulizitoa katika Bunge hili si mara moja ili Kamati ndogo itakapokuwa inafanya kazi ijue kwamba vilevile inaweza ikaja kwetu ikapata msaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni kwamba fedha hizi dola milioni 10 zilitolewa mwezi Februari, 2005 kwa makubaliano kwamba kila baada ya miezi mitatu *General Tyre* wawe wanatoa taarifa Serikalini na wawe wanatoa taarifa kwa *NSSF* ambao ndiyo walikuwa na fedha kila baada ya miezi mitatu, lakini hawakutoa taarifa. Mwezi Novemba, 2005 *General Tyre* wakaomba tena fedha nyingine kutoka *NSSF*, Serikali ikasema kabla hawajatoa dhamana kama waliyotoa pale mwanzoni ni vizuri ikajiridhisha kama zile fedha dola milioni 10 zilitumika sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya hilo Serikali iliamuru kwamba ifanyike *special financial audit* ili kuona kama matumizi hayo yalifanyika kama tulivyokubaliana na *audit committee* iliyokaa ikatoa taarifa na taarifa hiyo ikaonesha kuna upungufu mkubwa. Upungufu huo ni kwamba *management* ya kiwanda haikufuata masharti ya mkopo ule, *management* ya kiwanda haikuwasilisha taarifa *NSSF* wala Wizara ya Fedha kama tulivyokuwa tumekubaliana, *management* iliiza mali za kiwanda bila kufuata taratibu na vilevile *management* ilitumia fedha za mkopo tofauti na mkataba wa dhamana.

Sasa taarifa hii ikapelekwa kwenye Kamati ya Serikali ya Majadiliano, Kamati hiyo ilikaa na baada ya kuona kwamba yote ambayo yalisemwa katika hiyo *audit*

committee ni sahihi, Kamati hiyo ikaamuru kwamba ifanyike *management audit* ya kuona kwamba *management* hii ambayo iko *General Tyre* inafanya yale ambayo tulikubaliana na siyo tu kwa dola milioni 10 lakini kwa maana ya uzalishaji mzima wa *General Tyre*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko taarifa iliyopatikana ni kwamba *management* hii haikuwa inafanya kama tulivyokubaliana na kwa sababu hiyo Serikali ikafikia maamuzi ya kuvunja mkataba na huyu mbia na ukizingatia kwamba mbia huyu ndiye ambaye alikuwa na *management* ya kiwanda hiki. Tukavunja naye mkataba baada ya kuonekana kwamba mbia huyu hakuwa na dhamira ya dhati ya kuendeleza uzalishaji katika kiwanda kile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kilichofanyika baada ya Serikali kufanya maamuzi yale ni kwamba *Consolidated Holding Company* wameshafanya uhakiki wa mali za *General Tyre* ili kuisaidia Serikali, tunapofikia hatma ya mkataba huu maslahi ya nchi yetu yazingatiwe. (Makofi)

Vilevile kinachofanyika sasa hivi Serikali inaendelea kuwasiliana na mbia huyu ili tuweze kufikia muafaka na wabia wengine watafutwe, hivi sasa tunao Wachina, Waturuki na wengine kutoka India wanaotaka kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeyasema haya ili Bunge lako tukufu lifahamu kwamba Serikali imelifanyia kazi suala hili lakini tutakuwa tayari kuisaidia Kamati yako tukufu endapo itapenda kupata taarifa zaidi juu ya suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana na naomba kuunga mkono hoja hii. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nianze kuwashukuru na kuwapongeza sana Kamati zote tatu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kipekee sana nipongeze Kamati ya *POAC* kwa kutusaidia sana kuimarisha usimamizi katika Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, kwa msingi huo naomba niseme kwamba pendekezo la Kamati namba 4.1.7 nakubaliana nalo kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kusema mawili, kwanza pamoja na kukubaliana na pendekezo hilo lakini ninapenda Bunge lako tukufu lielewe mazingira ya maamuzi yaliyofanyika wakati ule hasa kujaribu ku-*clear* hisia ambazo zimekwishaanza kujengeka kwenye umma kwamba maamuzi yale yalikuwa hayazingatii maslahi ya umma. (Makofi)

Mwaka 2007 tulikuwa tumeanza kuingiza kwenye mtikisiko wa uchumi duniani, utalii wetu wa Tanzania zaidi ya 90% ni *wildlife based* yaani unategemea wanyamapori

na hao wanyamapori wako kwenye hifadhi na zaidi ya 95% ya huduma zote zinatolewa na sekta binafsi katika mazingira ya ushindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo tulikuwa tumefanya utafiti na kulikuwa na *indications* kwamba chochote ambacho kingefanyika cha kuweza kuongeza bei kingeweza kuathiri sekta nzima ya utalii kwa maana tunaendesha utalii ambao tunaita *low volume high yield tourism*, na kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba kuna hatari ya kitu kinachoitwa *price increase* ukiongeza gharama kwa wawekezaji. Lengo lililokuwepo lilikuwa ni kuokoa sekta ya utalii na niseme kwamba zoezi hilo lilifanyika kwa mafanikio makubwa sana. *low volume height yield tourism*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 wakati tunakwenda kwenye uchaguzi tulitegemea tungepata watalii milioni moja na tungepata fedha dola za Kimarekani bilioni 1.4, tusingefanya chochote kwenye *financial crisis* iliyokuwepo tulitegemea watalii wangepungua kwa 30% lakini kwa jitihada zilizofanyika ikiwemo kupungua *cost increases* kwenye maeneo mbalimbali watalii walipungua kwa asilimia chache na tukapata watalii 896,000 na fedha tulizopata tulipata jumla ya dola bilioni 1.2. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusingefanya hivyo *revenue* ambayo ingepatikana kwenye utalii ilikuwa inakisiwa kupungua kutoka dola bilioni 1.4 ingefikia dola za Kimarekani milioni 980. Kwa hiyo, kwa kuzuia kuongeza gharama kwa kipindi hicho ya shilingi bilioni 21 za Kitanzania, utalii wetu uliweza kunufaika kwa kuwa *resilient* kwenye *pressure* ya mtikisiko wa uchumi na kuweza kuongeza *revenue* dola za Kimarekani milioni 420 na wakati huo wageni badala ya kupungua hadi kufikia 700,000 kutoka *projection* ya milioni moja, wageni mpaka tunafika mwaka 2010 tulikuwa na wageni 896,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niliombe Bunge lako tukufu lielewe kwamba mazingira yaliyokuwepo yalilenga zaidi kuokoa sekta ya utalii na Waziri mwenye dhamana ya sekta ya utalii alitumia Mamlaka yake kuhakikisha kwamba athari hizo ambazo zingeweza kujitokeza hazijitokezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hali hiyo kuwa imepita na ndiyo maana nakubaliana kimsingi na mapendekezo ya Kamati, mwaka 2010 tarehe 20 Desemba nilipokutana na Bodi ya *TANAPA* kwa mara ya kwanza moja ya vitu vya kwanza kabisa binafsi nilivyoanza kuzungumza nao ni kuwaambia kwamba sasa mtikisiko wa uchumi haupo tena kwa hiyo naomba muanze kufanya *revision* na kutekeleza mapendekezo yenu ambayo mliyaleta Wizarani mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye Kamati ya Bunge na yenyewe ikawa imependekeza kitu kile kile. Naomba tu kwamba katika kuyafanya haya Waheshimiwa Wabunge muwe na imani na sisi na muelewe kwamba tunafanya kwa nia njema na kwa kutumia utafiti mahususi. Naomba nishukuru sana.

NAIBU SPIKA: Asante sana, Mheshimiwa Ezekiel Maige na sasa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya atafuatiwa na Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Wiliam Ngeleja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kutoa rambirambi zangu kwa familia na vilevile Jumuiya yote ya wanareli kwa kifo cha Ndugu Sylvester Rwegasira ambaye nilifanya naye kazi nikiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amini!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati hizi zilizowasilisha leo taarifa na ninaziunga mkono zote. Mimi nitajielekeza kwa kifupi tu kuhusu suala la upotevu wa maji jijini Dar es Salaam hasa kupitia mfumo wa maji wa DAWASA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tatizo kubwa lililopo au changamoto kubwa na kwa nini maji yanapotea kwa wingi ni kwa sababu hakika mahitaji ya maji ni makubwa kuliko uwezo wa kuzalisha maji. Matatizo mengine yote ni matokeo ya hilo. Mahitaji ya Dar es Salaam ni karibu lita milioni 450 hadi lita 500 kwa siku, lakini uwezo uliopo sasa ni kuzalisha lita milioni 300 kwa siku na uzalishaji tunaoweza sasa ni lita milioni 273 kwa siku. Kwa hiyo, unaona kwamba karibu 57% tu ndiyo tunaweza kutoa kwa mahitaji ya Dar es Salaam. Sasa mengine haya yanatokana na kugawana kitu ambacho hakipo. Kwa hiyo, ni matatizo makubwa kwani mji unakua haraka, bomba zisizofuata mitaa za aina ya spageti, uchakavu wa miundombinu lakini niseme vilevile kwamba mradi wa mwisho wa kuongeza maji jijini Dar es Saalam ulikuwa ni mwaka 1976 ambao ni mradi wa Ruvu Chini, kwa hiyo, tangu hapo ilitegemewa kwamba mwaka 1986 tungefika kikomo cha uwezo kwa hiyo, tumekuwa tukiishi na deni la maji Dar es Salaam kwa muda wote huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inafanya nini? Tumbaini kwamba tukiweza kutatua tatizo la upatikanaji wa maji Dar es Salaam haya mengine yote tunaweza tukaya-*solve* yaani tunaweza tukayapatia ufumbuzi. Kwa hiyo, Serikali tayari imeshakubali kwamba tutatekeleza mradi mkubwa katika kipindi cha miaka minne ijayo kwa ajili ya maji Dar es Salaam, nao utahusu ujenzi wa bwawa la Kidunda kwa udhibiti wa maji katika mto Ruvu, utahusu upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu kwa kiasi cha lita milioni 60 kwa siku, utahusu upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini kwa kuongeza lita milioni 90 kwa siku na ni mradi ambao tayari umeshaanza. Vilevile uchimbaji wa visima Kimbiji na Mpera ambao tayari tumeshaanza kulipa fidia na tutaanza kuchimba visima hivyo mwaka huu ambao ongezeko jumla kwa shughuli zote hizi nilizozitaja itakuwa tunategemea kupata lita milioni 710 ifikapo mwisho wa mwaka 2013. Kwa hiyo, tutakuwa na ziada kuliko mahitaji ya Dar es Salaam, tukiweza kupata maji hayo na jambo ambalo ndiyo tayari tunalifanyia kazi basi mengine haya yote tunaweza kuyatatua. *(Makofi)*

Niseme tu baada ya hapo tukipata maji zaidi ya mahitaji basi juhudi hizo zitaelekeza vilevile kuwafahamu watumiaji, kuwafungua mita watumiaji, kuzisoma mita

kwa ufanisi zaidi na tutaongeza mapato na tutaboresha mfumo wa maji kwa Dar es Salaam. Mradi huu ni mkubwa tayari Serikali kupitia Baraza la Mawaziri imeshaupitisha na tunaamini kwamba Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Maji hili suala litakuwepo na tunaweza kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia kati ya 57% mwaka 2009, 55% mwaka 2010 kufikia hata 30% ifikapo mwaka 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashukuru sana kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili na ninaunga mkono hoja zote hizi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Wiliam Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana na mimi naungana na wenzangu kuwapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati hizi tatu ambazo wamewasilisha taarifa zao leo na kwa ujumla na mimi naunga mkono katika taarifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda na naomba radhi kwa sauti yangu hii ilivyo, nitajielekeza katika baadhi ya maeneo nikiungana mkono wachangiaji wengine ambao wameongea kabla yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo nataka nijielekeze ni kwenye taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma iliyowasilishwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto na hasa sehemu ya mapendekezo na nijielekeze zaidi kwenye pendekezo namba 4.1.5 ukurasa wa 45 hadi 47 inayohusu Shirika la *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwashukuru na kuwapongeza sana Kamati hii ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa kutambua na hatimaye kusifia mipango mizuri iliyo ndani ya Shirika la *TANESCO* ambayo inaratibiwa pia na Serikali kwa namna ambavyo ikitekelezwa vizuri inaweza kututoa hapa tulipo sisi kama Taifa na kutosogeza katika hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mheshimiwa Kabwe Zitto imesema bayana kwamba mipango iliyopo sasa hivi ni mizuri sana lakini changamoto iliyopo mbele yetu ni ukosefu wa fedha, mipango ipo mizuri na miradi mingi imebuniwa. Kwa kifupi tu niseme miradi ambayo tunayo na ninawakumbusha kwa sababu Kamati inafahamu na Bunge linafahamu.

Katika upande wa uzalishaji tuna miradi mingi imebuniwa ukiondoa hii ya megawati 160 ambayo tunatarajia mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka kesho itakuwa kamili, bado tuna mradi wa Somangafungu megawati 230 tumepata mwendelezaji, mradi wa kule *Artumas* mkoani Mtwara megawati 300, mradi wa Kinyerezi megawati 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi mingine itaendelezwa na wawekezaji binafsi hasa miradi inayozalisha umeme kutegemeana na upepo pale Mkoani Singida na zipo kampuni mbili na zinakwenda vizuri na tuna mradi huu wa Kiwira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisema hapa ni kwamba katika miradi hii hata kama tunaishirikisha sekta binafsi pamoja na mashirika mbalimbali ya umma bado kuna ushiriki wa shirika ama Serikali. Sasa katika miradi hii kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Omari Nundu, naomba sana Waheshimiwa Wabunge hasa kupitia Kamati zetu za Kudumu za Bunge, tutakapokuwa tunajadili wakati wa Bajeti tunaomba miradi hii itengewe fedha hasa kwa maeneo ambayo Serikali inahitaji kushiriki ama kupitia Shirika la *TANESCO* kwenye ile *counter part fund* zipo kama 15% *almost* kwa kila mradi, tukishapata fedha miradi itatekelezwa kwa wakati na itatutoa hapa tulipo na kutusogeza mbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kwamba miradi ya kuiunganisha Mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, tuna mradi umebuniwa kutoka Kahama tunapitia Geita, Nyakanazi kuunganisha Mkoa wa Kigoma, Rukwa pamoja na Mbeya lakini tuna mradi ambao sasa hivi upo katika hatua za utekelezaji kutoka Makambako kwenda Mikoa ya Ruvuma, Songea, Mbinga hadi Namtumbo. Miradi hii yote tuna wafadhili lakini ina sehemu ya ushiriki wa Serikali, kwenye sehemu ya usambazaji tuna Wakala wetu ambaye tumeubuni kama Taifa Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA*. (*Makofi*)

Kwa kipindi kilichopita tumewatengea zaidi ya shilingi billion 100 na ni kweli tunaona miradi katika Mikoa 16 inatekelezwa na nafahamu Waheshimiwa Wabunge hapa wakiwemo rafiki yangu Mheshimiwa Moses Machali, kule Kasulu na Kibondo miradi inaonekana tunasema jenereta zimeshafungwa lakini usambazaji sasa nafahamu nimemueleza kwamba nyaya ziko kwenye meli zinakuja, zilikuwa zimeagizwa China na wakandarasi wanakuja. Lakini kitu ninachosema ni kwamba bado tunahitaji kuyafikia maeneo mengi zaidi ya Watanzania kupitia Wakala wa Nishati Vijijini. Maana yake ni nini? Yote hii itajitafsiri katika Bajeti zetu.

Kwa hiyo, ombi langu hapa pamoja na kwamba ni ombi la awali na tunafahamu kanuni haziruhusu kuwahisha jambo kwenye Bunge hili Tukufu, lakini ni angalizo la awali kabisa kwamba utakapofika wakati tupeni Wizara ya Nishati na Madini hasa kwenye nishati mwaka huu. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu ajalie tuwe namba moja katika makadirio ya fedha tutahakikisha kwamba tunatekeleza miradi hii kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kiwira liko chini ya Shirika Hodhi ya Mashirika yaliyokuwa ya Umma (*CHC*), wanaendelea kulisimamia, kuratibu taratibu na wawekezaji wafadhili wameshaonekana wamejitokeza wengi zaidi ya mmoja, lakini utaratibu unaendelea vizuri na hivi karibuni tutatoa taarifa ya utekelezaji wake. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. *(Makofi)*

Kwanza napenda niungane na Waheshimiwa wenzangu kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Sylvester Rwegasira, aliyekuwa Katibu Mkuu wa *TRAWU*. Tunaiomba familia iwe na moyo wa subira. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nizipongeze taarifa zote ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti wa Kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nichangie katika eneo linalohusu masuala mazima ya watumishi hewa. Ofisi yangu ilifanya uhakiki katika Wizara ya Elimu kwa upande wa walimu wa wa shule za sekondari, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na sekta ya Mahakama na sasa hivi tunaendelea katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona ukubwa wa tatizo hili ofisi yangu sasa hivi tunafanya maandalizi ya kufanya uhakiki katika Wizara zote na katika Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba suala hili la kufanya uhakiki wa watumishi hewa linafanyika katika Utumishi wa Umma wote na pia sasa hivi tunaboresha mifumo yetu ya kompyuta ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na taarifa sahihi za watumishi ambao wanapaswa kulipwa mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hii ya sasa hivi ambayo tunaifanyiakazi ambayo tayari baadhi ya Halmashauri zimeshaanza kuitumia itakuwa inawezesha kila mwajiri, ndani ya utumishi wa umma kuweza kuingiza wenyewe takwimu za watumishi wao wanapoajiriwa na kupandishwa vyeo na hata wanapostaafu na sisi kazi yetu Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, itakuwa ni kuwahakiki na kuthibitisha na kuwapelekea wenzetu wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani kabisa kwamba utaratibu huu na mfumo huu utatusaidia sana kupunguza tatizo la watumishi hewa na pia kuweza kuwachukulia hatua wale watumishi ambao wanahusika katika kuitia Serikali hasara. Hata hivyo sasa hivi ofisi yangu imeanza kuwafuatilia wale wote ambao wamehusika katika kuisababishia Serikali kupata hasara kupitia watumishi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, amesema kwamba utaratibu huu tuhakikishe kwamba unafanyika kwa haraka. Napenda nimhakikishie kwamba ni lengo la ofisi yangu kwamba ifikapo mwezi wa Kumi na Mbili mwaka huu, mamlaka zote za ajira chini ya utumishi wa umma wawe wameanza kutumia mfumo huo. Utakuwa tayari umeboreshwa na hivyo utatusaidia kuweza kupata kwa haraka zaidi na kuwabaini watumishi hewa na hivyo kuweza kuwaondoa. Lakini pia utaweza kutusaidia kuwabaini waliosababisha watumishi hewa kwa sababu mfumo uliokuwepo ni vigumu sana kuweza kufahamu kama hilo tatizo limesababishwa na Halmashauri au utumishi au Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa utaratibu ambao sasa hivi tunao unaweza pia hata kufahamu watu ambao wanatumia cheti kimoja katika maeneo tofauti, utasaidia kuwaingiza watumishi kwa haraka zaidi na hasa halmashauri zile ambazo wameanza kutumia wameona manufaa yake. Pia itapunguza suala zima la malimbikizo ya mishahara kwa watumishi na pia itawezesha mwajiri mwenyewe kuwaondoa wale wanaofariki katika mwezi unaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa niombe ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge. Nimepewa mamlaka ya Kikanuni kwamba kwa kutegemea shughuli zinazoendelea ndani ya ukumbi wa Bunge, ninaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge. Kwa hiyo naomba kwa mamlaka hayo niongeze muda huo, tuvumiliane ili tutende haki kidogo kwa sababu wanafuata Mawaziri wawili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao hizi taarifa kimsingi Wizara zao ndiyo zimeshughulika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwapa dakika tano tutakuwa tumewaminya kidogo na baada ya hapo tuwape Wenyeviti wetu dakika kumi, kumi, lakini mnaweza mkaruka majina na nini mkaenda kwenye hoja moja kwa moja ili tuzitendee haki ripoti hizi. Moja kwa moja naomba nimuite Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa dakika 10. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizojitokeza leo. Kwanza, nilikuwa nimejiandaa kujibu kila kitu kilichojitokeza, hata hizo dakika 10 hazitoshi lakini itoshe tu kwamba nawashukuru sana Wenyeviti wote na Wajumbe wote wa Kamati hizi tatu kwa maoni yao yote na mimi ninasema Wizara ya Fedha itashirikiana na Kamati hizi katika yale yote ambayo wameyaona na kuyapendekeza na hasa yale ambayo moja kwa moja yamegusa Wizara ya Fedha. Lakini pili nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuturuhusu mimi na mwenzangu angalau tutumie hizo dakika 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie tu mambo machache ambayo yamezungumzwa. Kwanza Wizara ya Fedha imeguswa na Kamati zote lakini vilevile imeguswa na karibu kila aliyezungumza na katika yote tuliyoyapata kwa maandishi karibu yote nayo asilimia 75 yamegusa Wizara ya Fedha. Sasa kwa sababu ya muda niseme tu kwamba tumeyapokea na tutayafanyia kazi na kama itabidi kuyaandikia tutayaandikia lakini nishukuru kwamba tumeyapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na moja ambalo lilizungumzwa na Kamati ya Mashirika ya Umma, nalo linahusu mikataba kwa wafanyakazi wa *PPF*. Tanzania imekuwa ikibadilisha sera, kuna wakati viongozi hata mimi nilipokuwa kiongozi wa *NSSF* nilikuwa kwenye *pension terms* kwa hiyo nilikuwa nafanyakazi mpaka nifikie umri wa ku-*retire* nikapata *pension* yangu nikaondoka zangu. Lakini

baadaye tukaja tukapata ushauri kutoka kwa wataalamu kwamba ni vizuri viongozi hawa wapatiwe mikataba badala ya kuwa *pensionable*. Nadhani Mheshimiwa Mbunge Deogratias Ntukamazina atakumbuka sana kwa sababu alikuwa Katibu Mkuu wa Utumishi wakati ule na hili likakubalika. Kwa hiyo, viongozi wengi siyo *PPF* peke yake wakapewa mikataba, wengine ya miaka mitatu, mitatu na wengine ya miaka mitano, mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pale *PPF* kuna wafanyakazi wa aina mbili, kuna wafanyakazi ambao wako kwenye mikataba na kuna wafanyakazi ambao wako kwenye masharti ya kudumu. Wale ambao wako kwenye mikataba ndiyo hawa ambao akimaliza mkataba wake kwa sababu kama ni mkataba unaandikiwa barua ambayo ina-*spell* masharti ya ajira yako, utapata hiki, utapata hiki na mwisho wa miaka yako ya mkataba utapata kiinua mgongo au kwa kingereza *gratuity* ya asilimia fulani. Sasa ndiyo hiyo *gratuity* ambayo wanapata wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Shirika la Bima ambalo *PPF* ilitokea ilikuwa ni mfumo wa *endowment scheme*. Sasa wafanyakazi hawa walikuwa wanachama wa hii *endowments scheme* na walihama nayo. Kwa hiyo, *endowment scheme* imeendelea mpaka hivi ninavyozungumza *endowment scheme* ipo hata wale wafanyakazi ambao wako kule Bima wanapata hiyo *endowment scheme*.

Kwa hivyo bodi yao iliidhinisha hiyo na inaendelea. *Gratuity* ina masharti tofauti lakini *endowment scheme* inalipiwa kodi 30% kwa hiyo unapopata hiyo *endowment scheme* yako wakati wa mwisho wa ajira yako ama umestaafu au mkataba wako umekwisha au umeachishwa kazi au mfanyakazi amefariki kabla ya muda wake wa kustaafu haujafika analipwa lakini zile fedha kuna kiwango kinapelekwa kwa *TRA*, *TRA* wanafanya *assessment* inalipiwa kodi. Kwa hivyo, si kweli kwamba wamekiuka sheria au kwamba wamekiuka sheria za *TRA*, sheria za *TRA* zinafuatwa na *TRA* wanaruhusu na wanaikata kodi. (*Makofi*)

Ningependa pia nizungumzie *Consolidated Holding Corporation (CHC)*. Hili napenda mia kwa mia nikubaliane na mapendekezo ya Kamati kwamba *CHC* kwa miaka mitano iliyopita imefanyakazi nzuri sana na tumekubali mapendekezo ya Kamati na kwa bahati nzuri Serikali iliishaanza kulifanyiakazi hili kabla hata Kamati haijaja na mapendekezo yake. Waraka wa Baraza la Mawaziri umeshaandaliwa sasa hivi uko kwenye *Cabinet Secretariat*, baada ya hapo utakwenda kwa Makatibu Wakuu na baadae nitaupeleka kwenye Baraza la Mawaziri. Nina matumaini kwamba utapitishwa na tena kabla ya tarehe 30 Juni, 2011 kwa sababu uhai wa Shirika hili unafikia kikomo chake tarehe 30 Juni. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba tutafanikiwa kuupitisha katika hizo *processes* zote kabla ya mwezi Juni.

Mapendekezo ni ya aina mbili; pendekezo la kwanza ninalopendekeza ni kwamba Shirika hili liruhusiwe kuwa shirika *perpetually* kwa sababu lina kazi ya kufanya mpaka hizo kazi zikiisha ndiyo tuseme kwamba shirika hili sasa hatulihitaji basi lifutwe. Lakini mbadala maana huwezi kusema kwamba kila mtu ata-*approve* hivyo nilivyopendekeza lakini mbadala wake ni kwamba ikiwa hili la kwanza halitapata idhini ya Baraza la

Mawaziri basi shirika hili liruhsuwiwe uhai mwingine wa miaka mitano ili liweze kukamilisha zile kazi ambazo zinafanyika, kwa hiyo, Kamati naishukuru kwa mapendekezo haya na nasema tunayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni dhamana. Imezungumzwa na karibu Wajumbe wote, kila nilichokiona hapa nikisoma suala la dhamana limo. Suala la dhamana lina sheria yake, kuna Sheria ya mwaka 1974 kwa wakati wangu mimi nikiwa Waziri kwa miaka mitatu na nusu iliyopita tunafuata ile sheria, kwa hiyo, si kweli kwamba hatufuati ile sheria. Tuna Kamati maalum (*a mixed grill committee*) *across the whole corners, private sector*, Benki Kuu na wengine wengine. Ile Kamati inakaa *ina-assess* maombi, wakikubaliana nayo ndiyo wanapendekeza kwa Waziri na Waziri naye sio kwa sababu wamependekeza anakubali, lazima aridhike kwamba yale mapendekezo yana manufaa kwa Taifa, ukiidhinisha ndiyo yanatokea. Sasa hivi Wizara yangu haitoi tena dhamana kwa makampuni binafsi kwa sababu Benki Kuu wameunda mifuko kadhaa ikiwepo *small and medium enterprises guarantee fund* na *export and credit guarantee fund*. Sasa *private company* yoyote ambayo inapenda kupata *guarantee* wanatakiwa kupitishia maombi yao kwenye mabanki yao na Benki Kuu ikikubali inawapa *guarantee* kule. Kwa hiyo, zile ambazo zilikuwa zimetokea, zimetokea lakini tunazi-*enforce* kwamba zilipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba kuanzia sasa Wizara ya Fedha haitoi *guarantee* kwa makampuni binafsi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama naweza kuruhusiwa niseme moja la misamaha. Basi naunga mkono hoja, mengine tutakuja kuyajibu wakati tutakapoleta Muswada wangu wa Bajeti. Asante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumeapishwa hapa ndani leo ni siku yangu ya kwanza kusimama kwa hiyo, ningependa nichukue nafasi hii kwanza niwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Newala kwa kunirejesha tena kwa kishindo humu ndani kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue pia nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzangu wote tuliomo humu ndani. Kila mmoja kaja kivyake amepitia kwake, hoja ilikuwa kuingia hapa ndani, tumepata sasa ila imani ambayo wananchi wametupatia tushirikiane ili tujenge nchi yetu Tanzania paendeleo kuwa mahali pazuri pa kuishi. *(Makofi)*

Napenda pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu kunikabidhi Wizara hii ambayo ndiyo Wizara ya maendeleo vijijini na maendeleo mijini katika nchi hii, kwa kunipanga mimi nimsaidie Waziri Mkuu katika kuendesha Wizara hii. Mimi pamoja na Naibu Mawaziri wangu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Hai, aah Mbunge wa Siha, yule wa Hai yuko Waziri Kivuli,

pamoja na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kule Lindi. Tumeahidi kwamba tutafanya kazi kwa juhudi na maarifa, kwa ujasiri, kutenda haki bila kuonea mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ambayo sisi tuko chini yake, Kamati ya LAAC ambayo iko chini ya Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema. Watu wamekaa kule nje kutafuta Mtanzania gani mwenye akili tumpe udaktari, wala hakujaza fomu, wala hakufanya mtihani ikamuangukia kura Augustino Lyatonga Mrema. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa huyu mzee huko nyuma kafanya mambo mengi, katuambia aliwahi kukamata dhahabu na nini, na nini, sasa tuna amini kwamba ukali ule ule katika kusimamia maslahi ya Watanzania ataendelea nao ndani ya Kamati na sisi tumeshakutana na Kamati, tumeelewana kwamba Kamati pamoja na Wizara tuna kazi moja tu ya kusafisha maovu katika Serikali za Mitaa na kuhakikisha fedha zinazopelekwa zinafanyakazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu sisi walituita kutaka kujua tumetekeleza vipi maagizo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Walifoka foka pale kabla hatujawaeleza, lakini tulipowaeleza mambo yaliyofanyika wakasema basi kumbe ninyi hapo hamkupelekwa kwa makosa. Kwa hiyo, tumeahidi sisi na wao kushirikiana kufanya kazi na kuhakikisha kwamba Serikali za Mitaa zinafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Napenda pia nipongeze Kamati ya wenzetu wanaohusika na Mashirika ya Umma na Kamati ya Hesabu za Serikali. Nitagusia yale ya kwenye Serikali za Mitaa kwa sababu kule sisi ndiko tupu. Mimi napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu, mmeongea kwa uchungu kuhusu Serikali za Mitaa maana mnafahamu kwamba Serikali za Mitaa ndiyo nguzo ya maendeleo vijijini na mijini katika nchi hii. Mapendekezo yenu na maelekezo tumeyasikia, tutayafanyia kazi na kuwapa mrejesho na kwa vile muda ni mfupi nitagusia tu baadhi ya yale maeneo ambayo yamegusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa lililozungumzwa hapa ndani ni ubadhirifu katika Serikali za Mitaa. Mimi nataka nichukue nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Watanzani wenzangu kwamba wasimamizi wakubwa wa mamlaka za Serikali za Mitaa ni Waheshimiwa Madiwani katika maeneo yao tukiwemo na Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya TAMISEMI haiwezi kuleta miujiza ikakomesha wizi, ubadhirifu bila msaada wa Waheshimiwa Madiwani. Kwa hiyo, sisi Wizarani tumeamua kwamba tutakuwa wakali, tunaomba Mabaraza ya Madiwani nao wawe wakali, wasimamie fedha zinazopelekwa katika maeneo yao na kuwachukulia hatua watumishi wanaohusika bila kuwaonea. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kwamba kila mmoja ana wajibu wa kutekeleza kwa hiyo, tunaomba na sisi katika maeneo yetu tuwe wakali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa habari ya ukaguzi hapa. Serikali imekwishafanya maamuzi kwamba si sawa sawa Mkurugenzi akawa anaendesha

Halmashauri akawa huyo huyo ndiye anamwezesha Mkaguzi wa Ndani kufanya kazi. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2011, Wakaguzi wa Ndani kwenye Halmashauri zote wanahamia kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili waweze kutukagua vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi palikuwa na michango hapa Mheshimiwa mmoja amelalamikia akasema wananchi wanachangishwa kwa nguvu. Sasa naomba niseme hivi michango chini ya Serikali inayoongozwa na CCM ndiyo sera zetu na wale waliotuchagua wamejua kwamba sisi tunapotaka mambo yaende haraka fedha za Serikali kama hazitoshi tunaomba wananchi waongeze nguvu zao. Tumefanya hivyo ndio maana leo Tanzania kila Kata ina shule za sekondari. Tunesema tunangoja tu hela za Serikali leo tusingekuwa na shule za sekondari kila Kata. Wapo watu walinadi kwamba kila kitu tutafanya bure, tuta-*provide* bure, lakini Watanzania wamesikiliza wakasema hapana tuwapigie hawa wanaosema tukachangie nguvu zetu wenyewe. (*Makofi*)

Sasa michango haiwezi kuwa ya nguvu kwa sababu kama sheria inafuatwa, michango ya kijijini inaidhinishwa na Serikali ya Kijiji. Mradi kwenye Kata unaidhinishwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata chini ya Mheshimiwa Diwani. Sasa suala la michango ya nguvu linatoka wapi? Sasa kama ipo michango hiyo mnayoisema ya nguvu ambayo haikupita kwenye *WDC* ambayo haikupitishwa kwa Kamati ya Serikali ya Kijiji naomba Waziri wa TAMISEMI ajulishwe. Watanzania wenzangu wote simu ya Waziri wa TAMISEMI ni 0784 245300. Nipigieni simu nileteeni *message* kama mnavyoleta na nitazifanyia kazi. Hiyo ndio simu ya Waziri wa TAMISEMI na unampata Waziri wa TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mahali Tigo inafanya kazi namba ya Waziri ni 0713 245300. Kwa hiyo, tunachosema sisi tutaendelea kuunganisha nguvu za wananchi na nguvu za Serikali katika kutafuta maendeleo yetu. Hata hapa Tanzania hiyo mikoa ambayo wamepiga hatua kwenye elimu, shughuli mbalimbali wala tusidanganyane wananchi wamechangia maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ilijitokeza hoja hapa kwamba miradi haimaliziki kwa vile fedha zikipelekwa Halmashauri zinarejeshwa Hazina. Mheshimiwa Mbunge mmoja alijaribu kuweka mambo sawa hapa, lakini nadhani hakueleweka. Sasa mimi Waziri ninayemsaidia Waziri Mkuu kwenye Wizara hii nataka kutoa kauli ya Serikali kwamba hakuna, hii si kweli, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri mwaka wa fedha unapokwisha wana *carry forward* wanarudishiwa waendeleo. Kwa sababu wakati mwingine inakuwa hawajalipa kwa sababu mkandarasi yuko *site* hajamaliza. Sasa ukimnyang'anya zile pesa wakati tayari Halmashauri imeji-*commit* utaingiza Halmashauri katika matatizo na itashitakiwa. Kwa hiyo, fedha hizi hatuzichukui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja hapa kukosekana kwa usahihi wa taarifa za mapato na matumizi, sisi tunakubali. Serikali kwa sasa inaimarisha mfumo wa utoaji taarifa za mapato na matumizi. Wataalamu kwenye kompyuta wanaita mfumo wa *EPICOL* kwamba kila Halmashauri nchini wako katika mafunzo na itakapofika Julai 1, 2011 Halmashauri zote zitakuwa zimeingia katika mtindo huu. Faida ya mtindo huu ni

kwamba unawazuia kutumia fedha nje ya malengo na shughuli zilizoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Sasa nataka kurudia kusema mabadiliko chanya ya maisha ya Watanzania yatapatikana tu endapo kutakuwa na ufanisi wa utendaji katika Serikali za Mitaa. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Madiwani na wadau wengine kuchukua hatua za haraka badala ya kusubiri Wizara peke yake. Sisi tunapokwenda kutembelea, mimi na Naibu Mawaziri wangu, tumekwenda mahali tukakuta miradi ambayo haipo katika ratiba lakini wananchi wametupigia simu kwamba mahali fulani hela imeliwa. Sisi tunalazimisha, tunawaambia Mheshimiwa DC nimeambiwa kuna mradi mahali fulani mzuri sana nataka nikaukague maana umepata sifa nzuri sana. Ukienda kule unakuta jengo, hela imelipwa yote awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu lakini jengo limepauliwa tu. Ndio maana nimetoa namba hapa. Mkituletea habari kama hizo na pale yupo Mheshimiwa Mwanri kada, pale yuko Majaliwa kada, mwalimu hapa yuko mwalimu lakini askari mstaafu kweli huyo jambazi atapona? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, tayari? Kengele imeshapigwa?

NAIBU SPIKA: Tayari.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa kuunga mkono hoja zote tatu, tutashirikiana kufanya kazi ili Tanzania paendeleo kuwa pahali pazuri pa kuishi. Asante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli tutakubaliana kuwa muda umekuwa ni mdogo na mambo ya kuyaelezea ni mengi.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi taarifa hii ya Hesabu za Mashirika za Umma. Pia nawashukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa imani yao kwangu, nami naahidi kuwatumikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mifuko ya Pensheni imekuwa tatizo kubwa sana hususani kwa watumishi ambao baada ya kufikia ukomo wao wanapata shida kupewa mafao yao. Mifuko hii imeanzishiwa kwa mujibu wa Sheria, taratibu na kanuni za mashirika husika. Leo hii kuna tofauti kubwa sana katika malipo ya uzeeni. Mtumishi anayestaafu chini ya Mfuko wa *NSSF* anatofauti kubwa sana ukilinganisha na mtumishi aliye chini ya mifuko mingine mfano *PSPF*, *LAPF* na *PPF*. Mfuko huu kila mara wanafanya tathmini ya wafanyakazi na mpate *update list* lakini bado kupata malipo yao

ni kazi kubwa sana katika mazingira mengine watumishi wanalipwa pesa kidogo sana ukilinganishwa na kile wanachopaswa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu unaendesha au unafanya biashara. Mfano kandarasi za ujenzi wa majumba na kadhalika. Lakini fedha inayopatikana kutokana na miradi wanachama hawapewi au kuongezewa gawio la faida katika akiba zao. Kitu ambacho pesa yao inatumika kama mitaji lakini faida haitolewi kwa aliyetoa mtaji. Jambo hili si haki kwa wanachama wa mfuko huu wa *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mfuko huu ufanye yafuatayo, kwanza kufuatilia kwa waajiri michango ya wanachama wao ili kutunza *record* ya michango ya watumishi wanachama wa mfuko, pili, kuwepo na taarifa ya mara kwa mara kwa maendeleo/hesabu za wanachama, tatu, kupunguza asilimia ya makato ya matibabu kwa wanachama wa mfuko, nne, kuwepo na Bodi na ndani ya Bodi hiyo kuwepo na wawakilishi wa wanachama wa mfuko (wadau) na tano, pindi mikataba ya ukandarasi/ujenzi au shughuli ya kibiashara inapofanyika basi kuwepo na gawio linalotokana na faida hiyo kwa wanachama wa mfuko kwani mtaji ni pesa ya wanachama na mfuko huo. Naomba kuwasilisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja ya Hesabu za Mashirika ya Umma katika utendaji wa Mashirika ya Umma. Kuna baadhi ya mashirika/mamlaka wanafanya kazi moja katika eneo moja lakini mashirika/mamlaka tofauti.

Mfano *EWURA* na *TBS* katika upande wa mafuta mamlaka hizi zote zinafanya kazi moja kiasi cha kuwachanganya wananchi. Huo ni mfano tu. Lakini bado yapo mashirika/mamlaka nyingi za aina hii.

Mheshimiwa Spika Naibu, naunga mkono hoja ya usimamizi wa Mashirika ya Umma wayachambue na kuwawekea mipaka ya shughuli zao kwa maslahi ya wananchi.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Hesabu za Serikali Kuu, Hesabu za Serikali za Mitaa na Hesabu za Mashirika ya Umma pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unagusa hasa katika maeneo mawili. Kwanza ni kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma katika kutekeleza miradi na shughuli husika, suala hili halistahili kufumbiwa macho, hatua za kunidhamu zichukuliwe. Pili, suala la malipo hewa ya watumishi takribani milioni 700 ni nyingi nadhani hiyo inatokana na mlolongo wa ku-*track record* za watumishi wa Serikali. Hiyo inajidhirisha wazi, mfano kwa watumishi waliostaafu au wamekufa, utakuta muda unaotumika kufuatilia malipo hayo ni mrefu na kila wakati mtumishi anaelezwa kuwa faili lake halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuulize Mheshimiwa Mrema anieleze kwa mfano kaka yangu Godfrey Manyanya Komba alifariki mwaka 2009 akiwa mtumishi wa

Halmashauri ya Wilaya ya Temeke na amefanya kazi pale zaidi ya miaka miwili amefariki wanasema faili lake halipo. Nieleze Mheshimiwa huu kweli ni uungwana au utendaji mzuri wa eneo unalosisimamia (*local government*)?

Nashauri utaratibu huo uboreshwe na ikibidi mashirika hayo ya *pension* yakusanye taarifa ya watumishi kabla ya kustaaifu au kufa. Pia iwe ni wajibu mwajiri ku-*update records* hizo angalau kila mwaka. Kwa hiyo, mbali ya Serikali kuibiwa pesa zake kwa malipo hewa, nayo haitendi haki kwa kutowalipa wadai pesa zao kwa ajili ya kukosa kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mashirika ya Umma yahapati pesa za kutosha na kwa wakati katika kutimiza malengo yake. Wakati wa Bajeti Bunge linasisitiza matumizi makubwa kwa ajili ya shughuli za matumizi kuliko uzalishaji. Hali hiyo inafanya mashirika ambayo yapo *responsible* katika kukuza uzalishaji na Pato la Taifa kusinyaa na kutokuwa na tija. Tunakamua kwa ng'ombe aliyekonda au mgonjwa. Hali hiyo inafanya kuchelewesha kwa ukuaji wa uchumi. Maamuzi yetu ya kuwekeza hayaendi kwa wakati ndiyo maana matatizo yanazaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya *EPZ* kama vile Bagamoyo, Songea nayo muda mrefu hayajalipwa fidia, wananchi wanakosa imani na malengo yaliyokusudiwa. Nashauri umuhimu ujitokeze katika Bajeti hii ili kutoa fidia kwa wananchi. Naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza taarifa zote tatu za Hesabu za Serikali za Mitaa, Hesabu za Mashirika ya Umma na Hesabu za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kuwepo malipo ya mishahara kwa watumishi hewa ni suala ambalo limekuwa linajirudia rudia kila mwaka. Hii ni aibu kubwa kwa Taifa na inaonesha ni jinsi gani Serikali isivyokuwa makini katika utendaji wake. Hazina wanawezaje kutuma pesa za mishahara kwenye *account* za watumishi pasipo kujua mtumishi huyu yupo kazini, amekufa au amesimamiswa kazi? Wakati walimu wakilia waongezewe mishahara hasa wale wanaoishi vijijini kwenye mazingira magumu bila kufikiwa tunaambiwa shilingi milioni 792.9 zimelipwa watumishi hewa. Hii ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Halmashauri za Wilaya wanajua sana kwamba kuna udhaifu wa ufuatiliaji Serikali na hata wakipatikana na makosa ya ubadhilifu sana sana wanahamishwa kwenda kuiba pahala pengine. Kukosekana utaalum na utashi wa kuingia mikataba yenye manufaa kwa Halmashauri ya Wilaya na Majiji nayo ni tatizo. Kituo cha mabasi cha Ubungo ni mradi mkubwa na kitega uchumi ambacho kinawanufaisha watu fulani fulani na siyo Taifa. Pale Ubungo yoyote anayeingia ndani ni shilingi 200/=, gari dogo shilingi 500/= gari kubwa shilingi 1000/= kwa siku pesa inayokusanywa ni nyingi sana. Pesa ya Kituo cha Ubungo peke yake mapato yake yangeweza kuyapa miundombinu ya maji na barabara kwa jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *M/S Smart Holding Company Ltd.* Ndiyo inanufaika na kituo cha Ubungo kwa siku wanakusanya shilingi milioni 4.6 *per day* kwa uchache. Kinachotolewa Halmashauri ya Jiji ni shilingi milioni 1.5 (32.6%) Kampuni inachukua 67.4% kweli?? Nani mwenye Kampuni hii? Tunaitaka Serikali kufuatilia kwa makini kituo hiki na kuhakikisha mapato ya kituo hiki yananufaisha Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani ndiyo wasimamizi wakuu wa fedha za wananchi kwenye Halmashauri zetu. Ni muda umefika sasa Serikali ikajenga uwezo kwa Madiwani wote wa Halmashauri zote. Kamati zote za fedha za madiwani zijengewe uwezo wa jinsi gani ya kudai taarifa mapema kutoka kwa watendaji na kudhibiti matumizi.

Wakati wa Baraza la Madiwani muda unaotolewa kwa Madiwani kupitia taarifa za Halmashauri ni mdogo mno na haumpi mjumbe wasaa wa kusoma kwa undani na kugundua udhaifu, litolewe agizo kwenye Halmashauri za Wilaya siku saba kabla ya kikao ili waweze kuzipitia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho watendaji wanapatikana na kosa la ubadhirifu wa fedha za wananchi wachukuliwe hatua madhubuti ili iwe ni fundisho kwa wengine na sio kuwahamisha kutoka kituo kimoja kwenda kingine. Huku ni kulingana na Serikali inalea uzembe na hivyo kuruhusu vitendo kuendelea.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kukaimu kwa muda mrefu hivyo kushindwa kufanya maamuzi makubwa na magumu. Wakati mwingine watumishi wa Halmashauri za Wilaya kushindwa kuelewa ni kwa nini Kaimu huyo hathibitishwi wakati ni mchapakazi na mwadilifu. Mfano mzuri ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro *Engineer* Maziku. Naomba athibitishwe kwani Ngorongoro ni Wilaya ya pembezoni na yenye mazingira magumu.

Pili, fedha nyingi za Halmshauri zinaliwa na Wakandarasi kupitia *tender* mbalimbali zenye mgao kwa wakuu wa Halmashauri wa Wilaya waliotoa kandarasi hiyo kama *DED* na kadhalika.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo zitolewe kwa wakati muafaka ili wafadhili waweze kujenga imani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazorudishwa Serikalini ikiwezekana ufanyike utaratibu wa *re-allocation* zitumike kwenye vitu vingine. Muda wa Kamati ni mdogo uongezwe. Asante.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Kamati kwa kazi kubwa ya uchambuzi ambayo imefanywa. Naunga mkono taarifa iliyoletwa na Mwenyekiti na maainisho yote ambayo Mwenyekiti ameanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwenye Halmashauri zetu nchini kwa dhamira ya kuboresha maendeleo kwa wananchi wetu, kama ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ambazo Serikali imekuwa inatoa zitawekewa mikakati thabiti na usimamizi wa kina toka kwetu Wabunge na Madiwani katika Halmashauri zetu. Ni dhahiri kuwa dhamira ya Serikali katika kutoa huduma stahili kwa wananchi wetu, itakamilika na wananchi wataona matunda ya Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Halmashauri na viongozi wa kuchaguliwa katika Halmashauri zetu nchini wamekuwa ndio chanzo cha Serikali kushindwa kutekeleza majukumu yake. Wote wameweka mbele mahitaji au maslahi binafsi badala ya umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kuonyesha wametumia shilingi 15,000,000/= kwa ununuzi wa *injector pump* ya gari *Toyota LandCruiser* na Kamati kugundua kwamba gharama halisi ya *Injector pump* hiyo ni shilingi 3,000,000/= ni kielelezo tosha Halmashauri nyingi nchini kuna ubadhirifu mkubwa katika fedha za Serikali na ubinafsi kwa watendaji badala ya kutumikia watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wizi wa makusudi na ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji hawa wabadhirifu katika Halmashauri zetu na Serikali kuu kwa ujumla. Kwa kuwapeleka Mahakamani kwa kosa la wizi wa kuongeza gharama halisi za kusudio. Watendaji hata kama wamehamishwa katika Halmashauri husika warudishwe kule kule walikoharibu na kushitakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningepomba kwa Serikali nadhani wakati umefika kuajiri Watendaji Wakuu wa Halmashauri, Wakurugenzi (*DED*) wakaajiriwa kwa mikataba ya miaka miwili, miwili ili tuweze kupima uwezo wao na kuona kama kuna haja ya kuendelea nao. Wakimaliza mikataba yao na wakishindwa wasipewe mikataba mipya, itasaidia kufanikisha malengo ya Serikali. Nashukuru.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja ya Hesabu za Serikali za Mitaa kama ilivyoletwa mbele yetu.

Kwanza naiomba Kamati hii kuwa makini sana na mahesabu hayo ya Serikali za Mitaa, kwani kuna mishahara hewa mingi sana, kuna walimu wa shule za msingi ambao pia ni watendaji wa mitaa. Swali langu mtu huyo hulipwa kama mwalimu au hulipwa kama mtendaji wa mtaa? Akilipwa kama mwalimu, pesa ya mishahara wa mtendaji wa mtaa inakwenda wapi?

Nadhani mfanyakazi wa Serikali hulipwa mishahara mmoja tu. Kama mfanyakazi huyu analipwa mishahara miwili ya ualimu na utendaji wa Serikali ya Mitaa hii ni halali, kama si halali inaieleza nini Serikali? Mimi binafsi naona hili ni tatizo kubwa na pia

linapunguza ufanisi wa kazi za watendaji wa mitaa na elimu kwa watoto wetu ambao wanakosa masomo kwa wakati mwalimu akiwa anahudumia kazi za mtaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iliahidi kuwa inarudisha asilimia ishirini za mapato ya mtaa kwenye mtaa ili Wenyeviti wa Mitaa waweze kupata mishahara lakini siyo hivyo, Wenyeviti ambao hufanya kazi kubwa hawana mishahara hata kidogo na wao hufanya kazi mchana na usiku lakini watu hawa wamesahaulika. Naiomba Kamati hii iingie ndani zaidi kwani Wenyeviti wa Mitaa wanagandamizwa zaidi na maslahi yao, hawayapati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna baadhi ya Madiwani kuingilia pia kazi za Wenyeviti wa Mitaa, ni vizuri zaidi na ni wajibu wa diwani na Wenyeviti katika kata husika kufanya kazi kwa pamoja, lakini baadhi ya madiwani siyo hivyo, hivi kweli kama ndivyo hivyo si rahisi diwani kuwa pamoja na kuwatetea Wenyeviti wake. Naiomba Kamati ihimise Halmashauri zake kutenga pesa kwa mafunzo kwa Wenyeviti wa Mitaa na madiwani kuwaelimisha ukomo wa kazi zao na umuhimu wake kwa wananchi na Wenyeviti dhidi ya madiwani. Cha muhimu ni kufanya kazi kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Waheshimiwa wote ambao wanaisababishia Serikali hasara wachukuliwe hatua za kisheria na kufikishwa mbele ya Mahakama. Pia kufilisiwa mali ambazo wamezipata kwa ubadhirifu. Wengi wao huandika majina ya watoto au ndugu zao, ni vizuri yote kwenda kwa pamoja ili iwe fundisho kwa watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mishahara hewa, mipango inayofanywa kwa ulipaji. Asante.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika suala laa wafanyakazi hewa (*ghost workers*). Suala hili limejitokeza katika Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina mbili za wafanyakazi hewa, wale ambao tunawaelewa mfano waliokufa na waliostaafu kazi na kuna wafanyakazi hewa wa kutengenezwa kwa makusudi. Aina hii ya pili wanatengenezwa ama katika Wizara au Idara, kwani hujitokeza katika *payroll* bila ya kujulikana wanafanya kazi katika eneo lipi la Wizara, bali *payroll* inaporejeshwa aliyefanya vile hujichotea mamilioni ya fedha na kuitia hasara Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayefanya hivi anajulikana na hachukuliwi hatua yoyote. Huu ni udhaifu mkubwa wa Wizara kwa kupoteza mabilioni ya fedha. Haiwezekani wala sitaki kuamini kwamba Afisa Masuuli haijui idadi ya wafanyakazi wake, ikiwa hivi ndivyo basi ni vizuri. Afisa Masuuli kuweka mikakati yake ili kuzuia upotevu fedha hizi za umma Mwalimu Nyerere alisema *It can be done, play your part*.

Suala la manunuzi nalo ni tatizo katika Wizara. Wizara zina udhaifu wa kuweka stakabadhi, Mkguzi wa Nje pamoja na Mhakikimali wanapokwenda kukagua katika

Wizara au Idara, hawapati stakabadhi wala vitabu na wakivipata huwa havijaorodheshwa, lakini baada ya wiki mbili zinapatikana na kuwasilishwa kunakohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu huu ni wa kutia shaka. Hapa pana mchezo mchafu, kwani fedha nyingi inapotea. Ni vizuri wawekaji wa kumbukumbu katika Wizara uwe wa kuridhisha, wahusika wa ununuzi katika Wizara wapewe mafunzo ili kazi zao wafanye kwa ufanisi. Asante na naomba kuwasilisha.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuongeza usimamizi katika Halmashauri zao ili kuleta tija kwa miradi mbalimbali ya maendeleo. Pili, Wakurugenzi na Maafisa Utumishi wawajibishwe kwa kushindwa kuwasilisha mafao ya wafanyakazi na tatu, kuboresha Idara ya Manunuzi kwa kuweka wafanyakazi hodari walio katika kusimamia shughuli za manunuzi.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2) Mbunge kwa niaba ya wananchi ana wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo ni wajibu wa Serikali kukubali ushauri na kuutekeleza ushauri huo kwa manufaa ya nchi hii.

Hivi karibuni Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda amekiri hadharani kuwa Tanzania sio maskini lakini anashangaa kuwa Watanzania ni maskini wa kutupwa. Jibu lake ni rahisi, Serikali haijaweza kuufanya utajiri wa nchi hii kwa manufaa ya Watanzania walio wengi, badala yake ni Watanzania wachache sana wanaofaidika. Kama 80% ya Watanzania ni wakulima na kilimo cha Tanzania ni duni sana huwezi kutegemea maisha bora kwa Watanzania kama uchumi wetu umekuwa kwa 7% ni wazi kuwa asilimia kubwa ya Watanzania ukuaji wa uchumi kwao ni 0% na wachache sana kwao wao ukuaji ni kwa asilimia kubwa sana. Sera ya kupeleka madaraka Wilayani (*D by D*) kwa lengo zuri la kuwashirikisha wananchi kwa miradi ijayo ya maendeleo kumeibua kundi kubwa la ufisadi wa mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama 70% ya fedha ya Bajeti ya miradi ya maendeleo inapelekwa katika Halmashauri ya Wilaya katika miradi kwa mfano ya umwagiliaji na kilimo lakini uwezo wa watendaji wa Halmashauri ni mdogo, kitakachofuatia ni pesa hizo kutumika tofauti na malengo yaliyokubaliwa. Hivyo Serikali inalaumika kwanza kwa kutenga pesa nyingi kwa Halmashauri zisizo na uwezo lakini pili kwa kutofuatilia hatua kwa hatua utekelezaji wa miradi hiyo.

Jambo lingine linahusu Mashirika ya Umma ambayo hayazalisha kwa ufanisi ni mzigo kwa Serikali. Mara nyingine Mashirika hayo yamekuwa maficho ya baadhi ya vigogo kufanya ufisadi wao. Ni vyema basi Mashirika ya aina hiyo yavunjwe. Jambo lingine linahusu suala zima la manunuzi ya umma. Hii ni sehemu inayopigiwa mfano na Watanzania wengi kuwa taasisi nyingi za Serikali zinashindwa kufuata utaratibu wa manunuzi. Pamoja na kuwepo kwa sheria ya manunuzi bado wizi mkubwa umejikita katika eneo hili na Serikali haiwachukulii hatua muafaka wahusika.

Mwisho, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu kwa taarifa zao nzuri zinazotoa picha halisi ya jinsi nchi yetu ilivyo. Ni juu ya Serikali kuchukua hatua haraka.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *procurement*, Serikali imeajiri na kutoa mafunzo ya ziada kwa wahasibu na wakaguzi wa Halmashauri zote nchini. Jambo hili ni zuri sana. Sasa umefika wakati wa Serikali kuajiri na kutoa mafunzo kwa wataalam wa ununuzi na ugavi kwenye Halmashauri zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine mengi sana yanayotokea katika Halmashauri ni kwa sababu ya kutokuwa na wataalam wa ugavi na ununuzi. Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 haitumiki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *accountability* Halmashauri nyingi hapa nchini hazina uwajibikaji kabisa. Naomba Serikali itoe mafunzo maalum kwa Halmashauri zote kuhusu uwajibikaji ili kulinda fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Pensheni mfano *PPF* na *NSSF* inafanya kazi nzuri sana ya uwekezaji. Kwa mfano, inafanya kazi nzuri sana ya kujenga nyumba mbalimbali kwa ajili ya kupangisha. Lakini kwa bahati mbaya nyumba hizi wamekuwa wakifaidika watu wenye vipato vya juu kama vile Wabunge, wafanyabiashara wakubwa na kadhalika. Wafanyakazi wa chini kama vile walimu, manesi na kadhalika wanashindwa kupanga kwenye nyumba hizi kutokana na uwezo mdogo kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa wa nyumba za walimu na watendaji wengine wa hali ya chini hapa nchini. Napendekeza *NSSF* na *PPF* waanze kujenga nyumba za gharama nafuu kwa watumishi hawa. Itasaidia sana kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba kwa watumishi hawa.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Naomba pia niipongeze Kamati ya Mheshimiwa John Momose Cheyo kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali imeonesha kutoridhika na mwenendo wa makusanyo ya mapato mbalimbali katika Wizara na taasisi za Serikali na Kamati hii imetaja baadhi ya maeneo kama vile Wizara ya Maliasili, Sekta ya Uvuvi, Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia katika maeneo mawili, Wizara ya Maliasili na Sekta ya Madini. Wilaya ya Liwale imo ndani ya hifadhi ya wanyama ya *Selous Game Reserve* na watalii na wawindaji wanaoingia ndani ya hifadhi hii ni kubwa na idadi ya vitalu vilivyoko ndani ya hifadhi hii pia ni kubwa.

Sisi tunaokaa katika maeneo hayo tungetegemea kwamba mapato yanayoingia kwenye Halmashauri yetu (Liwale) ambayo ni asilimia 25 kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii yangukuwa makubwa kutokana na idadi yangukuwa wanaoingia hifadhini humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, gawio la 25% linakwenda ndani ya Wilaya hiyo ni ndogo kiasi kwamba tulikuwa tunashindwa kufahamu tatizo liko wapi. Kwa ripoti hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali, mimi naunga mkono kwamba Serikali ijipange vilivyo iweze kujua kuna makampuni mangapi yanafanya shughuli za uwindaji ndani ya hifadhi hiyo, kuwa kambi ngapi zimejengwa ndani ya hifadhi hiyo na je, shughuli hizi za utalii na uwiindaji zinaendana na mapato tunayopata sasa? Kwa kufanya jitihada hizi na nyingine zitasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali kwa kupitia Wizara hii ya Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale ina madini ya aina mbalimbali na kwa sasa wachimbaji mbalimbali na wamiliki wa viatu walio rasmi na wasio rasmi wanaonekana kuingia na kutoka ndani ya Wilaya hii kwa shughuli hizi za uchimbaji wa madini. Haieleweki watu hawa wanaoingia Wilayani humo na kuchimba madini au kujipimia vitalu vya kuchimba wanalipia wapi. Je, Serikali ina *proper records* za wachimbaji hawa? Je, Serikali inalipwa ipasavyo? Je, Halmashauri yetu ina taarifa ya kutosha kuhusu shughuli hizi za uchimbaji madini? Na je, maeneo husika kwa maana ya vijiji vina taarifa za kutosha na inafaidika na shughuli hizi za uchimbaji wa madini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali ifuatilie na ijipange kukabiliana na changamoto hizi, ili tuweze kuboresha makusanyo ya mapato yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wote watatu wa Kamati za PAC, POAC na LAAC kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushirikiana na Wajumbe kusimamia mali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, enzi za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Serikali ilikuwa na mashirika na viwanda vingi vilivyofanya kazi kwa faida na kupelekea kuwepo na ajira nyingi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ubinafsishaji mashirika mengi pamoja na viwanda hayafanyi kazi na mengine yamekufa. Lakini kwa watendaji waliopelekea mashirika yale kufa je, Serikali imewachukulia hatua gani waliofikisha mashirika hayo kufa? Ni jambo la kusikitisha unakuta mtendaji kufanya vibaya kutoka taasisi moja na kumhamishia shirika ambalo unakuta linafanya vizuri. Huu ni udhaifu wa Serikali, ni vizuri ikatoa adhabu kwa wanaoharibu au kuleta hasara na kuwapa nafasi watu wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie shirika letu la ATCL kwa sasa hivi shirika hili halifanyi kazi lakini katika miaka ya 1970 na 1980 lilikuwa linafanya kazi vizuri kabisa, ndege zake zilikuwa zinaruka mpaka nje ya nchi yetu. Cha kusikitisha

kwa sasa hivi shirika hili lina deni linalofikia shilingi bilioni 23.3 lakini katika Kamati ya PAC Afisa Masuuli alitueleza ATCL ni mzigo kwa Serikali, sasa ATCL itafufukaje wakati hata ile ruzuku ya shilingi milioni 500 imesitishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama mdau wa utalii kwa ATCL kutokufanya kazi kunaipotezea nchi mapato na zaidi tunashindwa kufanya biashara nzuri ya utalii kama walivyo wenzetu mfano Kenya. Tukiwa katika maonyesho ya utalii kampuni za Kitanzania unaweza kutengeneza *package* nzuri, unapofika suala la jinsi ya kufika Tanzania inakuwa aibu inabidi u-*cross over* kwenye banda la Kenya au Ethiopia ujue bei ya *ticket* na hii inapelekea sisi tunakuwa *very expensive* ukilinganisha na wenzetu wa Kenya ambao wanaweza kupunguziwa bei kwa kutumia *Kenya Airways*.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani karibia kila Mbunge anaimba viwanja vya ndege vijengwe vingine vitengenezwe. Hivi viwanja hivi tunavijenga ili ndege gani ziruke huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu naomba Serikali ibebe mzigo wa shilingi bilioni 23.3 na iwapatie ATCL fedha wanazohitaji za USD bilioni 31 ili liweze kujiendesha na kuongeza Pato la Taifa, tuache kulalamikia *management* iliyopo sababu hata ruzuku hawapati. Je, watatoa wapi pesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *General Tyre*. Hii ni moja ya kampuni ambayo Serikali ina hisa 74%. Shirika hili lilikuwa linapata na linajiendesha kwa faida hadi 1977 na hatimaye kufungwa mwaka 2008 sababu ya kujiendesha kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuhusu Sheria ya Manunuzi kwamba aweje atoa bei nafuu ndani anayepata *tender* ningeomba Serikali tujali kwanza utaifa wetu na mali zetu kwa matairi yote ya magari ya Serikali na taasisi zake yakaagizwa yanunue matairi kutoka *General Tyre*, kiwanda hiki kitafanya kazi na ajira zitakuwepo na Taifa litapata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Mashirika ya Umma ambayo Serikali ina hisa lakini Mkaguzi na Mdhambi Mkuu wa Hesabu za Serikali hana mamlaka ya kuyakagua. Mashirika hayo ni BP hisa 50%, *Zain Tanzania* 40%. *Abood Soap Industries* 23%, *NBC* 30% na *Kilombero Sugar* 25%. Mashirika yote haya yanapata fedha nyingi sana, huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali kama hata tulichonacho hatujui kama tunapata faida kiasi gani.

Kuhusu mishahara hewa, hili limekuwa ni tatizo kubwa katika kila Wizara hata katika Halmashauri kuna malipo mengi hewa kwa wafanyakazi waliofariki bado wanalipwa.

Ushauri, tunaiomba kila Wizara wawe na *database* ya wafanyakazi wao wanaohudhuria kazi na walipwe kutokana na *data* hizo. Hii itasaidia sana upunguzaji wa malipo hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niungane na Kamati ya *POAC* Wabunge wasiwe wajumbe wa *board* ili kuondoa mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono.

MHE. MADGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu viwango vya malipo ya *concession fees* katika hifadhi za Serikali. Viwango vinavyolipwa sasa kutoka kwa wamiliki wa hoteli za kitalii *USD 7 – 10 per person* ni viwango vya miaka zaidi ya 10 iliyopita wakati viwango hivyo vinawekwa kitanda kimoja kiliuzwa kwa *USD 40 – 50* kwa mtu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo gharama zimepanda kitanda kwa mtu mmoja kinaunzwa *USD 200 – 1000*, cha ajabu Serikali haijaona hilo imeendelea kuwanyima *TANAPA* kuongeza *concession fee* kwa sababu ya kuwalinda wenye hoteli lakini wanadidimiza shirika ambalo lina kazi kubwa ya kuhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenye hoteli ndani ya hifadhi wananufika sana wakati kinachotozwa kwa ajili ya kuendeleza hifadhi hizo ni *just a very small* hata kiwango kinachopendekezwa kuongezwa yaani *USD 20- 30* bado naona ni kidogo sana kulinganisha na kile hoteli wanachopata.

Suala la Wabunge kuwepo kwenye Bodi za Mashirika ya Umma ni tatizo kubwa sana. Huwezi kuchanganya siasa na utendaji. Shirika moja lenye bodi ya wajumbe kumi kati yao wajumbe watano ni Wabunge, tena wale ambao hawajui lolote kuhusu shirika hilo (hawana uelewa wowote hata *professional* kuka *input* kwenye shirika. Wengine wamekuwa ni mzigo kwa mashirika wanachotaka ni safari, posho, vikao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waondolewe kwenye bodi mapema, Mawaziri wanawaweka pale kwa manufaa yao tu na siyo kuendeleza shirika.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kwa taarifa nzuri na pia kazi nzuri ya wanakamati. Kwa kawaida, bajeti yote ina pande mbili ambazo ni Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taarifa inavyosema Serikali haijafanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato. Sehemu kubwa ya mapato ya Serikali hayakusanywi na iwapo yanakusanywa yanakuwa *'under declared'*, ni kidogo tu yanayokusanywa. Gharama za *customs* na kodi mbalimbali hazilipwi kikamilifu. Hapa Serikali inahitaji kusimamia vizuri ili mapato yote yaweze kuingia Serikalini. Mifano umeitaja katika taarifa yako, ni vyema kwa Serikali kuangalia vyanzo vingine vya mapato na ni vyema tufike mahali ambapo kila Mtanzania analipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali haijajipanga vizuri katika kubana matumizi. Serikali yetu ina magari mengi sana na hai-*reflect* nchi masikini. Ni vizuri Serikali ikabana matumizi katika maeneo haya kwa kupunguza idadi ya magari

yasiyo ya lazima na pia magari hayo ni makubwa (*engine capacity*) na yanatumia mafuta mengi. Inabidi Serikali kubana matumizi hasa ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo halina udhibiti ni eneo la ununuzi. Takribani asilimia 70 ya matumizi ya Serikali ni '*procurement*'. Serikali isimamie vizuri suala la manunuzi ili kuona kwamba vifaa na mali zinazonunuliwa zina thamani ya fedha inayohusika (*value for money*). Tunaishukuru Serikali kwa kuanzisha Kitengo cha (*Value for Money Audit*) Serikali ilete taarifa hiyo ili Bunge liweze kushauri ipasavyo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni matumizi yetu ya vifaa vya ofisini kama vile shajala (*stationeries*). Hatutumii vifaa vya ofisi kwa uangalifu, ule mpango wa kutumia *Economy label* kwenye bahasha umekwenda wapi? Huu ni mfano tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine kwa dharura ambazo pengine sio dharura, Serikali hufanya manunuzi nje bajeti. Wakati mwingine Serikali na Taasisi zake huji-*commit* kufanya manunuzi ambapo pesa hazipo na huharibu mfumo mzima wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutoa fedha nyingi kama *subvention* kwa mashirika ambayo ni *non-performing*. Serikali itabidi ione kama kuna haja ya kuwa na utitiri wa mashirika hayo. Ni wakati muafaka sasa kufanyia tathmini mashirika hayo na kama kuna haja ya kuwa nayo. Hili ni eneo ambalo Serikali inapoteza fedha nyingi kwani haipati gawio '*dividend*'

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapongeza tena na ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara hewa, wataalamu wa fani ya uhasibu kutokuwa makini katika pesa wanazotoa kwa mfano upande wa manunuzi wanatangaza tenda na kiwango huwa kikubwa sana. Wakati mwingine anayepewa dhamana kuwa ameshinda anaweza kupotea na asichukuliwe hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakandarasi wanaposhinda tenda, utekelezaji wao mara nyingi unakuwa ni chini ya kiwango. Kabla hata ujenzi haujakamilika anaongeza kiwango na hii yote inatokana na mikataba mibovu na hali kama hii pia ipo katika Wakandarasi wa majengo. Kesi zikienda Mahakamani Serikali inapoteza kesi hivyo kupoteza matrilioni ya shilingi na vilevile Serikali yetu kubezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vinavyonunuliwa haviingizwi kwenye kumbukumbu, lakini kibaya zaidi wanapokwenda Wakaguzi kutoka ofisi ya CAG wanakuta hakuna risiti, ukienda kesho yake risiti zipo. Hii inaashiria nini? Ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuwa na ufanisi zaidi, ningeshauri kuwe na uadilifu zaidi, *in-house training* za mara kwa mara, mtumishi asikae kwenye kituo kwa muda mrefu na akiboronga *solution* isiwe kumhamisha maana atakwenda kuweka sumu huko atakakokwenda, isipokuwa anatakiwa achukuliwe hatua kali za kisheria. Naomba kuwasilisha.

MHE. KHERI K. AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari naomba kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge za Hesabu za Mashirika ya Umma, Serikali za Mitaa na Kamati ya Hesabu za Serikali. Ni kazi nzuri wameifanya na inastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika mapungufu tuliyonayo Watanzania tunasema zaidi kuliko kutenda, wepesi wa kugundua makosa na wazito kujisahihisha. Mfano, hapakuwa na sababu ya kufa kwa shirika la *ATCL*, shirika ambalo lilisimama toka miaka ya 1960. Tulipoliingiza katika ubia na Afrika ya Kusini na tukalipa ruzuku, lilipovunjika, tukalinyima ruzuku, jambo ambalo limesababisha kusimama kabisa. Hatukujisahihisha. Kumbe tumefanya kinyume chake, msingelipa ruzuku walipoingia ubia na tungepaswa kulilipa lilipovunjika. Lakini ni kwa nini *ATCL* bado ina wafanyakazi wanaolipwa bila tija? Ni kwa nini wasingesimamishwa au kufukuzwa? Ndege mbili zilizopo siyo haba, ni kwa nini hazifanyi kazi? Hatujifunzi, tunalaumu tulipoangukia bila ya kuangalia tunajikwaa wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba shirika lianze kazi, wafanyakazi wapunguzwe na ruzuku ya shilingi 500,000,000/= irejeshwe na pia pateuliwe Bodi na Menejimenti mpya, sio hiyo. Watafutwe vijana katika Menejimenti wakabidhiwe kwa makubaliano waliendeshe shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuongelea Kampuni ya *General Tyre*. Kiwanda hiki hakiwezi kuachwa kama kilivyo, hasa ukizingatia wakati huu wa muungano wa kibiashara na soko huru la *EACO*. Tanzania tutakuwa wasindikizaji katika umoja huu endapo hatutakuwa na viwanda vyenye chimbuko la Tanzania yenyewe. Kiwanda kipo, fika kaone majengo na zana, mashine na malighafi zipo, pateuliwe Bodi na Menejimenti ya muda wafanye mageuzi waendeshe kiwanda hiki. Suala la madeni lisimamiwe na Serikali kwa muda. La sivyo, basi na wapewe vijana wa Tanzania wa Vyuho Vikuu waliendeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kubaini kosa hilo na Serikali nao kuulipa Mfuko wa Pansheni wa Watumishi wa Umma, *PSPF* kwa mpigo jumla ya shilingi bilioni 30 kati ya wanazodaiwa shilingi bilioni 2.61, ni kidogo lakini wameonesha mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali kwa ujumla wake, wakae chini kuangalia mustakabali wa mashirika niliyoyataja hapo juu na mengine kama vile *TTCL*, *NDC*, *TPA*, *TANESCO*, *MSCC*, na kadhalika, bila kulisahau shirika la reli. Mashirika haya ndio mhimili wa Serikali na watanzania. Lingine ni usemi wa wazee, “Kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi.” Ahsante.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni tabia ya Serikali kutoa pesa kidogo kusaidia mashirika, mfano *SIDO*, *NDC*, *TBS*, *EPZA*, *SEZ*, na kadhalika. Mashirika haya yakipatiwa fedha za kutosha kwa mujibu wa mahitaji yao, zitachangia kwa kiasi kikubwa katika kuinua uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kucheleweshwa kwa malipo ya fidia ya ardhi, yanayofanywa na *EPZA* imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanyonge ambao wameshawishika kutoa ardhi zao kwa ajili ya maendeleo ya Taifa lao. Serikali itoe pesa za kutosha kwa *EPZA* ili iweze kulipa fidia kwa wakati unaostahili, kuliko kuchelewesha na pale pesa inapokuja kulipwa inakuwa imeshuka thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaisaidia *NDC* kwa dhati, tatizo la umma litakuwa ni historia katika nchi hii. Serikali ielekeze nguvu zake mchuchuma na Ngaka, pia isaidie uendeshaji wa Liganga kwa ajili ya upatikanaji wa chuma ambao utaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha *SIDO* na *EPZA* kutaongeza pato katika nchi hii na pia tuta-*create* ajira kwa wananchi na kuifanya *SIDO* kuwa na pato maalum la uwekezaji wa wazalishaji wa ndani na wadogo wadogo – *SIDO street*, mitaa ya *SIDO*. Pia kutapunguza unyanyaswaji usio wa lazima kwa wafanyabiashara ndogo ndogo. Naunga mkono hoja.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati imerejea Taarifa ya Mkaguzi Mkuu ya mpaka Juni, 2009, ya ukaguzi maalum wa hesabu za Kituo cha Mabasi ya Ubungo (*UBT*) wakati mkataba wa ukusanyaji mapato ukiwa chini ya *Smart Holdings*. Kamati na Bunge lizingatie kuwa baada ya ukaguzi huo kampuni nyingine ya *Konsord* sasa inapewa jukumu hilo. Serikali izingatie kuwa bado ukusanyaji wa mapato hauridhishi na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeandaa mapendekezo ya kuongeza malipo kwa kampuni hiyo na kuwaongezea gharama za viingilio kwa wananchi wa kipato cha chini wanaoingia kituoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya TAMISEMI ielekeze Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuweka wazi ripoti kamili ya ukaguzi wa *CAG* kuhusu Kituo cha Ubungo – ripoti hiyo ijadiliwe na Baraza la Madiwani kabla ya kufanya maamuzi ya kuongeza malipo kwa kampuni ya *Konsord* ili kuepusha kujirudia yaliyojitokeza kwenye ukaguzi huo.

Pili, kutokana na uzito wa mapungufu yaliyoainishwa kwenye ripoti ya *CAG* kuhusu Manispaa ya Kinondoni na Jiji la Dar es Salaam, ni muhimu ufuatiliaji mahususi ukafanyika ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na taarifa ya Kamati na ripoti ya CAG kuhusu DAWASCO na DAWASA hatua za haraka zinahitajika. Hivyo, pamoja na mapendekezo ya ujumla ya Kamati, ni muhimu maelekezo mahususi yakatolewa kwa CAG kufanya ukaguzi maalum, (*Special Audit*) ya DAWASA na DAWASCO ambayo itahusisha pia *Management Audit* kwa kuwa kuna udhaifu mkubwa wa kiutendaji DAWASCO Makao Makuu na pia ofisi za maeneo mbalimbali, (*Area, Offices*) zimepewa wajibu bila mamlaka ya kutosha, matokeo yake kuna udhaifu katika usimamizi wa miundombinu na mgawanyo wa maji. Aidha, kuwe na mgawanyo wa kimajukumu baina ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 19 wa Taarifa ya Kamati, yametajwa majina ya makampuni ambayo Serikali ina hisa za chini ya asilimia 50, naomba iongezwe kampuni ya urafiki ambayo Serikali ina hisa asilimia 49. Hali ya shirika ni mbaya, wafanyakazi wanapewa likizo ya lazima kwa mshahara wa asilimia 75, mitambo mingi imefungwa, baadhi ya mali za kampuni zinatumiwa kwa biashara tofauti na mtu binafsi. Mfano, ni Kituo cha Mafuta ambacho kimekodishwa kwa wafanyabiashara wengine. Nitawasilisha maelezo binafsi kuhusu suala hili. Lakini natoa wito kwa Kamati kutembelea kampuni na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pendekezo la Kamati kuhusu TANESCO kuongezewa mtaji, ni muhimu Bunge likaazimia kuitaka Serikali kupitia upya mikataba ya gesi na umeme kama ilivyofanya kwa madini. Baadhi ya mikataba hiyo ni ya SONGAS, Pan African, IPTL, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009, Fungu 22 linahusu deni la Taifa na matumizi mengine ya kitaifa, Serikali ilibadilisha deni la *account* ya malipo ya nje (*EPA*) la zaidi ya shilingi bilioni 135 kuwa dhamana ya Serikali zitakazolipwa pamoja na riba kwa miaka 20 hali itakayofanya deni kuwa shilingi bilioni 230 zitakapolipwa. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa ambayo Serikali inapaswa kuyatolea maelezo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itoe maelezo Bungeni kwa kuwa Bunge lilielewa kuwa Tume iliyoundwa na Rais iliwezesha fedha kurejeshwa. Hivyo Serikali ieleze ni kampuni zipi zilirejeshwa na kiasi kilichorejeshwa. Kadhalika, Serikali ilieleze Bunge kuhusu kiwanja ambacho kimerejeshwa na kampuni ya Kagoda. Pamoja na kuwa Serikali inasema uchunguzi wa Kagoda unaendelea, suala la kurejeshwa kwa fedha linapashwa kutangulia kwa kuwa Serikali ina mawasiliano na wahusika wa Kagoda.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine, kutokana na Fungu 49 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji ieleze Bunge sababu za kuchelewa kukaguliwa kwa taarifa za fedha na *account* maalum za Chuo cha Rasilimali za Maji cha Rwegarulira kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009. Aidha, Bunge lipewe maelezo na Wizara husika kuhusu matokeo ya Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) ya fedha za mpango wa maji Vijijini, yakiwemo maeneo ya Dar es Salaam na hatua zilizochukuliwa na Wizara kutokana na Ukaguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, kama sehemu ya usimamizi wa fedha za umma, Kamati ya Hesabu za Serikali ifanye uchambuzi na mikataba hususan katika sekta ndogo ya gesi na umeme kama iliyofanywa kwa madini. Wizara ya Nishati na Madini itoe ufafanuzi wa mikataba hiyo inavyoongeza mzigo wa madeni kwa *TANESCO* na kusababisha kupanda kwa gharama za umeme kwa wananchi kutokana na viwango vya *capacity charges* na gharama ambao walishaji wanaingiza. Baadhi ya mikataba hiyo ni ya *IPTC, SONGAS, PAN AFRICAN* na kadhalika.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu pamoja na Wajumbe wa Kamati hizo kwa kazi nzuri ya kuishauri Serikali kutokana na matatizo sugu yanayoibuliwa na *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ikakubaliana na ushauri wa Wabunge kuhusu udhamini wa Serikali kwa makampuni binafsi kwa kiasi kisizidi asilimia 70 kama Sheria ya Mikopo na dhamana ya mwaka 1974 ilivyorekebisha mwaka 2004 inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia nashauri Serikali itumie mtandao - *ICT* kwa kuweka kumbukumbu za wafanyakazi ili kuepuka ulipaji na mishahara hewa kwa wafanyakazi ambao hawapo kazini. Serikali ione uwezekano wa kuiwezesha *NDC* kiasi cha shilngi bilioni 4.8 ili iweze kuingia ubia na Wachina ambao wako tayari kuanza mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na mradi wa chuma Liganga Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* hupoteza umeme mwingi kutokana na msongo wa umeme kuwa chakavu. Serikali iweke mkakati madhubuti kwa kuiwezesha *TANESCO* kujenga msongo wenye uwezo mkubwa ili kukabiliana na matatizo ya umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue uamuzi wa kubinafsisha shirika la huduma za meli au Kotobinafsisha kwani shirika hili haliwezi kufanya jambo lolote la kuajiri, kufanya biashara na kadhalika. Wafanyakazi na uongozi wa kampuni wanafanya kazi katika hali ngumu kwani hawapewi ruzuku na Serikali. Naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Katika hesabu hizi inaonyesha kuwa lipo tatizo la malipo kwa watumishi. Watumishi hawapati malipo yao kwa wakati huku wakisumbuliwa na Wakurugenzi ama Maafisa Watumishi wengine ilhali wapo watumishi hewa wanaolipwa kwa wakati na hawafanyi kazi wala hawajulikani walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wakandarasi na wazabuni wengine yanagarimu pesa nyingi sana na inaonyesha upotevu mkubwa sana. Huu ni mwanya ambao unastahili kuzibwa. Lakini pia eneo la miradi kupitishwa kwa wakati na utekelezaji wake, kwa maana lipo tatizo la ucheleweshaji, unasababisha gharama kupanda na kukwamisha ukamilishaji kwa kupungua kasma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ichukue hatua za haraka kutatua kero hizi kwa kuzingatia ushauri wa Wabunge na wataalam. Asante. Naunga mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Taarifa ya Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Serikali za Mitaa. Nawapongeza Wenyeviti wote kwa mawasilisho mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hesabu za Serikali Kuu. Ipo Taasisi moja inaitwa TEMESA inayotengeneza magari ya Serikali. Utendaji kazi wa Taasisi hii huko Mikoani ni mgumu. Yapo malalamiko mengi kuhusu utengenezaji wa magari ya Serikali zinapoharibika. Gari ikipelekwa TEMESA kwa matengenezo gharama zinakuwa kubwa ukilinganisha na utengenezaji binafsi ambapo watengenezaji wenye gereji binafsi wanakuwa makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Watendaji wa TEMESA wanaosimamia zoezi hili huko Mikoani ni mafundi waliobobea katika fani hiyo na ninashauri Serikali iwape mafunzo ya kujinoa zaidi katika utaalamu wao ili kuokoa fedha nyingi za Serikali za kutengeneza magari katika gereji za binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Bureau de Change* nyingi mjini Dar es Salaam asilimia kubwa hazitoi risiti kwa wanunuzi wala wauzaji wa fedha za kigeni. Sina uhakika kama *BoT* ina takwimu ya *capital flight* (fedha zinazoondoka nchini) kama hizi *Bureau de Change* hazitoi risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa *TRA* wanakosa mapato kutokana na upungufu huu. Nashauri Serikali ilianganalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa hatua iliyochukuliwa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *against* Watendaji wabovu wa Halmashauri. Ninaishauri Serikali iendelee na mtindo huu wa kutokuhamisha Watendaji wabovu na kupeleka katika Mkoa au Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hatua za kisheria zichukue mkondo wake pale pale Mtendaji huyu alipo na asihamishwe kuficha ubovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zinaweza kufanya vizuri sana katika usimamizi wa miradi na fedha za Serikali popote ambapo Waheshimiwa Madiwani watasimamia shughuli za maendeleo kikamilifu. Hili liende sambamba na wao Waheshimiwa Madiwani kutokufanya biashara na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono ushauri wa Kamati kwa Serikali kwa kuwahamisha Watendaji ambao wamekaa eneo moja kwa muda mrefu. Hawa wamejijengea Halmashauri ya Wilaya na utendaji kazi wao ni wa mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la Watendaji wa Vijiji kukaimu utendaji wa Kijiji kwa muda mrefu na bila *incentive*/malipo yoyote. Watendaji hawa wanavunjika moyo na ufuatiliaji wa mali ya Serikali, mfano, mbao zinazovunwa kiholela bila vibali katika misitu ya Hifadhi ya Taifa au Hifadhi za Halmashauri za Wilaya, uchomaji wa matanuu ya mikaa na kadhalika, unakuwa mdogo au unakuwa haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ilianganalie hili na iweke muda wa kukaimu na pale unapofika kikomo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya amlipe hata kama ni fedha kidogo. Nashauri mtiririko huu uende pia kwa Watendaji wa Kata na Maafisa Tarafa. Serikali iwape umuhimu wanaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, lipo tatizo la Watendaji wa Vijiji kutokusoma mapato na matumizi ya fedha za michango mbalimbali za wananchi. Tatizo hili linadumaza uchangiaji na ushiriki wa wananchi katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Wakurugenzi wa Halmashauri wahakikishe Watendaji hawa wanaita mikutano mikuu ya vijiji na kusoma taarifa ya mapato na matumizi. Nashukuru sana na naunga mkono hoja za Kamati za fedha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati za Usimamizi wa Fedha za Umma (*PAC, LAAC na POAC*) kwa kazi nzuri na kuwasilisha vizuri ripoti zao. Napenda kushauri yafuatayo:-

Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) ina miradi mingi iliyoko chini ya *Mtwara Corridor* kama vile upanuzi wa Bandari ya Mtwara, Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga, reli kati ya Mtwara na Makambako. Ajabu ni kuwa miradi hiyo inakwenda pole pole sana na hivyo wananchi wanakata tamaa na miradi hiyo. Hivi tatizo ni nini? Ni kuwa tu miradi hiyo ipo kusini mwa Tanzania. Aidha, zipo taarifa kuwa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuanzia mradi uitwao *Southern Agricultural Development Corridor of Tanzania (SAOCOT)* mradi huu una lengo la kusaidia kuboresha kilimo kusini mwa Tanzania. Lakini kusini pamoja na Mtwara na Lindi ambako pamoja na mradi kutaja kusini lakini kusini haipo. Kuna jambo gani hapa? Ni vyema mradi huo uhusishe Mikoa hiyo miwili iliyo kusini mwa nchi hasa Mtwara na Lindi.

Pili, ni vyema sasa Bunge lisimamie kupitia Kamati ya *POAC* Mashirika yote yenye hisa chini ya asilimia 50. Kampuni kama *BP Tanzania (50% Share) NBC (30% share) AIRTEL (40% Share)* ingawa zinaonekana Serikali kuwa na hisa chache, lakini kimsingi kuna kiwango kikubwa kinachohitaji usimamizi wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hisa za Serikali kwa *Airtel (Celtel)* zisajiliwe kwenye soko la hisa (*DSE*). Hii itasaidia kupata thamani ya hisa halisi na pia tuone namna ya kupata *capital gain tax* iliyotokana na kuuzwa kwa kampuni hiyo kwa *Airtel* kama ambavyo wenzetu wa Nigeria walivyofanya.

Tatu, Serikali ifuate Sheria zinazopitishwa na Bunge. Hivi ni tatizo gani Serikali inalo kiasi cha kushindwa kupeleka *export levy* kwa zao la korosho kwa Halmashauri zinazolima korosho na badala yake kupeleka Bodi ya Korosho? Je, hii siyo hujuma? Kwa nini kilichopitishwa hapa Bungeni kisifanywe kwa mujibu wa Sheria hiyo? Kuna nini?

Nne, Uafisa Ugavi au Uhasibu ni taaluma. Taaluma hizo ziheshimiwe. Tatizo hili ni kubwa. Kwa mfano, maeneo mengi ya umma kama vile Shule za Sekondari anawekwa yeyote kufanya manunuzi au uhasibu na hivyo kuchangia manunuzi na uhasibu unaotia doa Serikaoli yetu. Ni vyema ijulikane kuwa manunuzi ni sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali, hivyo tuajiri basi wataalam hawa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo kubwa la udhamini na mikopo kwa Serikali na Taasisi zake kupitia mifuko yetu ya jamii. Ni vyema tujipange sawasawa kwenye kuhakikisha mikopo hiyo inarudishwa kwa wakati ili *pensioners* wetu wasije kuadhirika kwa namna yoyote. Naunga mkono hoja.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taaifa za Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa, naweza kusema kuwa ni nzuri kwa sababu tu zimesema ukweli. Lakini kinyume chake ni taarifa mbaya, kwani zinatuoonyesha hali halisi ya Watendaji wetu kuwa hawawajibiki ipasavyo.

Pamoja na mapendekezo ya Kamati husika, yafuatayo ni mapendekezo yangu ambayo nadhani hayakugusiwa au yamedokezwa kidogo tu.

Kwanza Serikali yetu inapaswa sasa kusimamia kwa nguvu zote dhana ya uwajibikaji chini ya utaratibu wa uwajibikaji, mtendaji anapewa majukumu ya kusimamia au kutekeleza. Sambamba na majukumu anapashwa kupewa mamlaka ya kutekeleza majukumu aliyopewa. Katika utaratibu huo, endapo mtendaji atashindwa kutekeleza wajibu aliyopewa au endapo wale walioko chini yake watafanya madudu, mtendaji mwenye wajibu anapaswa kuwajibika. *Responsibility, Authority and Accountability*.

Sambamba na pendekezo hilo hapo juu, elimu na mawasiliano kati ya Watendaji na wadau wanaowatumikia nayo ni njia ya pili ambayo tunaweza kuitumia kupunguza matatizo haya. Watendaji wa Halmashauri wanapaswa waelimishwe juu ya wajibu wao na nafasi/wajibu na Madiwani katika utendaji mzima wa Halmashauri. Watendaji lazima wawasiliane na Madiwani na wananchi kwa ujumla. Lazima Watendaji hawa wawaheshimu na kuwatambua wadau na kinyume chake wadau hawa watapata fursa ya kuona na kudhibiti raslimali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napendekeza wananchi waendeleo kutiwa moyo ili kujenga na kuboresha utamaduni wa kuchangia maendeleo yao kama ujenzi wa shule, zahanati na kadhalika.

MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kupongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ucheleweshaji kupeleka pesa kwenye Halmashauri za Wilaya kutoka Wizara ya TAMISEMI. Hivyo, kuchelewesha utendelezaji wa miradi mbalimbali. Pili, maslahi kwa Madiwani katika Serikali za Mitaa ungaliwe upya. Tatu kuna baadhi ya Ma-DC huwaingilia Wakurugenzi katika kazi zao na nne, kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali na usimamizi mbaya wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza tena Mwenyekiti pamoja na Kamati yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja kwa maandishi kuhusu Hesabu za Serikali Kuu kama ifuatavyo:-

Kwanza malipo hewa kwa watumishi wa umma. Hili ni tatizo kubwa sana kwa Taifa letu la Tanzania kuwapo kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuhusu kuwapo na watumishi hewa. Wanalipa watu ambao hawapo kazini, watu waliokufa, watu walioacha kazi, watu waliofukuzwa kazi, hasa katika Idara ya Afya na Idara ya Elimu. Napendekeza hatua kali zichukuliwe kwa watumishi watakaobainika wanafanya hiyo tabia mbaya ya kutokuwa waaminifu katika kazi zao. Naomba Serikali kutumia Wahasibu au Wakaguzi wa Ndani kwa kuwapa uwezo mkubwa wa kukagua kwa usahihi na kuchukua hatua kwa watakaolipa watumishi ambao hawapo kazini.

Pili, miradi mingi haiishi kwa muda uliopangwa. Miradi ya maendeleo katika Wilaya/Halmashauri haiishi kwa muda uliopangwa. Sababu kubwa ni kwamba miradi mingi inategemea fedha kutoka kwa wafadhili. Naomba Serikali katika kutekeleza miradi, isitegemee fedha ya wafadhili. Bajeti yetu itenganishe fedha za ndani na fedha za wafadhili. Kwa hiyo, miradi mingi ipangwe kwa kutegemea bajeti ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu Serikali kuchelewesha kutuma fedha katika Halmashauri na hivyo kusababisha Halmashauri kushindwa kufanikisha shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa kwa muda muafaka. Pia kusababisha Halmashauri kuwa na madeni ya ndani ambayo yanasababisha uguvu wa upangaji wa bajeti kwa mwaka unaofuata. Naomba Serikali isimamie katika uharaka wa kutuma fedha kwa Halmashauri zetu.

Nne, Serikali kutoa fedha pungufu ya bajeti iliyopangwa na Halmashauri au Wizara zetu. Naomba Serikali kutoa fedha za Maendeleo kwa muda uliopangwa na Wizara ili kutokwamisha shughuli za maendeleo na kukamilisha kwa muda uliopangwa na Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia kuhusu Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza na kushauri kwamba ili kuokoa fedha za Serikali za Mitaa (*Local Government*) tuwajengee uwezo Madiwani wetu na tuboreshe maslahi yao.

Nipendekeze Madiwani walioko kwenye Wilaya za pembezoni kama vile Ludewa wapewe vyombo vya usafiri kama vile pikipiki. Asante.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusiana na Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa ninaomba kuipongeza Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupitia kwa undani utekelezaji wa shughuli katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni dhahiri kwamba mara nyingi imejitokeza kuwa miradi mingi imetekelezwa chini ya kiwango. Miradi haina thamani ya viwango vya fedha inayotolewa. Kuna matatizo makubwa mawili. Kwanza, bado pamoja na Serikali kupeleka watumishi wa kutosha katika Halmashauri mbalimbali, wengi wao ni wale wanaokaimu tu katika nafasi za Idara wanazosimamia. Hivyo, uwajibikaji wao katika kazi uwe na umakini zaidi. Naishauri Serikali kwa ujumla wake iharakishe kuwateua Wakuu wa Idara kamili ili kuleta uwajibikaji katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili linahusu ufuatiliaji wakati wa utekelezaji wa miradi. Siyo busara kuona miradi inayoendelea, kwa mfano, ujenzi wa madarasa, *dispensary* au madaraja yakijengwa kwa kiwango cha chini wakati wataalam wenye ujuzi wakiangalia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi nao kwa upande wao waweze kufuatilia miradi inayotekelezwa na Serikali katika maeneo yao ili kuona kama kuna viwango hafifu vya ujenzi na utekelezaji wa miradi mingine havikubaliki, wawe tayari kuzitaarifu mamlaka husika na kuona kwamba tabia hiyo inakomeshwa kabisa.

Kuhusu suala la watumishi kukaa kwa muda mrefu katika maeneo yao ya kazi, limezungumzwa mara nyingi hapa Bungeni. Umefika wakati sasa kufanyike sensa ya watumishi wote walioko katika Halmashauri ili kufahamu kiwango cha muda na hali ya utendaji wa watumishi hao. Mara nyingi imedhihirika kuwa wafanyakazi waliokaa muda mrefu katika Halmashauri, hao ndio mafundi wa kuziibia Halmashauri zao kwa kiwango kikubwa. Lakini pia utendaji wa wafanyakazi hao ni wa chini sana. Nashauri wafanyakazi hao wapangiwe vituo vingine vya kazi ili kuongeza ufanisi wao. Baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

MHE. NAOMI M. KAIHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuweza kuchangia kwenye Ripoti ya Hesabu za Serikali za Mitaa kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Augustino Mrema.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza sana ni kwa jinsi gani ambavyo vyombo vya kusimamia mienendo ya Halmashauri ili kuleta maendeleo ya wananchi wasio na hatia, vyombo hivi ni pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa vimezembea sana kuchukua hatua mwafaka za kukomesha maovu haya yanayolirudisha nyuma Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maovu haya manne sugu yaliyofupishwa au kuainishwa hapo chini ni kweli kabisa na yanajulikana kabisa, lakini hatua za kuwawajibisha wahusika hazichukuliwi. Mambo hayo ni kama yafuatayo:-

- (i) Udhaifu katika udhibiti wa ndani;
- (ii) Kutozingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma. Ni kweli watumishi wananeemeka kupitia njia hizi;
- (iii) Ukusanyaji usioridhisha wa mapato ya ndani ya Halmashauri, na siyo hivyo tu, bali hata ufuatiliaji wa kile kidogo kilichokusanywa hakielekezwi mahali kinakotakiwa kwenda kufanya kazi, matokeo yake ni mambo kuwa hovy hovy tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kuwa kama hizo hitilafu hapo juu zingeshughulikiwa, bila shaka uchumi wa nchi yetu hasa huko kwa wananchi ungetengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo haya yataendelea kulitesa Taifa hadi lini? Kwa ushahidi wa ripoti hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, wahusika wote wale wachukuliwe hatua kali kuwa mfano kwa wengine ili kukomesha tabia hizi chafu zinazoota mizizi na kuwa kansa ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Sheria ya kuwafilisi hadi wafilisike na kuwatangaza nchi nzima, itumike na iwapo haipo, basi itungwe haraka na Bunge lako Tukufu ili kuliokoa Taifa hili la Tanzania .

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji vitendo zaidi ya nadharia. Ahsante. Naomba kuwasilisha.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa za Kamati zetu za Bunge zinazohusiana na Taasisi hizo, inaonesha wazi kwamba fedha nyingi za umma zinapotea kupitia wajanja wachache ambao wana sura ya Watendaji wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC, Mheshimiwa Agustino Mrema inaonesha kwamba fedha ndani ya Serikali za Mitaa ni kwamba zinatumiwa kulipana posho kwa Wajumbe kuliko miradi iliyokusudiwa, lakini pia kumekuwepo na mishahara hewa. Hili linaonesha kwamba Serikali kuu imekuwa haiwajibiki vizuri katika zoezi la kusimamia utendaji kwa watendaji kama vile Serikali iko likizo, jambo ambalo linaleta dhana kwamba Serikali imewagawia baadhi ya watu maeneo ya kujipatia nao kupitia nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, taarifa haikuonesha kwamba kwa matokeo yote hayo kuna ambao wamewajibishwa kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya mashirika ya Umma kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma - Mheshimiwa Kabwe Zitto inaonekana kwamba hata utaratibu katika kuajiri haufuatwi ipasavyo na ajira inaonekana kwamba wakuu wanaohusika wamekuwa na utaratibu wao wenyewe wa kuajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu kama huu wa kutoshauriana kwa watendaji ndani ya Idara moja na kutoa maamuzi ya kuajiri, jambo hili linaleta dhana kwamba kila mwenye nafasi anamsogeza jamaa au ndugu yake karibu, jambo ambalo linaweza kudhoofisha jitihada za kiutendaji kwa Watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mitindo au taratibu hizi za Serikali Kuu kukosa usimamizi madhubuti, ndio maana tunavuna matunda ya wabadhirifu, kukosekana na mara nyingine kupewa taarifa za kwamba wanaohusika na ubadhirifu wa fedha kwamba wameshafariki lakini taarifa za vifo wala makaburi yao hayaonekani.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kupongeza taarifa zote tatu zilizowasilishwa na Kamati za PAC, LAAC na POAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la matengenezo ya magari yasiyo na uhalisia wa pesa zinazotumika katika kununulia vipuri na mafuta ya magari, kumekuwepo na udanganyifu mkubwa kwa Watendaji wa Halmashauri katika kipengele hiki, kwa mfano gari inapelekwa kwa ajili ya kufanya *wheel allignment* na *wheel balance* kwa Sh.450,000/= wakati hali halisi haizidi hata Sh. 50,000/=.

Eneo lingine ninalopenda kulizungumzia ni usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo. Tatizo hili linatokana na uzembe wa Watendaji katika Idara za Ujenzi kwa sababu wao wanatakiwa kusimamia mradi kuanzia hatua ya mwanzo hadi mradi ulipokamilika, lakini kwa makusudi wanajiandikia posho na kubaki ofisini badala ya kwenda katika eneo ambalo mradi unatekelezwa. Kwa mfano, miradi ya barabara inayotekelezwa na Wakandarasi, mingi inatekelezwa chini ya kiwango kwa sababu ya usimamizi mbovu wa Wahandisi katika Halmashauri zetu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. INSHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa shukurani zangu kwa kunipatia nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwa mmojawapo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe na Wenyevit wote wa Kamati za kudumu kwa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kushukuru chama change cha Mapinduzi pamoja na Jumuiya ya UWT kwa kunitewa na nikaweza kuchaguliwa. Nawashukuru wapendwa wangu wanawake wa Mkoa wa Morogoro kwa upendo wao kunichagua nikaingia katika Bunge lako Tukufu. Akina mama, nawapenda, tuko pamoja, tufanye kazi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Viongozi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuongoza nchi yetu, kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu. Pesa zinazopelekwa kwenye Halmashauri ni lazima ziendelee kusimamiwa, kwani fedha hizi hasa ni za miradi mbalimbali ya wananchi. Kwa hiyo, fedha hizo zitumike kama zilivyopangiwa. Serikali ya Awamu ya Nne inaendelea kuwadhiti wale wote kwenye Halmashauri wanaosimamia vibaya fedha hizo. Kwa hiyo, Wakurugenzi pia na Wakuu wa Idara husika na viongozi husika inabidi wasimamie vizuri fedha hizo, kwa kufanya mambo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, waheshimiwa Madiwani na Wabunge inabidi wafuatilie ili kwenda sambamba na Halmashauri zetu. Wafahamu kabisa miradi yote iliyopangwa kwa kipindi husika. Fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri ni fedha za wananchi. Kwa hiyo, lazima ni vizuri zitumike vizuri na watakaobainika wanatumia fedha hizi vibaya Serikali mara kwa mara huwa inawachukulia hatua. Naomba udhibiti uendelee kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mara nyingi fedha za maendeleo huwa zinachelewa. Kwa hiyo, mara inapobidi fedha za miradi hii ya wananchi ziwe zinawahi kufika na kufanya kazi yake kama iliyopangwa. Narudia kusema kuwa nawashukuru Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye Ripoti ya Kamati ya Mashirika ya Umma katika eneo la Mashirika yaliyobinafsishwa na hadi leo hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilombero, Kata ya Mang'ula, palikuwa na Kiwanda cha Kuchonga Vipuli na Mashine za Kusaga na Kukoboa.

Kiwanda hicho kilikuwa na faida kwa Wananchi na Nchi kwa kupata kodi na ajira. Ningependa Kamati ikitembelee Kiwanda hicho na kuona kama mmiliki amekitumia Kiwanda hicho ambacho kilikuwa na tija kwa Wananchi wa Kilombero na Taifa kama ilivyokusudiwa.

Pia katika Kata hiyo ya Mang'ula palikuwa na Shamba la Mpira na Kampuni ya *General Tyre* ilikuwa inanunua utomvu na lilikuwa na tija kubwa kwa Wakazi wa Mang'ula, lakini hivi sasa mmiliki wa Shamba hilo haeleweki na wafanyakazi hawajui kinachoendelea katika Shamba hilo na haijulikani utomvu unaovunwa unapelekwa wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za kufungwa kwa Kiwanda cha *General Tyre* Arusha, zimeemewaathiri pia Wananchi wa Kilombero. Hivyo, napendekeza Kamati iliyoundwa na *POAC* iangalie na itembelee Kata ya Mang'ula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia Ripoti ya Kamati ya *LAAC* katika eneo la fedha zinazopelekwa shule za msingi na sekondari kwa kila mwanafunzi ambapo shule za msingi toka dola kumi hadi shilingi 5,000 – 6000 kwa mwanafunzi. Hivyo hivyo kwa wanafunzi wa sekondari. Je, hatuoni kwamba fedha hizo haziwafikii walengwa kama ilivyokusudiwa na kuzorotesha elimu?

Kwa kuwa Madiwani ndiyo wasimamizi wa Miradi iendayo na kutekelezwa katika Halmashauri; ni muhimu posho za Madiwani zikaongezewa fungu maalum toka Serikali Kuu na pia kupewa dhamana ili wapate mikopo katika mabenki ili kuwaongezea *morale* ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. NAOMI M. KAIHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii adimu ili kuchangia katika Taarifa ya Kamati ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba, Bunge lako Tukufu limepata taarifa mbaya za utendaji mbaya wa mashirika yake ya umma. La kusikitisha zaidi ni tatizo la kufa kwa Kiwanda cha *General Tyre* na Shirika la *ATCL* na mengine kunusurika kama vile *PSPF* na *TANESCO*, lakini yamechungulia kaburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasaha zangu ni katika kuitahadharisha Serikali kuliokoa Shirika la *ATCL* kwa heshima ya Nchi yetu ya Tanzania; ni aibu kwa Taifa kubwa kama la Tanzania kutomiliki ndege zake yenyewe. Hatujaingia katika historia ya umaarufu wa ndege zetu na marubani wake tangu ilipovunyika toka Shirika la Ndege za Afrika ya Mashiriki. Zamani Shirika hili liliweza kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Shirika letu lingesaidiwa kwa dhati toka mwanzo, lisingefikia mahali hapa lilipo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri tujaribu kulifufua Shirika hili kwa gharama zozote zile. Ikiwezekana, Serikali irekebishe Utawala (*Management*), unaoelekea kuleta

hasara na kuweka mwingine. Vilevile Watanzania waaminifu na wenyewe uwezo, washauriwe kuwekeza au kununua hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu Ndege za Kenya sasa kuwa zinatamba katika anga yetu na kuzoa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine linalokera ni suala la Mikataba mibovu. Hadi sasa kila mara tunaona kuwa, Mikataba imekuwa kwa faida ya upande mmoja tu; ule wa wawekezaji; ni kitu gani kinafanyika wakati wa mikataba ambayo inawawebeba kiasi cha kwamba tunapotaka kuivunja kwa kushindwa kutoa huduma au kutupatia bidhaa walizotuahidi wanatushtaki wao; je, hao wafanyao Mikataba mibovu kwa ajili ya *ten percent* kama siyo *forty percent* wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri tutunge sheria ya kuwatupa ndani kama wahujumu na kuwafilisi ili tukomeshe tabia za kifisadi zinazolishambulia Taifa kama kansa ya damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia juu ya matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Kwa ujumla Serikali inatakiwa kuchukua hatua sasa, juu ya matumizi mabaya ya fedha za umma, jambo ambalo ni kero kubwa kwa Watanzania. Tatizo kubwa ni uwajibikaji mbovu wa baadhi ya Watendaji, ambao kwa makusudi wamesababisha hasara kubwa.

Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma katika utendaji wa DAWASA, Juni 30, 2008, lilipata hasara ya shilingi bilioni 26.6. Katika taarifa yake ya mwisho wa mwaka, kwa hesabu zilizoishia Juni 30, 2007 DAWASA ilipata hasara ya shilingi bilioni 10.4. Hii inaonesha ni namna gani utendaji mbovu ulivyo kwenye Mashirika ya Umma. Serikali imekuwa ikijitahidi sana kuwekeza kwenye Mashirika ya Umma, lakini Gawio limekuwa likishuka kutoka shilingi 76,951,126,934.16 mwaka 2007/2008 hadi kufikia shilingi 31,223,253,590.26 mwaka 2008/2009. Hii inaonesha upo utendaji mbovu katika Mashirika yetu ya Umma.

Ukiangalia upande wa hesabu za Serikali za Mitaa, nako kuna upotevu mkubwa wa fedha za Serikali. Tatizo la Serikali la kujenga mazingira rafiki kwa Watendaji wabovu, haitasaidia kuinua uchumi wa Taifa hili. Ifike wakati sasa Serikali ichukue hatua ya kuwawajibisha Watendaji wote wasio waadilifu katika matumizi ya fedha za umma. Ninashauri kufanyike mabadiliko makubwa kwa kuchukua hatua kwa viongozi wabovu wote, ambao kwa makusudi wanafuja fedha za umma bila woga, kwa vile hakuna mfano wowote uliochukuliwa kwa Mashirika ya Umma ambayo yameshindwa kuleta tija kiutendaji.

Tulikuwa na mashirika mengi, viwanda vyote vilikufa kwa kuwaheshimu wabadhirifu waliochangia kuua mashirika hayo na ndiyo maana hatutafaulu hata mara moja kudhibiti Uchumi wa Taifa, kwani kila anayepata nafasi ya kuyasimamia, anajua

amepewa ulaji. Ukiacha utaalumu wa kugundua matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kukagua mahesabu, imefikia hatua hata Wananchi wa kawaida wanajua Mtendaji yupi ni mbadhirifu wa fedha za umma; inakuwaje Serikali inashindwa kujua na kuchukua hatua? Wananchi wamechoka na wanaumia.

Uvumilifu wa Serikali kwa Watendaji wabovu, utalipeleka Taifa pabaya. Serikali ikifanya kazi vizuri kwa kusimamia Watendaji wa Halmashauri na kusimamia Mashirika ya Umma bila kulindana, tutalinda Uchumi wa Taifa letu na hivyo maisha bora kwa kila Mtanzania itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niipongeze Kamati, kwa kazi nzuri. Ninakubaliana nao kwamba, kuna uzembe mkubwa kwenye kuzingatia Sheria na Taratibu za Manunuzi pamoja na ubadhirifu wa kuongeza bei ya vitu. Halmashauri hususan Uongozi, hauna nguvu au meno ya kuwashughulikia Watendaji wabovu, kwa sababu Watendaji wa Manispaa hizo ni waajiriwa wa TAMISEMI; hivyo, wamekuwa jeuri na hawajali na mara nyingi hatua zinazochukuliwa ni kuwahamisha na hatimaye kutoa tatizo katika Manispaa moja hadi nyingine.

Niwapongeze TRA kwa mapato mazuri. Ukusanyaji wa mapato ni mdogo na pesa nyingi zinapotea bila kukusanywa. Hivi sasa Dar es Salaam makusanyo ya kodi ya majengo inafanywa na TRA, siyo rahisi kwa TRA kuzifikia Kata zote 90 za Mkoa huo na hasa ukitilia maanani kwamba, majengo mengi tena mengine ni makubwa hayajatathminiwa. Ingekuwa ni bora Manispaa zikajengewa uwezo ili waweze kukusanya wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa ruzuku utambue ukubwa wa idadi ya wakazi na kutoa kipaumbele kwa Manispaa za Dar es Salaam, ambayo sasa ina wakazi wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni tano; Kinondoni peke yake ina watu zaidi ya milioni moja na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie jinsi ya kutumia kuwepo kwa biashara nyingi ndogo ndogo kuwa wachangiaji kupitia malipo ya kila siku kwa biashara zao. Hivi sasa mahali kama Jiji la Dar es Salaam, lina Wamachinga na Wafanyabiashara ndogo ndogo zaidi ya laki mbili, inasemekana wanatakiwa kuchangia asilimia 0.3 ya mapato ya mwaka. Hivi ni nani anajua vipato vyao vya mwaka; kwa nini wasikate leseni za biashara kwa siku au wiki au mwezi hata ikiwa ni shilingi 500 tu kwa siku itaweza kuingiza si chini ya shilingi milioni 100 kwa siku au bilioni 2.2 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabango ya biashara ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Hivyo basi; ni lazima kuwe na utaratibu mwafaka kwa wenye mabango na Manispaa wa jinsi ya kuyasogeza ili Manispaa isikose mapato hayo ambayo Kinondoni inapata mapato si chini ya shilingi bilioni mbili.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja iliyopo mbele yetu katika maeneo ya usimamizi wa fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu wa Wakurugenzi wa Halmashauri, unachangia sana katika kusababisha upoteaji mkubwa wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Halmashauri, Mkurugenzi anashindwa kujiamani kabisa katika nafasi yake au mamlaka yake aliyopewa, anawategemea Wakuu wa Idara ndiyo wampangie mipango au taratibu zote zinazohusu fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utendaji huo, Wakurugenzi wa aina hiyo hufanyiwa mambo mengi hewa ambayo yanasababisha fedha za Halmashauri zipotee na utekelezaji wa Miradi usiwepo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali katika upande wa uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara, wateuliwe watu waadilifu na wenye maadili mazuri katika utendaji wao wa kazi na wawe wachapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ni kuepusha utaratibu wa kuwakaimisha Wakurugenzi au Maafisa kwa muda mrefu. Tabia hiyo ya kukaimisha, yule anayekaimu anafanya matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa makusudi akijua yeye hatakuwa mjibuji wa hoja pale tatizo linapotokea; hivyo ni bora wawepo wahusika katika nafasi zao, ambao watawajibika pale upungufu unapoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa, naomba niunge mkono hoja.

MHE. MOHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu pamoja na Kamati yake. Ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikiaangalia upya kwa kupunguza idadi ya maofisa wanaoongozana na Viongozi Wakuu wakati wa misafara ya nje.

(ii) Ni vema Serikali ikaacha kupeleka Maofisa wa Serikali wanaopenda kusoma nje ya nchi kwa taaluma ambazo zinapatikana hapa hapa nchini; kusoma nje ni gharama sana ukilinganisha na hapa nchini.

(ii) Ni vema Serikali ikaacha kupeleka maofisa kwenda kwenye semina nje ya nchi badala yake iweke utaratibu wa kuwaleta wataalam hapa hapa nchini; kwanza, kutapunguza gharama na pia kutotoa nafasi kwa wadau wengi kupata mafunzo hapa hapa nchini.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema TRA wakaweka utaratibu mzuri wa kuwaelimisha Watanzania ili kila Mwananchi ajue wajibu na faida ya kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa lake. Kuna baadhi ya Maofisa wa TRA wamegeuka kuwa

polisi; suala hili hili linajenga mahusiano mabaya na walipa kodi na kusababisha walipa kodi wengi kujificha.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha wafanyabiashara wanaofanya biashara nje ya nchi kwa mgongo wa Tanzania wanafahamika na wanalipa kodi hata kama makampuni hayo na taasisi hizo si za Kitanzania. Mfano, *inspection money* ya dola 150 inayolipwa kwa magari yote yanayoingia Tanzania.

Naunga mkono hoja.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza na kuishauri Serikali itoe kipaumbele kwa Miradi ya Liganga na Mchuchuma ili Wananchi wa Ludewa waweze kunufaika na Miradi hiyo na Watanzania wote kwa ujumla tuzalishe umeme wa makaa ya mawe. Kampuni ya Sichwan HONGDA ipewe Mkataba upesi ili ianze kuzalisha umeme toka Mchuchuma kwa manufaa ya Watanzania wote. Kampuni ya *CHC* (Shirika la *CHC*), liongezewe muda wa kufanya kazi ili kulinda mali zilizokuwa za Mashirika ya Umma na pesa zake. *CHC* wana uzoefu mkubwa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu uwezo wa Madiwani katika kusimamia Halmashauri kwa kuzingatia Madiwani ndiyo wenye chombo hiki na wanasimamia chombo hiki kwa niaba ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani walio wengi elimu yao iko chini. Uwezo wa kusoma na kuzitafsiri taarifa unakuwa mdogo na hasa zile zenye mahesabu. Kutokana na hali hii, Madiwani hujikuta wanaburuzwa na Wakurugenzi. Mkurugenzi anakuwa Meya pia! Inakuwa vigumu kama *executive* imejaa wasomi na upande wa wanasiasa elimu ni duni; si rahisi kwenda kwa pamoja ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee dhamira ya kweli kwa Madiwani ya kusimamia chombo hiki (*seriousness*). Madiwani hawasomi taarifa zinazotoletwa aidha kwa kuzipata zimechelewa au kwa kutojali. Siyo rahisi kujadili jambo usiloliewa vizuri. Uwezo wa Madiwani kusoma na kujiridhisha taarifa hizi ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika kwa nchi yetu kuruhusu watu walio Serikalini katika Idara mbalimbali kama wahasibu, madaktari, waandishi na kadhalika, kugombea na kuwa Madiwani na wakibaki kwenye kazi zao ili waweze kuchangia kusimamia Halmashauri kama nchi nyingine zinavyofanya, lakini pia Serikali iendelee kutoa elimu ya maboresho kwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kidogo katika Hesabu za Mashirika ya Umma. Mkoa wa Kagera unapata umeme kutoka Uganda. Zipo taarifa kuwa Mkoa wa Kagera unapata mega watt kati ya 8 – 12, lakini umeme unaotumika ni chini ya hapo na Serikali imekuwa ikilipa umeme wote unaonunuliwa Uganda. Serikali

haioni kuwa umeme huo ungeweza kutumika katika Wilaya za Chato, Biharamulo na Ngara, zinazotumia *generators* kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata hasara kubwa kwa kulipa umeme usiotumika. Serikali ifanye mpango wa kutumia umeme huo kwa kupeleka umeme maeneo mengine ili *TANESCO* (Serikali), ilipe malipo yanayolingana na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono Taarifa za Hesabu za Mashirika ya Umma na *LAAC*.

MHE. MOZA ABEID SAIDY: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kama ilivyoletwa mbele yetu.

Kwa kuwa Kamati imebaini ubadhirifu na udanganyifu mkubwa na kuisababishia Serikali hasara na Wananchi kukosa imani na Serikali yao kutowatendea haki Wananchi. Serikali ijipange upya na kuchukua Sheria za kinidhamu za matumizi ya mali za umma katika Serikali za Mitaa zote nchini, kwa ubadhirifu wa mali za umma kwa wale walioitia hasara Serikali, kutaifishiwa mali zao na kufukuzwa kazi, ikawa ni mfano kwa wengine.

Vilevile ni vizuri Serikali iweke wazi suala zima la ulipaji wa Wenyeviti wa Mitaa; hujituma na kukusanya mapato ya kutosha na kukabidhi Halmashauri, lakini bado hushindwa kuwatekelezea maendeleo Wananchi na kukosa imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi za Wananchi hupotea kuanzia ngazi za chini kwenda juu; hivyo, Serikali inapaswa kuwa makini na Watendaji wa Halmashauri zote hapa nchini. Naomba kuwasilisha.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Wenyeviti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga matumizi kulingana na vipaumbele ni jambo moja, lakini kutumia vizuri kile kilichoidhinishwa na Bunge ni jambo la pili.

Tatizo kubwa ni nidhamu na uadilifu wa matumizi, juhudi kubwa ielekezwe kwenye kujenga nidhamu na uadilifu wa matumizi ya fedha za Serikali.

Wadau na wamiliki wakubwa wa taarifa hizi zote tatu ni Watanzania. Taarifa au Ripoti zetu ziwe na tija kwa Watanzania ndipo tutaonekana tumewajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tupate mafanikio makubwa ni lazima tuondokane na dhana ya itikadi katika masuala yanayogusa maslahi ya Taifa letu.

Katika ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya 2009, idadi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa maskini ni milioni 14, kati ya milioni 40+. Kati ya hao; 14 milioni, 12.5, sawa na asilimia *around 84* wanaishi vijijini.

Sasa naomba kuuliza; hivi tunapopanga matumizi ya fedha za Serikali katika Halmashauri ni kwa asilimia ngapi zinawalenga hawa 84%?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Wenyevitani wa Vijiji na wa Vitongoji, Watendaji wa Vijiji na Waheshimiwa Madiwani; hawa ndiyo wanaosimamia utekelezaji wa Miradi yote ya Maendeleo na Programu zote zinazobuniwa na Serikali na kadhalika; lakini Viongozi hawa hawafikiriwi hata kidogo kujengewa uwezo ili wafanye kazi vizuri. Viongozi hawa wapewe motisha walau mishahara ya kima cha chini ya Serikali.

Naishauri Serikali iwe sambamba na udhibiti wa fedha na uratibu wa Miradi ya Maendeleo. Tubuni mpango mahususi wa kuwajengea uwezo Viongozi hawa ili waweze kusimamia vizuri rasilimali nyingi zinazoelekezwa ngazi ya Halmashauri kutoka Serikali Kuu. Mara chache sana wanakwenda kwenye semina, warsha na mafunzo mbalimbali, tofauti na Viongozi wa Juu wanaoenda kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, haifai watu wanaosimamia fedha nyingi na miradi mingi, maisha yao yakaendelea kuwa duni. Uratibu au udhibiti hauna tija kama wazalishaji hawana tija.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa, kuwapongeza Wenyevitani wa Kamati zote za Fedha, yaani Kamati ya Fedha za Serikali, Fedha za Serikali za Mitaa na Fedha za Mashirika ya Umma pamoja na Wajumbe wote walioshiriki kuandaa Taarifa hizi nzuri ambazo zimeonesha umakini wa juu wakati wanapohoji na kuandaa Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo nitaacha kumpongeza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali na Timu yake, kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika kukagua mahesabu yote pamoja na kutoa semina kwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati, kwani zimesaidia sana Wabunge kupata uelewa wa kukagua hesabu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya matatizo yanayojitokeza kwenye Taarifa za Hesabu kwa Kamati zote tatu ni Wakuu wa Idara kukaimu kwa muda mrefu. Jambo ambalo halileti tija katika utendaji, kwani daima kaimu hana hakika na nafasi yake ama utendaji wake; ninaishauri Serikali iwe na utaratibu wa haraka kujaza nafasi pale Mkuu wa Idara anapostaafu, kufariki au kuachishwa kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuungana na Taarifa za Kamati ya Fedha za Serikali na Kamati ya Fedha za Serikali za Mitaa kuwa, kuna tatizo kubwa sana la fedha za ruzuku au za Miradi mbalimbali kuchelewa kupelekwa au kupelekwa kidogo tu. Tatizo hili linakwamisha sana utekelezaji wa Miradi mbalimbali au hukwamisha kabisa uendeshaji wa Halmashauri zetu pamoja na Ofisi za Mikoa yetu. Ninaishauri Serikali iwajibike ipasavyo ili kuzifanya Halmashauri zetu pamoja na Ofisi za Mikoa yetu, zifanye kazi vizuri kwani utekelezaji wowote ni lazima uwe na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la watumishi kukaa kituo kimoja muda mrefu kiasi kwamba, utendaji wao hushuka kwani huanza kufanya kazi kwa mazoea. Ninaishauri Serikali izingatie utaratibu wa watumishi kukaa kituo kimoja siyo zaidi ya miaka mtano. Hii itasaidia utendaji kuwa wenye tija na faida kubwa hasa kwenye Halmashauri za Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushauri wa mambo mbalimbali ya Kamati zote za Fedha, kila wanapomaliza kazi ya kukagua, Serikali yako hutekeleza machache na mengine hayafanyiwi kazi kabisa. Ninaiomba Serikali kwamba, maoni ya Kamati yafanyiwe kazi ili tupate maendeleo makubwa katika Taasisi zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono maoni ya Kamati zote kuwa, yapo malipo hewa ya watumishi. Hili ni tatizo kubwa sana kwani sioni sababu ya kuendelea kuwepo malipo hewa wakati Serikali inafanya uhakiki wa watumishi mara kwa mara. Ninadhani wanafanya makusudi kuiibia Serikali. Ninaishauri Serikali itoe adhabu kali kwa Watendaji wanaogundulika na makosa haya; huu ni wizi mtupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiunga mkono Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma juu ya Serikali kutokuwa na Mikataba ya wazi juu ya mikopo ya fedha kwenye Mashirika ya Serikali; mfano, *NSSF*, *PPF* na kadhalika. Napenda kuishauri Serikali kuwa, ili Mashirika ya Umma yapate Hati Safi; ni vema Mikataba ya Mikopo iwe wazi. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kuwa na uhakika kuwa fedha za shirika fulani ziko salama na zinaleta faida kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Watendaji wanapotekeleza Miradi ya Maendeleo kutumia kiwango kinachotakiwa (*value for money*); mfano, simenti kwenye ujenzi, kiwango cha moramu kwa barabara, bati geji inayotakiwa na kadhalika ili kuondokana na adha ya Miradi yetu huharibika mapema. Kamati hizi zinashauri kila mara bali upungufu bado upo.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie sehemu ya pili, 2.2, inayohusu TRA. Mimi nashauri Serikali ingefuta misamaha ya kodi ya mafuta na misamaha mingine yote ambayo inatolewa na *Custom and Excise Department* ya *Tanzania Revenue Authority* na ipelekwe kwenye *Income Tax Department*, maana wawekezaji watatulipa pesa nyingi *customs* tutamia. Serikali itakuwa imepata pesa nyingi bila riba na ile misamaha ihame *income tax*, maana wao wanafanya biashara kwa faida yao, wana-*deduct* ile *benefit* ambayo wangeipata kwenye *customs*. Hii itawafanya waoneshe faida ndani ya biashara zao ili waweze kurudisha pesa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya dhahabu na almasi yananyonywa na wawekezaji. Ninashauri madini haya yauzwe kupitia Benki ya Tanzania ili pesa za malipo zilipwe kwenye akaunti itakayokuwa BoT. Hii itaipa Serikali fursa ya kupata pesa za kigeni kwa gharama za juu na pia tutaweza ku-*monitor* mali yote wanayo-*export*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuchangia mapato ya Serikali kwenye makampuni makubwa; kwa mfano, BP Tanzania, Mbeya Cement, TIPER na Airtel. Tunaomba yafuatiliwe mapato kwenye mauzo ya Zain, Celtel na Airtel; *capital gain tax* tumepata shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kuchangia matumizi mabaya ya fedha yanayofanywa na Wizara ya Miundombinu, kwa kubomoabomoa nyumba bila sababu na kufanya Serikali ilipe pesa nyingi sana ambazo zingefanya kazi nyingine za maendeleo. Nashauri Wizara ya Ujenzi ijipange kulipa Wakandarasi ili wajenge barabara na waache kufuata watu. Ahsante.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kwanza, kukushukuru kwa kunipa nafasi japo ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kunisimamisha mimi miongoni mwa Watanzania wote kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nichukue nafasi hii pia kukishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Shukurani za pekee pia ziwaendee Wananchi wote wa Tanzania, kwa imani yao kubwa kwa chama changu, ambayo imesababisha mimi kuwepo Bungeni leo hii. Ninawaahidi kuwa, tutafanya kazi walivyotutuma katika kuhakikisha rasilimali za nchi yetu zinatumika ipasavyo kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mwisho, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wana-Mara wote hususan Wana-Tarime, familia yangu; Bibi na Babu Mantago, Baba na Mama Matiko, mume wangu mpenzi Dkt. Mukani na watoto wangu Maria na Nizole.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani zangu, ningependa kuchangia katika maeneo yafuatayo kwenye Hesabu za Mashirika ya Umma:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu imekuwa ikiingilia sana katika kazi za kiutendaji za Mashirika ya Umma. Ningependa kuishauri Wizara na Watendaji wengine, wajikite zaidi katika mambo ya Sera, yaani *Policy Issues* na kuwaachia shughuli zote za *decision making* kwa Bodi ya Wakurugenzi. Tumeona hili na jinsi gani limeathiri baadhi ya utendaji wa TANESCO katika kupata mzabuni ambaye Bodi ilimkataa, ambaye ni RICHMOND na baadaye DOWANS.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuweka wazi, changamoto mojawapo ambayo ilitupata ni kuhusu *contingency liability* ambayo imekuwa ni *debate* kuwa itokee kwenye vitabu vya TANESCO au lah! Ingawa Kamati iliekeza kuwa *contingency liability* ya kiasi cha bilioni 94 zisitokee kwenye Vitabu vya TANESCO. Hili ni kwa kuzingatia kuwa, Serikali ilishakubali kugharamia gharama za ukodishaji wa matanki au ununuzi wa mitambo ya uzalishaji wa umeme wa dharura kwa maana halisi kuwa gharama za uwekezaji, yaani *capacity charges* na kuwa TANESCO wao wagharamie gharama za uzalishaji, yaani *energy charges*.

Hivyo, ninaishauri Serikali ikubali hii *contingency liability* iingie kwenye vitabu husika. Kwa upande wa Serikali wawe na utamaduni wa kutimiza ahadi zao, kwani kutokufanya hivyo, kutalikosesha Serikali mapato kwa kugharamia gharama ambazo zingeweza kuepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusiana na utumiaji mbadala wa rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na Kamati yangu tulifanikiwa kufanya ziara Kanda ya Kusini, ambapo tulitembelea maeneo mbalimbali yenye makaa ya mawe na chuma. Tulikwenda Liganga, Mchuchuma, Ngaka na Kiwira.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi, nilisikitishwa sana kuona nchi yetu ina rasilimali nyingi kiasi kile, za kuweza kutupatia umeme wa uhakika kwa zaidi ya miaka 150 na tukaondokana kabisa na mateso ya kukaa gizani na hivyo kuzorotesha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda kueleza masikitiko yangu makubwa juu ya Shirika la ndege la *ATCL*. Inasikitisha kuona Serikali haioni umuhimu wa kulifufua Shirika letu hili na kulifanya kitega uchumi wetu kwa kulipatia kiasi cha mtaji linaloomba. Aidha, pia ikiwezekana kulisaidia mkopo kwa masharti ya kurejesha pindi litakapoweza kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri ikiwezekana iwepo Sheria ambayo italiweka Shirika la *ATCL* kwenye ushindani wa kibiashara, ambayo itaelekeza kuwa, Watumishi wote wa Serikali na wale wa Mashirika ya Umma ni lazima watumie *ATCL* kwa safari zao zote za anga. Hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia kuhusu upelekaji wa fedha katika Halmashauri zetu ili ziweze kufanya kazi za maendeleo kwa wakati. Hii itasaidia utekelezaji mzima na maendeleo ya nchi yetu. Pia ninashauri kuwa, iwapo utafika wakati wa kufunga mahesabu na matumizi ya mwaka husika, iwepo fursa ya kubakizwa pesa kwa Miradi ambayo imeshaanza ili iendeleo kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu inabidi iweke misingi imara ya kudhibiti ubadhirifu katika Halmashauri zetu. Dhana ya kuhamisha Mkurugenzi toka Wilaya moja kwenda nyingine ni ubadhirifu na utumiaji mbaya wa mali ya umma; na hii inakuwa kama Mkurugenzi anazawadiwa badala ya kuadhibiwa; hivyo, iwepo Sheria Mama na ianishwe kwenye Mikataba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo utaratibu wa mrejesho wa hela na viambatanisho vya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kama ilivyoelekezwa kwa vyanzo vyote vya mapato, kwa maana ya mapato ya Halmashauri na ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kero ya makusanyo ya kodi katika sekta mbalimbali ndani ya Halmashauri, inabidi iainishe viwango husika ili kuepusha

unyanyasaji wa Wananchi. Tumeona ni jinsi gani unyanyasaji unafanywa katika Sekta ya Biashara hasa kwa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni ubadhirifu wa mali za umma; ningeiomba Serikali ichukue hatua za makusudi za kusajili magari hayo ili yaweze kufanya kazi za Halmashauri na kama uagizwaji wake ulikiuka sheria, basi wahasika hao wachukuliwe hatua za kinidhamu na suluhisho lipatikane ili magari hayo yaweze kusajiliwa.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa Taarifa yao waliyowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo madogo madogo ambayo yanazisababishia baadhi ya Halmashauri zetu dosari mpaka kufikia Halmashauri hizo kupata Hati Chafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani na adhabu inayotolewa kwa Halmashauri zinazopata hati hizo kuwa ni kucheleweshwa kupata pesa za Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu hizo ni mbaya sana kwa sababu zinamnyima haki Mwananchi aliyetakiwa kupata huduma kutolewa na pesa zile za maendeleo. Inawezekanaje kosa au uzembe wa baadhi ya Watendaji wa Halmashauri aje aadhibiwe Mwananchi ambaye hajui lolote?

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu kwa Serikali ni kwamba, adhabu hiyo apewe Mtendaji wa Halmashauri aliyesababisha upatikanaji wa Hati Chafu katika Halmashauri yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali ijitahidi sana kuwahisha pesa za maendeleo ya miradi katika Halmashauri zetu. Kwa kuwa pesa zinapopelekwa kwa kuchelewa zinakwenda tena kukutana na sheria ya manunuzi matokeo yake utaona miradi mingi ya Halmashauri haikamiliki kwa wakati na kusababisha tuhuma nyingi katika Halmashauri zetu kuonekana kama pesa za miradi zinaliwa na watendaji na madiwani wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Halmashauri, Watendaji wanapobainika au kutuhumiwa kwa shutuma mbalimbali za kuziletea sifa mbaya Halmashauri hizo, utaona hatua wanazochukuliwa kwa kosa au ubadhirifu walioufanya ni kuhamishwa vituo na hivyo kusababisha matatizo waliyokuwa nayo kuhamia katika Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ichukue hatua za kisheria mara moja ili kuwa fundisho kwa Halmashauri nyingine na ninawalaani Watendaji mafisadi na wabadhirifu wa mali za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine ambalo baadhi ya Halmashauri zetu zilinunua magari ya mitumba, matokeo yake mpaka hivi sasa magari hayo hayana namba za usajili na yamekaa tu bila kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni ubadhirifu wa mali za umma; ningeiomba Serikali ichukue hatua za makusudi za kusajili magari hayo ili yaweze kufanya kazi za Halmashauri na kama uagizwaji wake ulikiuka sheria, basi wahusika hao wachukuliwe hatua za kinidhamu na suluhisho lipatikane ili magari hayo yaweze kusajiliwa.

MHE. ANAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa maandishi katika hoja hii ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unatoka katika kipengele namba 2.2, sura ya 10, kinachoongelea matengenezo ya magari na ununuzi wa mafuta ya magari. Kamati imeeleza japo kwa mifano michache, baadhi ya mianya ya matumizi mabaya ya pesa za Serikali katika matengenezo ya magari na ununuzi wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inatakiwa kujua kwamba, katika Halmashauri zetu kuna mianya mingine inayosababisha pesa ya Serikali kupotea. Mfano, katika matengenezo ya gari, badala ya gari kusimamiwa na Fundi Mkuu wa Karakana ya Halmashauri, badala yake anapewa dereva wa Halmashauri kupeleka gari kwenye karakana nyingine binafsi, hali ambayo dereva wa Halmashauri na mkuu wa karakana hupandisha bei ya vipuri na matengenezo na kisha kugawana pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna baadhi ya maofisa wana tabia ya kupitisha vibali vya mafuta kwa safari zisizokuwepo na mafuta hayo hutumika kwa shughuli zao binafsi au kuchukua pesa taslimu. Ninashauri urudishwe mfumo uliokuwepo zamani, magari yote ya Serikali yawe yanatengenezwa katika Karakana za Idara ya Ujenzi na mafundi *mechanics* waajiriwe sasa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaliwe mkakati madhubuti wa kuzuia matumizi mabovu ya mafuta. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Sasa moja kwa moja niwaite Wenyeviti husika kwa utaratibu ule ule wa asubuhi. Tuanze na Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ambaye aliwasilisha Taarifa yake asubuhi ajitahidi kupitia kwa kifupi, mkinibakizia vidakika viwili, vitatu, nitashukuru. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI ZA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako nikitaja yale majina hayatahesabiwa katika wakati?

NAIBU SPIKA: Hapana, hata kama usipotaja haina neno mimi ningeomba tu mjitahidi kutumia muda wenu mtakavyoona muda wenyewe ni mdogo.

MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI ZA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nisitaje?

Mheshimiwa Spika, asante sana kwa mwongozo wako. Kwanza kabisa nataka kusema kitu kimoja tangu nimekuwa Mbunge leo nimefurahi sana kwamba Bunge Zima limekuwa hapa na linatoa maneno mazuri na makali kuhakikisha kwamba fedha ya Serikali inatumika sawa sawa. Hii inaonyesha kwamba Bunge hili linajali sana kwamba fedha ya Serikali itumike sawa sawa. Basi tuendeleo na mtindo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la jumla, mimi naona mwaka unaokuja tuwaalike pia Makatibu Wakuu waje wasikilize Waheshimiwa Wabunge wanasema nini juu ya Wizara zao hili pia litaongeze *level* ya uwajibikaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi ambayo yamesemwa na nataka kuwahakikishia tu wote ambao wameleta michango yao kwa maandishi pia hiyo michango tutaipeleka na itaonekana kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

La tatu, mambo yote ambayo tumezungumza Serikali ndiyo tulikuwa tunaiambia katika hoja ya kwanza kabisa ambayo imezungumzwa na watu wengi ni kwamba Serikali kutotekeleza mapendekezo ya *CAG* na Kamati. Sasa hapa nataka kusema kwamba mwaka 2008 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaiwajibisha Serikali baada ya mkutano kama huu basi Serikali ijibu na tunategemea wameshafanya mwaka jana na tunategemea mwaka huu wafanye hivyo hivyo. Lakini kubwa tutekeleze basi mapendekezo ambayo yametolewa na *CAG* pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, Serikali kutochukua hatua zaidi za kinidhamu kwa wale ambao hawafuati sheria za fedha. Hii imezungumzwa na watu wengi sana, mtu anahamishwa au mtu haadhibiwi ipasavyo. Basi mimi nafikiri kwamba wito wa Bunge hili ni kwamba kama ilivyo katika Makampuni binafsi ukiboronga unafukuzwa, ukiboronga katika Serikali unahamishwa. Basi utaratibu huu tunaomba waajiri na mwajiri namba moja ni Rais wa Tanzania ndiyo yeye anasema wewe utakuwa Katibu Mkuu. Basi kama kweli wote tunasema tunataka pawepo na nidhamu, sheria ichukue mkondo wake, wale wanaoboronga kama ni kufukuzwa kazi wafukuzwe, kama ni kuadhibiwa waadhibiwe, lakini wasipate *promotion*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni mikopo ya wanafunzi zaidi kwa elimu ya juu. Hili ni jambo ambalo nina imani Waziri wa Fedha ameliona basi litafutiwe ufumbuzi. Huwezi ukawa unaanzia shilingi bilioni 130 inaelekea shilingi bilioni 240 na kitu mwaka kesho sijui itakuwa shilingi bilioni 300 na ngapi basi kwa hali kama hii lazima tunategemea Serikali ije na utaratibu ambao ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dhamana, tunafurahi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hatoi tena dhamana kwa Mashirika Binafsi. Tulichokuwa tunasisitiza hapa ni kwamba sheria ifuatwe. Sheria inakataza kutoa dhamana zaidi ya asilimia 70 na tumeona kwamba dhamana ya asilimia 100 ya shilingi bilioni 25 imetolewa. Basi kama hii imesikika sasa tunategemea jambo hili litakuwa sawa sawa. Deni la Taifa hapa tunachotaka kusema tu kwamba tusirudi tena miaka ya zamani ambapo tunakuwa ni watumwa wa Deni la Taifa. Naomba liangaliwe na liende katika utaratibu ambao linahimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *liabilities* na *commitments* hii tumeelezwa tulipokuwa tumezungumza na Kamati kwamba karibu tuta-move kutoka kwenye *cash budget* na kwenda *IPSA-accrue*. Kwa hiyo, tuki-move kwa upande huo ni matumaini yetu basi tutaona kwamba *liabilities* na *commitments* zitakuwa *part* ya Bajeti inayokuja katika Bunge lako Tukufu.

Kuhusu mapato Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza *obviously* kwamba hii ni sehemu ambayo tunapaswa kupanua wigo wa mapato yetu na pia yale ambayo tunayapata basi kila Mtanzania anapaswa kulipa kodi afanye hivyo. Jambo la utegemezi ni wito wetu hapa kwa miradi ambayo ni ya maana sana katika Taifa letu tujitahidi kutumia fedha za ndani kuliko kutumia fedha za kutoka nje ambayo unaahidiwa asilimia 100 unapata asilimia 50. Natumaini hili Waziri wa Fedha ataliangalia kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi imezungumzwa na ni matumaini yetu kwamba tutaanza kuona misamaha ya kodi inaanza kupungua. Matumizi ya Serikali kama yanazidi kwenda juu kila siku hata kama tukipata fedha kiasi gani hatutaweza kupata fedha ya kutosha. Kwa hiyo, hapa tunachotaka tudhibiti, sheria ifuatwe, masurufu yarudishwe na mambo kama haya. Watumishi hewa hili tumeshukuru kwamba angalau Serikali imeanza kulifanyia kazi kwa hiyo, tunachoomba hapa tuwe wakali ili tuhakikishe hatupotezi fedha nyingi kwa watu wasiokuwemo kwenye ajira ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kutoa hoja kwamba naomba sasa Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali. Naomba nimwite Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali za Mitaa. Tafadhali kwa muda ule tuliokubaliana pia. *(Makofi)*

MHE. AUGUSTINO L. MREMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati za moyoni, za upendo kwa Wabunge wote waliochangia Muswada wa Mahesabu ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Kwanza, wapo waliochangia kwa maneno, kwa mdomo yaani hapa hadharani na Wabunge kama 24 wamenandikia maoni yao ambayo sitaweza kuyajibu yote. Lakini la kwanza ninalotaka kuwaambia Watanzania ambao wametusia leo wameniona mimi Augustino Lyatonga Mrema nasimamia Hesabu za Serikali za Mitaa na ni mpinzani nipo *TLP*. Wamemwona John Momose Cheyo akisimamia Mahesabu ya Serikali Kuu na Mheshimiwa Kabwe Zitto akisimamia Mahesabu ya Mashirika ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kuwaambia Watanzania kama mambo yanaharibika, mambo ya fedha, mambo ya mapato hatuwezi kukwepa lawama sisi watatu tuliopo hapa kwa sababu tangu nimepewa kazi hii sijaona kiongozi yeyote au wa CCM au wa Serikali ananinyooshea kidole kwamba Mrema mbona unatuharibia mtandao wetu, mbona unatishia watu wetu. Ninachokiona ni Wabunge wengi wanataka niende kwenye Halmashauri zao. Ni kuona viongozi wenu wa Serikali wakiniambia ongeza *speed* na hatutakuwekea *speed governor*, uendeleo kufichua haya maovu na kuchukua hatua kali zinazostahili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama kazi yangu itanishinda ni kutokana na uwoga wangu labda au ugoigoi wangu au labda nimeshindwa kutimiza wajibu wangu lakini sio kwa sababu nimepata shinikizo la mtu yeyote nasema hapa. Siku ile Mheshimiwa Mkuchika tulipokuita nilitaka ku-*test* kama hii kazi ni dharti au ya *chat* kwamba hebu tumwite Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeenda Rombo tukasema yule mtumishi tumemkuta kule amekula fedha za wananchi amehamishwa, amehamia sehemu nyingine. Sisi kama Kamati tunasema arejeshwe. Mheshimiwa Mkuchika alipokuja akasema hilo litatekelezwa mara moja. Mimi nilifurahi sana nikasema kama mambo yenyewe ndiyo hivyo kwa nini nchi hii maovu yasiondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukafika Mwanga tukakuta kuna *DED* mmoja zamani amechukua hela pale taarifa ya *CAG* inaonyesha vizuri tukasema lazima mtu yule akamatwe na ashtakiwe apelekwe Mahakamani. Mheshimiwa Mkuchika alipokuja kwenye Kamati yetu ya *LAAC* akasema hilo litatekelezwa mara moja. Kuna watu tuliwapa maonyo waandikiwe na yeye ndio *disciplinarian authority* tukafikiri hataandika akaja akatuhakikishia wale wote tuliowaonya tutawaandikia barua. Wengine tulisema wakatwe tozo asilimia 15, watu walifikiri labda sisi tumepotea njia. Tulipomwita je, na hawa Wakurugenzi ambao wanatakiwa watozwe tozo ya asilimia 15 vipi? Akasema mishahara yao itakatwa mwezi huu. Kilichobaki ni kwenda kuvizia kwake je, wameshakatwa kweli au hawajakatwa? (*Makofi*)

Kwa hiyo, tumekubaliana yale mambo ya kuhamisha mtu anaiba hapa anavuruga hapa anafanya ubadhirifu halafu unahamisha ubadhirifu katika Halmashauri nyingine haitafanyika, haitakuwepo. Haya watu wananunua vitu kwa bei, tumeenda pale Morogoro, Kilosa *injector pump* ya shilingi milioni 15 ambayo bei yake ni shilingi milioni tatu inanunuliwa kwa milioni 15. Vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachosema Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Waziri Mkuu mmenitia moyo sana, mmenipa imani kwamba nikifanya kazi zangu kama nilipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani zamani tuna uwezo wa kuibadili hii nchi. Kwa hiyo, ninachotaka kuwaambia Watanzania ile ya kufikiria kwamba kuna mtandao, kuna watu ambao wanaendeleza maovu katika nchi hii si kweli, mimi sijaona ningeona. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashukuru sana kwanza kwa kuniamini kwa sababu kama si Bunge hili nilikwishapotea kisiasa huku, lakini nilipokuja hapa mkasema Augustino Lyatonga Mrema kwa historia yake, kwa rekodi zake tutampa hii kazi afanye. Nawahakikishia Watanzania, nalihakikishia Bunge hili na Kamati yangu ya LAAC tutafanya kazi kwa uaminifu, kwa bidii ili kuweka historia ya nchi yetu kama nchi safi yenye utawala bora, utawala unaozingatia haki za binadamu Serikali inaaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, yapo mambo mengi yamezungumzwa hapa ambayo tayari yamekwishajibiwa na Waziri Mkuchika. Ninachokuomba niishie hapa kwa kuomba basi ile taarifa yangu na yale mapendekezo niliyotoa sasa yakubaliwe na Serikali iyatekeleze yote bila kuacha hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Asante Mheshimiwa Mrema, Mwenyekiti wa Kamati ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mrema, makofi haya yanakubali kazi yako Mzee. Mheshimiwa Kabwe Zitto Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma karibu. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mawaziri wamezitoa kufuatia taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa maandishi na wale ambao wamechangia kwa kusema. Waliochangia kwa kusema masuala ya Mashirika ya Umma wapo 18 na kwa maandishi wapo 16, hii inaonesha namna gani ambavyo Bunge sasa linaona umuhimu wa Mashirika haya katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni suala la *General Tyre*. Sasa Kamati ndogo imekamilika, Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara imetuletea Wabunge wake wawili ambao inawataka waingine huko ambaye ni Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Godbless Lema, kwa hiyo, wataungana na Wabunge wale watatu wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shughuli hizi zinafanyika. Kwa hiyo, mchango wa Mheshimiwa Godbless Lema alioutoa hapa uingie kwenye Kamati na maelezo ambayo Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami

ameyazungumza, Kamati itayazingatia ili kuweza kutoa taarifa ambayo itaweza kuinufaisha nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara ametutaka tuendeleze nguvu zaidi kuhusu suala la Mchuchuma na Liganga. Kamati ilikwenda Mchuchuma na Liganga na nilipata taarifa kwamba Serikali kupitia Baraza la Mawaziri limeshapitisha Waraka wa Uwekezaji wa Mchuchuma na Liganga. Napenda kuishukuru sana Serikali na kwa kweli ni aibu kwa nchi yetu. Kwa rasilimali ambayo tunayo pale mpaka leo tuwe tunahangaikia tatizo la umeme. Kwa hiyo, Kamati inaiomba Serikali ihakikishe kwamba inatekeleza kwa haraka sana suala hili. Kuna zaidi ya Megawati 1500 pale kwa miaka 150. Kwa hiyo, naomba hili liweze kuzingatiwa jinsi ambavyo inavyotakiwa na naomba Waziri wa Nishati na Madini suala la Kiwira liweze kukamilishwa kwa haraka kwa watu ambao wameomba ili tuweze kuifanya nchi yetu iweze kuondokana na tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL*. Mheshimiwa Waziri ametoa majibu hapa, napenda nilifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hakuna *justification* yoyote ya kwa nini tumeshindwa kuendesha *ATCL*. Sisi ni mabingwa wa kutafuta sababu, lakini hakuna *justification* yoyote ile. Tunachoomba Kamati ya Miundombinu, Wizara ya Usafirishaji na Kamati ya Mashirika ya Umma tuhakikishe tuna-*rescue ATCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mmoja hapa amesema kwamba *ATCL* bora ifutwe, haiwezekani. Huwezi kuwa na nchi ambayo haina *national carrier* na wala tusingie kwenye mtego wa kugeuza kampuni binafsi kuwa *national carriers* wala tusifikirie. Tuifufue *ATCL*, tuipe mtaji kama tatizo ni menejimenti tubadilisha menejimenti, kama ni Bodi tubadilisha Bodi. Lakini haiwezekani, ni aibu, ni aibu Taifa letu tunashindwa na Rwanda wametoka kwenye vita juzi wana *Rwandan Air* sasa hivi inafanya kazi. Tuondokane na hii aibu, Bajeti ikija tutenge fedha tufufue *ATCL*. Leo mtu anayetaka kwenda Kigoma, anapita Mwanza analipa shilingi 980,000/= kwa ndege. Sasa na mtu anayeenda Ulaya, haiwezekani. Naomba hili Waziri tusitafute *justification* zozote tufanye kazi tuhakikishe kwamba Shirika hili linarudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumzia kwamba kuna malalamiko kuhusiana na mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwanza kama tulivyoeleza tunashukuru na Mheshimiwa Halima Mdee amelizungumzia sana hili ku-*rescue PPF*. Lakini pia kuna malalamiko kwamba mifuko inawezeza katika maeneo ambayo hayawajali watu wa kawaida, inawezekana.

Lakini lazima tu-*appreciate* pale ambapo kuna mambo mazuri yamefanyika. Kwanza *Dodoma University* ni Mifuko ndiyo imejenga, pili sasa hivi kuna mradi mkubwa sana pale Mchikichini Dar es Salaam kwa watu wa kawaida mradi ambao unaendeshwa na watu wa *NSSF*. Lakini pia *PSPF* wana mradi Mwanza, *LAPF* wana mradi ambao wame-*design*, *PSPF* sasa hivi wanatafuta maeneo ya kujenga miradi ya watu wa kawaida. Kwa hiyo, nadhani kwamba tukienda vizuri na Serikali ikiacha kuingilia mifuko na kulipa fedha zake itaweza kwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala la *governance*. Mheshimiwa Peter Serukamba amelizungumzia kwa uchungu sana. Kwanza ifahamike hili suala si langu binafsi. Kama kuna Mbunge ambaye anafikiria kwamba suala hili ni la Wabunge ambao wasiokuwa kwenye Bodi, ni la Mheshimiwa Zitto peke yake hapana. Hili suala ni la Kamati nzima na wala si jipya na ni suala ambalo limekuwepo Mikutano mitatu ya Bunge la Tisa. Suala la *expertise* tunakubali kuna Wabunge wana-*expertise so we have to choose*. Kaa Bungeni au unaenda kwenye Mashirika, *so simple*. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge kuna *abuse* kubwa sana ya uteuzi wa Bodi. Kuna *abuse* kubwa. Kuna Wabunge hapa na tunawajua, tuna-*privilege* ya kuwa na hizo *information* wana Bodi zaidi ya moja, zaidi ya mbili au tatu na Sheria inasema Bodi zisizidi tatu kwa mtu mmoja. Sheria inasema Waziri kabla hajateua *Treasury Registrar* aweze kukubali. Hakuna Waziri anayefanya hivyo. Tukubali tu kwamba ni makosa tuweze kurekebisha twende mbele na kama imewezekana kwenye Bodi za Mifuko ya Fedha kwa nini isiwezekane kwenye Bodi zingine? Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili tuweze kuliangalia na kuweza kuhakikisha kwamba tunalitua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni mapato. Mheshimiwa John Cheyo amezungumzia, *deal* ya *Airtel* na *Zain*. Serikali yetu imeshindwa, imepoteza kwa sababu ubovu wa Sheria kukusanya *380 million USD*. Juzi tumesikia *Vodacom* na wenyewe wameuza, *we don't know yet*. Kamati imewaomba *TRA* walivyokuja kwenye Kamati wafanye *study* na tumewaambia ndani ya mwezi mmoja watuletee *report* ili tuweze kuona katika hizi *deal* ambazo zinatokea na zipo kwenye maeneo mengi sana, zipo kwenye makapuni ya madini na kadhalika. Ni kiasi gani cha fedha ambacho tunaweza kukipata na Serikali iweze kuleta Muswada hapa Bungeni tuweze kuziba hii mianya ya upotevu mkubwa sana wa mapato. *Deal* ya *Airtel/Zain* ambayo tumepoteza zaidi ya *380 million USD* ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 470 ni barabara ya lami kutoka Iringa mpaka Babati, *one transaction*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali iweze kuona hii mianya ambayo inatokea. Naamini kabisa kwamba tunao uwezo wa ku-*raise revenue* ya kutosha. Mwisho kabisa ni *concession fee* za *TANAPA*. Naona muda umeisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma pamoja na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. ESTER N. BULAYA: Meshimiwa Naibu Spika, naafiki. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma na nawashukuru Wenyeviti wote na Kamati zao kwa kazi nzuri ambayo mnatufanyia kwa niaba ya Bunge Zima na mimi niseme mawili kidogo kwamba yapo mambo yanatakiwa kuyatazama kwa upana wake. (Makofi)

Moja ni hili linalosemwa mara kwa mara kwamba Wabunge wasiwe Wajumbe wa Bodi. Nataka kuwakumbusha tu kwamba katika kulifanyia kazi Wabunge wote hapa ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri za Wilaya kwa maana hiyo baadhi yetu tulio wengi ni wajumbe wa Kamati za Fedha za Halmashauri na Wajumbe hao hao baadhi yetu tunaunda LAAC ambayo Halmashauri hizo zinakuja huko na sisi tulikuwa ni sehemu kule. Kwa hiyo, je, sasa Wabunge wote watoke kwenye Halmashauri zote Tanzania? Haya ni mambo ya kujiuliza.

Lakini vilevile tumekuwa tukichagua baadhi ya Wajumbe kwenye Bodi za Vyuo Vikuu si Serikali peke yake, sisi wenyewe Bunge tumekuwa tukichagua hapa nao watoke huko? Je, Hesabu za Bunge letu, Bunge kama Taasisi zinaenda kwenye Kamati ipi katika Kamati hizi tatu? Zinaenda PAC si ndiyo jamani. Sasa inakuaje Hesabu za Bunge zinakwenda POAC? Kwa maana hiyo inabidi kitafutwe chombo kingine ili Hesabu za Bunge zikakaguliwe huko?

Kwa kumalizia tu, miaka minne iliyopita niliwahi kuongoza Ujumbe wa Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwenda nchini Denmark. Tulienda Denmark tukatembelea kule, moja ya vitu tulivyojifunza Denmark ni kwamba Kamati ya PAC ambayo hapa kwetu ndiyo hizi zote tatu inaundwa na Wajumbe saba au nane lakini wote wanatoka nje ya Bunge. Wanachaguliwa watu wanaelewa masuala ya mahesabu nje ya Bunge. Hiyo ndiyo hoja, kama tunataka kwenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hatua tuliyoifikia ni hatua ya mimi kuwahoji kuhusiana na hoja zilizotolewa hapa na hoja yenyewe ni kwamba sasa Bunge likubali kupokea Taarifa za Kamati za Hesabu hizi tatu, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati za Hesabu za Serikali Kuu pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hizo. *(Makofi)*

(Taarifa za Kamati za Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati za Hesabu za Serikali Kuu Pamoja na Mapendekezo na Maoni Zilipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunazipokea Taarifa hizi na tunaiomba Serikali izifanyie kazi na kwa kuwa Kamati hizi zinaendelea kufanya kazi na Serikali basi tuendeleo taratibu. *(Makofi)*

Nina matangazo mafupi tu hapa, la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Iddi Azzan anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho mazoezi yanaendelea Jamhuri Stadium kwa maandalizi ya mechi za mpira wa miguu na mpira wa pete wiki ijayo. Hivyo anawaomba wote wale ambao wanashiriki na waliokuwa wamelegea legea kidogo wajitahidi kushiriki kwenye mazoezi. *(Makofi)*

Tangazo la pili, naomba niwatangazie kwamba Wabunge waliokuwa wanavitambulisho vya muda ambao wameshapiga picha warejeshe vitambulisho hivyo leo mapokezi hapa ukumbini ili usiku huu watengenezewe vitambulisho vya kudumu na

watapewa kesho na wale ambao hawajapiga picha wajitahidi kesho wahakikishe kwamba wanapiga picha ili zoezi la vitambulisho liweze kukamilika. (*Makofi*)

Tangazo la tatu na la mwisho naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge taarifa ya uchaguzi wenye nia ya kugombea nafasi za uwakilishi zifuatazo, kuwa wanaweza kuchukua fomu Ofisini kwa Katibu wa Bunge na kuzirudisha kabla ya saa kumi jioni siku ya Jumanne tarehe 12 Aprili, 2011, aidha, maelezo kuhusu chaguzi hizi yamebandikwa katika sehemu ya matangazo jengo la utawala. (*Makofi*)

Nafasi hizo za uwakilishi ni tatu, ya kwanza uwakilishi katika Bunge la Afrika (*PAP*) ambapo kuna nafasi tano. Undani wake uko katika matangazo. Ya pili ni nafasi ya uwakilishi katika Bunge la *SADC (SADC PF)* nafasi mbili na tulishaelezwa kwa nini tunajaza nafasi hizo mbili na tatu uwakilishi katika Bodi ya *APRM Tanzania*. Tulimchagua Mheshimiwa Magale Shibuda na tumeambiwa nafasi za kule ni mbili kwa hiyo imebaki nafasi moja na hii nafasi ni kutoka Chama Tawala. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu, shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika zote nasema asanteni sana kwa ushirikiano mlionipatia. (*Makofi*)

Naomba sasa kwa fursa hii niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho kutwa siku ya Ijumaa, tarehe 8 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi. Lakini tukumbuke kwamba kesho japo ni sikukuu hapa Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar Kamati ya Katiba na Sheria itakuwa na vikao vya kuwasikiliza wadau kwa ajili ya Muswada ule wa Sheria ya kuwezesha mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya nchi kuweza kutekelezeka. Kwa hapa Dodoma zoezi hilo litakuwa katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa nne kamili asubuhi. Asanteni sana.

*(Saa 2.20 usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 8 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi)*